

**MWELEKEO WA KIUBWEGE KATIKA TAMTHILIA YA KISWAHILI
MINTARAFU YA *AMEZIDI* NA *BELUWA***

**NA
ACHIENG VIVIAN ODHIAMBO**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KATIKA KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI
ZA JAMII, IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA
ILI KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA
UZAMILI KATIKA KISWAHILI**

CHUO KIKUU CHA MOI

2024

IKIRARI**Mtahiniwa**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine ili kutimiza baadhi ya mahitaji ya shahada ya Uzamili ya Kiswahili.

Sahihi: _____

Tarehe: _____

Achieng Vivian Odhiambo**SASS/PGK/04/19****Wasimamizi**

Hii tasnifu imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi ambao waliteuliwa na Seneti ya Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi: _____

Tarehe: _____

Bw. Collins K. Mumbo

Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika

Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii

Chuo Kikuu cha Moi

Sahihi: _____

Tarehe: _____

Dkt. Harriet Ibala

Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za kiafrika

Kitivo cha Sanaa na Sayansi za Jamii

Chuo Kikuu cha Moi

TABARUKU

Kwa:

**Edward Le Quense na marehemu Albert Le Sueur
(Dadie na Grandpa)**

SHUKURANI

Furaha niliyo nayo moyoni ni tele. Shukurani zangu za dhati ni kwa Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kukamilisha kazi hii. Wema wake ni wa daima na milele kwani amenipa afya na fursa ya kushuhudia neema zake.

Aidha, ninashukuru Chuo Kikuu cha Moi kwa kuniwezesha kujielewa na kujiendeleza kitaaluma ili kufikia ndoto yangu. Vile vile sitawasahau wahadhiri wote katika idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika kwa kunikuza na kuwa tayari kunipa msaada na kuniongoza kila nilipokuwa na hitaji.

Isitoshe, kazi hii imekamilika kutokana na ukarimu, juhudi na hisani za wasimamizi wangu; Bw. Collins K. Mumbo na Dkt. Harriet Ibala. Ushauri wao ulinifaa zaidi na kuniwezesha kutia shime na kujizatiti kuikamilisha tasnifu hii. Ninawashukuru sana kwa uvumilivu wenu na kujitolea kwenu kwa dhati kunirekebisha pale ambapo niliweza kukosea, kweli mmevumilia makosa yangu na katu hamkuchoka kunikosoa. Daima nitakumbuka ushauri wenu.

Sina budi kusema asante kwa Shirika lililonipa ufadhili; The Jersey Charitable Trust for Commonwealth Students. Ninashukuru sana kwa kutochoka kubeba mzigo wangu wa masomo, naomba Mola aunyooshe mkono wake wa Baraka kwa wote walioshiriki katika kunifadhili.

Kadhalika, shukurani za dhati zimwendee baba yangu mpendwa, Augustus Odhiambo kwa juhudi na fadhila zake kwangu. Neema za Maulana naomba zimiminike kwako kwa kunijali na kunipa malezi mema.

IKISIRI

Utafiti huu umeshughulikia mwelekeo wa kiubwege katika tamthilia ya Kiswahili, mintarafu ya *Amezidi* (1995) na *Beluwa* (2012). Nadharia iliyoongoza kazi hii ni nadharia ya Ubwege iliyoasisiwa na Albert Camus ambayo, kimsingi imeangazia ukosefu wa maana ya maisha ya binadamu ulimweguni. Data za uchunguzi huu zilitokana na uhakiki wa kazi hizi mbili kwa misingi ya mihimili ya nadharia ya ubwege. Madhumuni ya utafiti huu ni pamoja na; kuchunguza vipengele vya kiubwege kimaudhui na kifani katika tamthilia ya *Amezidi na Beluwa*, kujadili mwelekeo wa kiubwege katika tamthilia ya *Amezidi na Beluwa* pamoja na kutathmini mwelekeo wa kiubwege katika *The Myth of Sisyphus*. Kutokana na madhumuni haya, utafiti huu umejiegemeza kwenye nadharia tete kwamba *Beluwa* na *Amezidi* ni tamthilia za kiubwege, kuna kufanana kwa mwelekeo wa kiubwege katika tamthilia ya *Amezidi na Beluwa* na Albert Camus aliweka msingi wa nadharia ya Ubwege katika *The Myth of Sisyphus*. Tofauti na tafiti zilizofanywa hapo awali, utafiti huu umejikita katika mwelekeo wa kinadharia ambao wahakiki wengi hawakuzingatia katika tamthilia ya *Amezidi*. Aidha, utafiti huu umehusisha ulinganifu kinadharia ambao haukuchunguzwa na wahakiki wa awali. Huu ni utafiti wa kiuhakiki, na hivyo mbinu zilizotumiwa kukusanya data ni utafiti maktabani ambapo usomaji makinifu wa tamthilia hizi mbili ulichangia katika kudondoa vipengele vya kiubwege kama vinavyojitokeza katika tamthilia hizi mbili, na kudhihirisha mwelekeo wa kiubwege wa watunzi hawa pamoja na kubainisha mwelekeo wa kiubwege katika *The Myth of Sisyphus* (1942). Maktaba tuliyotumia ni ya *Margaret Thatcher* ya Chuo kikuu cha Moi, ambamo tulisoma majarida, vitabu na makala zinazohusiana na mada ya utafiti. Kadhalika tulitembelea tovuti mbalimbali zinazozungumzia Ubwege pamoja na kupakua makala mbalimbali yanayohusu ubwege. Mbinu ya kitaamuli ilitumika katika uchanganuzi wa data tuliyokusanya na kueleza matokeo ya utafiti. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kwamba tamthilia ya *Amezidi na Beluwa* ni kazi za kiubwege na watunzi walifuata mwelekeo wa kiubwege wake Albert Camus; ambaye anashikilia kwamba Mungu yupo japo binadamu hapaswi kuishi kwa matumaini ya kukombolewa naye bali, afanye juhudi za kujipatia maana ya maisha yake akisubiri kifo-ambacho ndicho hatima ya binadamu wa kiubwege. Mbali na utafiti huu kuweka wazi mwelekeo wa kiubwege wa Albert Camus katika *The Myth of Sisyphus* (1942), utaongeza maarifa yaliyopo kuhusu tamthilia za kiubwege na fasihi kwa jumla.

ABSTRACT

This research sets out to examine the approaches to absurdity as portrayed in the Swahili play; *Amezidi* (1995) and *Beluwa* (2012). It was guided by the Absurdity theory by Albert Camus which puts emphasis on the absence of meaning of human life. The Data was collected through the critique of the two plays in relation to the tenets of the Absurdity Theory. The objectives of the study includes; one, examining absurdity as portrayed through themes and styles in *Amezidi* and *Beluwa*, two, examining the approaches to absurdity as portrayed by the selected writers in the two plays, and lastly, analysing the approaches to Absurdity as portrayed in *The Myth of Sisyphus* (1942). On the account of these objectives, the study was based on the following hypothesis: that *Amezidi* and *Beluwa* are absurd plays, the two plays portray the similarity in approach to absurdity and Albert Camus used *The Myth of Sisyphus* (1942) to lay the foundation for his philosophy of Absurdity. Most studies have been done on the analysis of the Swahili play *Amezidi* in relation to its themes and summary of the play without being guided by the theory (absurdity theory) as is the case in this study. Again the study emphasized on theoretical comparison which has not been worked on in any of the two plays selected. This is a literal analysis research; hence most research was basically done in the library whereby we critically read the two plays and cite the various aspects of absurdity as portrayed in the two plays and how these aspects exhibit similarity in the approach to Absurdity. Being a qualitative study, qualitative techniques were used in data analysis. We made use of the *Margaret Thatcher Library* in Moi University, where we studied various research works, books and journals in regards to the topic of study. We also used the internet and websites to obtain relevant data to the area of study. The results for the research has shown that *Amezidi* and *Beluwa* are absurd plays and the writers followed the Albert Camus' approach to Absurdity; that God exists but man should not live with hopes of being saved from the absurdity of life. The absurd man should create his own meaning of life through his absurd actions as he waits for death-which is the last step in absurd man's life. Apart from that, the results for the research have given a fresh theoretical approach to critique swahili plays. Aside from the study being based on Albert Camus' Absurdity theory, it will add new knowledge to the existing knowledge of absurd plays and Kiswahili literature in general.

YALIYOMO

IKIRARI	ii
TABARUKU.....	iii
SHUKURANI.....	iv
IKISIRI	v
ABSTRACT.....	vi
YALIYOMO	vii
UFAFANUZI WA ISTILAHU.....	xi
SURA YA KWANZA	1
MISINGI YA UTAFITI	1
1.0 Utangulizi.....	1
1.1 Usuli wa Suala la Utafiti	1
1.2 Suala la Utafiti	5
1.3 Madhumuni ya Utafiti.....	7
1.4 Nadharia Tete	7
1.5 Sababu za Kuteua Mada.....	8
1.6 Umuhimu wa Suala la Utafiti	9
1.7 Misingi ya Nadharia.....	10
1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada	15
1.9 Upeo wa Utafiti.....	23
1.10 Mbinu za Utafiti	23
1.10.1 Uteuzi wa Sampuli	24
1.10.2 Mbinu za Ukusanyaji Data.....	24
1.10.2.1 Utafiti Maktabani.....	25
1.10.2.2 Vifaa vya Utafiti	26
1.10.3 Uchanganuzi Data na Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti	26
1.11 Hitimisho.....	27
SURA YA PILI.....	29
HISTORIA NA UAINISHAJI WA TAMTHILIA YA KISWAHILI	29
2.0 Utangulizi.....	29
2.1 Historia ya Tamthilia ya Kiswahili	29
2.1.1 Tamthilia ya Kiswahili kabla ya Ukoloni.....	29
2.1.2 Tamthilia ya Kiswahili wakati wa Ukoloni.....	30

2.1.3 Tamthilia ya Kiswahili baada ya Uhuru	32
2.2 Uainishaji wa Tamthilia	34
2.2.1 Aristotle na Uainishaji wa Tamthilia	34
2.2.2 Tamthilia ya Masimulizi-ongezi.....	36
2.3 Mawazo ya Aristotle kuhusu Tanzania	37
2.3.1 Ploti	38
2.3.2 Wahusika	39
2.3.3 Wazo.....	39
2.3.4 Lugha.....	40
2.3.5 Korasi/ nyimbo	40
2.3.6 Uigizaji	40
2.4 Mawazo ya Aristotle kuhusu Futuhi	40
2.4.1 Uainishaji wa Tamthilia kwa mujibu wa Method (2015).....	42
2.4.2 Uainishaji Kwa Kigezo cha Maudhui	42
2.4.3 Uainishaji kwa Kigezo cha Kusudio	44
2.4.4 Uainishaji wa Tamthilia kwa mujibu wa Wamitila	45
2.4.5 Melodrama	46
2.4.6 Vichekesho	47
2.4.7 Tanzania-ramsa	47
2.4.8 Tamthilia ya Kihistoria.....	49
2.4.9 Tamthilia Tatizo.....	49
2.5 Dhana na muktadha wa ubwege	49
2.5.1 Tamthilia ya Kiubwege	53
2.5.2 Mielekeo ya Tamthilia ya Kiubwege.....	55
2.6 Hitimisho.....	58
SURA YA TATU	59
MWELEKEO WA KIUBWEGE KATIKA TAMTHILIA YA AMEZIDI NA	
<i>BELUWA</i>	59
3.0 Utangulizi.....	59
3.1 Muhtasari wa Tamthilia ya <i>Amezidi</i> (S. A. Mohamed, 1995)	59
3.2 Muhtasari wa Tamthilia ya <i>Beluwa</i> (Pauline Kea Kyovi, 2012).....	61
3.3 Mlingano Kimaudhui katika Tamthilia ya <i>Amezidi</i> na <i>Beluwa</i>	63
3.3.1 Dhana ya Maudhui	64
3.3.2 Dhamira.....	64

3.3.2.1 Dhamira katika <i>Amezidi</i>	65
3.3.2.2 Dhamira katika <i>Beluwa</i>	68
3.3.3 Mandhari	72
3.3.3.1 Mandhari katika <i>Amezidi</i>	74
3.3.3.2 Mandhari katika <i>Beluwa</i>	77
3.3.4 Suala la Mungu (Dini).....	80
3.3.5 Suala la Kifo na Kaburi.....	84
3.3.6 Ukengeushi.....	87
3.3.7 Ukosefu wa uthabiti katika Elimu.....	93
3.4 Mlingano Kifani katika Tamthilia ya <i>Amezidi</i> na <i>Beluwa</i> kiubwege.....	98
3.4.1 Dhana ya Fani.....	99
3.4.2 Uhusika.....	100
3.4.3 Uchache wa wahusika	100
3.4.3.1 Wahusika wa kiutopia.....	101
3.4.3.1.1 Wahusika wa kinjozi.....	106
3.4.3.1.2 Wahusika Vibonzo.....	109
3.4.4 Ukosefu wa ruwaza za mazungumzo.....	115
3.4.5 Utupu.....	119
3.4.6 Matumizi ya Nyimbo	122
3.4.7 Matumizi ya vicheko na vilio.....	130
3.4.8 Lugha.....	134
3.4.9 Ploti	137
3.5 Hitimisho.....	141
SURA YA NNE	143
MFANANO WA MWELEKEO WA KIUBWEGE KATIKA <i>THE MYTH OF Sisyphus</i>, <i>AMEZIDI</i> NA <i>BELUWA</i>	143
4.0 Utangulizi.....	143
4.1 Historia ya The Myth of Sisyphus	143
4.1.1 Dhana za kiubwege za Albert Camus zinavyojitokeza katika <i>The Myth of Sisyphus</i>	145
4.1.1.1 Wazo la kiubwege.....	145
4.1.1.2 Binadamu wa kiubwege.....	146
4.1.1.3 Ulimwengu wa kiubwege (Uumbaji wa kiubwege)	147
4.1.1.4 Mukhtasari wa <i>The Myth of Sisyphus</i>	147

4.1.2 Mwelekeo wa Kiubwege Katika <i>The Myth of Sisyphus</i>	150
4.1.2.1 Vipengele vya kiubwege kutokana na dhana ya wazo la kiubwege	150
4.1.2.1.1 Suala la Kifo na Kaburi.....	150
4.1.2.1.2 Suala la Ukengeushi.....	152
4.1.2.2 Vipengele vya kiubwege kutokana na dhana ya Binadamu wa kiubwege	155
4.1.2.2.1 Maana ya Maisha na Uhuru wa Kiubwege	155
4.1.2.3 Vipengele vya kiubwege kutokana na dhana ya Ulimwengu wa kiubwege na uumbaji wa kiubwege	158
4.1.2.3.1 Ukosefu wa matumaini na kukata tamaa	158
4.2 Hitimisho.....	160
SURA YA TANO.....	161
MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....	161
5.0 Utangulizi.....	161
5.1 Matokeo ya Utafiti	161
5.2 Hitimisho.....	165
5.3 Mapendekezo	168
MAREJELEO	170
VIAMBATISHO	176
Kiambatisho A: Said Ahmed Mohamed na Uandishi Wake.....	176
Kiambatisho B: Pauline Kea Kyovi na Uandishi wake	179
Kiambatisho C: Albert Camus na Uandishi Wake	181

UFAFANUZI WA ISTILAHU

- Drama :** Ni hali ya kuishi tendo fulani kwenye jukwaa au mahali popote pale pa kuigizia kwa kipindi maalum. Ni uigizaji wa kisanaa wa maisha ya watu katika jamii kwa lengo la kuwasilisha ujumbe maalum.
- Fani:** Hurejelea muundo au mpangilio wa kazi fulani ya kifasihi au hata sehemu zake. Aghalabu wahakiki hupenda kutofautisha kati ya fani na yaliyomo au maudhui. Hurejelea mbinu na mtindo wa kuyawasilisha yaliyomo au maudhui.
- Maudhui:** Ni jumla ya mambo yote yanayozungumziwa katika kazi ya kifasihi. Maudhui hutumiwa kwa upana kujumlisha dhamira, falsafa, itikadi na msimamo.
- Mwelekeo:** Ni dhana inayotumiwa kuelezea mtazamo au mkabala anaochukua msanii au unaochukuliwa na jamii kuhusiana na jambo, tukio, suala au wahusika fulani. Huweza kupatikana katika fasihi andishi na fasihi simulizi.
- Tamthilia:** Ni mchezo wa kuigiza au mchezo ambao umeandikwa kama mazungumzo kati ya watu. Ni kazi ya kimaongezi ambayo huigizwa mbele ya hadhira au kazi iliyoandikwa kusomwa. Kimuundo tamthilia hugawika katika matendo na maonyesho na mazungumzo huchukua sehemu kubwa katika uwasilishaji wake wa maudhui.
- Tamthilia ya Masimulizi-ongezi:** Hii ni aina ya tamthilia ambayo huzua matumizi ya mbinu ya usimulizi katika mazungumzo; yaani wahusika wanawasiliana kupitia masimulizi na maongezi.
- Ubwege:** Ni dhana inayotumiwa kurejelea upumbavu au ujinga.

SURA YA KWANZA

MISINGI YA UTAFITI

1.0 Utangulizi

Sura hii ya kwanza inajadili usuli na suala la utafiti, sababu zilizopelekea kuteuliwa kwa mada ya utafiti, umuhimu wa utafiti, malengo ya utafiti huu, nadharia tete na nadharia iliyoongoza katika utafiti wetu. Tumeleza vilevile yaliyoandikwa kuhusu mada yetu ya utafiti, upeo wa utafiti pamoja na mbinu za utafiti zilizotumika.

1.1 Usuli wa Suala la Utafiti

Utafiti huu unahusu tamthilia; mojawapo ya tanzu kuu za fasihi andishi. Istilahi “*tamthilia*” imetokana na kitendo “*mithilisha*” kwa maana ya *kufananisha*. Wasomi na wataalam mbalimbali wanaifafanua dhana ya tamthilia kwa msingi mbalimbali kama tutakavyoeleza.

Uigizaji; ambapo Wafula (1999) anasema kuwa tamthilia ni ule utungo ulioandikwa kwa ajili ya kuigizwa. Hivyo yeye anaihusisha na drama ambayo anaieleza kuwa ni somo linalohusu uigizaji wa hali fulani, iwe ni vitendo au tabia au hata hisia za binadamu kwa kufuata utaratibu maalum. Aidha, ni utungo ambao unaweza kuwa umeandikwa au haukuandikwa, ambao unaliweka wazo linalotakiwa kuwasilishwa katika umbo la tukio la kuliwezesha kutendeka mbele ya hadhira (Mlama, 1983).

Clark (katika Killam, 1973) naye anaifafanua dhana ya tamthilia kwa kutumia neno drama, ambapo anasema ni uigizaji wa hali ya juu wa kitendo fulani muhimu kwa watu huku vipengele vya uwasilishaji vikiwa, vitendo, uzungumzi, muziki, nyimbo na densi. Vile vile, tamthilia inaelezwa kuwa ni utanzu wa fasihi uliokusudiwa kutendwa jukwaani kwa ajili ya hadhira fulani. Hivyo, tamthilia ni mchezo wa kuigiza (Mulokozi, 1996) ambazo kwa mujibu wa Muhando na Balisidya (1976) ni kitendo

chochote chenye sifa nne ambazo ni; mchezo, mchezaji, uwanja wa kuchezea na watazamaji.

Kutokana na vijezezi hivi, inadhihirika kwamba tamthilia ni utungo ambao huweza kuandikwa au kukosa kuandikwa; na kwamba utungo huo huwa na matukio ambayo yanauwezesha kutendeka mbele ya hadhira.

Utunzi wa tamthilia umechukua mikondo mingi tangu enzi za Aristotle (384-322 K.K), mwanafalsafa aliyechangia pakubwa kwa kutoa vipengele vya kimsingi katika uandishi wa tamthilia. Aristotele (1934) alipendekeza kuwa tamthilia iwe na sehemu tatu kuu; utangulizi (prologue), kitendo (exode) na kimalizio (epilogue). Kila sehemu ina sifa zake bainifu. Kwenye kitabu chake “*The Poetics*” Aristotle alitoa mwelekeo wake kuhusu uandishi wa tamthilia. Aristotle ameathiri sana utunzi wa tamthilia ingawa vigezo vyake vinajikita zaidi katika tanzia ya Kigiriki, kama vile tamthilia ya *Mfalme Edipode*, tafsiri yake Mushi, S. (1971)

Utafiti huu umetumia msingi wa uandishi wa ki-Aristotle kwa kulinganisha vipengele vya ubwege katika tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* ambavyo hatimaye vimedhihirisha mwelekeo wa kiubwege katika tamthilia ya Kiswahili.

Lewis (1962:1) akidai kwamba uandishi wa tamthilia umepitia historia ndefu, anasema yafuatayo;

“Historia ya drama ni historia ya binadamu kwa sababu jukwaa la drama hushughulikia maisha na mgogoro kati ya binadamu na ulimwengu anamoishi.”

Mtindo wa tamthilia ya Kiswahili umetokana na ule wa fasihi ya Uingereza ambayo ililetwa Afrika kupitia kwa elimu ya kikoloni (Bertoncini, 1989). Maandishi ya Shakespeare (2001), *Julius Caesar* ni mojawapo ya mfano mzuri. Tamthilia hugawika katika matendo na kila kitendo huwa na maonyesho kadhaa. Kila onyesho huwa na

waigizaji ambao hutekeleza majukumu maalum. Hata hivyo, siyo tamthilia zote hufuata mtindo huu. Wasanii wengine huzingatia hali ya kuitaja migawanyiko, yaani matendo na maonyesho, huku wengine wakitumia maonyesho pekee kama vile Said Ahmed Mohamed katika *Amezidi* na Pauline Kea Kyovi katika tamthilia ya *Beluwa*.

Tamthilia hushirikisha wahusika katika mazungumzo na vitendo ambavyo hubainisha mgogoro uliopo; kipengele kinachoonyesha tofauti iliyopo kati ya tamthilia na tanzu nyingine za fasihi. Aidha, tunakubaliana na Magare (2002) anapotoa kauli kuwa, tamthilia hudhihirisha hali ilivyo kwa uwazi zaidi mbele ya hadhira kwa muda mfupi na maudhui yote huhitimishwa. Kinyume na riwaya na ushairi, tamthilia ina uwezo wa kuyatongoa kwa urahisi maudhui yaliyomo kwa dakika au masaa machache mno.

Mtu aisomapo tamthilia yoyote humbidi aiandae katika jukwaa la bongo lake na kujaribu kuwahisi wahusika wa kuibainisha na kuutatua au kujaribu kuutatua mgogoro au matukio ambayo ndiyo viini hasa vya tamthilia nyingi. *Amezidi* na *Beluwa* ni miongoni mwa tamthilia za kisasa na zenye utata katika kuzielewa.

Tamthilia za kiubwege zilizuka kwa mara ya kwanza kule Uropa, hasa Paris baada ya vita vya pili vya Dunia miaka ya (1939-1945). Wasanii wa kazi za kiubwege walikuwa; Samuel Beckett, aliyeandika "*Waiting for Godot*" na Eugene Ionesco ambaye aliandika "*The Rhinoceros, The Lesson, The Killer, The Bald Prima Donna*". Aidha Albert Camus aliandika *The Myth of Sisyphus* katika kuweka misingi ya nadharia ya Ubwege.

Drama ya kiubwege ni tapo mojawapo ya matapo ya drama yanayotambulika katika karne ya ishirini na moja na inaweza kugawanywa katika makundi matatu. Kundi la kwanza ni la wanaoamini kuwa "Mungu yupo" linawakilishwa na mwanatheolojia wa Ki-Deni Soren Kierkegaard (1813-1855), ambapo Wamitila (2003:248) anaeleza

kwamba “katika maandishi yake mbali mbali na hasa *The Concept of Dread, Fear of Trembling* na *Sickness unto Death*, Kierkegaard alieleza kuwa mwanadamu hupata kimbilio kutoka mivutano ya maisha kupitia kwa Mungu. Hii ni imani ambayo iliishia kushika nguvu sana katika Ukristo...”. Albert Camus pia anajihusisha na imani hii kwamba “Mungu yupo”, japo anadokeza katika kueleza suala la *binadamu wa kiubwege* na *uhuru wa kiubwege* kwamba, binadamu asitarajie ukombozi wa kiumbe hicho bali afanye juhudi za kujitafutia uhuru wake mwenyewe kwa kukubali ubwege wake.

Kadhalika, kundi la pili ni la wasioamini kuwepo kwa Mungu ambalo linawakilishwa na Friedrich Nietzsche (1844-1900). Mtazamo huu unadhihirisha msukumo mpya uliopatikana katika utunzi wa tamthilia ambao ulijitokeza katika karne ya ishirini. Kando na Friedrich Nietzsche, Wamitila (2003) anataja kuwa wataalamu walioshikilia kwamba “Mungu hayupo” ni pamoja na Martin Heidegger, Karl Jaspers na Samwel Beckett. Anaendelea kueleza kwamba Nietzsche anajulikana kwa tamko maarufu katika *Joyful Wisdom* kuwa “Mungu amekufa.” Maelezo haya na misimamo ya wenzake, inadhihirisha kuwa wanaamini kwamba Mungu hayupo.

Waidha, kundi la tatu ni la wasio na uhakika kuhusu suala la Mungu (tuliliita *Kundi la Kati*) ambalo linahusishwa na Jean-Paul Sartre (1905-1980) ambaye; kutokana na utunzi wake pamoja na historia ya maisha yake ni wazi kwamba hana uhakika wa suala la kuwepo kwa Mungu. Maandishi yake ya mwanzo kama vile *Being and Nothingness* yanasawiri msimamo wake kwamba Mungu hayupo lakini baadaye hata alipokaribia kifo chake, alibadilisha msimamo wake na hata kuita Mkuhani wa kidini kwake. Kutokana na kusoma kwake kwa kazi ya Nietzsche (1943) “*New Mystic*” alikiri kwamba “Mungu amekufa” lakini akadai mwishoni kwamba; Hatufai kuelewa

kutokana na hili kwamba Mungu hayupo; amekufa, alikuwa akinena nasi na kwa sasa amenyamaza, tunagusa tu mfu. Miongoni mwa kazi za kifasihi alizozitunga ni kama vile; *The Wall, Existentialism is Humanism, The Reprieve, The Age of Reason*.

Hata kama kuna makundi haya matatu, kijumla drama ya kiubwege hudhihirisha wazo la binadamu kupatikana katika ulimwengu katili unaokatisha tamaa kutokana na Maisha duni yasiyo na maana. Kauli hii inaungwa mkono na Kitchin (1966) anapoeleza kwamba haja ya drama za kiubwege ni hali ya kukatisha tamaa ambayo hutawala binadamu katika ulimwengu katili anamoishi.

Wafula na Njogu (2007) wanatoa dai kwamba mhakiki aliyeshughulikia suala la ubwege kwa mapana na marefu ni Martin (1974), ambaye alitumia tamthilia za Beckett katika kutoa msimamo wake, kuhusiana na mihimili ya nadharia ya ubwege.

Katika bara la Afrika, watunzi walioegemea katika uandishi wa kazi za kiubwege ni pamoja na Robert Serumaga, aliyeandika “*Majangwa*” na “*The Elephant*”, Athol Fugard aliyeandika; “*The Coat, The Island, No Good Friday, The Blood Knot, Sizwe, Bansi is Dead na Nangogo*”.

1.2 Suala la Utafiti

Utafiti huu umejikita katika kuchunguza mwelekeo wa kiubwege katika tamthilia ya Kiswahili mintarafu ya *Amezidi na Beluwa. The Myth of Sisyphus*; ilitumika kwa kazi hii ilikuweka wazi msingi wa nadharia ya ubwege na vilevile kufaniksha lengo la tatu la utafiti huu. Wahakiki wengi walitoa mwongozo wa *Amezidi* kwa ajili ya kuwatayarisha wanafunzi kwa mtihani kitaifa wa kidato cha nne Nchini Kenya bila kuihusisha na nadharia ya Ubwege kama tulivyofanya katika utafiti huu. Aidha, hakuna makala au tahakiki yoyote mtandaoni kuhusu *Beluwa*. Kadhalika, hakuna uhakiki wowote wa kiulinganifu wa mwelekeo wa kiubwege ambao umefanywa

katika *Amezidi*, *Beluwa* pamoja na *The Myth of Sisyphus* kama tulivyofanya katika utafiti huu. Ni kutokana na haya ndipo utafiti huu ulifanywa ili kutoa mwelekeo wa kiubwege katika tamthilia ya Kiswahili. Utafiti huu umetathmini jinsi tamthilia ya *Amezidi* iliyoandikwa na Said Ahmed Mohamed (1995) na *Beluwa* ya Pauline Kea Kyovi (2012), zinavyolingana kiubwege. Mlingano huo ulichunguzwa kupitia kwa juhudi za kuzihakiki na kuzichambua tamthilia hizi mbili kwa kuzingatia vipengele vya kiubwege kimaudhui vikiwemo dhamira, mandhari, suala la Mungu (Dini), kifo na kaburi, ukengeushi na ukosefu wa uthabiti katika elimu. Kifani, tulichunguza vipengele kama vile; Uhusika ambao ulijumuisha uchache wa wahusika, wahusika wa kiutopia na wahusika wa kinjozi. Vipengele vingine vilivyochunguzwa ni ukosefu wa ruwaza za mazungumzo, utupu, matumizi ya Nyimbo, Vilio na Vicheko, matumizi ya Lugha inayotatiza mawasiliano pamoja na ploti mvingo. Vipengele hivi basi ndivyo vilivyodhihirisha mwelekeo wa kiubwege katika tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa*; kutokana na uchunguzi wa jinsi ambavyo waandishi hawa wawili wanavyovizingatia katika kazi zao.

Tamthilia ya *Amezidi* imefanyiwa uchambuzi na wahakiki kadha japo wapo wachache mno ambao wameihakiki kazi hii kinadharia hasa nadharia ya Uwege. Wahakiki wengi walijishughulisha na kutoa mwongozo wa kazi hii kwa ajili ya kutayarisha wanafunzi kwa mitihani ya kitaifa ya kidato cha nne wa 8-4-4, Nchini Kenya.

Wataalamu kama vile Wafula na Njogu (1999) na Njogu na Chimera (1999) hawakufanya uchanganuzi wa kiulinganifu kwa kutumia nadharia ya ubwege kama ilivyofanywa katika utafiti huu. Aidha, hadi sasa hakuna uhakiki wowote unaopatikana kwenye mtandao, majarida au vitabu kuhusiana na Mwelekeo wa kiubwege katika tamthilia ya Kiswahili mintarafu ya *Amezidi* na *Beluwa*, kama

tulivyofanya katika utafiti huu.

Kadhalika, tahakiki yoyote ya tamthilia ya *Beluwa* haijajitokeza mtandaoni au hata kwenye majarida hadi sasa. Utathmini wa Mwelekeo wa kiubwege katika *The Myth of Sisyphus* na tamthilia ya Kiswahili, haujafanywa licha ya kuwa Makala haya ndiyo yaliweka msingi wa nadharia ya ubwege. Utafiti huu basi umechangia katika kulinganisha mwelekeo wa kiubwege katika *Amezidi, Beluwa* pamoja na *The Myth of Sisyphus*; ambayo ilitumika kwa kazi hii ilikuwika wazi msingi wa nadharia ya ubwege na vilevile kufaniksha lengo la tatu la utafiti huu. Hivyo, uchunguzi wa kazi hizi kiubwege, umechangia pakubwa katika kuendeleza taaluma ya Fasihi kinadharia hasa nadharia ya ubwege na vile vile kutoa mwelekeo tofauti wa kuhakiki tamthilia ya Kiswahili.

1.3 Madhumuni ya Utafiti

- i. Kuchunguza vipengele vya kiubwege kimaudhui na kifani katika tamthilia ya *Amezidi na Beluwa*.
- ii. Kujadili ulinganifu wa usawiri wa kiubwege katika tamthilia ya *Amezidi na Beluwa*.
- iii. kutathmini mlingano wa mwelekeo wa kiubwege katika *The Myth of Sisyphus, Amezidi na Beluwa*.

1.4 Nadharia Tete

Utafiti huu umeongozwa na nadharia tete kwamba;

- i. *Beluwa* na *Amezidi* ni tamthilia za kiubwege.
- ii. Kuna kufanana kwa mwelekeo wa kiubwege katika tamthilia ya *Amezidi na Beluwa*.

- iii. Kuna mfanano wa Mwelekeo wa kiubwege baina ya *The Myth of Sisyphus*, *Amezidi* na *Beluwa*.

1.5 Sababu za Kuteua Mada

Wahakiki wa awali walijikita katika kutoa mwongozo wa tamthilia ya *Amezidi* (1995) kwa minajili ya kuwatayarisha wanafunzi kwa mtihani wa kidato cha Nne katika Shule za Upili nchini Kenya. Aidha, tamthilia ya *Amezidi* imehakikiwa kiubwege kwa ufinyu sana na wahakiki wachache, hivyo utafiti huu ulijikita katika kuchanganua tamthilia hii kwa kina zaidi kwa kuongozwa na nadharia ya ubwege, na umedhihirisha mwelekeo wa kiubwege katika tamthilia ya Kiswahili pamoja na kubainisha mfanano wa mwelekeo wa kiubwege unavyojitokeza katika *The Myth of Sisyphus* (ambayo ni kazi ya kwanza kabisa ya Albert Camus inayoangazia ubwege) *Amezidi* na *Beluwa*.

Ingawa uchambuzi wa tamthilia ya *Amezidi* umewahi kufanywa na wahakiki mbalimbali wakiwemo; King'ei (1997), Vuzo (1997), Ndalu (1998) na Maneno (1997), tahakiki zao zimeshughulikia zaidi vipengele vya maudhui na fani. Wafula (1999) pamoja na Njogu na Chimera (1999) wameshughulikia Ubwege kwa ufinyu sana.. Kwa upande wake Daniel (2017), alijaribu kumulika vipengele vya kiubwege katika *Amezidi* lakini hakushughulikia vipengele hivyo kiundani; kwa mfano aliangazia kipengele cha wahusika kwa kuchunguza maana ya majina ya wahusika, ambapo kulingana nasi si kipengele cha ubwege. Uhakiki wa wataalam hawa, haukuzama kumulika vipengele vya kiubwege kwa undani. Aidha, hawakujikita katika ulinganifu kinadharia hasa nadharia ya ubwege; ambayo ndiyo msingi wa utafiti huu.

Utafiti wowote kuhusu tamthilia ya *Beluwa* haujajitokeza mtandaoni wala kwenye majarida, hivyo basi tumeishughulikia ili kurahisisha uelewekaji wake kwa wasomi

au wahakiki wengine. Vile vile uhakiki ambao tumeufanya umetoa picha ya jinsi tamthilia hii na ile ya *Amezidi* zinavyolingana na kutofautiana kiubwege; hivyo kudhihirisha mwelekeo wa kiubwege kwenye tamthilia ya Kiswahili. Isitoshe, wahakiki ambao wameweza kuichambua *Amezidi*, hawakujikita katika ulinganifu kinadharia; hasa kwa kuchunguza vipengele vya nadharia ya Uwege kama tulivyofanya katika utafiti huu.

Tunaamini kwamba uchanganuzi wa tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* umetoa mchango mahususi katika kuongeza maarifa katika fasihi hususan kwa kutoa mwelekeo tofauti wa kuhakiki tamthilia ya Kiswahili kinadharia. Aidha, utafiti huu umerutubisha mambo ambayo tayari yalisemwa na kufanywa na wahakiki wengine kuhusiana na tamthilia ya *Amezidi*.

Ufasiri wa maandishi haya yamechukua mkondo wa kuzingatia masuala ya kiubwege; kama yalivyowekewa msingi na Albert Camus pamoja na kuonyesha mlingano wa mwelekeo wa kiubwege aliouchukua na ule wa Said A. Mohamed na Pauline Kea Kyovi.

Tumejikita katika kuchanganua tamthilia hizi mbili kiubwege kwa kuangazia vipengele vya kiubwege kimaudhui na kifani, na hatimaye kudhihirisha mwelekeo wa kiubwege uliochukuliwa na watunzi hawa pamoja na kuonyesha mfanano wa mwelekeo wa kiubwege katika *The Myth of Sisyphus*, *Amezidi* na *Beluwa*.

1.6 Umuhimu wa Suala la Utafiti

Utafiti huu umeweka wazi mwelekeo wa kiubwege wa Said A. Mohamed katika *Amezidi* (1995), Pauline Kea Kyovi katika *Beluwa* (2012) na Albert Camus katika *The Myth of Sisyphus* (1942). Aidha, umeongeza maarifa yaliyopo kuhusu tamthilia za kiubwege na fasihi ya Kiswahili kwa jumla. Kama tulivyoeleza hapo awali kwamba

watafiti wengi wameshughulikia tamthilia ya *Amezidi* kwa kuegemea kwenye vipengele vya kimaudhui na kifani, na hata wengine kutoa mwongozo kwa ajili ya kuwatayarisha wanafunzi wa shule za upili kwa mtihani wa kidato cha Nne nchini Kenya bila kuongozwa na nadharia, hasa Ubwege katika uhakiki wao. Utafiti huu, tofauti na tafiti zilizofanywa hapo awali, ulilenga kuchunguza mwelekeo wa kiubwege katika tamthilia ya Kiswahili hususan *Amezidi na Beluwa*. Yaani ulichunguza jinsi ambavyo tamthilia ya *Amezidi na Beluwa* zinadhihirisha vipengele vya kiubwege na hatimaye kuzilinganisha na utunzi wa awali ulioweka msingi wa nadharia ya Ubwege yake Albert Camus; *The Myth of Sisyphus*. Kwa ujumla, utafiti huu ulijikita kwenye mwelekeo wa kinadharia katika uhakiki wa tamthilia ya hizi mbili; *Amezidi na Beluwa*.

Kadhalika, utafiti huu umechangia katika taaluma ya Fasihi linganishi kwa kutumia nadharia ya Ubwege, kwa vile tumechunguza vipengele vya kiubwege vinavyojitokeza katika tamthilia ya *Amezidi, Beluwa* na jarida la *The Myth of Sisyphus*, ambavyo vilitusaidia katika kubainisha mwelekeo wa kiubwege katika tamthilia ya Kiswahili.

Utafiti huu umeongeza maarifa yaliyomo kuhusu tamthilia za kiubwege na fasihi kwa jumla. Suala hili halijatafitiwa kwa mapana, kwa hivyo utafiti huu umedhihirisha mwelekeo wa kiubwege katika tamthilia ya kiswahili pamoja na athari ya Albert Camus katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Maarifa zaidi yamefafanuliwa kuhusu ubwege ambalo litawanufaisha watafiti wa siku zijazo.

1.7 Misingi ya Nadharia

Kimsingi, nadharia huwa chombo muhimu zaidi kwa mhakiki yeyote. Hii ni kwa sababu nadharia ndiyo hutoa mwongozo bora zaidi wa utafiti. Utafiti huu

umeongozwa na nadharia ya ubwege. Kando na mwasisi wa nadhari hii, Albert Camus, kuna wataalamu wengi wanaohusishwa na ubwege wakiwemo; Cruickshank, Martin Esslin miongoni mwa wengine.

Mwandishi na pia mwanafalsafa wa Kifaransa Albert Camus, ambaye aliweza kuiingiza nadharia hii katika fasihi mwaka wa 1913-1960. Kulingana na Camus, ubwege ni kitu ambacho hakiwezi kuguswa bali ni uhusiano wa kidhahania, kati ya akili pevu na ukweli wa kuweco kwa binadamu humu ulimwenguni. Camus anaendelea kueleza kuwa hali hii ya ubwege hujitokeza kwa sababu ya kutoridhika kwa akili kulingana na matarajio yake juu ya utaratibu wa mambo yanavyotendeka ulimwenguni; kinyume na hayo matarajio, hali ambayo inajitokeza ni ile yenye fujo na ambayo hukosa muwala. Hali hii inaungwa mkono zaidi na Cruickshank (1960) kwa kusema kwamba Camus alimaanisha kuwa ubwege ni ukosefu wa muumano mzuri au usawa kati ya mahitaji ya kiakili na ukosefu wa uwiano ulimwenguni. Aidha Camus anaeleza kwamba hakuna furaha ya kudumu katika maisha ya binadamu wa kiubwege; maisha yake yamejaa huzuni tupu.

Camus (1955) anatoa dai kwamba hali ya kukosa kuridhika kwa moyo husababisha kuteseka kwa akili. Aidha hali hii hutoa suluhisho aina mbili kwa binadamu; ama akubali ukweli wa hali ya Maisha yake duni na kuukabili au aamue kujiua. Hata hivyo, anapochagua kujiua, binadamu anaangamiza akili yake ambayo inapaswa kuhisi ubwege. Halikadhalika, anapokubali hali ngumu iliyojaa mateso, ambayo ndiyo ukweli wa Maisha ya kiubwege, anadhihirisha utata ambao ndio ubwege.

Naye Martin (1961:5) akimnukuu Ionesco, anadai kwamba;

“Ubwege ni kilichokosa nia na kimetengwa kutoka kwa Imani zinazohusiana na dini, tabia za kiungu na misingi ya kiakili pamoja na mawazo. Binadamu amepotea na matendo yake yote ni ya kijinga na hayana maana.”

Martin anaeleza dhana ya ubwege kuwa inahusishwa zaidi na mchezo wa kuigiza na hufungamana na futuhi zenye vipengele vya kitanzia. Wahusika wanajipata katika hali ya kutamauka na wanalazimika kurudia matendo ambayo hayana maana yoyote. Anaendelea kueleza kuwa ploti za michezo ya namna hii ni mviringo, ni wigo wa kubeza na kukiuka uhalisia. Wahusika dhahiri wanajikuta wanaishi pasipo na matumaini hivyo, wanajitahidi kukubaliana na hali yao ili waweze kuishi, yaani wanaishi kwa sababu wapo na shida zao hukosa mantiki.

Kwa upande wake Alembi (2000), anaeleza kwamba ubwege ulitumiwa kwa mara ya kwanza na Albert Camus kuonyesha tofauti kati ya mawazo ya binadamu na matarajio yake na ulimwengu katili. Anaendelea kueleza kwamba mnamo 1942, Albert Camus tayari alikuwa ameanza kudadisi kwa nini binadamu aendelee kuishi katika ulimwengu katili, ilhali dunia ilikosa maana tena? Katika makala yake “*The Myth of Sisyphus*” Camus ameeleza jinsi ambavyo ukosefu wa matumaini wa wahusika, ulivyosababisha hali ya ubwege. Hali hii ndiyo ilitawala katika kipindi cha na baada ya vita vya pili vya Dunia.

Martin (1961) anatoa maelezo yake kuhusu tamthilia za kiubwege kwa kusema kuwa, tamthilia za kiubwege hukosa hadithi inayofululiza vizuri au ploti inayoweza kuelezwa kikamilifu. Aidha anasema kuwa, kama hadithi nzuri hutambulika kwa usawiri na umotishaji mzuri wa wahusika wake, basi tamthilia za kiubwege mara nyingi huwa hazina wahusika wa kutambulika vyema ila hudhihirisha wahusika batili tu. Martin anaendelea kueleza kwamba tamthilia za kiubwege hukosa maudhui pevu

na muwala wa maudhui. Isitoshe, anadai kuwa tamthilia za kiubwege hutawalwa na ndoto nyingi tu bila uhalisia.

Zaidi ya hayo, tamthilia hizi pia hubainisha utengano na upweke wa mazungumzo. Lewis (1962:259) anaeleza hii hali duni ya binadamu ulimwenguni kwa kutokeza yafuatayo;

“Binadamu ni pweke na ni yule aliyepotea katika ulimwengu ambamo ametupwa na Mungu. Sayansi na fikira za binadamu ni uongo; binadamu amefungwa na ulimwengu katili anamoishi na kitu kilichobaki ni kifo ambacho ndicho hatima ya binadamu wa kiubwege. Mawasiliano hayawezi kutekelezwa tena kwa vile hata lugha imekufa. Ulimwengu ni ule wenye fujo.”

Katika Ubwege kuna ukosefu wa utaratibu. Binadamu anaishi kwenye ulimwengu katili na amekosa uwezo wa kupanga matendo yake. Hivyo, anayotenda na kusema huwa yamekosa muumano. Hali inayojitokeza ni ya kiubwege.

Fasihi ya ubwege hubainisha ukweli juu ya maisha ya binadamu ulimwenguni. Kama anavyoeleza Webb (1972) fasihi ya kiubwege hudhihirisha hali ya fikira za binadamu. Binadamu anajaribu kutafuta ukweli ila hizo fikira zinamfanya kuukosa. Tamthilia za kiubwege huwa na kusudi la kuonyesha kushindwa kwa binadamu kujielewa na hali yake ulimwenguni.

Kwa upande wake Mbatiah (1997) anasisitiza umuhimu wa mandhari kazi ya kiubwege. Anadokeza kuwa suala la mandhari ni muhimu sana katika fasihi ya kiubwege. Wasanii wa ubwege, wanatumia mandhari kudhihirisha msimamo wao kuwa ulimwengu ni duni, wa kukatisha tamaa, wa kinasibu na yanazua hisia za huzuni na uchovu Pamoja na ukosefu wa matumaini.

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), katika kitabu chake *“Kamusi ya Kiswahili-Istilahi na Nadharia”*, Dhana ya ubwege huelezea tamthilia ambazo huelekea kutokeza kuwa

maisha yana uwazi usiokuwa na maana. Anaendelea kueleza kuwa sanaa ya kiubwege hutumiwa kueleza aina ya sanaa inayoelekea kupuuza kaida zinazotarajiwa kwa utunzi wa tamthilia.

Kadhalika, kuna mikabala ya kinadharia kuhusu kazi za tamthilia za kiubwege. Nayo ni; ukosefu wa mantiki, mandhari dhahania, wahusika wa kiutopia, wahusika si wa kiuhalisia bali ni wa kubuniwa tu akilini mwa mwandishi, kuna kupotea kwa nafsi bila wokovu na ugumu wa mawasiliano. Fasihi ya kiubwege hukosa muumano mzuri wa vitushi; ambao ni mhimili wa ploti. Hivyo basi, matukio huwa yamevurugwa sana kiasi cha kukosa uwezo wa kuunganishwa. Mambo hujitokeza tu kiupweke; yaani kila jambo linasimama kivyake bila kutegemea kingine. Wahusika wa kiubwege hukosa umotishaji na matendo yao hutokea tu bila sababu wala msingi wowote. Pia msuko wa kazi hizi hauwezi kuelezwa kikamilifu kwa kuwa kuna ukosefu wa mtiririko wa matukio.

Aidha, wahusika wa kiubwege hawana uwezo wa kufanya hali zao kuwa bora. Vitendo vya wahusika hukosa muwala wala umuhimu wowote ila huonyesha ubatili tu. Mambo kama vile kutoa viatu, kuomba, kupika kukamilisha kazi ya kuingirisha mwamba hadi kwenye kilele cha mlima kunawashinda kutenda. Hii ndiyo hali inayojitokeza katika *The Myth of Sisyphus*, *Amezidi* na *Beluwa*.

Isitoshe, wahusika wanaopatikana katika tamthilia za kiubwege huweza kujitokeza katika sura mbalimbali; kubadilisha jinsia, yaani mhusika hujitokeza kama wa jinsia ya kike na wakati mwingine huchukua jinsia ya kiume. Tamthilia ya *Beluwa* ni mfano mzuri inayoonyesha ubadilishaji wa jinsia katika mchezo mmoja.

Vile vile kuna ukosefu wa uhalisia wa wahusika bali ni wahusika wa kidhahania tu. Aidha matendo yao ni ya kijinga na hayana maana kabisa. Aidha, kuna ukosefu wa

ruwaza za mazungumzo ya wahusika; lugha inayotumika katika tamthilia za kiubwege hutatiza mawasiliano. Waaidha, Katika tamthilia za kiubwege, kuna jazanda ya ukanganyifu wa jamii isiyojielewa na lugha hutumiwa tu kwa minajili ya mawasiliano ya kidhahania.

Watafiti na wahakiki anuwai wamejishighulisha na kuhakiki tamthilia ya *Amezidi* bila kutumia nadharia ya ubwege, hawa ni pamoja na King'ei (1997) ambaye alitoa mwongozo wa *Amezidi* kwa kushughulikia dhamira na muhtasari wa tamthilia.

Kutokana na vipengele hivi vya kiubwege, nadharia hii ilituwezesha kufanya utafiti ambao ulidhihirisha mwelekeo wa kiubwege katika tamthilia ya Kiswahili, kutokana na jinsi ambavyo vipengele hivi vya kiubwege vinavyojitokeza kulingana katika tamthilia ya *Beluwa*, *Amezidi* pamoja na *The Myth of Sisyphus*.

1.8 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Sehemu hii imeangazia kazi mbalimbali zilizoandikwa kuhusu suala la utafiti. Kazi ambazo zimeangaziwa hapa zinaegemea kwa kiasi kikubwa tamthilia kwa jumla, tamthilia ya *Amezidi* pamoja na Ubwege.

Wamitila (2008) anaihusisha tamthilia na drama ambapo anaeleza kwamba inarejelea kazi ya kifasihi ambayo iliandikwa kwa ajili ya kuwasilishwa kwenye jukwaa kupitia kwa ishara na maneno. Aidha, katika uchunguzi wa matini za kidrama, anasema kwamba unapaswa kuanza kwa kutenganisha kati ya aina mbili za matini. Kwanza, matini ya kimsingi au kuu; ambayo huyarejelea yale maneno yanayozungumzwa na wahusika wenyewe kwa wenyewe. Pili, ni matini tegemezi; ambayo huhusu sehemu za matini ambazo haziwasilishwi jukwaani kiusemi na hujumuisha tabaruku, kichwa cha tamthilia, maelekezo ya jukwaa na utambulishaji wa mzungumzaji. Tunakubaliana na mtaalamu huyu kwamba tamthilia hutungwa kwa minajili ya

kuwasilishwa mbele ya hadhira kwa wakati maalum.

Kadhalika katika kueleza drama na riwaya, Wamitila (2008) anadai kwamba drama na riwaya zinategemea vipengele vya kimsingi ambavyo ni sawa. Uchanganuzi wa tanzu hizi mbili hutegemea sifa sawa kama vile msuko, mazungumzo, uhusika na wahusika, wakati na mandhari na jinsi kazi husika zinawasilisha masuala yanayofungamana na maisha ya binadamu.

Katika *Amezidi* tulivyoeleza hapo awali, imehakikiwa na wahakiki mbalimbali. Hadi sasa, tahakiki nyingi zinazopatikana kuhusu tamthilia hii ni miongozo inayosaidia walimu na wanafunzi kuelewa vyema *Amezidi*. Kwa upande mwingine ubwege unavyojitokeza katika hii tamthilia pia haujashughulikiwa kiulinganifu na wahakiki waliochunguza *Amezidi*. Nayo kuhusu tamthilia ya *Beluwa*, hatukufanikiwa kupata tahakiki wala uchanganuzi wowote kwenye mtandao, majarida au hata vitabuni, hivyo hakuna maelezo mengi kuhusu.

Kwa kuanzia Vuzo (1997) katika mwongozo wa *Amezidi* anasema kwamba, mwongozo huo umeandikwa ili uwe kitulizo cha kilio cha watu wengi katika masomo ya Kiswahili na kwenye magazeti wanaposema kuwa *Amezidi* kimezidi kwa ugumu... anaendelea kueleza kuwa mwongozo wa *Amezidi* unatarajiwa kuwasaidia wanafunzi na wasomaji wa tamthilia ya *Amezidi* kuweza kukielewa zaidi na kukipenda sana.

Isitoshe, mhakiki Vuzo (1997) pia amejairbu kutoa maelezo kuhusu mtunzi wa *Amezidi*; Said A. Mohamed, jalada la kitabu hicho na mtiririko pamoja na uchambuzi wa kila onyesho. Katika kuangazia maudhui, aliyataja kama vile; tamaa, unyonyaji, uzembe, hongo, ukoloni, njaa na ukame. Aidha katika kitengo kingine cha maudhui alitaja ubwege kuwa mojawapo ya maudhui yanayodhihirika wazi. Aliangazia pia mtindo, umbo, muundo, wahusika pamoja na matumizi ya lugha. Ingawa alifanya

uchanganuzi huu, Vuzo hakujikita katika kudhihirisha uhusiano wowote kati ya vipengele hivi alivyovitaja na kigezo cha ubwege. Pia hakuzama katika kulinganisha na kutofautisha *Amezidi* na tungo nyingine kiubwege jinsi ambavyo tumetekeleza katika utafiti huu.

Kwa upande mwingine, King'ei (1997) kwenye *Mwongozo wa Amezidi*, anatoa maelezo kuhusu dhamira na muhtasari wa tamthilia, muhtasari wa maonyesho, wahusika, dhana ya kuzidi, maudhui kama vile , uvivu, uzembe, ufiada na wizi, kutegemea misaada kutoka ng'ambo, kiburi na ubadhirifu. Halikadhalika, ameangazia mbinu za usanifu, matumizi ya lugha Pamoja na nyenzo nyingine za Sanaa. Mhakiki huyu hakufanikiwa kushughulikia kigezo cha ubwege katika uhakiki wao ambacho ndicho nguzo katika utafiti huu.

Mhakiki Njogu (1999) amefafanua maudhui kama vile; maana ya uhuru, ufiada, ukoloni mamboleo, umasikini wa Mwafrika, elimu na mapenzi. Aidha amechanganua vigezo vya wahusika, lugha, dhamira pamoja na fani. Hakuzama katika kigezo cha ubwege wala kulinganisha *Amezidi* na kazi nyingine kiubwege, kama ambavyo tumefanya katika utafiti huu.

Kwa upande wake Sarara (1997), ameangazia maudhui katika tamthilia tatu za Said A. Mohamed, nazo ni *Pungwa (1988)*, *Kivuli Kinaishi (1990)* na *Amezidi (1995)*. Uhakiki huu umetoa mchango mkubwa kwa utafiti huu kwa kuongeza maarifa Zaidi katika taaluma ya fasihi kwa jumla pamoja na kuweka wazi mwelekeo wa kiubwege katika tamthilia ya Kiswahili kiulinganishi.

Naye Maneno (1997) katika *Mwongozo wa Amezidi* alifanya tu kama wenzake. Baada ya dibaji fupi, aliandika utangulizi ambapo alieleza fasihi, tanzu za fasihi Pamoja na sanaa ya maonyesho. Aidha anaeleza kuhusu mwandishi wa tamthilia, kisha

muhktasari wa kila sura, kiini na dhamira ya mwandishi, maudhui kama vile umasikini na athari zake, ubadhirifu, uchoyo, ujinga, ufisadi, mapuuzi, uhaba wa kazi, athari za tamaduni za kigeni na ubinafsi. Pia ameweza kutoa ufafanuzi wa wahusika, muundo, umbo, mtindo, fani na lugha.

Tamthilia ya *Amezidi* ni kazi ya kiubwege. Baadhi ya vipengele vinavyodhihirisha ubwege katika tamthilia hii ni kama vile, ukosefu wa matumaini, wahusika na kukata tamaa. Haya ni maelezo ya Njogu na Chimera (1999). Tofauti na utafiti huu wa awali, tumebainisha mwelekeo wa kiubwege katika tamthilia ya Kiswahili, ambayo haikushughulikiwa na wahakiki hawa.

Wafula (1999) naye anatofutisha kati ya tamthilia ya *Amezidi* na kazi nyingine za Said A. Mohamed. Anadokeza kuwa wasomaji waliozoea kusoma kazi za kisanaa za mwandishi huyu, watahangazwa na mtindo mpya uliobuniwa na huyu mtunzi katika *Amezidi*. Aidha Wafula (1999) amechambua kwa kifupi vipengele vya tamthilia ya *Amezidi*, Amefafanua *Pango, Wimbo, Sauti, Kicheko*. Katika kigezo cha ubwege anasema,

“Said A. Mohamed ametumia mtindo ule wa wasanii kama vile Samuel Beckett – yaani maisha ya wahusika Ame na Zidi ni ya kiubwege.”

Tamthilia ya *Amezidi* inatajwa na baadhi ya wahakiki kuwa ni mojawapo ya tamthilia za kiubwege. Njogu na Chimera (2008) wanaeleza kuwa tamthilia hii ni ya kiubwege lakini isiyokatisha tamaa kama zilivyo tamthilia za kiubwege za kimagharibi. Aidha wataalamu hawa wamejadili juu ya sifa tofauti tofauti za fasihi ya kiubwege kama vile kutumia wahusika wa kidhahania, kutumia lugha isiyorahisisha mawasiliano, kutumia msuko wa kimzunguko (kiduara) na ukosefu wa mtiririko wa vitushi vinavyosababishana.

Ingawa uchambuzi wao unakiri kuwa *Amezidi* ni tamthilia ya kiubwege, uchambuzi wao si wa kina kwani wanaeleza sifa za mkabala wa kiubwege kwa jumla bila kubainisha kwa undani namna sifa hizo zinajitokeza katika tamthilia hii. Badala yake, wanajikita zaidi katika maudhui ya tamthilia hii jinsi yanavyosawiri Bara la Afrika. Vile vile katika uhakiki wao, hawakutumia vipengele vya kiubwege katika kudhihirisha mwelekeo wa kiubwege katika kazi hiyo kama tulivyofanya katika utafiti huu. Aidha, athari ya Albert Camus kama mwasisi wa nadharia ya Ubwege kwenye tamthilia ya Kiswahili haijaangaziwa.

Isitoshe, Wafula na Njogu (2007) nao wanaeleza kuwa katika tamthilia ya *Amezidi*, Said Ahmed Mohamed anabuni msuko na wahusika ambao wanaongozwa na mihimili ya ubwege, kwa kuwa kazi hiyo haina mtiririko bainifu na haina wahusika waliopevuka kimwili na kimawazo. Mtunzi huyu alichagua kutunga kazi hiyo ili idhihirishe tuhuma zake dhidi ya mantiki inayoelekeza maadili ya jamii inayohusika.

Kulingana na Panumas (2019), Albert Camus alifafanua ubwege kuwa ubatili wa kutafuta maana katika ulimwengu katili usioeleweka, na ambao umekosa maana.

Madai haya yanawiana na wazo la Chukwuka (2016:32) anaposema yafuatayo;

“Dhana ya Ubwege inahusishwa sana na udhanaishi na asili yake hutokana na mwanafalsafa wa Ki-Deni Soren Kierkegaard....Camus anapojaribu kueleza asili ya ubwege, anadai kwamba ubwege ulitokana na mvutano baina ya akili za binadamu na kushindwa kutambua uwepo wake katika ulimwengu katili anamoishi...”

Naye Martin (1961:5) anasema yafuatayo kuhusu ubwege kwa kumnukuu Ionesco (1962),

“Ubwege ni kilichokosa nia na kimejitenga kutokana na Imani za kidini, tabia za kiungu na misingi ya kiakili Pamoja na mawazo. Binadamu amepotea na matendo yake yote ni vya kijinga na hayana maana.”

Kulingana na Martin (1961), dhana ya ubwege inahusishwa zaidi na mchezo wa kuigiza na hufungamana na futuhi zenye vipengele vya kitanzia. Wahusika wanajipata katika hali ya kutamauka na wanalazimika kurudia matendo ambayo hayana maana yoyote. Anaendelea kueleza kuwa ploti za michezo ya namna hii ni mviringo, ni wigo wa kubeza na kukiuka uhalisia. Wahusika dhahiri wanajikuta wanaishi pasipo na matumaini hivyo, wanajitahidi kukubaliana na hali yao ili waweze kuishi, yaani wanaishi kwa sababu wapo na shida zao hukosa mantiki.

Kuhusiana na ubwege, Mugaris (2014), alichunguza Drama za kiubwege kwa kutumia mifano ya tungo za Serumaga, Imbuga na Kasigwa. Shabaha ya utafiti huu ulikuwa kudhihirisha uhusiano kati ya mtindo wa drama za Kiubwege na hali katika drama za Afrika Mashariki. Utafiti huu ulilenga kutathmini sababu za matumizi ya taathira za kimuziki katika tamthilia za kiubwege. Tamthilia zilizochunguzwa ni pamoja na; tamthilia za Serumaga; *A Play, Majangwa na The Elephant* ambazo ziliwakilisha hali ya Uganda. Aidha katika tamthilia za Imbuga, alichunguza *Game of Silence* ili kuwakilisha Kenya. Kadhalika, alitumia tamthilia za Kasigwa; *The Trials, The Conflict, The Absurd na The Scum* ili kuwakilisha hali za mataifa mawili; Uganda na Kenya kwa sababu mwandishi huyu alizaliwa na kukulia Uganda lakini baadaye akawa Mkenya. Utafiti tulioetekeleza ni tofauti na utafiti huu uliofanywa na Mugaris kwa kuwa, umejikusisha na tamthilia za Kiswahili na lengo kuu ni kutathmini mwelekeo wa kiubwege kwenye tamthilia ya Kiswahili na wala si katika tamthilia ya Kiingereza.

Mary (2017) anadai kuwa utunzi wa Serumaga ni Zaidi ya Ubwege kwa sababu anatomia mbinu za kipekee katika kutoa mawazo kupitia utunzi wake. Mary alitekeleza utafiti uliochunguza jinsi ambavyo ubwege umejitokeza katika kazi za

Serumaga; *A Play*, *Majangwa* na *The Elephant*. Aidha, utafiti huu ulibainisha athari za mtunzi Beckett katika utunzi wa Serumaga. Tofauti na utafiti huu, tumebainisha mfanano wa mwelekeo wa kiubwege kwenye utunzi wa Albert Camus; *The Myth of Sisyphus*, *Amezidi* na *Beluwa*.

Gilgen (1980) anasema kwamba dhana ya ubwege hutokana na mvutano baina ya matamano na fikra za binadamu na ukatili wa ulimwengu anamoishi. Anaendelea kueleza kwamba shujaa wa kiubwege hutambua kuwa njia ya kuishi katika huu ulimwengu katili ni kuishi maisha ya kiubwege kupitia ukengeushi.

Wilson & Goldfarb (1991) wanaeleza kuwa, katika tamthilia za kiubwege, mazungumzo na majibizano ya wahusika huonekana kukosa maana na huenda wahusika hawa wakashindwa kuwasiliana ipasavyo. Hii ina maana kwamba katika tamthilia za kiubwege mazungumzo ya wahusika huwa ni ya kubwabwaja yasiyofuatana kimantiki. Mawazo haya yanajitokeza pia katika maandishi ya Wilson na Goldfarb (2002:348) wakisema yafuatayo;

“Ubwege ulihusishwa na Martin Esslin (1950), ambaye alitambua kwamba drama zilizochukua mwelekeo wa kiubwege ulidhihirisha mambo mawili makuu; kwanza ni kwamba yanayotendeka maishani mwa binadamu ni ya kiubwege na hayana mantiki. Pili, ni kwamba ubwege unafaa kuonyeshwa katika matendo ya kidrama. Wanaokubaliana na wazo hili ni pamoja na; Samuel Beckett (1906-1989), Jean Genet (1910-1986), Eugene Ionesco (1912-1994), Edward Albee na Harold Pinter (1930). Kazi za kiubwege huwasilisha kuwepo kwetu na mahusiano ya binadamu na lugha yake kuwa ya kipuzi na hayana maana. Ili kudhihirisha haya, watunzi hutumia mbinu za kidrama zisizo na mantiki. Ploti huwa ya mviringo, wahusika si wa kiuhalisia, mandhari huwa ya kigeni na hayatambuliki, lugha hutatiza mawasiliano na wahusika hukosa kufanikisha mawasiliano baina yao.”

Waandishi hawa wanaendelea kueleza drama za kiubwege kuwa drama za kisasa na kazi ambayo wanatambua sana ni kazi ya Samuel Beckett; *Waiting For Godot* (1953).

Wanachambua kazi hii kiubwege, ambayo kwa kiasi kikubwa umenufaisha utafiti huu

kwa kueleza vipengele vya kiubwege hasa maudhui ya suala la Mungu.

Waidha, Daniel (2017:25-26) anatoa ufafanuzi wa tamthilia za kiubwege kwa kusema yafuatayo;

“Tamthilia za mkabala wa kiubwege hutumia mtindo wa kindoto. Tumeuita mtindo hivyo kutokana na kuwa wahusika huyaona maisha katika ulimwengu wa kidhahania iliyojaa ndoto na si katika uhalisia wake...wahusika huishi maisha yasiyo na uhalisi kwani mambo yote wanayoyafanya huwa yamo katika fikra zao tu...vile vile usingizi na kukoroma na hali ya kulala muda wote ni suala ambalo linatawala sana katika tamthilia hizi...”

Wazo hili limetusaidia katika kudondosha vipengele vya kiubwege vilivyojiegemeza kwa ndoto; na kubaini kwamba maisha ya binadamu wa kiubwege yanatawaliwa na ndoto, ulimwengu wao ni wa kidhahania tu.

Halikadhalika, Ndalu (1998) hajaangazia ubwege katika tamthilia ya *Amezidi*, ila ameeleza vipengele kadha vya uchambuzi wa kazi husika. Amejaribu kutoa utangulizi, muhtasari wa jumla juu ya tamthilia husika, muhtasari wa maonyesho pamoja na dhamira na maudhui yaliyomo kwenye tamthilia hiyo. Maudhui aliyoyataja ni kama vile, siasa, uchochole, uzalishaji mali, susuhuba, era potovu za elimu na ufisadi. Pia alishughulikia wahusika, mtindo, mandhari na matumizi ya lugha.

Kila uhakiki wa kazi ya fasihi una manufaa yake, basi hatuwezi kupuuza mchango wa mhakiki yeyote kama vile Vuzo, Maneno, Ndalu Pamoja na Wafula ambao wameangazia zaidi maudhui na fani. Hivi ni vipengele muhimu, chambilecho Ngara (1990), ambaye anaeleza kwamba msomaji anapaswa kufahamu yaliyomo na fani yake ili kuelewa kazi ya kisanaa, msomaji anapaswa kufahamu yaliyomo na fani yake.

Tunaamini kuwa kwa kuchunguza vipengele vya kiubwege, tumepiga hatua katika kuzihakiki *Amezidi* na *Beluwa* na vile vile tumebainisha mwelekeo wa kiubwege katika kazi hizi pamoja na kudhihirisha mfanano wa mwelekeo wa kiubwege katika *The Myth of Sisyphus*, *Amezidi* na *Beluwa*

1.9 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu umejikita katika tamthilia ya *Amezidi* yake Said Ahmed Mohamed (1995) na *Beluwa* iliyoandikwa na Pauline Kea Kyovi (2012). Tumejikita katika uchanganuzi wa vipengele vya kiubwege ili kudhihirisha mwelekeo wa kiubwege katika kazi hizi pamoja na kutathmini mfanano wa mwelekeo wa kiubwege katika *The Myth of Sisyphus* (1942), *Amezidi* na *Beluwa*.

Tumetekeleza utafiti huu kwenye maktaba ya Chuo Kikuu cha Moi, maarufu kama “*Magaret Thatcher Library*” kwa sababu tulihitaji vitabu na majarida ambayo yamechapishwa katika Chuo hiki, ambavyo vinahusiana na Uwege. Aidha, makala yanayohusu nadharia ya ubwege pamoja na tasnifu za wasomi walioshughulikia suala la ubwege ama kwa kutumia tamthilia ya *Amezidi* au kazi yoyote ya kisanaa zilitufaa zaidi. Uwepo wa tarakilishi katika maktaba ya Chuo Kikuu cha Moi pia ulituwezesha kutumia tovuti katika kukusanya data zinazohusiana na suala la utafiti.

1.10 Mbinu za Utafiti

Mbinu za utafiti ni mchakato na hujumuisha vifaa ambavyo hutumiwa wakati utafiti wa jambo fulani unatekelezwa. Njia hizi huruhusu data kukusanywa, kuchunguzwa na kuonyeshwa jinsi zilichangia katika kufikia malengo ya utafiti (Kothari, 2004). Katika sehemu hii, tumeonyesha mchakato wote wa utafiti huu na hatimaye kuonyesha jinsi tuliyafikia malengo ya utafiti. Mwanzo, tumejadili uteuzi wa sampuli, mbinu za

ukusanyaji data pamoja na uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti.

1.10.1 Uteuzi wa Sampuli

Katika utafiti huu, tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* ziliteuliwa kimakusudi. Tamthilia ya *Amezidi* imesheheni vipengele kadha vya kiubwege kwa kiwango kikubwa ikilinganishwa na tamthilia nyingine za Said A. Mohamed zikiwemo; *Kimya Kimya Kimya (2011)*, *Janga la Werevu (2016)* na *Mashetani Wamerudi (2016)*. Mwandishi huyu ana umahiri wa kutumia ubwege katika kujenga dhamira katika kazi zake hasa kwenye tamthilia ya *Amezidi*.

Vile vile tuliteua Tamthilia ya *Beluwa* kimakusudi kwa sababu imetungwa kwa msingi wa kiubwege. Tamthilia hii imesawiri wahusika wa kiutopia na pia, ina sifa kadha za nadharia ya ubwege tofauti na kazi nyingine za Pauline Kea Kyovi kama vile; *Kigogo*. Hivyo, tuliweza kufasiri upya kazi hizi kulingana na maendeleo ya taaluma ya fasihi na jamii ya kisasa.

Kando na hayo, makala ya *The Myth of Sisyphus* yake Albert Camus, pia yaliteuliwa kimakusudi kwa sababu mwanafalsafa huyu aliweka msingi wa nadharia ya ubwege kwa kutumia kazi hii. Hivyo basi makala haya yalitunufaisha kwa kutupa mwelekeo wa kiubwege katika kazi ya fasihi pamoja na kufanikisha lengo la tatu la utafiti huu.

1.10.2 Mbinu za Ukusanyaji Data

Kwa mujibu wa Kothari (2004), Ukusanyaji data ni shughuli ambayo huhusisha kuweka habari muhimu katika kikundi au kukusanywa kwenye mada fulani. Utafiti huu ulikuwa wa Maktabani kwa hivyo, data zilikusanywa kutoka kwenye vitabu teule na makala katika majarida.

1.10.2.1 Utafiti Maktabani

Utafiti huu ni wa maktabani, kwa vile unahusu kitabu *Beluwa* kilichoandikwa na Pauline Kea Kyovi (2012) na *Amezidi* yake Said Ahmed Mohamed kilichoandikwa (1995). Vitabu hivi ni nyaraka fuatizi za kibinafsi na kwa hivyo tumevishughulikia maktabani hasa maktaba ya Chuo Kikuu Cha Moi (*Margaret Thatcher Library*). Vile vile, tumeyasoma maandishi yanayohusiana na tamthilia au fasihi kwa jumla ili kupata historia na maendeleo ya tanzu ya tamthilia. Makala na tasnifu mbali mbali kuhusu tamthilia hususan tamthilia za kiubwege zilitusaidia kupata mwelekeo na mtazamo tofauti katika utafiti huu. Kando na mbinu hii, kuna njia zilizotuongoza katika utekelezaji wa utafiti huu kulingana na madhumuni ya utafiti. Njia hizo zilituwezesha kukusanya data na kuweza kupata maelezo kuhusu suala la utafiti wangu.

Hatua zifuatazo zilituelekeza katika mchakato wa ukusanyaji data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data. Kwa vile sampuli za utafiti huu zilihusu Makala fuatizi na mbinu tuliyotumia katika utafiti huu ni utafiti wa maktabani, hivyo mbinu za ukusanyaji wa data tulizozihitaji ni mbinu ya Usomaji Makinifu; ambao ulihusisha kusoma makala, vitabu na kazi mbali mbali za kitaaluma ambazo pia zilihusu tasnifu zilizoandikwa kuhusu ubwege. Aidha, tulisoma Tamthilia ya *Amezidi* (1995), *Beluwa* (2012) na makala ya *The Myth of Sisyphus* (1942) na kuzihakiki kwa kuzingatia vipengele vya kiubwege. Isitoshe, tulizilinganisha kazi hizi kiubwege ili kuweza kudhihirisha mwelekeo wa kiubwege katika Tamthilia ya Kiswahili. Vilevile, tulitazama kanda za video za Albert Camus zilizoonyesha filamu ya *The Myth of Sisyphus*.

1.10.2.2 Vifaa vya Utafiti

Katika utafiti huu ambao unahusu mwelekeo wa kiubwege katika Tamthilia ya Kiswahili; mintarafu ya *Amezidi* na *Beluwa*, tulitumia vifaa vilivyofanikisha shughuli hii. Vifaa hivi ni pamoja na; tarakilishi iliyotusaidia katika kupata maarifa kwenye tovuti mbalimbali, Kamusi za fasihi katika kueleza na kufafanua dhana muhimu katika utafiti huu pamoja na vitabu vya kitaaluma vinavyoeleza vipengele vya kiubwege na uhakiki wa kazi za fasihi. Hatimaye tulitumia kalamu na karatasi na kitabu katika kunakili taarifa tuliyoipata wakati wa kutekeleza utafiti huu.

Kijumla, Kuna vifaa tulivyohitaji ili kufanikisha shughuli nzima ya utafiti. Hivi ni pamoja na, Kamusi za fasihi katika kueleza na kufafanua dhana muhimu. Pili, tulitumia tarakilishi katika utafiti kwenye mtandao na tovuti mbalimbali. Vitabu na kazi mbalimbali za kitaaluma zinazoeleza vipengele mbalimbali vya ubwege katika kazi za kifasihi zilitusaidia sana katika utafiti huu.

1.10.3 Uchanganuzi Data na Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti

Tulichanganua data kwa kuchunguza na kubainisha vipengele vya kiubwege jinsi vinavyojitokeza katika tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* pamoja na kutathmini utofauti na mlingano wa mwelekeo wa kiubwege katika tamthilia hizi mbili. Usomaji makinifu ndio mbinu ya kimsingi iliyotumika katika uchunguzi wa vipengele husika vya kiubwege. Tulikusanya na kupanga vipengele hivyo vya kiubwege kutegemea sifa za vipengele hivyo, kama anavyoeleza Kothari (2004) kwamba data zenye sifa sawa huwekwa kwenye kundi moja na kwa hivyo, data zote zilizokusanywa huwekwa kwenye makundi kadhaa. Makundi haya hutegemea aina ya data na aina ya utafiti unaotekelezwa. Kwa mfano, katika utafiti huu, vipengele vya kiubwege kimaudhui viliwekwa pamoja na vile vile vipengele vya kiubwege kifani pia viliwekwa pamoja.

Uchanganuzi wa data uliongozwa na nadharia ya Ubwege iliyoasisiwa na Albert Camus (1984) inayosisitiza kwamba maisha ya binadamu hayana maana hivyo binadamu huishi kwa sababu yupo. Nadharia hii inasisitiza uwepo wa binadamu kwanza ndiposa mambo mengine yafuate kutokana na ulimwengu anamoishi. Aidha mwandishi huyu anadai kwamba tamthilia za kiubwege hutawaliwa na kukata tamaa maishani, ambayo hutokana na utupu katika Maisha ya binadamu na ukosefu wa nguvu za kubadilisha hali hiyo duni.

Katika uchanganuzi huu, tumetumia mbinu ya kimaelezo kwa kuzingatia mwongozo wa Kothari (2004) kama tulivyoeleza hapo juu na vile vile mihimili ya nadharia ya Ubwege kuonyesha mwelekeo wa kiubwege katika *Amezidi* na *Beluwa*. Vipengele vya kiubwege vilichunguzwa ili kufanikisha utafiti huu. Vipengele vilivyochunguzwa ni vya kimaudhui na kifani. Kimaudhui, tulichunguza dhamira, mandhari, suala la Mungu, suala la kifo, ukengeushi na ukosefu wa uthabiti kwa elimu. Waaidha, kifani tuliangazia uhusika (uchache wa wahusika, wahusika wa kiutopia, wahusika wa kinjozi/dhahania na wasiokuwa na historia), ukosefu wa ruwaza za mazungumzo, utupu, matumizi ya nyimbo, vicheko na vilio lugha inayotatiza mawasiliano pamoja na ploti mviringo.

Hatimaye, kwa kutumia nadharia ya ubwege, tulitathmini mwelekeo wa kiubwege kwenye tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa*.

Baada ya kuchanganua data, tumefanya uwasilishaji wa matokeo ya utafiti kwa kuwasilisha ripoti yetu katika mtindo wa tasnifu.

1.11 Hitimisho

Sehemu hii imechunguza msingi wa utafiti wetu. Tumeweka wazi suala letu la utafiti, malengo yetu, nadharia tete, sababu na umuhimu wa utafiti, misingi ya kinadharia,

mapitio ya maandishi na pia uchanganuzi wa data. Sura ifuatayo inazamia historia na uainishaji wa tamthilia ya Kiswahili, hivyo ilifafanua msingi wa tamthilia kwa jumla na hatimaye kudhihirisha chimbuko la tamthilia za kiubwege. Kwa kufanya hivi tuliongeza maarifa kuhusu msingi wa tamthilia za kiubwege na kubainisha sifa za tamthilia hizo.

SURA YA PILI

HISTORIA NA UAINISHAJI WA TAMTHILIA YA KISWAHILI

2.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumemulika historia ya tamthilia ya Kiswahili kwa jumla ambapo tuliangazia vipindi mbali mbali vya kihistoria vikiwemo kipindi cha Kabla ya Ukoloni, kipindi cha Ukoloni pamoja na kipindi cha baada ya Uhuru. Aidha, Uainishaji wa tamthilia ya Kiswahili pia umeangaziwa. Kando na hayo, tumejadili dhana na muktadha wa ubwege, tamthilia ya kiubwege pamoja na mielekeo ya kiubwege.

2.1 Historia ya Tamthilia ya Kiswahili

Kama anavyoeleza Method (2015), tamthilia ya Kiswahili imepitia katika vipindi mbalimbali vya kihistoria. Katika kila kipindi cha kihistoria, tamthilia ilibeba maudhui ya aina yake kulingana na wakati husika. Kwa kuongozwa na maelezo ya Method (2015), tuliibuka na vipindi vya kihistoria vifuatavyo;

- i. Kipindi cha kabla ya Ukoloni
- ii. Kipindi cha Ukoloni
- iii. Kipindi cha baada ya Uhuru

2.1.1 Tamthilia ya Kiswahili kabla ya Ukoloni

Ukoloni uliingia Afrika Mashariki na Afrika kwa jumla katika nusu ya pili ya karne ya 19, baada ya mapinduzi ya viwanda huko Ulaya. Mageuzi hayo yalitokana na mbinu mbali mbali za ukusanyaji wa mtaji zilizokosa ustaarabu zilizotumika tangu awali.

Katika kipindi cha kabla ya Ukoloni tamthilia ya Kiswahili ilikuwa simulizi ambayo ilitendwa katika mazingira mbali mbali. Tamthilia simulizi hizo zilihusisha michezo ya kuigiza, majigambo, tondozi, miviga na vichekesho.

Tamthilia simulizi zilitendwa na jamii mbali mbali za wakati huo kama anavyosema Mulokozi (1996) zilifaraguzwa na hazikuwekwa kwenye maandishi.

2.1.2 Tamthilia ya Kiswahili wakati wa Ukoloni

Ukoloni ulianza katika bara la Afrika na Afrika Mashariki katika mwaka wa (1885), baada ya mkutano wa Berlin ulioligawa bara hilo miongoni mwa mataifa ya kikoloni. Katika kipindi hiki, nchi za Afrika Mashariki zilishuhudia utawala wa Wadachi-Wajerumani na Waingereza-Wajerumani walianza kutawala Afrika Mashariki katika mwaka wa 1885 hadi 1918 mara tu baada ya vita kuu vya Kwanza vya Dunia (Method, 2015).

Katika kipindi hiki, bado tamthilia simulizi ziliendelea katika maeneo mbali mbali ya Waswahili. Tamthilia hizi zilipata athari katika maudhui yake kwa kuanza kusawiri ukoloni, maudhui ya kupinga ukoloni yalianza kujibainisha. Aidha, tamthilia simulizi za kijadi zilianza kufifia kutokana na wakoloni kuanzisha kampeni za kupinga masuala ya kitamaduni ya waafrika. Masuala hayo yaliitwa ya Kishenzi na hivyo kuanza kuyadidimiza (Van Pelt, 1972; Omari na Wenzake, 1980). Mulokozi (1996) anabainisha kuwa tamthilia ya kigeni ilikuwa imeshaingia Afrika kwa ajili ya kuwastarehesha maofisa wa kikoloni pamoja na kufundishia masuala ya dini ya kikristo. Aidha, anabainisha kwamba nyingi kati ya tamthilia hizo zilichezwa mashuleni.

Kwa upande wa ukoloni wa Waingereza, tamthilia simulizi za jadi ziliendelea kutendwa lakini pia ziliitwa mambo ya kishenzi. Waingereza waliigiza tamthilia zao ili kuwaburudisha maofisa wa kikoloni na walowezi wa kizungu. Mulokozi (1996) anabainisha kuwa tamthilia hizi zilianza kuigizwa kwa Kiingereza katika miji ya Nairobi na Mombasa nchini Kenya tangu 1920. Anaiita tamthilia hii “tamthilia ya

Kizungu”. Tamthilia hii haikupingana na mfumo wa kikoloni na ubepari bali ilikusudia kuendeleza mfumo huo.

Aidha katika kipindi hiki paliibuka tamthilia za vichekesho ambazo zililenga kuburudisha waafrika. Hizi zilikusudia kupumbaza Waafrika wajisahau na wasifikrie kuupinga ukoloni. Tamthilia hizi hazikuwa na maudhui mazito kwa Waafrika na ziliwasawiri kama watu washamba na wasiostaarabika.

Kadhalika, wakoloni walianzisha mfumo wa elimu, ambao ulilenga kuwafunza waafrika masomo mengine pamoja na uigizaji wa tamthilia. Tunakubaliana na Method (2015) kwamba katika kipindi hiki, Mwingereza Graham Hyslop ndiye alikuwa mwalimu na mwigizaji wa tamthilia katika shule na vyuo tofauti tofauti kwa mfano; Shule ya Upili ya Alliance. Mulokozi anawataja baadhi ya wanafunzi wake kama vile; Henry Kuria, Gerishon Ngugi, B. M. Kurutu na Kimani Nyoike. Aidha, Graham Hyslop ndiye aliyeanzisha kazi za kidrama nchini Kenya na aliwasili Afrika Mashariki katika mwaka wa 1936 (Mulokozi, 1996; Wafula, 1999 na Bertoncini, 2009). Hyslop alianza kujihusisha na kazi za kidrama mnamo 1944, ambapo alitunga na kuongoza filamu ya *Akili Mali*.

Baadaye, Graham Hyslop alitunga tamthilia za Kiswahili (1957); *Afadhali Mchawi* na *Karibu Mgeni*. Mwandishi huyu alitambulika zaidi alipotunga kazi nyingine (1974) *Mchimba Kisima* na *Kukopa Harusi kulipa Matanga*. Katika utunzi wake, Hyslop alidhamiria kuonyesha ustaarabu wa wazungu huku akiwadunisha Waafrika. Ni kweli Method (2015) anapodai kwamba utunzi wa Hyslop ndio ulikuwa mwanzo wa tamthilia andishi ya Kiswahili.

Mwanafunzi wake Hyslop; Henry Kuria alifuata nyayo zake na kutunga *Nakupenda Lakini* ambayo iliigizwa (1954) na kuchapishwa (1957). Nyoike alitunga *Maisha ni*

Nini iliyoanza kuigizwa (1955), naye Ngugi alitunga *Nimelogwa Nisiwe na Mpenzi* iliyoigizwa (1956) na kuchapishwa (1957). Kurutu alitunga *Atakiwa na Polisi* iliyotungwa (1957) (Ngugi wa Thiong'o, 1986; Mulokozi, 1996; Wafula, 1999).

2.1.3 Tamthilia ya Kiswahili baada ya Uhuru

Nchi za Afrika Mashariki zilipata Uhuru miaka ya 1960; mathalan Tanganyika ilipata Uhuru (1961), Kenya (1963), Zanzibar (1964) na Uganda (1964).

Katika mwaka wa (1961-1971), tamthilia za kijadi zilifufuliwa na kutiwa shime. Huu ulikuwa wakati wa kufufua mila na desturi ya Kiafrika iliyokandamizwa na wakoloni. Tamthilia ya Kizungu bado iliendelea kuigizwa katika shule mbali mbali na kumbi za maonyesho. Mulokozi (1996) anabainisha kuwa hata hivyo, tamthilia hii ya Kizungu ilianza kufifia. Aidha kipindi hiki kilishuhudia kuanzishwa kwa magazeti yaliyochapisha tamthilia hizo, kama vile *Gazeti la Chuo Kikuu cha Dar-es Salaam* liloitwa *Darlite* (Wafula, 1999).

Tamthilia za wakati huu ziliukejeli ukoloni na kuusifia uhuru. Pia ziliwasifia wapigania Uhuru, kwa mfano; *Mkwawa wa Uhehe* yake Mulokozi (1968) na kutafsiriwa na Kahigi (1970). Aidha, Nkwera alitunga *Mkwawa Mahinga* (1968) na E. Hussein akatunga *Kinjeketile* (1971).

Tunaunga mkono dai la Mulokozi (1996) kwamba, tamthilia za Vichekesho zilizokuwepo kabla ya Uhuru ziliendelea lakini zilisuta wazungu na wazungu weusi. Kwa mfano; tamthilia ya G. Uhinga, Martin Kayamba ambayo ilichapishwa na *Gazeti la Darlite* nchini Tanzania.

Waidha, Kipindi cha baada ya uhuru kilishuhudia kutafsiriwa kwa baadhi ya tamthilia muhimu za kizungu katika Kiswahili. Tafsiri ya awali kabisa katika

Tamthilia ya Kiswahili ni *Tabibu Asiyependa Utabibu (Le Medecin Malge Lui)* ya Moliere (1945). Tamthilia nyingine zilizotafsiriwa ni pamoja na; *Mchuuzi Muungwana* (1961) na Marrison kutoka *Le Bourgeois Gentelhomme* ya Moliere, *Makbeth* (S. Mushi, 1968) kutoka *Macbeth* (Shakespeare), *Tufani* (S. Mushi, 1969), *Juliasi Kaizari* (Nyerere, (1964) kutoka *Julius Cezar*, *Mabepari wa Venisi* (1969), *Mnafiki* (L. Tabuaga, 1973) kutoka kwa *Tartuffe*, *Mfalme Edipode* (1969) kutoka *Oedipus the King*, *Masaibu ya Ndugu Jero (Yahya, 1974)* kutoka *Trials of Brother Jero* (Wole Soyinka) na kadhalika.

Katika mwaka wa 1971 Waafrika walikata tamaa ya maendeleo kwa sababu waliamini kwamba viongozi wa kiafrika waliochukua madaraka watafanya kazi kubwa kuleta haki, ustawi, maisha bora na mendeleo kwa waafrika. Kwa bahati mbaya, hali haikuwa hivyo, viongozi wengi walijisahau na kuendeleza matendo ya wakoloni. Waandishi wakaanza kuhoji maana ya Uhuru na utawala wa waafrika, kwa mfano; tamthilia ya *Mashetani* (E. Hussein, 1971), *Giza limeingia* (Mbogo, 1980), *Kilio cha Haki* (Mazrui, 1982).

Aidha, kipindi hiki cha Baada ya ukoloni, kilishuhudia mkondo mpya wa uandishi wa tamthilia ambao ulikuwa tofauti na tamthilia za awali ambazo zilifuata kanuni ya ki-Aristotle; kanuni hii ilisisitiza sana suala la Ploti, ambalo linahusisha mtiririko wa visa katika tamthilia. Mfano mzuri ni *Amezidi* (Mohamed, 1995).

Pia paliibuka tamthilia zilizoanza kujitoka katika kucha za utamaduni wa uandishi wa kikoloni na kuanza kukuza mila na desturi zao. Aidha paliibuka tamthilia zilizoanza kutumia mbinu za fasihi simulizi ndani ya fasihi andishi. Tamthilia hizi Method (2015) anaziita tamthilia za majaribio, kwa mfano; *Jogoo Kijijini* (Hussein, 1976), *Nguzo Mama* (Muhando, 1982)

Katika kipindi hiki pia kuliibuka utandawazi. Kulikuwa na maingiliano makubwa baina ya mataifa Ulimwenguni na kuathiriana kwa tamaduni. Katika kipindi hiki dunia ilikuwa kama kijiji kimoja kutokana na kuimarika kwa mawasiliano. Kutokana na mwingiliano wa kitamaduni na upatikanaji wa elimu, Waafrika walichangamkia ukombozi wa mwanamke. Mila Pamoja na desturi za jadi za Kiafrika zilianza kupingwa (Mair, 1964; Van pelt, 1971). Mila Pamoja na desturi za jadi za kiafrika zilikuwa kwa kiasi kikubwa zinakandamiza mwanamke, hivyo watunzi walitunga kazi zilizopinga mila hizo, kwa mfano; *Nguzo Mama* (Mhando, 1982), *Ukingo wa Thim* (Hussein, 1989). Kipindi cha utandawazi pia kilishuhudia kuibuka kwa tamthilia andishi zilizoisifu Afrika kabla ya ujio wa ukoloni. Tamthilia hizi zilibainisha kwamba Afrika kabla ya ujio wa ukoloni ilikuwa na maendeleo makubwa na viongozi na mashujaa wenye nguvu, hekima na busara mifano ni kama vile; *Sundiata* (E. Mbogo, 1995), *Fumo Lyongo* (E. Mbogo, 2009).

2.2 Uainishaji wa Tamthilia

Katika sehemu hii uainishaji wa tamthilia wa wataalam watatu umejadiliwa na hatimaye tumetoa msimamo wetu kuhusu suala hili. Tumeangazia uainishaji wa ki-Aristotle, Method na Wamitila. Aidha katika kujadili uainishaji wa wataalam hawa, tulichunguza na kuhakiki mawazo yao na hatimaye kutoa msimamo wetu wa kitaaluma kuhusu uainishaji wa tamthilia.

2.2.1 Aristotle na Uainishaji wa Tamthilia

Aristotle aliweka misingi kwenye kitabu chake cha *The Poetics* kwa kutoa maelezo kuhusu kazi za kifasihi, ambapo alisisitiza kipengele cha ploti katika uundaji wa kazi za kisanaa. Anadai kwamba ploti ni jinsi ambavyo hadithi inaendelezwa hadi ifikie matukio yanavyotokea. Kwa ujumla, wazo la Aristotle liliangazia masuala yafuatayo;

Kwanza, anadai kuwa fasihi si wigo wa kikasuku bali ni ubunifu unaomfanya binadamu kuwa karibu na Mungu, yaani fasihi itumike kumtukua binadamu na ina sifa ya kuumba na kumleta karibu na Mungu. Hali ya uigaji huu huchangia katika kuifanya fasihi kutukuka. Anaendelea kueleza kuwa Fasihi haiigi kikasuku bali huiga kiubunifu hivi kwamba huzingatia mambo ambayo yanayoathiri binadamu na Maisha yake. Hii inamaanisha kwamba sanaa huiga hali asilia inayomzunguka binadamu.

Aidha, mwanafalsafa huyu anasisitiza kwamba ploti/msuko ni ya maana sana katika ubunifu wa kisanaa. Msuko wa tamthilia kutokana na muundo wa ki-Aristotle, ni mtiririko wa vitendo vya lazima unaoanza kwa hali ilivyo, halafu tunaingizwa katika hali ya mgogoro mpaka kufika kileleni ndipo tunapoanza mshuko mpaka kufika katika suluhisho yaani hali mpya (Hussein 1983).

Kadhalika, anadai kuwa fasihi inaeleweka vyema zaidi ikigawanywa katika tanzu mbali mbali. Vile vile Aristotle anadai kwamba fasihi hujitosheleza na huweza kujitawala. Haihitaji kuegemea taaluma nyinginezo.

Kulingana na uainishaji wa ki-Aristotle kuna aina mbili kuu za tamthilia, nazo ni Tanzania na Futuhi. Aristotle alitambua orodha ya tamthilia zilizopatikana katika mazingira aliyoishi.

Alidai kwamba aina za tamthilia zigawanywe katika makundi mbali mbali na vipengele vifuatavyo;

- a) Usawiri wa wahusika : wahusika huweza kuchorwa katika upotovu wao (futuhi) au kwenye utukufu wao (Tanzania).
- b) Kuchanganya masimulizi na maongezi: Mtunzi ana uwezo wa kuchanganya masimulizi na maongezi katika utunzi wake kama anavyofanya Homer kwenye tenzi zake.

Wazo la Aristotle linaungwa mkono na Method (2015) anapoangazia kigezo cha kusudio na kusema kwamba tunaangalia lengo au dhamira ya tamthilia husika. Tunapaswa kujiuliza maswali kama vile; Je, lengo la tamthilia husika ni kutia simanzi, kuchekeka au lengo hasa ni lipi? Kigezo hiki basi hutupa aina za tamthilia kama vile Tanzania na Futuhi/ komedia.

2.2.2 Tamthilia ya Masimulizi-ongezi

Aristotle (1934) katika *The Poetics*, aliweka kanuni mbili kuu za kufuatwa katika uainishaji wa tamthilia; Usawiri wa wahusika na uchanganyaji wa masimulizi pamoja na maongezi. Kwa kutumia kanuni ya usawiri wa wahusika ndipo tunapata aina mbili kuu alizozibainisha; Tanzania na Futuhi. Aidha, kwa kuangazia kanuni ya pili ya kuchanganya masimulizi na maongezi, tumeibua aina nyingine ya tamthilia ambayo ni tamthilia ya Masimulizi-ongezi. Aina hii ya tamthilia huzua matumizi ya mbinu ya usimulizi katika mazungumzo; yaani wahusika wanawasiliana kupitia masimulizi na maongezi. Tamthilia ya masimulizi-ongezi ni aina ya tamthilia ambayo ilikuwepo katika jamii za kale za Kiafrika na ambayo inapatikana katika jamii za kisasa. Kwa ujumla, tamthilia ya masimulizi-ongezi ina sifa zifuatazo;

- a. Hutumia masimulizi ya hadithi kwa mfano; tamthilia ya Lwanda Magere hutumia kisasili cha Wajaluo.
- b. Hutumia majigambo ambacho ni kipera cha fasihi simulizi.
- c. Hutumia maudhui na wahusika wa kifantasia kama vile Zimwi katika Lina Ubani na Shetani katika *Mashetani*.
- d. Hutumia mbinu mbali mbali za kifani za fasihi simulizi kama mwanzo na mwisho kama fomula mathalan, “Hadithi! Hadithi!” katika Jogoo Kijijini.

2.3 Mawazo ya Aristotle kuhusu Tanzania

Dhana ya Tanzania ya ki-Aristotle ilitokana na matumizi ya mbinu za sayansi kavu katika utunzi wa kazi za kisanaa (Myers 1949). Kutokana na fasili kwenye *The Poetics* yake Aristotle, Tanzania ni: “Usanii uonyeshao anguko la mtu ambaye kimsingi huwa ni Shujaa au mbabe kutokana na kosa la mtu uamuzi mbaya ambao matokeo yake ni mateso na hatimaye Kifo (Mutembei, 2014). Kwa mujibu wa Aristotle, ni Maigizo ya matukio yenye ujumbe mzito yanayowasilishwa kwa lugha ambayo inanawiri, yanayozindua hofu na huruma kisha yalipue hisia za ndani kutoka kwa nafasi za hadhira. Ili kuelewa dhana ya Tanzania vya kutosha, istilahi zifuatazo zinapaswa kuwekwa wazi, msingi uliowekwa na Aristotle (Mutembei 2014; Wamitila 2003);

- i. **Zila (*Hamartia*):** kosa linatumbukiza shujaa katika ufu. Kosa hili huwa la kiuamuzi au dhambi au hata matendo maovu. Hili kosa ndilo husababisha aguko au kifo cha mhusika kama anavyoeleza Mutembei 2011 katika Wamitila 2003.
- ii. **Hibrisi (*Hubris*):** ni dhambi kamili, au kitendo chenyewe kinachomfanya shujaa aingie kwenye kosa la kufikisha kwenye ufu. Kosa hili hatimaye humfikisha mtu kukashifu au kudharau miungu au Mungu. Kutokana na haya, hii hibrisi huonekana kama dhambi kwa sababu ni hali isiyo ya kawaida.
- iii. **Utambuzi wa ndani (*Anagnorisis*):** mhusika mkuu anatambua kwamba ameshajiingiza kwenye matata kutokana na hatua mbali mbali, ni mabadiliko kutoka katika kutokujua au ujinga kwenda katika uelewa au ufahamu, mabadiliko haya ndiyo hutokeza au mapenzi au chuki dhidi ya mhusika ambaye mustakabali wake utakuwa ama mzuri (mapenzi) au mbaya.

- iv. **Mabadiliko ya bahati (*Peripateia*):** Hapa mhusika hufanya tukio au huchukua hatua ambayo humtoa katika “usalama” kumwingiza matatani
- v. **Adhabu (*Nemesis*):** hii inamaanisha “kupata kilichostahili”. Ni adhabu ambayo mtu anapata kutokana na matendo yake ya hibrisi (Mutembei 2009).
- vi. **Utakaso (*Catharsis*):** Kuna utakaso wa aina mbili: kwanza, utakaso wa kiroho ambapo ni lazima mtu ajute yaani aone huruma na ahisi woga. Pili, utakaso wa kiutambuzi (*cognitive catharsis*) ambao ni hali apatayo mtu akijifunza jambo. Ni starehe inayopata akilibaada ya kufahamu jambo Fulani. (Mutembei 2011; Wamitila 2003).

Waidha, Aristotle aliweka misingi muhimu katika kuainisha vipengele vya tanzia akidai kwamba tanzia lazima iwe na sehemu sita; *Mythos (ploti)*, *ethos (wahusika)*, *Dianoia (wazo)*, *Lexis (lugha)*, *Melos (Nyimbo/korasi)* na *Opsis (Uigizaji)*.

2.3.1 Ploti

Aristotle (1934) katika *The Poetics*, anaeleza kwamba ploti ni kama moyo wa tanzia na ndio huunganisha vitushi; ni mtiririko wa vitushi kuanzia mwanzo, kati hadi mwisho. Mwanzo huelekeza kisa kwa njia ya kupelekea kwa kingine, kati, huendeleza kilichotukia na kuelekeza kwenye kitakachotukia na Mwisho (tamati), huendeleza kilichotukia kwenye kati ila hauhitaji kupelekea kwa kisa kingine, yaani tumetosheka kwamba ploti imekamilika. (Chatman 1978) anakubaliana na Aristotle kwa kueleza kwamba ploti ni mfuatano wa vitushi au matukio kwenye kazi za fasihi. Pia huhusisha mtiririko na kutoa picha ya matukio na visa mbalimbali vikiwa vinabebwa na wahusika kuanzia mwanzo hadi mwisho. Kwa hivyo, Aristotle anadai kwamba tanzia sharti iwe na ploti ambayo husaidia katika kueleza kinachotendeka; kwamba lazima kitendo kinachokuzwa kisisimue na mhusika aelekezwe katika hali hatari isiyoepukika. Ploti ya tanzia hujengwa kwa sehemu tatu kuu nazo ni: Mwanzo,

katikati na mwisho.

Kijumla, kutokana na uchanganuzi wa ki-Aristotle, tanzia nyingi za Kigiriki zilikuwa na kusudi la kuthibitisha kuwa ‘jitihada haiondoi kudura’ katika sifa hii, tanzia ya Kigiriki ina mabadiliko katika mkondo wa matendo yanayofanyika hivi kwamba, mhusika mkuu anajikuta katika hali ambazo ni kinyume cha matarajio yake. Taharuki Pamoja na vinyume vya mambo na kejeli huyakumba maisha ya mhusika mkuu. Pia, mhusika katika tanzia huwa na Fahari ambayo inamsukuma hadi mwisho wa Maisha yake. Hiyo Fahari wakati mwingine huwa ni Kiburi kinachorutubisa mhusika na kushilia katika hali ya kuhuzunisha.

Tamthilia alizotumia Aristotle kukusanya data yake kuhusu sifa za tanzia ni kazi za mtunzi wa Kigiriki, Sofokile. Alitumia tamthilia ya *Mfalme Edipode* na *Antigone*.

Tamthilia ya *Antigone* ilitafsiriwa na Wafula Kwa Kiswahili mnamo 2009.

2.3.2 Wahusika

Katika kipengele cha wahusika, Aristotle (1934) anadai kwamba katika tanzia kuwe na wahusika wazuri na wale wabaya. Alidai kwamba wahusika ndio wanajenga msuko wa matukio jinsi ambavyo wanajituma kiuhusika ili kuleta athari kwa hadhira husika. Mhusika ambaye ni lazima awe ni mtu lazima awe ni mtu anayeweza kuleta mabadiliko ya bahati yake yakijitokeza (yaani kutoka hali nzuri kuwa mbaya sharti yalete athari yenye huruma.

2.3.3 Wazo

Aristotle (1934) anaeleza kwamba katika wazo, wahusika waeleze wanachokifanya au maisha yao ya awali. Aidha, anasema kwamba binadamu anayetoka kwenye tabaka la juu ndiye anakuwa na wazo linaloonekana.

2.3.4 Lugha

Lugha nayo huhusisha jinsi ambavyo wahusika hutumia lugha. Lugha hiyo iwe lugha yenye uwezo wa hali ya juu, na alisisitiza sana lugha ya majibizano ambayo hutumiwa katika mazungumzo ya wanadamu (Aristotle 1934).

2.3.5 Korasi/ nyimbo

Kipengele kingine alichokieleza Aristotle ni matumizi ya nyimbo/ korasi; ambapo anaeleza kwamba huchangia katika kupitisha ujumbe muhimu na vile vile kuleta msisitizo. Korasi pia huleta taharuki katika kazi ya tamthilia, hivyo ni muhimu kutumiwa katika tanzia (Aristotle 1934).

2.3.6 Ugizaji

Aristotle (1934) katika *The Poetics*, kipengele cha mwisho ni ugizaji ambao huhusisha jinsi ambavyo kazi fulani huwekwa kwenye jukwaa. Inajumuisha maleba na mapiku.

2.4 Mawazo ya Aristotle kuhusu Futuhi

Katika *The Poetics*, Aristotle (1913) anadokeza kuwa aina nyingine ya tamthilia ni Futuhi. Katika kuweka msingi wa futuhi, aliangazia suala la uigo. Aristotle aligawa kipengele cha uigo katika kategoria mbili; uigo wa kitendo duni, na uigo wa kitendo cha kishujaa. futuhi basi hujihusisha na uigo wa kitendo duni; hii inamaanisha kuwa vipengele vya kimsingi vya tanzia pia hutumiwa katika futuhi. Futuhi, sawa na tanzia, kipengele muhimu zaidi ni ploti; ambayo ni lazima ijengwe na vijishehemu kama vile mwanzo, katikati na mwisho. Kulingana na Aristotle, futuhi ni ugaji wa mwanadamu wa kitengo cha chini katika maisha. Wahusika hawa hudharauliwa kutokana na ugaji wa tabia ya wahusika wabaya, ambao wanadosari kitabia na ambao hawapendeki. Ugaji ambao ni mzuri ule wa matumizi ya mabarakoa ya kifutuhi ambayo yanasura

sura mbovu yaliyopinduka lakini huvutia macho.

Aristotle anaendelea kueleza kwamba, Futuhi hujiepusha na mambo yanayotia hofu na yanayoshua na kwamba futuhi huwa na athari ya kuchekesha ambayo hutokana na matendo, njia za wahusika pamoja hitilafu na ila zinazolingiliana kiusemi. Futuhi ina viwango kadha vinavyochekesha. Kiwango hafifu (duni) ndicho kiwango cha kwanza. Aidha, Kuna baadhi ya tungo ambapo kiwango cha kuchekesha si rahisi kutambulika na huhitaji utambuzi ambao ni mpevu. Futuhi hucusudia kurekebisha tabia ambazo zinadhiki au kuzicheka. Futuhi aidha inazungumzia masuala ambayo ni ya kijamii, kiuchumi na kisiasa kwa njia ambayo huchekesha. Aidha, kupitia matumizi ya kejeli na dhikata, futuhi inatumulikia maisha yetu ya ndani na kuficha msuto inavyoendelea kutuburudisha.

Aristotle aliweka msingi wa uainishaji wa tamthilia kwa kuchunguza Usawiri wa wahusika; ambapo alibainisha wahusika wa kitanzia na wa kifutuhi. Aidha, aliongozwa na kipengele cha uchanganyaji wa masimulizi na maongezi ambapo, mtunzi huchanganya masimulizi pamoja na maongezi kama anavyofanya Homer kwenye tenzi zake.

Tunakiri kwamba, uainisho huu wa Aristotle pekee hautoshi kwa sababu kuna aina nyingi za tamthilia hususan tukichunguza tamthilia ya Kiswahili na maendeleo yake katika karne ya isirini na moja. Aristotle anatuacha kwenye taharuki inayozua maswali kama vile; Je, drama zinazotawaliwa na nyimbo na muziki ni za aina gani? Ni kweli kwamba Aristotle aliangazia kipengele cha matumizi ya korasi kwenye utunzi wa kazi za tamthilia za tanzia, ambapo kulingana naye, korasi huchangia katika kupitisha ujumbe muhimu na kuleta msisitizo. Kwake, korasi hutumiwa tu katika Tamthilia za Tanzania, lakini hajaangazia tamthilia ya melodrama; ambayo ni aina

muhimu sana ya Tamthilia ya Kiswahili.

Swali la pili analotuacha nalo Aristotle kutokana na uainishaji wake ni; Je, kama kuna aina mbili tu za tamthilia ama tanzia au futuhi, zile tamthilia zilizojengwa kwa vitushi vya kuchekesha kuanzia mwanzo wa mchezo hadi mwisho zitakuwa za aina gani? Maswali haya yanaonyesha upungufu wa uainisho wa Aristotle ambaye, kwa kiasi kikubwa alifanikiwa kuweka mwongozo kuhusu utunzi wa tamthilia katika fasihi kwa jumla.

2.4.1 Uainishaji wa Tamthilia kwa mujibu wa Method (2015)

Method (2015) anakubaliana na Aristotle kwamba futuhi na tanzia ni aina mbili kuu za drama, zilizotawala majukwaa kwa kwa kipindi kikubwa, ila anadai kwamba mikondo mingine ya uainishaji wa tamthilia imejitokeza na haiwezi ikapuuzwa. Method (2015) anaainisha tamthilia kwa kuzingatia vigezo vya maudhui na kusudio.

2.4.2 Uainishaji Kwa Kigezo cha Maudhui

Kwa mujibu wa Method (2015), tunapoinisha tamthilia kwa kigezo cha maudhui, tunazingatia maudhui yabebwayo na tamthilia husika kama inavyobainishwa na wahakiki mbali mbali wa kifasihi. Kazi za kifasihi hubeba maudhui ambayo ni ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiutamaduni, hivyo katika uainishaji huu, tunapata tamthilia ya kisiasa, tamthilia ya kiuchumi, tamthilia ya kijamii na tamthilia ya kiutamaduni.

Aidha, Method (2015) anadai kwamba tamthilia ya kisiasa hubeba maudhui yanayohusu siasa, kwa mfano *Kinjeketile* (E. Hussein, 1969), *Mfalme Juha* (Topan, 1971), *Mkwawa wa Uhehe* (Mulokozi 1979), *Fumo Lyongo* (Mbogo, 2009). Aidha, tamthilia ya kiuchumi huangazia masuala ambayo ni ya kiuchumi kwenye jamii. Mifano ya tamthilia ya hii aina ni kama vile *Amezidi* (Mohamed, 1995), *Nitaolewa*

Nikipenda (Wa Thiong'o, 1982), *Marejeo* (Chacha, 1986). Vile vile, tamthilia ya kijamii huzingatia mahusiano baina ya wanajamii, kwa mfano, *Mwanzo wa Tufani* (Kahigi & Ngemera, 1972), *Kwenye Ukingo wa Thim* (Hussein, 1989). Kadhalika tamthilia ya kiutamaduni hujihusisha na masuala ya kitamaduni pamoja na itikadi za kijamii, kwa mfano; *Hatia* (Muhando, 1972), *Machozi ya Mwanamke* (Muhando, 1977).

Method (2015) anapoorodhesha tamthilia ya Kijamii na tamthilia ya Kiutamaduni, anaonyesha kuchanganyikiwa kwa kuwa, anapuuza ukweli kwamba utamaduni ni sehemu ya jamii na jamii vile vile hujengwa na utamaduni; yaani jamii na utamaduni ni vitu visivyoweza kutenganishwa. Tuchukulie mfano wa jamii ya Waluo, jamii hii imejengwa kutokana na tamaduni na itikadi ambazo ndizo nguzo yake, kwa mfano jinsi ambavyo mchakato wa ndoa unavyotekelezwa katika jamii hii ni tofauti na jinsi ulivyo katika jamii ya Wakuria au hata Wakalenjin. Hii inadhihirisha kwamba jamii na utamaduni hazifai kutenganishwa; na hivyo hatuwezi kuwa na tamthilia ya kijamii na tamthilia ya kiutamaduni kama aina mbili tofauti za tamthilia. Method alipaswa kuainisha tamthilia ya kiutamaduni chini ya tamthilia ya kijamii.

Waidha, upungufu mwingine unajitokeza katika maelezo anayoyatoa kuhusu tamthilia ya kisiasa. Kulingana nasi, tamthilia hizo alizoziorodhesha zinajitokeza kuwa za kihistoria zaidi ikiwa ni lazima kigezo cha maudhui kizingatiwe; ambapo hatukubaliani nacho. Ni vyema mtaalamu aangazie msingi aliouweka Aristotle; kwamba katika uhakiki na utunzi wa tamthilia, kipengele muhimu kinachopaswa kuchunguzwa ni usawiri wa wahusika.

2.4.3 Uainishaji kwa Kigezo cha Kusudio

Katika uainishaji huu, Method (2015) anasema kwamba tunaangalia lengo au dhamira ya tamthilia husika. Tunapaswa kujiuliza maswali kama vile; Je, lengo la tamthilia husika ni kutia simanzi, kuchekesha au lengo hasa ni lipi? Kigezo hiki basi hutupa aina zifuatazo za tamthilia; tanzia, futuhi/ komedia na tanzia-ramsa.

Mtaalam huyu anadokeza kwamba tanzia ni aina ya tamthilia ambayo matendo yanayoigizwa hukusudia kuleta simanzi na majonzi. Matendo yanayotendwa katika tamthilia hii huwa ya dhati kiasi ambacho huifanya hadhira kuingiwa na simanzi na hata kulia. Shujaa anayependwa na hadhira huanguka na kufanya hadhira kuhuzunikia anguko hilo, maana walitamani shujaa huyo ashinde na wala si kushindwa. Aidha anaeleza kwamba tanzia inasemwa kuwa ndiyo tamthilia ya awali kabisa iliyokuwa maarufu sana katika jamii ya Wayunani; ndiyo tamthilia iliyomshughulisha sana Aristotle (Wamitila, 2002). Mifano ya tamthilia ya kitanzia ni *Mfalme Edipode* (Mushi, 1971), *Kinjeketile* (Hussein, 1971), *Kifo Kisimani* (Kithaka wa Mberia, 2001), *Kilio cha Haki* (Alamin Mazrui, 1982).

Method (2015) anadai kwamba futuhi inakusudia kurekebisha tabia ambazo zinadhihaki au kuzicheka. Futuhi humulika masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa kwa njia inayochekesha. Mifano ya kazi za futuhi ni kama vile; *Aliyeonja Pepo* (Topan, F.) na *'Usaliti Mjini'* (Imbuga, F).

Vile vile, Method (2015) anabaini kwamba melodrama ni aina nyingine ya tamthilia kwa kutumia kigezo cha kusudio. Kwa mujibu wa Wilson na Goldfarb (2002) aina hii ya tamthilia huelezea michezo ya kuigiza inayotawaliwa na nyimbo/ muziki. Mfano mzuri ni *Amezidi* (Mohamed, 1995).

Method (2015) anaendelea kueleza kuwa tanzia-ramsa ni aina ya tamthilia katika kigezo cha kusudio. Wilson na Goldfarb (2002) wanadai kwamba aina hii ya tamthilia ina matukio ya dhati yanayohusisha mbinu za visa vya kuisisimua na kufurahisha. Wanaendelea kueleza kwamba huweza kuanza kwa matendo ya kuhuzunisha na kumalizia kwa furaha; matukio huzua huzuni na majonzi makubwa lakini baadaye huishia kwa furaha na kuisisimua. Mifano ni kama vile; *Mama Ee* (Mwachofi) na *Natala* (Kithaka Wa Mberia).

Uainishaji wa tamthilia kwa kutumia vigezo alivyovitumia Method (2015) vinaleta mwingiliano ambapo tamthilia moja huweza kupatikana katika vikundi tofauti tofauti kwa kutumia vigezo tofauti. Tuchukulie mfano *Kinjeketile*, ambacho amekiorodhesha kuwa tamthilia ya kisiasa na tanzia kwa kuangazia vigezo vya maudhui na kusudio mtawalia. Mtaalamu huyu anaeleza yafuatayo kuhusu udhaifu wa uainishaji wake;

Udhaifu mwingine ni kuwa aina moja ya tamthilia inabainishwa kwa kutumia vigezo tofautitofauti lakini ikiwa na maelezo tofauti kabisa. (Uk. 215)

Kutokana na dai hili ni wazi kwamba hata Method mwenyewe hana imani na uainishaji wake, huenda hata yeye unamkanganya. Hivyo mbinu alizozitumia Method (2015) zina changamoto kwa vile hazitoi mwanga kuhusu uainishaji wa tamthilia. Hata kama mtaalamu huyu alieleza kuhusu Tamthilia ya kisiasa, kijamii, kiuchumi, Kiutamaduni, tanzia, futuhi, tanzia-ramsa na melodrama, uainishaji wake haujitokezi kwa uwazi na pia unakanganya sana.

2.4.4 Uainishaji wa Tamthilia kwa mujibu wa Wamitila

Wamitila (2002) akimrejelea mwanafalsafa mkongwe wa Kigriki Aristotle, katika “*The Poetics*” aliyebainisha aina mbili tu za tamthilia kama vile tanzia pamoja futuhi, mtaalamu huyu anaongeza melodrama, vichekesho, Tanzania-ramsa, tamthilia ya

kihistoria na tamthilia tatizo kama aina nyinginezo za tamthilia ya Kiswahili. Kwa kifupi, kwake Wamitila, kuna aina zifuatazo za tamthilia;

- | | |
|----------------|-----------------------------|
| i. Tanzania | v. Tanzania-ramsa |
| ii. Futuhi | vi. Tamthilia ya kihistoria |
| iii. Melodrama | vii. Tamthilia tatizo |
| iv. Vichekesho | |

Wamitila (2002) anakubaliana na Semzaba (1997) kwa kutoa madai kwamba Tanzania ni tamthilia yenye huzuni kutokana na kuwa na hatima ya mhusika mkuu kuwa ya kupatikana na janga. Katika maelezo yake, Wamitila (2003:219) anasema yafuatayo;

Tanzania kimsingi hutumiwa kuelezea utanzu mmoja wa tamthilia ambao unahusu kuanguka kwa nguli au mhusika mkuu na kuishia kwa kifo. Katika drama, Tanzania hutokana na udhaifu na dosari fulani ya mhusika shujaa na kumsababishia kifo.

2.4.5 Melodrama

Anavyoeleza Wamitila (2002) ni kwamba aina hii ya tamthilia iliibuka enzi za urasimi ambapo ilitumiwa kuelezea tamthilia ambayo wahusika wake wanavutia na wanafurahisha sana huku matukio yakiambatanishwa na uimbaji au nyimbo. Mara nyingi melodrama huwa na dhamira ya mivutano baina ya wema na uovu/ubaya. Dai hili Wamitila (2003:120) analisisitiza kwa kusema haya, “Melodrama ni aina ya tamthilia itawaliwayo na uimbaji au nyimbo. Wahusika wanaopatikana katika kazi ya aina hii huweza kuvutia na kufurahisha lakini aghalabu hukosa sifa zinazoonyesha ushujaa. Miisho ya melodrama huwa ushindi wa mhusika mwema.”

Kutokana na maelezo haya ni dhahiri kwamba aina hii ya tamthilia hufanana na Tanzania lakini nguli katika melodrama anajipatia ushindi mwishowe. Aidha, matokeo yake ni ya kuisisimua sana. Tunapochunguza dhana ya ‘melodrama’, tunapata kwamba neno hilo limetokana na neno la Kifaransa “*me'lodrame*” ambalo pia limetokana na neno la

Kigriki “melos”(muziki/wimbo) na lile la Kifaransa “*drame*” (kwa maana ya drama). Melodrama ni tamthilia ambayo inatilia maanani Ploti pamoja na wahusika ili ishawishi hisia za hadhira husika. Ala za muziki na nyimbo zinatumiwa zikiambatana na matendo yanayotendwa na wahusika. Vitushi havidhamirii kujenga wahusika na vimekosa uzito. Kwa jumla, utunzi wa aina hii hujikita zaidi katika matumizi ya nyimbo.

2.4.6 Vichekesho

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), kichekesho ni aina ya futuhi ya aina ya chini inayohusisha matukio ya kiajabu, kuchezea maneno na elementi za wigobezi. Vichekesho hukusudia kuonyesha visa vitakavyochekesha tu bila kutilia maanani ujenzi wa wahusika wala msuko. Vichekesho hivi husababishwa kutokana na jinsi ambavyo wahusika wanasawiriwa hasa kupitia matukio ya jukwaani yasiyo ya kawaida. Mfano mzuri wa tukio linalochekesha ni wakati ambapo mhusika wa kiume amevalia kama mke na wake pia kuvalia kiume au hata wahusika hao wakikimbizana jukwaani. Kiini cha aina hii ya tamthilia ni kuwa na uwezo wa kusababisha kicheko kingi kutokana na mbinu za kifutuhi ya chini; yaani mbinu za ucheshi zinazotumiwa katika vichekesho huwa zimevutwa na kupanuliwa zidi.

2.4.7 Tanzania-ramsa

Kwa mujibu wa Wamitila (2003:219), “Tanzania-ramsa ni aina ya Tanzania inayohusisha mbinu za kifutuhi na aghalabu huishia kwa furaha. Hali hii hupatikana kutokana na kuwepo kwa hasidi au muwi ambaye anatubu na kujutia makosa yake au msimamo wake na uwepo wa mandhari ya kiulimbwende.”

Tanzania-ramsa inadhihirisha mabadiliko ya aina nyingine yanayougeuza mwelekeo wa matukio ya kitanzia, na kuuweka uwe wa kufurahisha; yaani ni Tanzania ambayo

huishia kwa furaha.

Kutokana na maelezo haya, tanzia-ramsa ni aina ya tamthilia ambayo ina vitushi vizito vya kitanzia ambavyo kadri ya mchezo unavyoendelea, vitushi hivyo hugeuka ghafla na kuwa vya furaha. Mara nyingi mabadiliko hayo ya matukio hutokea kipindi ambacho wahusika wake wapo katika hatua ya kuandamana na mambo mabaya na hatimaye mambo hayo hugeuka na kwenda vizuri, na haya hutokea mwishoni mwa mchezo.

Kando na hayo, tunakiri kwamba tanzia-ramsa ni tamthilia inayoundwa kwa sifa za Tanzania na za ramsa; hivyo ni vyema mtaalamu anapoainisha tamthilia ya aina hii, awe ameinisha Tanzania na Ramsa tofauti bila kupitia njia mkato alivyofanya Wamitila. Tunakubali kwamba aina nyingine ya tamthilia ni Ramsa; ambayo wahusika wake wanasawiriwa kwa hali inayovutia na kufurahisha. Furaha inayopatikana katika aina hii ya tamthilia hutokana na mkabala kati ya mategemeo ya jambo fulani na matukio halisi ya jambo lenyewe.

Ifahamike kuwa kuna tofauti iliyoko kati ya Futuhi, Kichekesho na Ramsa. Futuhi kama tulivyoeleza hapo awali ni aina ya tamthilia inayochangamsha na huishia kwa kufurahisha, kichekesho halikadhalika ni tamthilia iliyo na uwezo wa kusababisha kicheko kingi kutokana na mbinu za kifutuhi ya chini (athari ya kicheko kinatambulika kwa urahisi) ilhali Ramsa ni aina ya tamthilia ambayo huonyesha mkabala kati ya tukio fulani na matukio ya jambo hilo. Kinachodhihirisha tofauti kati ya Ramsa na Futuhi ni kuwa badala ya wahusika wake kupambana na vikwazo ambavyo dunia imeweka mbele yao, wanafanya juhudi za kuviepuka vikwazo hivyo na kujaribu kukomboa nafsi zao. Kwa kifupi tunakiri kwamba Ramsa ni futuhi ya kiwango cha juu.

2.4.8 Tamthilia ya Kihistoria

Anavyoeleza Wamitila (2003) ni kwamba, tamthilia ya kihistoria inatokana na matukio ambayo yaliwahi kujitokeza katika historia. Mifano anayotoa ni *Kinjeketile*, yake E. Hussein ambayo hueleza historia kuhusu vita vya majimaji na *Mkwava wa Uhehe*, yake M. Mulokozi.

2.4.9 Tamthilia Tatizo

Wamitila (2003:217) anadai kwamba tamthilia tatizo ni aina ya tamthilia inayojishughulisha na tatizo maalum la kijamii. Anaendelea kueleza kuwa mifano ya aina hii ya tamthilia ni pamoja na *Nguzo Mama* na *Lina Ubani* za P. Muhando na *Natala* na *Kifo Kisimani* za Kithaka wa Mberia.

Tamthilia Tatizo huwa na wahusika ambao wanakumbwa na tatizo fulani ambalo wanataka kulitatua. Mara nyingi tamthilia ya aina hii hutumia taharuki ya kuifanya hadhira iwe makini ili kuona jinsi tatizo husika linavyosuluhishwa.

Kwa kiasi fulani tunakubaliana na muainisho wa Wamitila kwamba tamthilia huainishwa kama Tanzania, Futuhi, Tanzania-ramsa, melodrama, vichekesho, tamthilia ya kihistoria na tamthilia tatizo lakini tunaongezea tamthilia ramsa na tamthilia ya Masimulizi-ongezi.

2.5 Dhana na muktadha wa ubwege

Tumefafanua ubwege pamoja na muktadha ambao ulijitokeza na baadaye tulijikita katika tamthilia ya kiubwege ili kupata msingi wa tamthilia hiyo.

Kwa mujibu wa Martin (1994) neno 'ubwege' lilitumiwa kwa mara ya kwanza na mtunzi wa Kifaransa aliyetwa Albert Camus, hivyo ubwege ulianza kutumiwa katika fasihi na Albert Camus kati ya miaka ya 1913-1960. Kulingana na Camus, ubwege ni

kitu ambacho hakiwezi kuguswa bali ni uhusiano ambao ni wa kidhahania kati ya akili pevu na ukweli wa uwepo wa binadamu katika ulimwengu. Hali hii ya ubwege hujitokeza kwa sababu ya kukosa kuridhika kwa akili kutokana na matarajio yake juu ya utaratibu wa matukio ulimwenguni. Kinyume cha matarajio hayo, hali inayojitokeza ni ile yenye fujo na ambayo hukosa umuwala, na haiwezi kutambulika. Cruickshank (1960:41) anaunga mkono dai hili kwa kusema kwamba kwa ubwege, mtunzi Camus anarejelea ukosefu wa muumano kati ya mahitaji ya kiakili na ukosefu wa uwiano ulimwenguni ambao akili inakumbana nayo.”

Aidha, Magare (2002) kwenye tasnifu yake anasema kuwa, Camus alidai kwamba ingawa binadamu anaongozwa na bahati isiyotabirika, bado ana uwezo wa kuyapanga maisha yake kwa kuongozwa na maadili ya kibinadamu. Maadili haya ya kibinadamu na kukosekana kwake katika jamii ndiyo yanayochochea rai yake kwamba fasihi ya kiubwege huyasawiri maisha yasiyokuwa na matumaini wala matarajio ya aina yoyote.

Naye Gilgen (1980) anasema kwamba dhana ya ubwege hutokana na mvutano baina ya matamano na fikra za binadamu na ukatili wa ulimwengu anamoishi. Anaendelea kueleza kwamba shujaa wa kiubwege hutambua kuwa njia ya kuishi katika huu ulimwengu katili ni kuishi maisha ya kiubwege kupitia ukengeushi

Martin (1961) ananukuliwa na Magare (2002) kwamba Ubwege hauna nia na kutengwa kutoka kwa imani za kidini, tabia za kiungu na misingi ya kiakili na mawazo. Yaani mwanadamu amepotea na matendo yake ni ya kijinga; kiubwege na yamekosa maana kabisa.

Aidha, Camus (1955) katika Magare (2002) anadokeza kuwa, hii hali ya kukosa kuridhika kwa moyo ndiyo huleta mateso ya kiakili. Aidha, hii hali humpatia

mwandamu suluhisho za aina Mbili. Kwanza akubali ukweli wa hali yake na kuukabili, au aamue kujiua. Anapojiua, anaangamiza akili yake ambayo inapaswa kuhisi hali ya ubwege. Halikadhalika, anapokubali hali ngumu ya maisha yenye mateso, ambayo ndiyo ukweli wa maisha, anathibitisha utata wake, ambao ni ubwege. Aidha Magare (2002) anaeleza kwamba Lewis (1962:259) anaeleza hii hali duni ya maisha ya binadamu ulimwenguni kwa kusema;

“Binadamu ako pweke na amejipoteza katika ulmwengu katili ambamo Mungu amemtupa. Anaendelea kufafanua kwamba sayansi na kufikiria ni uongo; mwanadamu amefungwa na ulimwengu huu katilikitu kilichobakia ni kifo, ambacho ndicho hatima ya binadamu wa kiubwege. Mawasiliano yamekosekana kwa vile hata lugha imekufa. Ubwege ni kukosa utaratibu. Binadamu amekosa uwezo hana uwezo wa kupanga matukio yake katika ulimwengu anamoishi,. Basi anatenda na kusema mambo yasiyo na muumano mzuri. Hali inayojitokeza ni ya kiubwege” (T.Y)

Kutokanana maelezo haya kijumla, wazo linalodhihirika ni kwamba, ubwege huashiria ukosefu wa utaratibu, matumaini pamoja na nguvu za kubadili hali duni katika maisha ya binadamu.

Chimbuko la ubwege hujitokeza katika Karne ya kumi na tisa na mwanzoni mwa Karne ya Ishirini. Wakati huu ulijikumba na mabadiliko kadha maishani mwa binadamu hasa Uropa. Misingi ya mtazamo huu ilirutubishwa na Vita vikuu vya Dunia, watu wengi na mali iliharibiwa. Kulikuwa na kuporomoka kwa maadili na thamani ya binadamu kwenye kipindi hiki. Hii ilisababisha kuibuka kwa ubwege. (Cruickshank 1960 katika Magare 2002).

Aidha, Imani za kidini zilianza kupingwa na wafuasi wa ubwege. Wanafalsala kama Friedrich Nietzsche walianza kushuku imani za kidini. Wakati huo huo, jaribio la kisayansi kuhusu ufafanuzi wa asili na hali ya dhana mbalimbali za maisha, bila mafanikio mema. Aidha, kukosa kufaulu kwa mawazo ya kisiasa na kiuchumi kama

yale ya Kimarx, kuliwafanya watu kama Camus kuwaza zaidi juu ya uwezo na umuhimu wa binadamu katika ulimwengu anamoishi. Maisha ya binadamu yalionekana kukosa maana kabisa na hali ya upweke wa binadamu katika ulimwengu katili ikajidhihirisha vyema.

Kulingana na Camus (1953:14), kulikuwa na vitendo vya kinyama alivyovigundua Camus na kudhihirika katika biashara ya watumwa, mawazo ya kiuchumi, vita ambayo yalienea Uropa na kutetewa kwa kutumia falsafa mbalimbali. Watu waliokosa hatia waliteswana wengine kuuawa. Vita vya pili vya Dunia vilileta uhalifu usiolinganishwa na mali na maisha. Kutoka na haya, maisha ya binadamu yalikosa maana na hivyo ubwege ukaenea ulimwenguni. Kwake Camus, dini ni kasumba ambayo imemziba macho binadamu asiweze kuuona ukweli. Ni lazima binadamu ajitenge kutoka kwa imani za kidini na falsafa zake ili aweze kujua ukweli wa maisha. Anaendelea kueleza kuwa binadamu anafaa kukabiliana na hiyo hali yake kikamilifu ama ajiue. Anasema kwamba wanasayansi ameshindwa kudhihirisha sababu inayofanya watu kutenda watendayo na kuwa na tabia zao. Hii hali ya kukosa kujua ndiyo msingi wa ubwege. Webb (1972) anadokeza kwamba hii ni hali ya sintofahamu kwa binadamu na ulimwengu wake anamoishi.

Fasihi ya Ubwege hudhihirisha ukweli wa maisha ya binadamu katika ulimwenguni. Webb (1972) anaeleza kwamba fasihi ya ubwege hudhihirisha hali ya fikra za binadamu. Binadamu hutafuta ukweli, lakini anazuiliwa na fikra zake, hivyo hupati ukweli. Tamthilia ya kiubwege hudhamiria kuonyesha kushindwa kwa binadamu kujielewa pamoja na hali yake duni katika ulimwengun anamoishi.

2.5.1 Tamthilia ya Kiubwege

Tamthilia ya kiubwege ni tamthilia inayojitenga na kujaribu kuvuruga vipengele vya kale kuhusu utunzi wa Tamthilia. Tangu enzi za Aristotle,, tamthilia/drama zimedhihirisha utaratibu tofauti wa utunzi. Tamthilia ya kiubwege hukiuka utaratibu huo, sawa na kukiuka hali ambazo hufahamika kama za kiuhalisia. Esslin Martin (1974) katika *The Theatre of the Absurd*, alitoa mawazo yake juu ya Ubwege. Martin amechangia sana katika tapo la ubwege na kutoa mukhtasari wa tamthilia ya kiubwege. Anaeleza kwamba tamthilia ya kiubwege haina hadithi inayofululiza vizuri, huwa zimekosa hadithi au ploti ya kuelezwa kikamilifu. Aidha, hakuna usawiri na umotishaji mzuri wa wahusika katika tamthilia ya kiubwege. Vile vile, hukosa maudhui pevu wala muwala wa maudhui. Tamthilia za kiubwege hutawaliwa na ndoto nyingi.

Kuhusiana na masuala haya, Wilson na Goldfarb (1991) wanadokeza kuwa, katika tamthilia za kiubwege, mazungumzo na majibizano ya wahusika huonekana kukosa maana na mara nyingi wahusika wa kiubwege hushindwa kuwasiliana ipasavyo. Hii inamaanisha kuwa, katika tamthilia za kiubwege mazungumzo ya wahusika huwa ni ya kubwabwaja yasiyofuatana kimantiki.

Miongoni mwa waandishi wa tamthilia za kiubwege ambao wametunga tamthilia zinazodhihirisha mtazamo wa mtinzi Esslin Martin, ni Eugene Ionesco ambaye aliandika; *The Killer, The Lesson, The Chairs, Rhinoceros*. Samwel Beckett, ambaye aliandika; *Waiting for Godot, End game*. Mawazo haya yanajitokeza pia katika maandishi ya Wilson na Goldfarb (2002:348) wakisema yafuatayo;

“Ubwege ulihusishwa na Martin Esslin (1950), ambaye alitambua kwamba drama zilizochukua mwelekeo wa kiubwege ulidhihirisha mambo mawili makuu; kwanza ni kwamba yanayotendeka maishani mwa binadamu ni ya kiubwege na hayana mantiki. Pili, ni kwamba

ubwege unafaa kuonyeshwa katika matendo ya kidrama. Wanaokubaliana na wazo hili ni pamoja na; Samuel Beckett (1906-1989), Jean Genet (1910-1986), Eugene Ionesco (1912-1994), Edward Albee na Harold Pinter (1930). Kazi za kiubwege huwasilisha kuwepo kwetu na mahusiano ya binadamu na lugha yake kuwa ya kipuzi na hayana maana. Ili kudhihirisha haya, watunzi hutumia mbinu za kidrama zisizo na mantiki. Ploti huwa ya mviringo, wahusika si wa kiuhalisia, mandhari huwa ya kigeni na hayatambuliki, lugha hutatiza mawasiliano na wahusika hulosa kufanikisha mawasiliano baina yao.”

Katika Uigizaji wa drama za kiubwege, (Anderson 1972:2 katika Magare 2002) anasema:

“Hadhira inakumbwa na vitushi vingi visivyo na muwala, na matukio hayana maana kimuktadha na hata kisaikolojia.

Kutokana na hali hii, binadamu hupata picha halisi juu ya maisha yake yasiyo na utaratibu wowote katika ulimwengu anamoishi. Aidha, matukio ya tamthilia ya kiubwege hudhihirika kimzunguko yaani, kuna matumizi ya duara ni kigezo muhimu katika aina hii ya drama. Esslin (1961:365) anadokeza kuwa tamthilia za kiubwege huwa na muundo wa kiduara, yaani huisha jinsi zilivyoanza; nyingine huendelezwa ile iliyotangulia.” (T.Y)

Wahusika katika tamthilia ya kiubwege huwa vibonzo, mazungumzo yao hukosa umantiki na kutatiza mawasiliano. Magare (2002) anadai kuwa Anderson (1972) anaeleza hali ya wahusika wa kidhahania katika tamthilia ya kiubwege kwa kusema kuwa mara nyingi wahusika hubadilisha hali zao, mazungumzo yao yamejaa ukinzano; hukataa kukubali yaliyomo ulimwenguni na badala yake kuamini matukio ya kidhahania. Maelezo yao juu ya hali na dhana mbalimbali hukosa maana.

Wahusika katika tamthilia za kiubwege huwa zimekosa umotishaji katika matendo yao jukwaani. Wahusika hawa huwa wametekwa na hali Fulani inayowashinda kujinasua. Wahusika hawa hujitenga na hadhira na hadhira hushindwa kuwalaumu kutokana na

matendo yao. Usawiri huu wa wahusika hubainisha hali ya maisha duni yanayokatisha tamaa. Aidha, wahusika hawa hukosa kujua nyakati za vitendo vyao bali vitu hujitokeza kama ndoto.

2.5.2 Mielekeo ya Tamthilia ya Kiubwege

Kabla ya kuangazia mielekeo ya tamthilia ya kiubwege, tulieleza dhana ya mwelekeo ili kutoa mwanga zaidi kuhusu mada tuliyoshughuikia. Wamitila (2003:157) kwenye kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia dhana ya mwelekeo imeelezwa ifuatavyo;

“Mwelekeo hutumiwa kueleza mtazamo au hata mkabala anaouchukua mtunzi ambao unachukuliwa na jamii fulani kuhusiana na tukio, jambo, wahusika au suala fulani. Huweza kupatikana katika Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi.”

Kwa kifupi, dhana ya mwelekeo ilivyotumika katika utafiti huu ni mkabala au mtazamo wa mtunzi kuhusu ubwege. Mwelekeo wa kiubwege basi huhusisha mtazamo wa kiubwege katika kazi teule zilizoshughulikiwa. Tumejikita katika uchanganuzi wa vipengele vya kiubwege katika tamthilia teule kimaudhui na kifani, ili kudhihirisha jinsi ambavyo watunzi teule waliviangazia na kudhihirisha msimamo wao kuhusu Ubwege.

Tamthilia ya kiubwege ni tapo la drama linalotambulika sasa. Kulingana nasi, aina hii ya tamthilia inagawanywa kwenye makundi matatu; Wanaoamini kuwepo kwa Mungu, Wasioamini kuwepo kwa Mungu na Wasio na uhakika kuhusu suala la Mungu (wale wa Kati).

Kundi la wanaoamini kuwa “Mungu yupo” linawakilishwa na mwanatheolojia wa Ki-Deni Soren Kierkegaard (1813-1855), ambapo Wamitila (2003:248) anaeleza kwamba “katika maandishi yake mbali mbali na hasa *The Concept of Dread, Fear of Trembling* na *Sickness unto Death*, Kierkegaard alieleza kuwa mwanadamu hupata kimbilio kutoka mivutano ya maisha kupitia kwa Mungu. Hii ni imani ambayo iliishia kushika

nguvu sana katika Ukristo...”

Kutokana na dai hili, ni wazi kwamba kundi hili lilishikilia kuwepo kwa Mungu, ambaye ni kitulizo cha roho ya binadamu wa kiubwege; asiyeweza kutua mzigo wa maisha yaliyojaa matatizo. Binadamu hawezi kuishi kwa nguvu zake mwenyewe bali kuna nguvu zinazomzidi ambazo humtawala, yaani nguvu za kiumbe cha ngazi ya juu zaidi, Mungu. Anavyoeleza Kierkegaard (2008) ni kwamba binadamu anapoishi ulimwenguni anajikuta ametenda dhambi na anapaswa kutubu ndipo apate utulivu wa kiroho. Aidha, anadai kuwa binadamu ni kikaragosi tu cha kiumbe ambacho kiliwaumba na ni katika kuzicha nguvu hizo, ndiposa apate utulivu wa kiroho. Albert Camus pia anajihusisha na imani hii kwamba “Mungu yupo”, japo anadokeza katika kueleza suala la *binadamu wa kiubwege* na *uhuru wa kiubwege* kwamba, binadamu asitarajie ukombozi wa kiumbe hicho bali afanye juhudi za kujitafutia uhuru wake mwenyewe kwa kukubali ubwege wake.

Kundi la pili ni la wasioamini kuwepo kwa Mungu ambalo linawakilishwa na Friedrich Nietzsche (1844-1900). Mtazamo huu unadhihirisha msukumo mpya uliopatikana kazi za kitamthilia ambao ulijitokeza katika karne ya ishirini. Kando na Friedrich Nietzsche, Wamitila (2003) anataja kuwa wataalamu walioshikilia kwamba “Mungu hayupo” ni pamoja na Martin Heidegger (1889-1976), Karl Jaspers (1883-1969) na Samuel Beckett (1906-1989). Wataalam hawa walitilia mkazo matatizo halisi yaliyomsibu mwanadamu huku wakikwepa imani potovu kuhusu maana ya maisha. Anaendelea kueleza kwamba Nietzsche anajulikana kwa tamko maarufu katika *Joyful Wisdom* kuwa “Mungu amekufa.” Hili tamko pamoja na msimamo wa wenzake, inadhihirisha kuwa wanaamini kwamba Mungu hayupo. Kwa kifupi, Wanafalsafa hawa wanakosa kuamini uwepo wa Mungu pamoja na uumbaji wake wa

ulimwengu. Hii ni Kwa sababu ya vifo vilivyotokea katika maisha ya wanadamu wakati wa vita vikuu vya dunia. Dai hili lilishika mkondo miongoni mwa wale wataalam walioshikilia kwamba, kama Mungu angekuwepo basi hangeruhusu watu kuzidi kutenda dhambi na hangewanyanyasa watu wasio na hatia kwa kuwafanya wapitie mateso yasiyo na kikomo; yaani angekuja kwa ukombozi wa binadamu ulimenguni.

Kundi la tatu ni la wasio na uhakika kuhusu suala la Mungu (tuliliita *Kundi la Kati*) ambalo linahusishwa na Jean-Paul Sartre (1905-1980) ambaye; kutokana na utunzi wake pamoja na historia ya maisha yake ni wazi kwamba hana uhakika wa suala la kuwepo kwa Mungu. Maandishi yake ya mwanzo kama vile *Being and Nothingness* yanasawiri msimamo wake kwamba Mungu hayupo lakini baadaye hata alipokaribia kifo chake, alibadilisha msimamo wake na hata kuita kiongozi wa dini kwake. Kutokana na kusoma kwake kwa kazi ya Nietzsche (1943) "*New Mystic*" alikiri kwamba "Mungu amekufa" lakini akadai mwishoni kwamba; Hatufai kuelewa kutokana na hili kwamba Mungu hayupo; amekufa, alikuwa akinena nasi na kwa sasa amenyamaza, tunagusa tu mfu. Miongoni mwa kazi nyingine za kifasihi alizozitunga ni kama vile; *The Wall, Existentialism is Humanism, The Reprieve, The Age of Reason*.

Ijapokuwa kuna makundi haya matatu kama tulivyovianisha, tamthilia ya kiubwege hutawaliwa na wazo la kuwako kwa binadamu na anavyoishi maisha yake duni katika ulimwengu katili unaomtesa na kumfanya akate tamaa. kiubwege kwa ujumla huongozwa na wazo la kuwako kwa binadamu ulimwenguni, maisha yake duni na yasiyo na maana katika ulimwengu huo katili na wa kukatisha tamaa. Anavyoeleza Kitchin (1966) kwamba dhamira kuu katika tamthilia za kiubwege ni kwamba

binadamu anasawiriwa akiwa ameishi katika maisha ya kukatisha tamaa na yasiyo na maana katika ulimwengu katili.

2.6 Hitimisho

Sura hii imedhihirisha historia na uainishaji wa tamthilia. Tumeeleza historia ya tamthilia kwa kuangazia vipindi vya kihistoria vikiwemo; kipindi cha kabla ya Ukoloni, wakati wa Ukoloni na Baada ya Ukoloni. Waaidha, tumechunguza mawazo ya Aristotle kuhusu uainishaji wa tamthilia kwa sababu, msingi wa utungaji wa tamthilia uliwekwa na mtaalamu huyu. Baadaye, mawazo ya Method (2015) na Wamitila (2002 & 2003) yalihakikiwa ili kutoa mwanga zaidi kuhusu uainishaji wa tamthilia ya Kiswahili. Hatimaye tuliibuka na aina nyingine ya tamthilia ambayo ni tamthilia ya Masimulizi-ongezi, kwa kuongozwa na kanuni ya kuchanganya masimulizi na maongezi ya Aristotle katika uainishaji wa tamthilia na kuzitaja sifa zake bainifu. Kando na hayo, dhana na muktadha wa ubwege, tamthilia ya kiubwege pamoja na mielekeo ya kiubwege zilijadiliwa na tulibaini kwamba Said Ahmed Mohamed na Pauline Kea Kyovi katika tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* mtawalia, walichukua mwelekeo ulio sawa kwamba Mungu yupo na hivyo kujihusisha na kundi la Soren Kierkegaard na Albert Camus.

SURA YA TATU

MWELEKEO WA KIUBWEGE KATIKA TAMTHILIA YA *AMEZIDI* NA

BELUWA

3.0 Utangulizi

Katika hii sura, tumeanza kwa kutoa muhtasari wa tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* kasha tukaonyesha mwelekeo wa kiubwege kwa kuchanganua jinsi tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* zilivyoathiriwa na mkabala wa utunzi wa kiubwege na hivyo kudhihirisha jinsi zinavyolingana kiubwege. Sura hii imehusisha vipengele anuwai vya kiubwege kimaudhui vikiwemo dhamira, mandhari, suala la Mungu na dini, suala la kifo na kaburi, ukengeushi na ukosefu wa uthabiti kwa elimu. Aidha tumejikita katika kuchambua vipengele vya kifani hususan; uhusika (uchache wa wahusika, wahusika wa kiutopia na wahusika wa kinjozi), ukosefu wa ruwaza za mazungumzo, utupu, matumizi ya nyimbo, ploti mviringo, matumizi ya vicheko na vilio, pamoja na matumizi ya lugha inayotatiza mawasiliano. Tuliweza kuhakiki na kuchanganua vipengele hivi na vingine zaidi hivyo, kulinganisha tamthilia hizi mbili kiubwege. Kwa kufanya hivi, mwelekeo wa kiubwege wa watunzi wa tamthilia hizi mbili umebainika wazi.

3.1 Muhtasari wa Tamthilia ya *Amezidi* (S. A. Mohamed, 1995)

Mchezo wa *Amezidi* unatangulizwa kwa wimbo wa Mzee, ambao unaangazia siku ya mwisho wa kuishi Duniani. Siku hiyo inaonyeshwa kuwa itampumzisha binadamu kutokana na mzigo wa matatizo ya Dunia.

Vitushi katika tamthilia hii vinatokea mawazoni na ndotoni mwa wahusika kwenye pango. Mwandishi alitumia mandhari ya Kidhahania naya kukatisha tamaa. Mtunzi

ametumia wahusika wawili wakuu, nao ni Ame na Zidi wanaobadilika na kuchukua nafasi za wahusika mbali mbali ili kufanikisha mchezo huu.

Katika onyesho la kwanza, tendo lote linatokea mawazoni na uhalisini...pangoni ambapo Ame anaonyeshwa akiwa usingizini japo jua liko utosini. Naye Zidi kwa upande mwingine anaingia na mihogo miwili na kuanza kuamsha mwenzake. Mihogo hii inazua ubishi baina ya wahusika hawa kuhusu jinsi ambavyo itachomwa na kuliwa kwa kuwa hawana Kiberiti, kisu na hata hawajui namna ya kuwasha moto. Hatimaye mihogo hii inaliwa ikiwa mibichi.

Mchezo huu unaendelea ndotoni ambapo Ame na Zidi wanaliona pango kuwa ni Kasri la kifahari lililo na vitu vya dhahabu. Ndoto hii baadaye inakashifiwa na Mhusika Mari (Ame), ambaye ni mpenziye Zidi. Anamwambia Zidi kuacha maisha ya kindoto, anamwambia afungue macho na aone kwamba anaishi kwenye pango na wala si kwenye kasri. Mhusika huyu pia anadhihirisha kukengeuka kwa kiasi kikubwa, baada ya kupata elimu ya kimagharibi, anatupilia mbali mila za kiafrika pamoja na desturi zake licha ya kuwa mwafrika halisi.

Aidha, baadaye mtunzi anatuonyesha tendo la shuleni ambalo linadhihirisha mandhari ya kinjozi na elimu yenye kukatisha tamaa. Zidi anakuwa mwalimu asiyejielewa; anaketi juu ya meza ya kufikirika tu, anaamrisha wanafunzi wasioonekana, mmojawao akiwa Ame, kucheka na kulia darasani. Mandhari mengine yanayotumika kwenye mchezo huu ni ya ofisini ambapo Ame anakuwa Bosi huku Zidi akiwa Msaidizi wake. Tendo katika mandhari haya yanadhihirisha jinsi ambavyo wakoloni wanajifaidi kutokana na uchumi wa nchi za kiafrika, kwa mfano; Wahandisi wakiafrika hawajui kutenda bali wanaufahamu tu wa kinadharia. Walifundishwa

nadharia pekee hivyo hawana uwezo wa kutatua matatizo ya nchi zinazohitaji maarifa yao. Hii inasababisha kuagizwa kwa wahandisi wengine kutoka nchi za nje.

Kadhalika, mtunzi anatuonyesha jinsi viongozi waafrika walivyowafisadi kupitia kwa wahusika hawa wawili. Wanatumia njia ya mkato kutajirika kwa kujilimbikizia mali ya umma. Baadaye mchezo unatamatishwa kwa kifo cha wahusika hawa wakuu, ambacho kinasababishwa na ulaji wa nyama ya paja la ng'ombe iliyovunda. Nyama hii walipewa kama msaada kutoka kwa EC. Ukosefu wa kiberiti, moto, kuni na mafuta ya kuchoma nyama hii inawafanya waile ikiwa mbichi na hivyo kuwasababishia ugonjwa wa kipindupindu unaowamaliza. Zidi anaaga dunia na kufuatwa na Ame. Wahusika hawa wanachorwa kushangilia kifo kwa madai ya kukombolewa kutoka kwa mateso ya dunia yasiyoisha.

Kwa kuhitimisha, mtunzi anafunga mchezo huu kwa wimbo wa mtoto asiyezaliwa, ambao unahusu ulimwengu mpya ulio na mapinduzi. Kimalizio cha tamthilia hii inatuarifu kwamba kuna tumaini la kuzaliwa upya kwa binadamu na kujielekeza kwake katika njia itakayomletea maendeleo na ufanisi.

3.2 Muhtasari wa Tamthilia ya *Beluwa* (Pauline Kea Kyovi, 2012)

Matendo katika mchezo huu yanatukia kwenye mandhari ya gerezani, Rumande. Mtunzi ametumia wahusika watatu, Beluwa, Tanda na Mtu; ambao wanaigiza wahusika wengine katika mandhari mbalimbali za kidhahania.

Katika onyesho la kwanza, Beluwa anaonyeshwa akiwa usingizini huku akizungumza kwa lugha isiyoieleweka, mara Tanda pia anasukumwa ndani ya chumba alimokuwa Beluwa; hivyo wanajipata wakiwa watuhumiwa wawili. Wahusika hawa wanaulizana kuhusu kilicholeta kila mmoja gerezani lakini kutokana na mazungumzo ya kiubwege, wanazushana tu bila kuelewana. Wahusika hawa wanajipata kwamba hata

wao wenyewe hawajielewi wala kujitambua hivyo, wanajituliza kwa vicheko vinavyobadilika na kuwa vilio.

Aidha, mtunzi anatuchorea mwili wa Beluwa ukichiriza damu huku yeye mwenyewe hatambui, hadi damu hiyo inapotumiwa na Tanda katika kukigawa chumba. Mvutano mdogo unasababisha vita baina yao; wanashindwa kuelewana na kutatua matatizo yao.

Kadhalika, Rumande inageuka na kuwa uwanja mkubwa wa kuchezea kandanda. Kuna timu mbili zinazohusika, timu ya Beluwa na timu ya Tanda. Tanda anakuwa Mtangazaji wa mpira huku Beluwa anakuwa mchezaji hodari wa timu ya Beluwa. Hata hivyo, timu ya Beluwa inaonyeshwa kukosa soksi za miguuni hivyo kusitisha mchezo kuanza. Wachezaji wa timu hii wanategemea ufadhili na usaidizi kutoka kwa wengine licha ya kwamba walijua kuwa walipaswa kucheza. Inabidi waombe usaidizi kutoka timu ya Tanda ili mchezo uanzishwe.

Baadaye, mtunzi anatupeleka katika tendo linalohusu mchezo wa Mahaba Kaburini unaodhihrisha ukengeushi mkubwa maishani mwa wahusika wake. Tanda anakuwa mwanamume huku Beluwa akiwa mwanamke. Tanda anadai kwamba anampenda Beluwa hata anamkumbatia na kutaka kumusu. Tanda anakiri kwamba tabia ya kupenda mwanamume mwenzake kama mke ilitokana na kusoma kwake kwa mabuku, majarida, mtandaoni na kutangamana na watu kutoka kwa nchi mbali mbali. Mahusiano haya yanasababisha kupangwa kwa harusi ya kifahari inayohusisha watu wenye hadhi na hata wanaotoka mataifa mengine. Licha ya kuwa wahusika hawa bado wako gerezani, wanajiona kuwa matajiri waliokuwa na uwezo mkubwa wa kupanga harusi ya kifahari.

Kutokana na tendo hili, Tanda anabadilika na kuwa Kasisi anayewaunganisha kama Bw. Harusi (Tanda) na Bi. Harusi (Beluwa). Baadaye Beluwa anasaliti Tanda kwa kubadilisha mapenzi yake kwenda kwa Mtu, ambaye alikuwa mmoja wa watuhumiwa kutoka Mashariki. Beluwa alionyesha kuwa Tanda alikuwa mtupu kwa kuimba wimbo wa ‘domo tupu’. Utupu huu ndio uliomfanya Beluwa kumtoroka Tanda.

Baadaye, tunaonyeshwa hali ilivyo kwenye nchi ya Azania, ambapo tunaonyeshwa kwamba nchi hiyo imejaa ulaghai, wanahitaji kuimarisha magereza na kuombea mvua. Tanda ndiye anaigiza Mwanahabari aitwaye Zaida pamoja na ripota, Tamimu. Wahusika hawa wanatazama taarifa kwenye runinga ya kinjozi isiyoonekana. Mtu naye anaigiza Rashia aliyekuwa mhojiwa wa ripota Tamimu kuhusiana na hali ya Jimbo la Makaburini.

Mtunzi anatamatisa mchezo huu kwa tukio linalotokea ndotoni mwa Beluwa. Tanda, Beluwa na Mtu wanajipata mahakamani huku Beluwa akiwa mshtakiwa, Tanda ni hakimu na Mtu akiigiza kiongozi wa mashtaka. Beluwa alishtakiwa kwa kosa la kuchochea na kuhusika katika mauaji ya halaiki. Kutokana na makosa haya mawili, anahukumiwa kwa kunyongwa mara mbili. Je mtu atanyongwaje mara mbili?. Tunaachwa katika hali ya taharuki kwa kuwa mtunzi hatuambii ikiwa Beluwa alinyongwa au alisamehewa.

3.3 Mlingano Kimaudhui katika Tamthilia ya *Amezidi na Beluwa*

Katika sehemu hii tumefanya uchanganuzi wa maudhui katika tamthilia ya *Amezidi na Beluwa* kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya ubwege. Aidha tulijikita katika kuchunguza mlingano wa mwelekeo wa kiubwege baina ya tamthilia hizi teule. Kando na dhana ya maudhui, tumeangazia dhamira, mandhari, suala la Mungu, ukengeushi na ukosefu wa uthabiti katika elimu.

3.3.1 Dhana ya Maudhui

Maudhui ni ujumbe kuhusu kitu, matukio, hali ya maisha au wahusika yanavyojitokeza katika kazi ya fasihi (Njogu & Chimera, 1999). Aidha, wanadai kwamba maudhui ni maana ya ndani ya kazi ya fasihi.

Naye Wamitila (2003: 189) anadokeza kwamba maudhui ni yaliyomo au ujumla wa masuala yanayoangaziwa katika kazi yoyote ya kifasihi. Kadhalika, maudhui huibuka kwenye ukuzaji na uendelezaji wa dhamira... Mtazamo huu unaifanya dhamira kuwa sehemu ya maudhui.”

Kwa upande wake Mbatia (2001), maudhui au yaliyomo ni jumla ya mawazo, fikra, dhamira na hisia zinazowasilishwa na kazi ya kifasihi, yanajibu swali la nini kazi ya kifasihi inazungumzia. Kijumla, maudhui ni jumla ya masuala au mambo yanayomulikwa katika kazi ya fasihi pamoja na dhamira ni sehemu ya maudhui kwa sababu huchangia katika kujenga masuala mengine ambayo hasa ndiyo maudhui.

3.3.2 Dhamira

Dhana ya dhamira imeshughulikiwa na waandishi tofautitofauti katika juhudi za kuifanya ieleweke. Masebo na Nyangwine (2008) wanaeleza dhamira kama wazo kuu au mawazo tofauti tofauti ambayo yanajitokeza katika kazi ya kifasihi. Wanaeleza kwamba dhamira hutokana na jamii. Kwa maoni yao dhamira huweza kuwa za kisiasa, kitamaduni na kiuchumi. Katika maandishi yoyote, tunaweza kuwa na dhamira kuu pamoja na dhamira ndogo.

Wamitila (2002) anasema kuwa dhamira hurejelea mada ya kazi fulani, ujumbe husika au lengo la kazi hiyo. Aidha, Wamitila (2008) anaeleza kwamba dhamira ni wazo kuu linaloitawala kazi ya fasihi kwanzia mwanzo hadi mwisho. Kwake mtaalam huyu, mwandishi anapoanza kutunga kazi ya fasihi, huwa anasukumwa na lengo fulani

hivyo msomaji atalazimika kuisoma kazi hiyo kwa makini na kuangalia ni wazo gani analolikuza au kuliendeleza mwandishi kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Aghalabu lengo hilo huweza kuakisika kwenye anwani ya kazi yake.

Kando na mawazo haya, tunakubaliana na Njogu na Chimera (1999) wanapotoa fasili ya dhamira kuwa ni sehemu ya maudhui; hivyo tumeifanyia uchanganuzi katika kama sehemu ya maudhui.

Kulingana na mkabala wa ubwege, tamthilia za kiubwege lazima zidhihirishe dhamira kwamba maisha yana uwazi usiokuwa na maana au hayana maana kabisa. Dhamira kama hii huweza kuundwa kupitia matumizi ya wahusika wa kinjozi, wahusika wa kiutopia, ukosefu wa mantiki, kutatizika kwa mawasiliano, kupotea kwa nafsi bila wokovu, mandhari duni (machafu) na mandhari ya kidhahania/kindoto.

Kwa kawaida fasihi ya kiubwege, hubeba dhamira inayoonyesha ubatili wa matendo ya binadamu katika ulimwengu anamoishi. Mara nyingi, wahusika wanaotumiwa huwa ni vibonzo ambao hawana uwezo wa kujielewa au kufikiria na hivyo hutekeleza yasiyo na maana. Binadamu anaonwa kama kinyago ambacho hakiwezi kubadilisha hali ya maisha yake duni. Vitendo vyao havina muwala na huonyesha ubatili; wanashindwa kutekeleza mambo kama vile kuwasha moto, kumenya mhogo, kuvua nguo au hata kupika. Kilicho cha maana kwa binadamu wa kiubwege ni kusubiri kifo ambacho ndicho hatima ya maisha yake yaliyojaa matatizo.

3.3.2.1 Dhamira katika *Amezidi*

Kulingana nasi, dhamira yake mwandishi wa *Amezidi*, Said Ahmed Mohamed, inaafikiana na dhamira ya mkabala wa Ubwege. Dhamira ya mtunzi katika kazi hii ni; Maisha ya kiubwege, ambayo yamejaa matatizo na yasiyokuwa na mantiki wala maana. Kutokuwa uwezo wa kubadilisha hali yao duni ya maisha, wahusika wake

Mohamed wanachorwa wakiomba msaada kutoka kwa nchi za kimagharibi (EC), lakini wanapewa msaada usioweza kuwa wenye manufaa kwao bali unaowaongezea matatizo chungu nzima.

Tukio linalodhihirisha hili linajitokeza wazi kwenye onyesho la nane ambapo, Ame na Zidi wanaonyeshwa wakiziba mapua kwa kuhisi uvundo wa mizoga kisha wanajishughulisha na kuimba wimbo wa kiubwege unaoonyesha kuwa hawana uwezo wa kubadili hali ya maisha yao duni. Baadaye, wanaonyeshwa wakihisi maumivu makali ya njaa na kugaragara chini, mara Pu! Msaada wa paja la nyama ya ng'ombe ya kuoza linawaangukia mbele yao kutoka nchi za kimagharibi, wanakosa kiberiti, mafuta na kuni ya kupikia nyama hii kisha wanalitafuna paja hilo mbichi. Vifungu vifuatavyo vinadhihirisha wazo hili;

Zidi: (anziba pua) Mmmmff

Ame: Nini?

Ame: Uvundo! (Anaziba pua)

Zidi: Mmmmff (Anaziba pua)

Ame: Harufu ya Mizoga

(Uk. 64)

...

Ame: Aaaaa; njaa!

Zidi: Njaa?

Ame: Njaa!

Zidi: Njaa?

Ame: Njaa!

Zidi: Njaaaaa! Aaaaa, naumia! (Naye anaanguka chini na kugaragara... wanafurukuta na kugaragara chini pamoja. Mara pu! Paja la nyama ya ng'ombe linawaangukia mbele yao. Haijulikani linatoka wapi.)

Ame: Ah, msaada (Ame pata nguvu alipoliona paja la nyama. Anainuka haraka)

Zidi: Msaada! (Anabwata) Ndiyo, msaada! ...

(Uk. 69)

...

Ame: msaada enh!

Zidi: Wana huruma, hawa EC!

Ame: Wana huruma enh...

Zidi: Mmmmff! (Anaziba pua na kuliachia paja la nyama lianguke chini.)

Ame: Nini?

Zidi: Linanuka Uvundo!

Ame: Uvundo?

Zidi: Limeoza

...

Ame: Huna kibiriti? Huna mafuta? Huna moto? Huna kuni?

Zidi: Kibiriti, mafuta, Kuni...Kwa nini havikuletwa na kige, hili paja la ng'ombe kutoka EC?

(Uk. 71)

...

Zidi:una meno?

Ame: N'na meno!

Zidi: Tuwe simba basi...

(wanalitafuna paja la nyama mbichi iliyooza)

(Uk. 72)

Mohamed alitumia kisa hiki ili kudhihirisha jinsi maisha ya wahusika wa kiubwege yalivyo. Wahusika wasiokuwa na uwezo wa kubadili hali mbaya ya maisha yao; yenye matatizo yasiyo na kikomo. Kwa kula nyama mbichi iliyooza bado wanajiongezea matatizo ya kiafya na hawatakuwa na uwezo wa kujinasua kutoka kwenye mtego wa ubwege wa maisha unaowazunguka.

Said Ahmed Mohamed alianza kuonyesha dhamira yake kuanzia Onyesho la Kwanza.

Suala la maisha ya kiubwege limeangaziwa katika onyesho hili, Ame na mwenzake

Zidi, wanajadiliana kuhusu mihogo iliyovunda, isiyofaa na mbinu ya kuitengeneza ili

waweze kuila. Baada ya majadiliano haya bado tunaonyeshwa wakishinda kikaka

mihogo hii wala kuichoma, na hatimaye wanajikuta wakilia tu ilivyo.

Haya yanajitokeza ifuatavyo;

Zidi: Mhogo uliovunda enh!

Ame; Mhogo tokea lini kuvunda?

Zidi: Ah, (anafanya kukumbukia kitu) kweli mhogo hauvundi Huambatwa na ukungu tu ambao ukiukwangurakwangura basi utalika...kwa hivyo mhogo...

Ame: Hauvundi (Uk. 5)

Ame: Na bora tuanze kuula sasa, maana kesho kuna Mungu...tena huu mhogo safi... bado haujavunda... (anacheka kwa kejeli)

Zidi: Haujavunda...haujavunda...mhogo haujavunda!...

Ame: Una kisu?

Zidi: Si unajua nyumba hii haina kisu?

...

Zidi: Aaa, usiri bwana-ukisema utanunua leo...kesho...kutwa hata...
 (anatafuna mhogo wake mbichi naye)
 (Uk.11)

Maisha ya binadamu yanapolinganishwa na wanyama wanaotafuna mizizi mbichi ni kipengele cha ubwege. Mwanadamu amepotea sana na amejiingiza katika ulimwengu wa kinyama. Wanyama wamekosa uwezo wa kuboresha hali ya maisha yao kama tunavyowapata Ame na Zidi ambao, tunaonyeshwa kwamba hawana kisu, wala kijiti hata kiberiti ambavyo vingewasaidia kutengeneza mihogo na inawalazimisha kuila kinyama; hivyo kudhihirisha maisha ya kiubwege katika ulimwengu katili.

3.3.2.2 Dhamira katika *Beluwa*

Pauline Kea kwa upande mwingine, amedhamiria kutoa wazo la Uhuru wa binadamu wa kiubwege; kwamba binadamu ana uhuru wa kujitafutia furaha licha ya kwamba matatizo yanayomsibu hayaonyeshi dalili za kukoma. Mtunzi huyu ametupatia picha ya jinsi ambavyo binadamu wa kiubwege anajitafutia uhuru na anatoa hatua ya “kuwako” ambapo wahusika wanajikuta gerezani na kuulizana kilichowafikisha humo. Kadhalika, katika onyesho la tatu tunaonyeshwa kwamba Ame na Zidi wamo uwanjani, wakitaka kucheza kandanda lakini timu ya Beluwa inaonyeshwa kukosa soksi za kucheza, hivyo wanasaidiwa na timu ya Tanda.

Uhuru wa binadamu wa kiubwege kama ulivyoangaziwa na mtunzi huyu unajitokeza wazi kupitia mchezo wa “Mahaba Kaburini”; ambao unajitokeza kuanzia Onyesho la Nne na Tano. Mtunzi aliwachora wahusika wake wakiwa na uhuru wa kujitafutia furaha kupitia mhusika Tanda ambaye, alihitaji starehe ya kimapenzi licha ya kwamba walikuwa gerezani. Mhusika huyu anatongoza mwenzake; Beluwa ambaye ni wa jinsia ya kiume na kuonyesha hisia zake za kimahaba kwake. Waaidha, katika

onyesho la tano, wanajihusisha katika uandalizi wa harusi ya kifahari licha ya kuwa gerezani, kwenye chumba cha futi kumi, mraba. Kinachojitokeza ni kwamba binadamu ana uhuru wa kufanya mapenzi/ngono kwa jinsia sawa (Ubasha/Ushoga).

Vifungu vifuatavyo vinadhihirisha wazo hili;

Tanda: Kwa nini mwandani wangu?

Beluwa: Mwandani, ndani ya nini? Baada ya kukoroma na kunikosesha amani.

Tanda: Pole, mwenzio sikunua, ni kwamba ninaumwa... (Anashika moyo na kufanya kama ambaye anahisi maumivu)

Beluwa: Nini tena? Unaugua nini?

Tanda: (Kwa unyonge zaidi na kwa sauti ya chini) Mtima, mtima wangu wafa!

Beluwa: Usife bwana, acha nimwite askari akupeleke hospitalini

Tanda: Wee! Wee! Wee! Sitaki daktari mwingine. Wewe wanitoshia.

(Uk. 34)

Dondoo hili linaonyesha jinsi ambavyo mhusika Tanda alivyoanza kuonyesha hisia zake za kimapenzi kwa Beluwa. Anamwambia kwamba mtima anaumwa mtima lakini hataki daktari kwa vile Beluwa ndiye dawa yake; kwa kukubali kufanya mapenzi naye. Kiubwege, Tanda ameshagundua kwamba yeye ni binadamu wa kiubwege na hivyo hawezi kubadilisha hali yake hivyo, anajitafutia uhuru na starehe za kutuliza nafsi yake. Kifungu kifuatacho pia kinaonyesha hisia zake Tanda;

Tanda: ... Pendo nililo nalo halijawahi kushuhudiwa.

Nami sitajizuia kuwa nawe popote niendapo, kwa kuwa ninakupenda. Ninataka nikuo, Beluu. Nipe Chanda chako nikuvishite pete ya mapenzi yaliyoufurika moyo wangu. (Beluwa anakataa kumpa Chanda) Ninataka uwe wangu milele hata kifo kisitutenganishe. Tuwe pamoja hata tuwapo kaburini.

(Uk. 38-39)

Licha ya kwamba Tanda anajitafutia uhuru, furaha na starehe za kiubwege, anatambua kwamba mwishowe kuna kifo (Kaburini); ambacho ndicho hatima ya binadamu wa kiubwege. Hii ndiyo maana anasema kwamba anataka Beluwa awe wake milele hata wakiwa Kaburini; yaani uhuru wanao lakini mwishowe watafika kaburini. Hiki ni kigezo muhimu sana katika nadharia ya ubwege.

Tanda: Mahaba yananipagawisha,
 Mahaba yananilewisha,
 Mahaba yananihangaisha.
 Njoo, Beluwa, njoo kwangu
 (Uk. 40)

...

Tanda: Njoo, njoo uniondolee janga hili.
 Njoo nikushike, nikumbatie, niku...
 (Anamshika Beluwa mara moja na kutaka kumbusu. Beluwa
 anamsukuma na kumwangusha)

Tanda: (Analia kwa maumivu huku akijishikilia moyo) Ooh! Ooh!

Beluwa: (Kwa ukali) Unataka kunifundisha nini wewe? Ushoga,
 Usege au uhayawani?

Tanda: (Kwa ukakamavu) sasa unajitia kutojua mambo haya?
 Unaishi sayari gani? Get serious, drama si fani yako!

Beluwa: Kwa hivyo wewe ni Gay? (Kimya kidogo)

Tanda: Unangoja jibu?

Beluwa: La! Dalili ya mvua ni mawingu. (Uk. 41)

Vifungu hapo juu vinaonyesha dhahiri kwamba mtunzi ametumia Ubasha/ushoga katika kuwapatia uhuru wahusika wake wa kiubwege. Hata kama walichorwa wakiwa kwenye mazingira ambayo hayakufaa mahaba; mazingira machafu yasiyofurahisha, bado wahusika hawa wanafanya juhudi za kujaribu kujipatia uhuru kwa kujistarehesha kimapenzi, licha ya kuwa wa jinsia sawa.

Aidha, wahusika hawa wanabuni mazingira ya harusi ya kifahari; harusi ya kimataifa Katika onyesho la tano, ambapo Tanda anakuwa Bwana harusi na Beluwa anakuwa Bibi harusi. Wahusika hawa wanatarajia wageni kutoka pembe zote za dunia na wanatarajia kwamba sifa za harusi ya zitagonga kwenye vyombo vya habari. Dondoo lifuatalo linadhihirisha haya;

Tanda: ... Wajua harusi yetu itakuwa ya kukata na shoka, yaani harusi ya kimataifa. Wageni watafika kutoka pembe zote za dunia. (Anazunguka kuonesha pembe zote). Lazima sifa za harusi hii zigonge kwenye vyombo vya habari.

Beluwa: Tayari tutakuwa mke na mume. Cha kututenganisha ni mauti tu!

Tanda: (Anashtuka) La! Kaburi.

Beluwa: Hilo kaburi na kifo kwangu havina tofauti ...
 (Uk. 49)

Kwa kifupi tu ni kwamba, Pauline Kea anatambua uhuru alionao binadamu wa kiubwege; kwamba anaweza kufanya chochote wakati wowote ili kupambana na hali yake ya maish duni ambayo hatima yake ni kifo. Uhuru wa binadamu wa kiubwege ni kipengele ambacho pia kiliangaziwa sana na Albert Camus alipoweka msingi wa Uwege katika *The Myth of Sisyphus*.

Mlingano uliomo baina ya tamthilia hizi teule kwa kuangazia dhamira hutokana na maisha duni ya wahusika; maisha ya kindoto. Wanaishi maisha ya kiubwege na wamekosa nguvu za kubadilisha hali yao ya maisha duni, hivyo inawalazimu kukubali ubwege wao, kubuni maisha yasiyo ya ukweli na kusubiri hatima yao ambayo ni Kifo.

Katika *Beluwa*, licha ya kwamba Tanda na Beluwa wamo gerezani, Rumande kwenye chumba cha futi kumi mraba, wanapewa uhuru wa kujitafutia starehe za kiubwege na furaha ya kindoto ili kudhihirisha kwamba wamekubali kupambana na maisha ya kiubwege; ambayo hawana uwezo wa kuyabadilisha. Vile vile, haya yanajitokeza katika *Amezidi* ambapo Ame na Zidi wanaonyeshwa wakiwa tu kama vikaragosi visivyoweza kutekeleza chochote. Wanapata msaada wa paja la nyama ya ng'ombe iliyoza na kukosa njia ya kuichoma hivyo inawalazimu kuila ikiwa mbichi. Kisa hiki kinaonyesha kwamba wahusika hawa wameshakubali hali yao duni; ambayo imewashinda kubadilisha hivyo wanasubiri tu hatima yao. Kwa kula nyama mbichi iliyoza; ambayo ilikuwa msaada tu kwa kukosa kibiriti, mafuta na kuni ya kuipikia ni ubwege. Hali hii ya ubwege hujitokeza kutokana na kukosa kuridhika kwa akili kulingana na matarajio ya binadamu juu ya utaratibi wa matukio katika ulimwengu.

Kwa kuongozwa na mhimili wa ubwege kwamba tamthilia za kiubwege huonyesha maisha yamekosa maana, tunakiri kwamba tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* zinamulika suala la ukosefu wa maana ya maisha ya binadamu wa kiubwege. Watunzi

wa kazi hizi wanaonyesha kuwa ikiwa binadamu ameshindwa kujikomboa kutokana na ukatili wa dunia isiyomjali, basi maisha yamekosa maana na kinachobaki ni kusubiri kifo ambacho ndicho hatima yake. Kiubwege, hakuna hata maana moja ya maisha na hatuwezi kutengeneza moja pia. Tunakubaliana na Camus anaposema kwamba haiwezekani kwetu kupata jibu la kuridhisha kwa swali la maana ya maisha, na jaribio lolote la kulazimisha ulimwengu kuwa na maana litaishia kwa msiba. Ni kweli kuwa mtu anayeweza kufahamu na kukubali ukweli kwamba maisha ni ya kiubwege na hayana maana, hivyo akayapitia kwa tabasamu, ni shujaa wa kiubwege.

3.3.3 Mandhari

Dhana ya mandhari inahusishwa zaidi na kazi za tamthilia kwa sababu hudhihirisha mazingira ya kijiografia ambapo tukio linatukia, kipindi cha wakati pamoja na mawanda ya kisa husika.

Mbatia (2001) anahusisha mandhari na drama moja kwa moja anapoeleza kwamba, mandhari ni istilahi inayohusishwa na utunzi wa tamthilia. Aidha anabaini kwamba mandhari yanarejelea sura mahususi ambayo hutokana na mapambo na vifaa ambavyo vimepangwa jukwaani. Sura hiyo huwa imedhamiriwa kuiga mazingira halisi yanayoelezwa katika tamthilia inayoigizwa. Mazingira kama hayo yanaweza kuwa nyumbani, njiani au kwenye uwanja wa vita. Hoja hili linaungwa mkono na Mwari, A. (2018) katika tasnifu yake anapoeleza mandhari kwa kuyahusisha na utendaji wa kidrama. Anadai kwamba mandhari ni mazingira ya utendaji. Anaendelea kueleza kwamba ni yale mambo katika kazi ya kifasihi yanayomwezesha anayesoma hiyo kazi kutambua ni mahali na wakati gani mambo yanayowasilishwa yanatukia.

Naye Gill (1985) anafafanua mandhari kama dhana pana na jumuishi. Mawazo yake yanaungwa mkono na Wamitila (2008) ambaye, katika maelezo yake kuhusu

mandhari anajumuisha dhana za mazingira, mawanda na wakati. Kwake Wamitila, mandhari sio mazingira ya kijiografia tu bali hurejelea masuala mengine kama kipindi cha wakati wa matukio kama unavyodhihirishwa na wahusika wanavyotenda.

Katika kazi hii, tumechukulia mandhari kama kipengele muhimu cha kuendeleza maudhui katika tamthilia ya kiubwege. Tunakubaliana na Murungi (2013) katika tasnifu yake anapodokeza kwamba, mandhari huwa ni kegezo muhimu sana katika uchanganuzi wa maudhui. Sababu ya kimsingi ni kwamba, matukio kwenye kazi ya fasihi na maudhui yanayosimuliwa hutendeka mahali, wakati na katika mwanda fulani. Nafasi ya mandhari katika kazi ya kifasihi hutegemea nafasi yake katika uendelezaji wa maudhui. Kwa mfano, ikiwa tamthilia inawasilisha masuala ya kijamii, sharti mandhari yawe mandhari bayana kijamii ili kutia uzito uthabiti wa kimaudhui. Madai haya yana uzito kwa kuwa tamthilia ya kiubwege lazima idhihirishe mandhari duni, chafu yanayokatisha tamaa ili kudhihirisha ukatili wa ulimwengu anamoishi binadamu wa kiubwege; ulimwengu wa kindoto usio na matumaini ya ukombozi.

Mbatiah (1997) anasisitiza umuhimu wa mandhari ya fasihi ya kiubwege kwa kusema kwamba watunzi katika mkabala wa ubwege, hutumia mandhari ili kudhihirisha msimamo wao kuwa ulimwengu ni duni, wa kinasibu, wa kukatisha tamaa na huzua hisia za huzuni, uchovu na ukosefu wa matumaini.

Kijumla, tunadokeza kwamba mandhari ya kiubwege huwa ni ya kindoto na yamo akilini mwa wahusika; wahusika hubuni mazingira ya kidhahania yasiyokuwepo. Aidha, mazingira hayo ya kiubwege hutumiwa kuonyesha kuwamaisha ya binadamu ni duni: ni yale yalijaa matatizo yasiyoweza kuepukika.

3.3.3.1 Mandhari katika *Amezidi*

Mandhari yaliyotumiwa katika *Amezidi* ni mandhari ya kidhahania. Mohamed ametumia mandhari ya Pango kuanzia onyesho la kwanza hadi onyesho la kumi, lakini wahusika wake wamebuni mandhari mbali mbali ya kidhahania ili kuonyesha uhuru wa binadamu wa kiubwege, msingi uliowekwa na Albert Camus (1942). Pango kuchukuliwa kama Kasri huwasilisha hali maisha ya binadamu wa kiubwege. Licha ya kuwa kwenye Pango; maisha ya ufukara, wahusika hawa wanabuni mandhari ya Kasri iliyopambwa kwa vifaa vya thamani. Mtunzi huyu anapoonyesha wahusika wakidai kuwa pango lao ni kasri inamaanisha kwamba jamii ya kiubwege inaishi katika umasikini lakini imeridhika na hali hiyo; binadamu wa kiubwege sharti akubali ubwege wake na kujitafutia uhuru wa kiubwege; ambao ni maisha ya kindoto. Haya yanajitokeza wazi katika onyesho la pili tunapoambiwa;

Ame: Kama umepata kuikagua kwa macho nyumba hii yetu...

Zidi: Humu pangoni?

Ame: Pangoni ama kasrini mwetu?

Zidi: Ah, kasri ndiyo, kwani ina nini?

Ame: Ukubwa wake...nafasi yake...mapambo yake...samani zake...vitu vyake vyote kwa ujumla! (uk.12)

Mohamed amewapa wahusika wake uhuru wa kubuni mandhari ya kidhahania; kasri kubwa iliyopambwa kwa samani na vitu vya kifahari. Ni kweli kwamba hatuwezi kuwa na vifaa vya kifahari kwenye pango; hii ni ndoto ambayo ni kipengele muhimu sana katika tamthilia za kiubwege.

Wahusika hawa wanaanza moja kwa moja kuvitaja vitu vilivyomo kwenye kasri pamoja na Nchi za mbali mbali ambazo zilitolewa, tunaambiwa;

Zidi: Ah, usitajie hayo...Tazama kwa mfano hili sofa la mahmeli ninalolikalia mimi (anamwonyesha mwenzake) na hilo unalolikalia wewe, na lile pale la tatu... masofa ya kijimwaya na kujimwaga...masofa ya kifahari na kitajiri tuliyoyaagizia...tuliyoyaagizia kutoka...kutoka...kutoka wapi vile? (anauliza kwa dhati kabisa)

Ame: wapi vile? (Anababaika)
 Zidi: Si Paris vile?
 Ame: Enhe, Paris ndiyo!
 Zidi: Ndiyo Paris
 Ame: Ah, Paris mji wa fenicha , mji wa mapambo, mji wa silka, mila na utamaduni...mji wa sayansi na teknolojia...tulikuwa tukisoma vile au siyo?
 Zidi: Sawa –tulipokuwa tukisoma...na hili meza kubwa la mpingo linaloanza hapa mpaka kule nje? (anaonyesha ukubwa wa meza kwa ishara tu lakini meza lenyewe halipo)
 Zidi: Ah, hii meza ya kahawa, enhe?
 Ame: Na kweli umenikumbusha... kahawa tuliyowekewa na mtumishi wetu inapoa...na keki, vileja na visheti...na tule Ame... (Uk.13)

Wahusika hawa wanaonyeshwa wakiishi maisha ya kistarehe yasiyo na tatizo lolote; wao ni matajiri ambao wana uwezo wa kuajiri watumishi wanaowaandalia vyakula rojorojo. Vyakula wanaoandaliwa wahusika hawa kama vile keki na vileja si vyakula vya masikini, hii inaonyesha kwamba wahusika hawa wamebuni vyakula hivi ili kudhirisha kwamba binadamu wa kiubwege sharti akubali hali yake na kukubali ndoto kutawala maisha yake. Hebu tuangalie aina ya zulia tunayopewa hapa, tunaambiwa;

Ame: Vipi hili zulia?
 Zidi: Zulia si limetoka Iran?
 Ame: Iran...nchi maarufu kwa mazulia yake...
 Zidi: Hebu...(anapeleka mkono kwenye zulia la ndoto) peleka mkono wako upapase mwili wake...shaari zake nyororo...ahhhhhh, raha...raha tupu...zinateleza laini. (Uk. 13-14)

Kwa kawaida mazulia kutoka Nchi za nje ni ya gharama ya juu na huweza tu kuagiziwa na watu matajiri. Mazulia kama hayo hupendeza sana. Tunaonyeshwa kwamba wahusika wa Mohamed wamepamba sakafu yao kwa zulia yenye bei ghali na ya kupendeza sana. Tazama makabati ya vioo, mabakuli, vitu vya mapambo, marashi na Televisheni tunayopewa hapa;

Zidi: Na yale makabati ya vitabu toka mtemu hadi mtemu...
 Ame: nay ale mabakuli ya fedha juu yake yanayobeba makocha na mashada ya maua mchanganyiko...

Zidi: Na ndani ya vile vioo vya makabati hayo, vile vitu vya mapambo...saraka ya juu, midele na marashi ya dhahabu...

Ame: Na ile pale TV na video yake imesimama pembeni...sijui tukaifungue kidogo? (Uk. 14)

Mandhari haya ya kasri ni ya kindoto; ambayo wahusika wamebuni ili kuonyesha uhuru wao kama wahusika wa kiubwege. Wahusika wanaonyesha vitu visivyokuwepo, visivyoweza kuonekana wala kuguswa. Kasri lao ni la kufikirika tu ndiposa Mohamed anatanguliza onyesho kwa kutaja kwamba;

Tendo hili lote linatokea ndotoni mwa Ame na Zidi...pahala ni pale pale pangoni. (Uk.12)

Kukubali ubwege kunamaanisha kukubali magumu yote ambayo ulimwengu unatupa. Bila maana maishani, hakuna kiwango cha maadili, kinachozingatiwa sio kuishi bora zaidi bali kuishi zaidi. Kwa kubuni mandhari ya kasri wahusika wanajitafutia furaha baada ya kukubali maisha yao ya kiubwege. Kiubwege kila kitu kinaruhusiwa, si mlipuko wa kitulizo au furaha, bali ni kukiri kwa uchungu ukweli; yaani kukubali ukweli hata kama ni chungu. Matumizi ya mandhari dhahania katika kutunga tamthilia ya kiubwege ni kipengele muhimu sana; hivyo mhimili wa mandhari dhahania umeongoza uchanganuzi katika sehemu hii.

Waidha, mandhari ya kiubwege yanadhihirishwa na tukio la shuleni kwenye onyesho la nne. Mandhari tunayopata hapa ni ya kindoto, vifaa vya kufanikisha masomo yanafikiriwa tu kwamba vipo lakini havionekani. Tunaambiwa;

Tendo limo fikirani...pangoni...tendo la shuleni. Zidi ni mwalimu, kaketi mbele ya meza ambayo haionekani. Pana ubao na chaki ambavyo pia havionekani. Ame (mwanafunzi) ameketi kwenye deski lisiloonekana pia. Kuna wanafunzi wapatao sabini. Pia hawaonekani ila Ame tu! Mwalimu Zidi anasinzia huku darasa limejaa zogo la wanafunzi...kitambo...kisha kengele inasikika kulia... Mwalimu Zidi anashtuka kutoka usingizini... (Uk. 29)

Suala la kubuni tukio akilini au fikirani ni ubwege, kutumia vifaa visivyoonekana hudhihirisha maisha ya kidhahania; ambao ni mhimili wa nadharia ya ubwege. Aidha,

kuwepo kwa zogo katika mazingira ya shuleni hudhihirisha ukosefu wa uthibiti wa elimu; mazingira ya kukatisha tamaa. Mazungumzo baina ya Mwalimu na wanafunzi huonyesha kwamba mazingira ya elimu tunayopatiwa hapa hayawezi kutekeleza shughuli hiyo kikamilifu bali yanazidisha matatizo maishani mwa binadamu wa kiubwege. Mwalimu na wanafunzi wanatumia mazungumzo ya kubwabwaja na kidhahania toka mwanzo hadi mwisho; mara mwalimu anaulizwa maswali asiyoyaelewa, anashindwa kuwaelekeza wanafunzi na hatimaye kubadilisha somo la Fizikia kuwa la Muziki. Hii huashiria kutojifahamu kwa binadamu wa kiubwege na hata kutoelewa uhusiano baina yake na binadamu wenzake.

3.3.3.2 Mandhari katika *Beluwa*

Kyovi kwa upande wake ametumia mazingira ya gerezani ndani ya chumba cha takriban futi kumi mraba; rumande. Kwa kawaida rumande si mahali pazuri ambapo shughuli za kifahari huweza kutekelezwa lakini tunapata harusi ya kifahari ya kimataifa ikiandaliwa na Tanda na Beluwa. Tanda anasema haya;

Tanda: ...wajua harusi yetu itakuwa wa kukata na shoka, yaani harusi ya kimataifa. Wageni watafika kutoka pembe zote za dunia (anazunguka kuonesha pembe zote) Lazima sifa za harusi hii zigonge vyombo vya habari... (Uk.49)

Tanda: ...sawa basi,nafasi mbili kwa marafiki. Mimi watu wangu wote watahudhuria. Baba, mama, ndugu na marafiki watakuwepo, lakini pia sitaki wengi sana. Harusi hii si ya every Tom, Dick and Harry. Itahudhuriwa na wateule wachache wenye ushawishi mkubwa. Majina ambayo yakitajwa yanatikisika. (Uk. 53)

Kutokana na haya, tunapatiwa mandhari ya harusi ya kindoto; ambayyo itakuwa ya kufana sana na itatangazwa kwenye vyombo vya habari. Harusi ambayo inawekwa kwenye kiwango cha kutangazwa kwenye vyombo vya habari ni harusi ya kifahari na inayothaminiwa na watu walioheshimika ulimwenguni. Hivyo wahusika Tanda na Beluwa wanajipatia uhuru wa kiubwege kwa kuonyesha uwezo wa kuandaa harusi ya

kifahari ya Kimataifa. Aidha, harusi hii iliweka mipaka ya wanaohudhuria. Wageni mashuhuri na walio na majina ya kutikisika yakitajwa ndio wanapaswa kuihudhuria harusi hii. Mandhari ya harusi hii ni ya kidhahania; kindoto kwa sababu harusi ya kufana kama hii haiwezi kusherekewa gerezani kwenye Rumande; mahali pachafu penye harufu mbaya. Nafasi ya chumba hicho pia ni ndogo na haiwezi kufanikisha shughuli ya harusi ya kifahari ya kimataifa. Mandhari ya kidhahania ni mhimili ya kiubwege na umejitokeza wazi katika tukio la mahaba kaburini na kuanikwa kupitia kisa cha harusi ya kifahari ya kimataifa.

Licha ya kwamba mtunzi alitumia mandhari ya gerezani kwenye rumande; chumba cha takriban futi kumi mraba, tunawapata wahusika wakibuni mandhari mbali mbali mawazoni ili kuendeleza maudhui katika kazi hii. Dai hili linathibitishwa na maelezo ya Kyovi katika utangulizi wa *Beluwa*, anadokeza kuhusu mandhari ya mchezo kwa kusema kwamba, mchezo huu unaigizwa gerezani, ndani ya chumba; rumande. Wahusika wanabuni mandhari mbali mbali wakiwa mumo humo rumande.

Mandhari ya kiubwege pia hudhihirishwa kutokana na zogo au fujo. Ni mazingira yasiyo na utulivu; matukio hujitokeza tu kiholela bila mpangilio. Hebu tuangalie onyesho la tatu, ambapo tukio la mchezo wa kandanda linajitokeza. Tanda anamwamsha Beluwa ambaye alikuwa amelala fofofu kwa fujo. Aliyelala usingizi wa pono si vyema akiamshwa kwa fujo lakini haya yanajitokeza katika ulimwengu wa kiubwege ili kukuza uhusika wa wahusika wa kiubwege. Kwa mfano tunaambiwa;

Tendo linatokea pale pale ndani ya chumba, rumande. Beluwa amelala usingizi wa pono kitandani. Tanda anatengeneza mpira kwa karatasi anazotoa ndani ya furushi. Anapomaliza anamwamsha Beluwa kwa fujo.(Uk. 15)

Mazingira ya kidhahania na iliyojaa fujo au zogo, ni mhimili ya nadharia ya ubwege; ambao huthibitisha kwamba vitendo vya mhusika wa kiubwege hukosa muwala wala

umuhimu wowote ila huonyesha ubatili mtupu. Waaidha, karibu maonyesho yote katika tamthilia hii yanatamatishwa kwa fujo. Mara wahusika wanashikana ukosi wa shati na kuanza kumenyana, mlango wa chumba chao unagongwa kwa nguvu na kila mmoja anajikunyatia kwenye pembe yake, mara mhusika mmoja anamrukia mwenzake na kumwangusha kisha wanamenyana, mara Tanda anampiga teke Beluwa na chakula chake kinamwagika. Haya ni matukio yanayoonyesha mazingira yasiokuwa na usalama na amani. Ni kweli kwamba ubwege si kitu kinachogusika bali ni uhusiano wa kidhahania kati ya akili iliyopevuka na ukweli wa wa kuwako kwa binadamu katika ulimwengu katili. Hali ya ubwege hujitokea kwa sababu ya kukosa kuridhika kwa akili kulingana na matarajio yake juu ya utaratibu wa matukio katika ulimwengu. Matarajio hayo yasipofikiwa ndipo binadamu anajipata katika hali yenye fujo.

Binadamu anaishi huku akiwa na woga wa kitakachotokea kighafla; yaani hata yeye mwenyewe hayaelewi mazingira yake hukosa uwezo wa kuyaboresha hivyo, inamlazimu kuyazoea na kujipatia uhuru wa kiubwege ambao ni maisha ya kindoto.

Kiubwege, mligano uliomo baina ya *Amezidi* na *Beluwa* kimandhari ni matumizi ya mazingira dhahania. Wahusika katika kazi hizi wamepewa uwezo wa kubuni mazingira mbali mbali ili kufanikisha kujenga, kukuza na kuendeleza maudhui ya kiubwege. Ifahamike kwamba kukubali ubwege kunamaanisha kukubali magumu yote tunayoyapata ulimwenguni. Kwa vile maisha hayana maana, basi binadamu wa kiubwege anapewa uwezo wa kujitafutia uhuru wake binafsi kwa kuishi maisha ya kindoto; ambalo ni suala muhimu sana katika nadharia ya Ubwege.

3.3.4 Suala la Mungu (Dini)

Dini ni kama imani inayohusiana na kuwepo kwa Mungu au miungu (Mdee 2011). Katika Kamusi ya TUKI (2004), Didi ni Imani ambayo inahusiana na mambo ya kiroho kwamba kuna muumbaji aliyeumba ulimwengu na ndiye mtawala wa kila kitu kilichomo ulimwenguni. Aidha, ni mfumo wa kuabudu, kusali na kuheshimu huyo muumba.

Katika mkabala wa kiubwege, dini ni kile chombo kinachomtuliza na kumliwaza binadamu anayeteswa na ulimwengu katili binadamu wa kiubwege anaposhindwa kutekeleza wajibu wake katika ulimwengu, anapitia mateso na hatimaye kukata tamaa ya maisha. Hivyo, anapokuwa matarajio ya usaidizi, analazimika kuota na kuwazia juu ya nguvu fulani ambayo inaweza kumwokoa, nguvu ambayo inazidi unyonge wake (Mungu).

Kama tulivyojadili katika sehemu iliyotangulia, kuna mitazamo mitatu kuhusiana na suala la kuwepo kwa Mungu. Kuna kundi linaloongozwa na Fredrich Nietzsche; ambalo linashikilia kwamba Mungu hayupo. Hii hutokana na matatizo yanayomkumba binadamu. Wanadai kwamba Mungu angekuwepo, binadamu hangekuwa anayapitia mateso anayoyapitia sasa. Halikadhalika, kundi linaloongozwa na Soren Kierkegaard ambalo linashikilia kwamba Mungu yupo na anatambua mateso ya binadamu. Aidha, kundi hili linashikilia kwamba binadamu hufarijiwa kutokana na mateso yake kupitia kwa nguvu zinazomzidi (Mungu). Kadhalika, kundi la tatu linahusishwa na Jean-Paul Sartre ambaye hakuonyesha msimamo thabiti kuhusu suala la uwepo wa Mungu. Alianza kwa Imani kwamba Mungu hayupo; amekufa, lakini baadaye akachukua mwelekeo wa ukristo hata akaita Mkuani wa kidini alipokaribia kifo chake.

Said A. Mohamed anamtambua Mungu katika utunzi wake wa *Amezidi*. Alianza kwa kumtanguliza Mungu katika utunzi wa kazi hii. Katika kianzio chake kwenye wimbo wa Mzee, tunapata;

...Nimeishi kusikia Mengi, pia nimedanganywa kwa mengi.
Mwanzo nilibeba dunia zito ;kadhani ni mzigo alionipa. Nikawa na kukidhi matakwa yake...(Uk.2)

Kwake huyu mzee, alibeba matatizo ya dunia na kuyavumilia akidhani kwamba ni huduma aliyopewa na kiumbe kilicho zaidi yake; Mungu. Anakiri kwamba alikuja kutambua kwamba mzigo huo alipewa na binadamu wala si Mungu, hivyo aliamua kuutua. Kutokana na haya, ni dhahiri kwamba Mohamed, anampa Mungu nafasi ya kwanza na kukubali kwamba kuna nguvu inayomzidi.

Kadhalika, Ame na Zidi wanapozidiwa na maisha yasiyo na mbele wala nyuma, wanatazamia usaidizi wa Mungu. Wanapokumba na haja ya kufanya kazi au mateso ya njaa, wanajaribu kusingizia msaada kutoka kwa Mungu. Katika onyesho la Kwanza tunaambiwa:

Zidi: lakini haina haja kuomba, si tuna mhogo wetu?
Ame Mhogo au Ruzuku ya siku moja?
Zidi: Sikiliza Bwana, kesho kuna Mungu!
Ame: Na bora tuanze kuula hasa, maana kesho kuna Mungu...(uk.9)

Aidha, mfano ufuatao unaonyesha jinsi ambavyo wahusika hutamani kifo ambacho wanaamini kitawafikisha kwa Mungu na wataokolewa kutoka kwa mateso ya Dunia.

Zidi: si wewe utanifuata? Ili tukutanie huko?
Ame: wapi?
Zidi: kuzimu!
Ame: Kuzimu nakuogopa!
Zidi: kuna nini?
Ame: Kuna shida!
Zidi: Hapana, hakuna shida...shida ipo duniani tu! Kuzimu kuna raha tu! (anacheka huku kajikamata tumbo)
Ame: kufa raha?
Zidi: Ndiyo, kufa ni raha; si ndiyo maana sisi tumekuwa tukikutafuta siku zote hizi? Tulikuwa tukikuhimiza kuje haraka haraka!
(Uk. 79)

Kutumainia Imani za Mungu pia hujitokeza katika ‘Wimbo wa mtoto Asiyezaliwa’. Tunapewa dhana ambayo inapatikana katika vitabu vitakatifu. Kupigwa kwa baragumu siku ya kiyama itakapofika, inasemekana watu wote watakuja mbele zake Mungu ili kuhukumiwa. Aidha tunaimbiwa kuwa hiyo siku ikifika, maiti yote itafufuka, huu ni ujumbe wa kibiblia. Mtunzi anasema;

Huo mwisho ukifika, maiti wote watafufuka
 Vipofu wataona, visiwi watasikia,
 Mabubu watasema, vichaa watatengamaa
 Wajinga ‘tarevuka na wal’olala ‘taamka
 Baragumu ‘tapolia. (uk. 86-87)

Halikadhalika, katika tamthilia ya *Beluwa*, mwandishi Pauline Kea ameonyesha imani ya kidini kupitia kwa mhusika Beluwa. Mwandishi huyu vile vile ameangazia suala la kuwepo kwa Mungu kwa mfano;

Beluwa: kaburi nalifahamu na ndio, ninaota. Lakini sioti ndoto tena.
 Ninaota mawazo yanachipuka mapya motomoto! sikuyajua
 yalivyo, mpaka nilipooneshwa na roho.
 Tanda: Roho gani?
 Beluwa: Roho mtakatifu...
 (Uk. 66)

Kutokana na Dondoo hili, mtunzi amedhihirisha msimamo wake kuhusiana na Imani zinazotokana na dini ya kwamba roho mtakatifu ina uwezo wa kuonyesha binadamu mambo asiyoyafahamu, hivyo roho imepewa sifa ya kuwa na uwezo dhidi ya matatizo yanayomkumba binadamu. Wahusika hawa wamechorwa kama wale wasio na mipango ya kubadili hali zao za maisha hivyo, baada ya kuota ndoto ambazo hazitimizwi, wanalazimika kutuliza roho na nafsi zao kupitia kwa imani ya kidini. Beluwa anadai kuwa ameonyeshwa ndoto na Roho mtakatifu na kuamini kuwa hatimaye ndoto yake ya maisha itakuja kutimizwa na kuwa kweli.

Kutokana na haya, tunakubaliana na wataalam wa Ubwege kuwa fasihi ya ubwege hutekeleza wajibu wa kujaribu kubainisha ukweli maishani mwa binadamu

ulimwenguni. Fasihi hii inadhihirisha hali duni ya fikra za binadamu; ambazo zinamfanya binadamu kujaribu kutafuta ukweli, lakini fikra hizo zinamfanya asiupate. Kwa kukosa kujielewa, wanakimbilia nguvu inayowazidi; Mungu.

Kadhalika mtunzi ameonyesha mwelekeo wake kuhusu kigezo cha dini kupitia dondoo lifuatalo;

Beluwa: Basi wewe ni kafiri, unamjaribu Mungu.
 Tanda: Mimi si kafiri. Nina Mungu na dini yangu
 Beluwa: Mungu yule mmoja wa mbinguni?
 Tanda: Nani aliyekwambia Mungu yuko mbinguni? Yuko mumu humu, yupo kila mahali.
 Beluwa: (Akitalia) Hata makaburini?
 Tanda: Hasa Makaburini... (uk. 18)

Ifahamike kwamba katika mkabala wa ubwege, dini huwa kitu kinachomtuliza na kumliwaza binadamu hivyo, inatumiwa kumpatia binadamu matumaini kuwa siku zijazo, huzuni wake utakwisha kwa kuapata neema za Mungu. Aidha Pauline Kea katika *Beluwa*, ameonyesha imani ya kidini kupitia kwa wahusika wake Beluwa na Tanda ambao walijaribu kumtanguliza Mungu katika shughuli yao ya kugawa chumba. Tendo hili linapatikana katika onyesho la pili;

Tanda: Na tuombe
 Beluwa: N'tafanya dua mimi.
 Tanda: Wewe una dini?
 Beluwa: Bila shaka.
 Tanda: Dini ya nani, Mungu au miungu?
 Beluwa: Itakavyokuridhisha wewe.
 Tanda: Omba basi.
 Beluwa: Ee Mungu nguvu yetu,
 ilete baraka kwetu, Haki iwe ngao na... (uk.11)

Maombi haya hayakumalizika bali yalikatizwa na Tanda ambaye aliyaona kama ya *stone age*, yaani maombi yaliyopitwa na wakati, hivyo basi hawakutilia maanani sheria na maadili yanayopaswa kuzingatiwa katika kutekeleza shughuli hii. Heshima inayopaswa kupewa Mungu, haikujitokeza.

Mohamed katika *Amezidi* na Pauline katika *Beluwa*, kupitia wahusika wao inabainika wanamtambua Mungu na wanaamini kuwa ana uwezo wa kumfariji binadamu anaposhindwa kujikomboa. Kiubwege, suala la Mungu huangaziwa kwa makundi matatu. Kuna wanaoamini kuwa Mungu yupo, wasioamini uwepo wa Mungu na wale wa kati wasio na msimamo kuhusiana na suala hili. Watunzi hawa basi walichukua mwelekeo kwamba Mungu yupo, na ana uwezo wa kumkomboa binadamu wa kiubwege kutokana na matatizo yanayomshinda kutatua.

3.3.5 Suala la Kifo na Kaburi

Kwa mujibu wa nadharia ya ubwege, kifo ndicho hatima ya binadamu wa kiubwege. Mkabala wa ubwege unashikilia kwamba maisha yake binadamu wa kiubwege huisha kwa kifo lakini binadamu hapaswi kujitia kitanzi; lazima aishi maisha yake yote huku akijitafutia uhuru wa kiubwege kwa kujipatia kitulizo cha furaha. Camus (1984) anasisitiza suala la kifo maishani mwa binadamu wa kiubwege kwa kusema kwamba maisha ya binadamu yanahusishwa na mateso na uhakika wa kifo. Ni kweli kwamba kifo ndicho hukamilisha ubwege wa maisha ya binadamu katika ulimwengu katili ambamo anaishi.

Said Ahmed Mohamed ameangazia suala la kifo na kaburi katika utunzi wa *Amezidi*. Amewachora wahusika wake wakiwa na uhakika kwamba, siku moja kifo kitawakomboa kutokana na mateso katika ulimwengu katili usio na huruma. Mfano ufuatao unathibitisha dai hili;

Ame: (Kwa mmoja wa wahusika kwenye ile hadhira) Wewe, lazima umeshapoteza mzee, ndugu, rafiki, mwenzi, mpenzi au muhisani kama mimi nilivyompoteza Zidi...lakini tunacheka na kuchekelea kaa vile mazigazi yatawarejesha... tunafurahi...na mbele yetu mazigazi..mazigazi... mazigazi... nini basi kama si ndoto na kujidanganya tu? Maneno makubwa makubwa, manene manene, lakini hayazui roho kupotea...na kesho ndugu yangu, (kwa Yule Yule jamaa kutoka hadhira) ni

siku yangu na yako...kesho tutakufa. (Kicheko) (Uk.83)

Kutokana na kifungu hiki, ni dhahiri kwamba Said Ahmed Mohamed anakubali kwamba ya maisha yake binadamu wa kiubwege ni kifo. Mhusika Ame anataja kwamba ameshampoteza Zidi ambalo wanafurahi tu kwa sababu kesho itakuwa siku yake ya kupatana na kifo. Waaidha, wahusika katika *Amezidi*, ni wale wanaothamini sana kifo; Ame anapokaribia kukata roho anakiri kwamba kifo ni raha, anasema;

Ame: Jamani raha...Kuzimu kule nakuona...Zidi yuleeeee...Zidi...
(Anaita) Njoo, Zidi (Anampungia mkono) Njoo nikamate, njoo unishike mkono. Njoo unionyeshe njia wewe mwenzangu umenitangulia...raha...raha...kifo ni raha...kifo cha raha...
Zidi ameniambukiza? Ah, labda ni sawa, itabidi twende sote kwa ujinga wetu!...aaaaa, sasa maumivu yanazidi, aaaaaa sasa raha inazidi. Raha ya maumivu na maumivu ya raha. Je, (anaigeukia hadhira) na nyinyi mnataka mwende nasi katika maumivu haya ya raha? Fanyeni basi au bora msifanye kitu basi! Ah, nakufa jamani. Kifo cha raha! Naku...na...naku...fa
...NAKUFA! (Ame anakufa) (Uk. 85)

Kifo katika ulimwengu wa kiubwege hushangiliwa na kuenziwa. Ame anafurahia maumivu na kukiri kwamba kifo ni raha; kadri maumivu yanavyoongezeke ndivyo raha pia huzidi. Ame anatuacha kwa shauri moja kwamba tusitende kitu chochote tukitaka kupata raha ya kiubwege; ambacho ni kipengele muhimu wa ubwege. Raha ya kifo pia ilidhihirishwa kupitia kauli ya Zidi kabla ya kupoteza roho yake, tunaambiwa;

Zidi: Niko safarini, Ame...kwaheri
Ame: Safari ya wapi?...
Zidi: Kurudi kwetu basi...narudi kwa wazee...
Ame: Kwenye asili yetu sote?
Zidi: Wapi?
Ame: Kuzimu... (Uk. 76)
Zidi: Na wewe si utanifuata? Ili tukutanie huko?
Ame: Wapi?
Zidi: Kuzimu
Ame: kuzimu nakuogopa
Zidi: kuna nini?
Ame: Kuna shida!
Zidi: Hapana, hakuna shida...shida ipo hapa duniani tu! Kuzimu kuna raha tu! (Anacheka huku kajikamata tumbo)

Ame: Kufa raha?

Zidi: Ndiyo, kufa ni raha; si ndiyo maana sisi tumekuwa tukikutafuta siku zote hizi? Tulikuwa tukikuhimiza kuje haraka haraka! ... (Uk.79)

Ame: Usiondoke, Zidi...

Zidi: Aaaaa...ma...mau...mau...mivu...maumivu...aaa, tumbo. Aaaaaa, nyama mbovu...EC...EC...EC...kifo...kifo... Aaaa, raha...raha...raha, ah, raha, ya kifo...hata kufa kunanipa raha, Ame! Ni...niku...nikumbuke...Mari...Mari...yuko wapi?...Mari...

Ame: Zi...Zi...Zidi...

(Zidi anakufa) (Uk. 80)

Hapa tunampata Ame akishikwa na woga wa kufikia kifo lakini mwenzake Zidi anampa moyo kwamba dunia ndiyo imejaa shida lakini huko kuzimu; makao ya wafu kuna raha isiyo na kikomo. Huko ndiko watashusha mzigo waliopewa na ulimwengu katili na kupumzishwa. Mwelekeo huu pia ulijitokeza katika tamthilia ya *Beluwa*, ambapo Pauline Kea Kyovi alitumia kaburi katika kuangazia suala la kifo. Tunapata tendo la mahaba kaburini ambapo, Tanda anaonyesha hisia zake za kimapenzi kwa *Beluwa* lakini licha ya mahaba, anakiri kwamba anakienzi na kukithamini sana kaburi. Tukichunguza onyesho la nne, tunapata yafuatayo;

Beluwa: (Anashtuka) Kaburi tena?

Tanda: Ndio, kaburi,*Beluwa*. Kaburi ndio mwanzo wetu na ndio mwisho wetu. Ndio Alfa na ndio Omega yetu. Kaburi. Oh kaburi, kaburi langu.

Beluwa: Letu basi!

Tanda: La! Langu mpenzi. Acha liwe langu tu! Nalipenda, naliabudu, nalisujudu, nalilia. (Uk.39)

Wahusika wa kiubwege wakisikia neno 'kaburi' likitajwa, wanagutuka kwa mshtuko kwa sababu hilo ndilo msaada wa ukweli utakao tamatisha ubwege wao. Tanda ana hisia za kimapenzi kwa *Beluwa* hadi ako radhi kumpa chochote lakini kaburi ni lake peke yake. Anakiri kwamba kaburi ndilo mwanzo wake na mwisho wake. Katika onyesho la sita, *Beluwa* anasema kwamba kaburi ni la binadamu wa kiubwege wote na pia anataja manufaa na umuhimu wa makaburi maishani mwa binadamu.

Anadokeza kuwa;

Beluwa: (Anampuza Tanda na kuendelea) Kaburi ni letu sote nishasema. Tujikazeni tulipate. Siku za kupanda huwa ngumu, watu hukosa starehe. Wakajibana na kununua mbegu hata mbolea. Siku yaja tutavuna. Tatalivuna kaburi na kuzijaza ghalazetu. Msijali kelele, vumbi au mmomonyoko wa udongo. Siku yaja.
Kaburi tukilipata hatutataka tukose.
Kaburi tukilipata tutatosheka.
Kaburi tukilipata tutapumzika...
Machozi yanayodondoka, yata...(Uk. 76)

Kaburi ni kitulizo cha roho, binadamu wa kiubwege akilifikia, atatosheka na atapumzishwa, machozi yanayodondoka yatatafutwa na maisha yatakuwa ya starehe. Beluwa anakiri kwamba atakapofika kwenye kaburi, atapumzishwa kutokana na uchovu, huzuni na mateso yaulimwengu. Anasema;

Beluwa: ...Umenichosha, heri nife n'ende kaburini! (Uk. 65)

Kwake Beluwa, mahali pa mapumziko ni kaburini. Raha yote hupatikana katika kaburi. Waaidha, anasema kwamba analifahamu kaburi na ndilo anaota kila wakati, tunaambiwa;

Beluwa: Kaburi nalifahamu na ndio, ninaota. Lakini sio ndoto tena.
Ninaota mawazo. Yanachipuka mapya moto moto!...(Uk. 66)

Katika dondoo hili, ni dhahiri kwamba wahusika wa kiubwege hufikiria tu kuhusu kifo; ambacho ndicho hatima yao. Kila wanaposikia kifo na kaburi zikitajwa, wanachangamkia sana na kuonyesha jinsi wanavyoathamini kifo na kaburi. Said A. Mohamed na Pauline Kea Kyovi wameangazia suala la kifo na kaburi kwa kuchukua mwelekeo ulio sawa katika tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* mtawalia.

3.3.6 Ukengeushi

Ukengeushi kama anavyoeleza Wamitila (2003: 285) ni ukiukaji wa kaida ili kupata hali anayoitarajia msanii. Alieleza yafuatayo akihusisha na sanaa za maonyesho;

“Katika Sanaa za maonyesho, dhana ya ukengeushi inahusishwa na Bertolt Brecht (1898-1956). Dhamira ya Brecht ilikuwa kuiunda hadhira ambayo iliweza kuhusiana na igizo kiakili wala sio kihisia. Ili kufanikiwa kupata hali hii, mwandishi huyu alitumia mbinu za kiukengeushi kama upunguzaji wa hadaa ya uhalisia jukwaani na ukatizaji wa tendo kuu...”

Tunakubali kwamba ukengeushi ni suala linalohusu kwenda kinyume cha matarajio, kaida au kanuni fulani ambayo inafahamika katika jamii na imewekwa ili kuongoza wanajamii husika.

Aidha, Kiubwege Wamitila (2003) alitaja ukengeushi kama sifa kuu inayohusishwa na udhanaishi. Alitoa kauli ifuatayo kuhusiana na suala hili;

“Sifa nyingine inayohusishwa na udhanaishi ni Ukengeushi... maendeleo ya kisayansi na kitasnia yamemkengeusha binadamu kutoka kwa Mungu, jamii na kutoka kwa nafsi yake.” (Wamitila, 2003:248)

Kutokana na maelezo haya, tunadai kwamba kukengeuka ni ukiukaji wa kaida fulani au kwenda kinyume cha matarajio ya jamii, nafsi au imani fulani; yaani kuasi au kupotea njia kabisa. Kwa maneno mengine, ni kwenda kombo na kufanya kinyume cha majukumu uliyopewa au matarajio ya jamii au kuacha njia na kufuata nyingine tofauti kabisa. Wahusika hukengeuka kimila, kikazi na hata kitabia. Kipengele cha ukengeushi ni muhimu sana kwenye nadharia ya Uwege.

Kitushi kizuri kinachodhihirisha ukengeushi kwenye tamthilia ya *Amezidi* ni kile cha mwalimu na wanafunzi darasani. Mwalimu tunayepatiwa ni mwalimu wa kiubwege; asiyelewa jukumu lake wala nafsi yake.

Mwalimu anashindwa kuwaelekeza wanafunzi wake, tunawapata wakilia na kucheka wakiwa darasani. Huyu ni mwalimu tunayetarajia kwamba amepitia mchakato wa ualimu na kupewa mafunzo ya kutosha kuhusu jinsi ya kuwaelekeza wanafunzi, lakini anashindwa kutekeleza wajibu wake darasani. Mada anayofundisha hata yeye

mwenyewe haielewi na anashindwa kuyajibu maswali anayoulizwa na wanafunzi. Ni mwalimu asiyefuata maadili ya ualimu.

Anaposhindwa kufundisha kulingana na maadili ya sekta ya ualimu, anajipata akisinzia darasani kuonyesha ubwege wake. Kwa kifupi tu ni kwamba, mazingira ya darasani tunayopewa hapa yanachukiza sana na huonyesha ukengeushi mkubwa kupitia kwa mhusika Mwalimu. tunaelezewa;

Tendo limo fikirani...pangoni...tendo la shuleni. Zidi ni mwalimu, kaketi mbele ya meza ambayo haionekani. Pana ubao na chaki ambavyo pia havionekani. Ame (mwanafunzi) ameketi kwenye deski lisiloonekana pia. Kuna wanafunzi wapatao sabini. Pia hawaonekani ila Ame tu! Mwalimu Zidi anasinzia huku darasa limejaa zogo la wanafunzi...kitambo...kisha kengele inasikika kulia... Mwalimu Zidi anashtuka kutoka usingizini... (Uk. 29)

Darasa hili tunalopata hapa ni lile lililokosa mwelekeo na matumaini ya kusoma mambo mengi, ni yale mazingira ya kiubwege, yanaoongozwa na binadamu wa kibwege aliyekengeuka. Mwalimu huyu wa kiubwege anabadilisha somo la fizikia kuwa la muziki anaposhindwa kueleza maana ya Archimides's principle na suala la Nyambizi. Wote wanaimba wimbo ufuatao;

Tajiri kasimama
Kasimama kwa maguu yake
Hana anacho!
Kope si zake
Kasimama kwa maguu yake
Kwenye mgongo wake mwenyewe
Magondi yake marefu...(Uk. 33)

Baada ya kuimba, Mwalimu huyu tunaonyeshwa akiamrisha wanafunzi kulala kwa dakika tano na baadaye wanaamshwa tu na uvundo wa mizoga; haya ni mazingira yasiyofaa kwa utekelezaji wa shughuli za ufundishaji. Tunapata yafutayo;

Mwalimu: Barabara. (anatabasamu) Dakika tano za kulala...tunza yenu! (wanalala na mwalimu wao juu ya meza zisizokuwepo) (Uk.35)

Mwalimu: Ninasikia harufu mbaya...kama kitu kimeoza.(Anaziba pua)

Wanafunzi: (Wote) Mmmf...mmmf...mmf (Wanaziba pua pia)

Mzoga, mzoga...mmf! (Uk. 35)

Aidha, Mwalimu anaonyeshwa akiwakataza wanafunzi wasiulize maswali. Akiulizwa maswali anakasirika na hata kushindwa kuyajibu. Tunaambiwa;

Mwanafunzi: suala...

Mwalimu: (Anakasirika) Suala...suala...suala...masuala; likiisha hili, hili! (Kicheko cha wanafunzi) (Uk.38)

Kukasirika kwa mwalimu anapotaka kuulizwa swali; ambalo hata hawezi kuling'amua ni ubwege. Mwalimu huyu hatambui kanuni za ualimu na hivyo ni kama tu kibonzo asiyeweza kutekeleza chochote katika taaluma ya ualimu.

Vile vile, mtunzi wa tamthilia ya *Beluwa* amewasawiri wahusika wake kama wale wapotovu, ambao wameuasi utamaduni wao na kuiga tamaduni za wageni hasa za uingereza pamoja na mtindo wa elimu yao. Mhusika Tanda anaonyeshwa kuwa mwenye amelelewa katika mazingira tofauti hivyo maisha yake yamezungukwa na matendo machafu. Anajitokeza kama "*Msenge au mbasha*" na kujionyesha kuwa ana ustaarabu kuliko Beluwa, ambaye ameushikilia utamaduni na maadili ya jamii yake. Suala hili linadhihirishwa kwa mfano, katika katika onyesho la nne, ambapo Tanda anasema kuwa matendo yake yameathiriwa sana na mazingira aliyolelewa, vitu alivyosoma kwenye mabuku, majarida, magazeti na mtandao.

Tanda: Njoo, njoo uniondolee janga hili. Njoo nikushike, nikukumbatie, niku...(anamshika Beluwa mara moja na kutaka kumbusu. Beluwa anamsukuma na kumwangusha)

Tanda: (analia kwa maumivu huku akijishikilia moyo) ooh! ooh!

Beluwa: (kwa ukali) unataka kunifundisha nini wewe? ushoga, usege au uhayawani?

Tanda: (kwa ukakamavu) sasa unajitia kutojua mambo haya? unaishi sayari gani? Get serious, drama si fani yako!

Beluwa: kwa hivyo wewe ni gay? (kimya kidogo)

Tanda: unangoja jibu?

Beluwa: La! dalili ya mvua ni mawingu....

Tanda: wananielewa si kama wewe unayeishi katika enzi za homo erectus. Zaitwa bling basi! Andika usije ukasahau. (uk. 41).

Katika tamthilia ya *Beluwa*, onyesho la tatu, Beluwa na Tanda wanajadiliana kuhusu siri ya maisha; ambayo hudhihirisha ukengeushi kutokana na utamaduni wa kiafrika.

Tanda: (akichekacheka) nina siri ya uhai

Beluwa: (anashtuka) eeh!

Tanda: Ninaweza kutungisha mimba mwanamke asiye na mayai ya uzazi....nitakufa vipi?

Beluwa: kweli huwezi kufa. Ninasikia inaitwa cloning, ati.

Tanda: Ndio.

Beluwa; (akionekana kuwa mawazoni) lakini...lakini si basi unaweza pia kutoa uhai?

Tanda: (kwa tuo) Bi-la-sha-ka. Huo ni ukweli uchi.

Beluwa: (kwa madaha) unaweza kutengeneza silaha za maangamizi ya halaiki; silaha zinazoweza kuangamiza dunia nzima kwa dakika chache tu?

Tanda: tunaziita atomic bombs.

Beluwa: ...Na unaweza pia kuzuia uzazi ...

Tanda: Hiyo nayo ni family planning. (Uk. 16-17).

Kupitia kifungu hiki, tunapata wahusika walio na maarifa ya kisayansi lakini wanashindwa kujikomboa; bado wamo gerezani kwenye chumba cha futi kumi mraba; mahali pachafu pasipo na uzuri wowote. Maarifa aliyoyapata Tanda kutokana na elimu ya kimagharibi, hayamsaidii kutenda chochote cha maana; anajitokeza kama kibonzo kisichoweza kubadili hali yake ya maisha duni na kujiingiza zaidi kwenye kifungo cha matatizo yasiyo na kikomo. Kwa kuangazia tamaduni za kiafrika, ni vyema mwanamke awe na uwezo wa kutungwa mimba na kujifungua mtoto wa damu yake, lakini tunaonyeshwa Tanda akiwa na maarifa ya kumtungisha mwanamke asiye na mayai ya uzazi mimba bila kujamiana. Suala hili hudhihirisha ukengeushi. Aidha, uwezo wa kutengeneza silaha zinazoweza kumaliza dunia nzima kwa sekunde moja ni hatari kwa jamii. Kwa kuangazia mhimili wa nadharia ya ubwege kwamba ukengeushi ni sifa muhimu ya ubwege; ambao umetokana na udhanaishi, tunakiri

kwamba wahusika kwenye tamthilia ya *Beluwa* wamesawiriwa wakiwa wapotovu na wanajenga maudhui yanayoonyesha uduni wa maisha yao.

Naye Said Ahmed Mohamed amelishughulikia suala la athari za utamaduni wa kigeni kwa waafrika kupitia kwa wahusika wake Zidi na Mari. Zidi anamwambia Mari ambaye amekuwa mpenzi wake;

Zidi: Sikutambui, Mari...umebadilika...siye tena Mari mtaramburamsichana wa kijiji cha mjomba wangu; kile kijiji cha Mpashambi...siye tena Mari mwenye ngozi ya ganda la fuu na gome la mpingo...sasa ni Mari wa jijini na ngozi ya kukoboa! (uk. 61)

Maisha ya mhusika Mari yanadhihirisha mkengeuko kwa sababu hathamini tena mambo ya kiafrika. Anaonyeshwa kupenda sana mambo na mienendo ya kizungu. Tunamwona akipenda lugha ya Kingereza kuliko ya kiafrika, anatumia mafuta ya kufanya rangi yake ya ngozi kuwa kama ya mzungu; yaani anapenda rangi ya wazungu. Haya yuanadhihirika katika mfano ufuatao;

Mari: Na Mapambo, mavazi, na urembo wa mwanamke kama mimi si hapa.. si ya fedha za madafu, lazia yatoke states of Canada, Japan, France, Italy au West Germany!
 Zidi: (Kejeli) Alaaaaa! Nimechelewa kutambua!
 Mari: Unanichezeshu kindumbwendumbwe charira, kikojozi kakojoa na nguo katia moto Ukanipa vitu viliopo visivyokuwepo!
 Zidi: (tashtiti) Alaaa!
 Mari: Enhe sasa nitazame, nimekuja makusudi unione! (uk. 60)

huu usemi wa Mari ni ule uliojaa dharau na kiburi kwa mwenzake Zidi, amabaye anawakilisha mwafrika. Kwake Mari, tamaduni za kiafrika ni ujinga na hazina ustaarabu.. Hakithamini cha Kiafrika. Huu ni ukengeushi mkubwa. Licha ya kwamba Mari anathamini utamaduni wa waingereza pamoja na mienendo yao, bado anabaki pale pale kwenye pango ambapo anaendelea kuishi maisha ya kindoto yasiyoweza kuboreshwa.

Kwa kuongozwa na mhimili wa ubwege kwamba drama za kiubwege lazima ziwe jazanda ya ukanganyifu wa jamii isiyojielewa, tumedhihirisha kwamba tamthilia hizi mbili zinaakisi mazingira yenye ubatili; yenye ukengeushi. Suala la Ukengeushi limeshughulikiwa katika tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa*; wahusika wameonyeshwa wakiwa waasi ambao wanakiuka kaida za jamii na kwenda kinyume cha matarajio ya jamii husika. Pia, wahusika katika kazi za kiubwege hukosa uwezo wa kuboresha hali zao na matendo yao hukosa muwala wala umuhimu wowote ila huonyesha ubatili mtupu.

3.3.7 Ukosefu wa uthabiti katika Elimu

Kama tulivyoeleza, ubwege haugusiki bali ni uhusiano wa kidhahania kati ya akili iliyopevuka na ukweli wakuwako kwa binadamu katika ulimwengu katili. Hali hii ya ubwege hujitokeza kwa sababu ya kukosa kuridhika kwa akili kulingana na matarajio yake juu ya utaratibu wa matukio katika ulimwengu. Elimu wa kiubwege, hukosa msingi thabiti ya kijamii. Yaani huwa ni ya kubuniwa na haiwezi kusaidia binadamu katika kuboresha maisha yake basi, huchangia katika kumwangamiza sana.

Kiubwege, matendo ya mhusika huwa hukosa umuwala na umuhimu wowote ila huonyesha ubatili tu. Dhana hii ni muhimu sana katika nadharia ya ubwege na hubaini kwamba matendo ya mhusika wa kiubwege ni ya kijinga na hayana maana kabisa. Katika tamthilia ya *Amezidi*, tunapatiwa mwalimu pamoja na wanafunzi wake wakilala kwenye darasa na hakuna aliye na uwezo wa kukomboa mwenzake kutokana na janga la kukosa kujua. Mwalimu akiwa na wanafunzi wake, wanalia na kucheka wakiwa darasani. Hii inaonyesha mtafaruku wa taaluma ya ualimu. Mwalimu tunayepatiwa hapa ni yule ambaye tunatarajia amepitia mchakato wa mafunzo ya kutosha katika taaluma ya ualimu na anaye uwezo wa kuwaelekeza

wanafunzi wake, ila anashindwa kutekeleza wajibu wake kama mwalimu. Mwalimu huyu Anafundisha mada ambayo hata yeye mwenyewe haelewi na hatimaye anashindwa kujibu maswali anayoulizwa na wanafunzi. Anafikia hatua ya kukasirika anapoulizwa maswali; hali ambayo ni kinyume cha matarajio. Ni mwalimu asiyefuata maadili ya ualimu. Kadhalika, mwalimu huyu anaonyeshwa akisinzia darasani kuonyesha ubwege wake. Kijumla, mazingira ya darasani ambayo Mohamed ametupa ni yale yanayochukiza sana na kudhihirisha elimu ya kukata tamaa. Tunapata maelezo yafuatayo mwanzoni mwa Onyesho la Nne;

Tendo limo fikirani...pangoni...tendo la shuleni. Zidi ni mwalimu, kaketi mbele ya meza ambayo haionekani. Pana ubao na chaki ambavyo pia havionekani. Ame (mwanafunzi) ameketi kwenye deski lisiloonekana pia. Kuna wanafunzi wapatao sabini. Pia hawaonekani ila Ame tu! Mwalimu Zidi anasinzia huku darasa limejaa zogo la wanafunzi...kitambo...kisha kengele inasikika kulia... Mwalimu Zidi anashtuka kutoka usingizini... (Uk. 29)

Darasa hili tunalopewa ni lile la wanafunzi wapatao sabini ambao ni watundu na wenye zogo wasiojielewa. Aidha, ni daasa la somo la fiziki linalofundishwa na mwalimu anayesinzia na ambaye hajui wala haelewi analofundisha.. Ni darasa lililokosa matumaini wala mwelekeo wa kupata maarifa mengi, mazingira haya ni ya kiubwege yasiyoweza kuthibiti elimu; kama inavyoshikiliwa na wanatapo la ubwege kwamba tamthilia ya kiubwege hudhihirisha jazanda ya ukanganyifu wa jamii isiojielewa na lugha hutumiwa tu kwa minajili ya mawasiliano ya kidhahania. Tunaambiwa;

Mwalimu: Na...na...nani atata...taja *Archimides's principle*... mikono juu...enhe. (kwa mwanafunzi Ame) Wewe, Ame!...

Mwanafunzi: Mwili wa kitu chochote uzamapo kwenye maji, wote au sehemu yake, utajaribu mwibuko...

Mwalimu: Vizuri...vizuri...bas...bas...vizuri, unajua, unajua- (anaandika kwenye ubao usiokuwepo. Anaandika kama kichina au kijapan kutoka juu kuja chini)

Mwanafunzi mwingine: (Sauti tu inasikika; kiwiliwili cha mwanafunzi hakionekani. Mwalimu anasinzia.)
Ku...(Anasita) Hivi kukariri mawazo za Archimides kuna faida gani?...kunasaidia nini?

Mwalimu: (Amekasirika) Tazama...(anasita huku akionekana amelisahau suala...wanafunzi wanasikika wakicheka kwa pamoja) Mnacheka? (Anakasirika zaidi)

Wanafunzi: (kwa pamoja) Hapana! Tunalia!

Mwalimu: Aha! Vipi...vipi vile? Aha...suala...uliza tena. (anacheka sasa)

Mwanafunzi: Suala?

Mwalimu: Jibu

Mwanafunzi: Jibu

Mwalimu: Suala

Mwanafunzi: Sawa

Mwalimu: Sawa nini?

Mwanafunzi: Sawasawa

Mwalimu: Sawa

(uk.29-30)

Hapa tunapata mwalimu ambaye hana uwezo wa kuwaelekeza wanafunzi wake.

Anaulizwa swali lakini anakosa kulijibu na hata analisahau kabisa. Mfano huu unatupa jazanda ya ukanganyifu wa jamii isiyojielewa ambayo hutumia lugha kwa ajili ya mawasiliano ya kidhahania. Mara suala, jibu, sawa, sawasawa; maneno ambayo hayatatui tatizo walilionalo bali hudhihirisha ukosefu wa mantiki katika mazungumzo ya kiubwege.

Waidha, mwalimu huyu anapoulizwa swali lile lile kwa mara ya pili, anamwambia mwanafunzi kuwa ajibu swali hilo mwenyewe. Tunaambiwa;

Mwalimu: (Kwa mwanafunzi aliyeuliza suala) Enhe...jibu mwenyewe basi... (Uk. 32)

Aidha, ukosefu wa uthabiti kwa elimu unajitokeza pale ambapo mwalimu pamoja na wanafunzi wake wanapobadilisha somo la fizikia kuwa la muziki. Mwalimu na Wanafunzi wanazozana kuhusu maana ya Archimides' principle na suala la nyambizi, na wanaposhindwa kutoa jibu mwafaka, wanageukia wimbo; yaani somo la fizikia linageuka na kuwa somo la Muziki. Wanatuambia wimbo ufuatao;

Tajiri kasimama kasimama kwa maguu yake
 Hana anacho!
 Kope si zake
 Kope ni zake
 Kasimama kwa maguu yake
 Kwenye mgongo wake mwenyewe (uk. 33).

Wimbo huu ulitumiwa ili kumtuliza binadamu wa kiubwege aliyekosa uwezo wa kufanya chochote katika ulimwengu katili anamoishi. Baada ya wimbo huu, tunapata mwalimu akiwaambia wanafunzi walale kwa dakika tano. Huyu ni mwalimu ambaye tunatarajia kuwaamsha wanafunzi wakiwa wameshikwa na usingizi darasani, lakini kinachojitokeza ni kinyume; anawaongoza wanafunzi kwa shughuli ya kulala darasani. Kitendo hiki kinaendeleza ubwege zaidi kupitia mwalimu na wanafunzi ambao wanaonyeshwa kuwa walikuwa wamesinzia huku redio ikitoa taarifa. Mwalimu anadokeza yafuatayo;

Mwalimu: Barabara (anatabasamu) Dakika tano za kulala...tunza yenu! (wanalaala na mwalimu wao juu ya meza zisizokuwepo) (uk. 35)

Ukosefu wa uthabiti katika elimu ni kipengele cha ubwege. Elimu tunayoonyeshwa hapa ni ile isiyoweza kuleta manufaa wala maarifa yoyote kwa jamii. Ni elimu ya kindoto inayokatisha tamaa. Mohamed katika *Amezidi* anaonyesha elimu ambayo imetengana na mahitaji ya nchi.

Mazingira ya elimu au shule hayajaonyeshwa kwa wazi kwenye tamthilia ya *Beluwa* japo athari ya elimu ya kigeni imeangaziwa kwa upana. Kuna vipengele ambavyo vinaonyesha athari za elimu za kigeni na maarifa yanayotokana na usomaji wa mabuku, majarida, magazeti na mtandao pamoja na mazingira yalimolelewa mtu ambayo yanamfanya akengeuke. Kukiuka kaida za jamii ni sifa mojawapo ya ubwege na husababishwa maendeleo ya kisayansi na kitasnia. Ukiukaji huu wa binadamu humtenganisha kutoka kwa Mungu, jamii na kutoka kwa nafsi yake.

Katika tamthilia ya *Beluwa*, mhusika Tanda ameathirika sana na vitu alivyovisoma kwenye mabuku, majarida, magazeti na mtandao. Isitoshe, pia ameiga mambo kutokana na mazingira aliyolelewa pamoja na yale aliyotendewa utotoni. Aidha, anajiona kuwa na ustaarabu kuliko mwenzake Beluwa. Ustaarabu wake huo unahusu kufanya mahaba na jinsia kama yake (ubasha), kumfanya mwanamume kuwa mke wake.

Beluwa: ulisoma nini?

Tanda: Mabuku, majarida, magazeti na mtandao.

Beluwa: ilikuwa lazima usome?

Tanda: nisingesoma ningebakia nyuma. (uk.43)

Kutokana na elimu aliyoipata Tanda kwenye mabuku, majarida, magazeti na mtandaoni, aliweza kuasi maadili ya Kiafrika. Alitaka kufanya mahaba na Beluwa, ambaye alimchukulia kama mpenzi wake licha ya kwamba wote ni wa jinsia ya kiume. Tunaambiwa;

Tanda: Njoo, njoo uniondolee janga hili. Njoo nikushike, nikukumbatie, niku...(anamshika Beluwa mara moja na kutaka kumusu. Beluwa anamsukuma na kumwangusha) (uk.41)

Kitendo cha mahaba ya kaburini kinadhihirisha ukosefu wa uthabiti katika elimu miongoni mwa waafrika, kwa vile kitendo cha ubasha ni kitendo ambacho hukiuka maadili ya jamii za kiafrika. Wahusika Tanda na Beluwa wanaonyeshwa wakiwa na uhuru wa kujistarehesha kwa njia ya kujiingiza kwenye mahaba licha ya kuwa viumbe wa jinsia sawa. Kikawaida, jamii za kiafrika huamini kwamba mtoto akienda nchi za nje kuendeleza masomo, anatakiwa kurudi Afrika akiwa na kazi nzuri na ajue kuumudu uhusiano wake na wenzake. Tunavyoipata katika tamthilia ya *Beluwa* ni kinyume ambapo mhusika Tanda anasawiriwa akiwa ameyasahau ya kiafrika na kuyaenzi ya ngámbo. Suala hili husababisha kukosa kuamini masomo ya kimagharibi,

ambayo hutazamwa kama msingi wa ukengeushi kutokana na maadili ya jamii za kiafrika.

Kijumla kinachodhihirisha mfanano wa mwelekeo wa kiubwege baina ya tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* ni jinsi watunzi walivyoangazia suala la athari za elimu isiyoweza kuthibitiwa wala kuaminiwa; elimu ya kukatisha tamaa. Ni elimu inayoongeza madhara na matatizo badala ya kuleta suluhisho kwa changamoto zinazokumba jamii za kiafrika. Wahusika katika tamthilia za kiubwege, licha ya kujaribu kutafuta ukweli, fikra zake zinamfanya asiupate ukweli huo na hatimaye wanakosa nguvu za kuboresha hali ya maisha yao duni. Elimu katika tamthilia hizi imejitokeza kuwa ya kukatisha tamaa na iliyokosa uwezo wa kuleta matumaini maishani mwa binadamu. Kwenye tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa*, watunzi wameonyesha kwamba licha ya kwamba binadamu anaweza kuwa na ujuzi wa kitaaluma, kisayansi pamoja na maarifa aliyoyatoa kutoka kwenye mabuku, majarida, magazeti na hata mtandaoni, bado hana uwezo wa kubadili maisha yake duni; bado anaishi ama pangoni au gerezani bila kujikomboa. Madai haya yanajikita katika mihimili ya nadharia ya ubwege; ambayo tulishaeleza hapo awali kwamba matendo ya wahusika wa kiubwege huwa hayana muwala, mantiki wala umuhimu wowote bali yanaonyesha ubatili tu na mtunzi utunzi wa kiubwege sharti atumie jazanda ya ukanganyifu wa jamii isiyojielewa.

3.4 Mlingano Kifani katika Tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* kiubwege

Katika sehemu hii, tumechunguza vipengele vya kifani kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya ubwege na hatimaye kudhihirisha mfanano wa vipengele hivyo kiubwege. Kando na kuhakiki dhana ya fani, tulichunguza vipengele vya kifani kiubwege vikiwemo; Uhusika (wahusika wa kiutopia, wahusika wa kinjozi, wahusika

wasiokuwa na historia), ukosefu wa ruwaza za mazungumzo, utupu, matumizi ya nyimbo, matumizi ya vicheko na vilio pamoja na ploti.

3.4.1 Dhana ya Fani

Fani ni jumla ya viambajengo vya kazi ya kifasihi vinavyotumiwa na msanii katika kupitisha ujumbe wake kwa hadhira. Wataalamu mbali mbali wanaeleza dhana hii kwa njia tofauti tofauti.

Kulingana na Mbatiah (2001), dhana ya fani huwa na maana mbili. Kwanza, ni jumla ya vipengele vya kimtindo na kisanaa kwenye kazi ya fasihi vinavyotumiwa kujenga kiunzi cha kubebea ujumbe au maana mahususi. Kando na maelezo haya, anasema kwamba maana ya pili ya fani ni kategoria ya fasihi, yaani utanzu kama vile ushairi, drama na ahata riwaya. Tunakubaliana na maana ya kwanza kwamba fani hujumuisha vigezo vya kimtindo na kisanaa.

Wamitila (2003) naye anachukua mkondo tofauti anapoeleza kwamba fani hueleza muundo au mpangilio wa kazi ya kifasihi au sehemu zake. Anaendelea kubaini kuwa fani inaeleza mbinu pamoja na mtindo wa kuyawasilisha yaliyomo au maudhui. Kwa njia nyingine, Wamitila (2010) anaelezakuwa fani ni jumla ya mbinu, mtindo na nyenzo anazoitumia mtunzi kuwasilisha dhamira na maudhui yake. Pia, anatoa kauli nzito mwishoni kwamba haiwezekani kwa mwandishi kuiwasilisha dhamira yake au kuyapitisha maudhui yake bila ya kuitegemea fani.

Tunakubaliana na Njogu na Chimera (1999) na Wamitila (2010) katika ufafanuzi wa dhana ya fani kuwa ni jumla ya viambajengo vya kazi ya fasihi ambavyo vinatumia na msanii katika kupitisha ujumbe wake kwa hadhira; vipengele hivyo huwa vya kimtindo na vya kisanaa.

3.4.2 Uhusika

Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999) uhusika ni umithilishaji wa matendo ya viumbe hadithini na vile vya viumbe katika dunia razini. Anaendelea kueleza kwamba, matukio ya viumbe hao husababishwa kuambatana na mazingira ya ubunifu. Kwa njia nyingine, katika *Kamusi ya Fasihi* (2001) dhana ya uhusika imeelezwa na Wamitila ni mbinu ya kuwajenga wahusika na hatimaye kuwatofautisha na ukuzaji wao.

Wahusika ni viumbe vilivyo hai na visivyo hai; vya kidhahania au halisi vinavyotumiwa katika kazi ya fasihi hivyo kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa na msanii kwa hadhira husika. Wahusika wa kiubwege ni wa kidhahania, yaani hawawezi kuonekana na kutambulika katika mazingira halisi bali hubuniwa akilini mwa mtunzi. Wahusika hao wanabadilika badilika na hawatendi chochote bali wanakaa tu huku wakijihusisha na mazungumzo ya kiduara yasiyo na mantiki, muwala wala umuhimu wowote.

Tunakubaliana na Wamitila (2002) anapofafanua kuwa, mtunzi katika fasihi huweza kutumia mbinu mbali mbali ili kuwasawiri wahusika wake na ana uhuru katika uhusika wa kuteua na kutumia wahusika wa aina mbalimbali, watakaoambatana na mahitaji ya kazi yake. Hali hii imejitokeza wazi kwenye tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* hivyo, tumeainisha wahusika wa tamthilia hizi teule kulingana na utendaji wao na walivyochorwa na waandishi wa kazi hizi.

3.4.3 Uchache wa wahusika

Watunzi tamthilia za kiubwege hutumia wahusika wachache katika kazi zao. Kiubwege, msani ana uhuru wa kutumia mhusika mmoja, wawili au watatu ambao wanaonyeshwa wakichukua nafasi mbali mbali za wahusika wengine. Kutokana na

tamthilia ya *Amezidi*, tunawapata wahusika wakuu wawili ambao ni Ame na Zidi. Majina ya wahusika hawa yametokana na anuani ya kitabu chenyewe. kwenye jalada, mtunzi anayatoa maelezo haya;

Amen a Zidi wanajikuta katika umaskini mkubwa katika bahari
iliyojaa mali... (jalada, nyuma ya kitabu)

Idadi ndogo ya wahusika katika *Amezidi* huonyesha sifa kamili ya nadharia ya ubwege, kwani Mohamed anatumia wahusika wawili tu toka mwanzo hadi mwisho wa mchezo.

Tamthilia ya *Beluwa* kwa upande mwingine imeundwa kwa wahusika wakuu watatu ambao ni Beluwa, Tanda na Mtu. Kwenye utangulizi, Kyovi anabaini kwamba mchezo wa *Beluwa* umeundwa kwa wahusika watatu ambao wanabadilikabadilika na hivyo kuwazalisha wahusika wengine. Anasema yafuatayo;

“Mchezo huu una wahusika watatu ambao wanazalisha wahusika wengine. Wahusika hawa ni; Beluwa, Tanda na Mtu” (kwenye utangulizi)

Uchache wa wahusika unadhihirishwa katika *Amezidi* ambapo kuna wahusika wawili na vile vile *Beluwa* ina wahusika watatu pekee. Kigezo cha uchache wa wahusika katika tamthilia za kiubwege ni dhahiri.

3.4.3.1 Wahusika wa kiutopia

Matumizi ya wahusika wa kiutopia ni mhimili wa nadharia ya ubwege. Mkabala wa ubwege una sifa ya wahusika wa kiutopia; ambayo ni hali ya kubadikabadilika kwa wahusika hata kubadilika kwa jinsia; yaani mhusika wa kike kuwa mume au mume kuwa mke.

Said A. Mohamed ameangazia mbinu ya mhusika ndani ya mhusika katika *Amezidi*. Ame na Zidi wanachorwa wakibadilikabadilikana kuchukua nyadhifa tofauti tofauti

kutokana na mahitaji ya mtunzi huyu. Kwa mfano tunampata Ame anakuwa Mari (mpenzi wa kike) kwenye onyesho la tatu, Mwanafunzi katika onyesho la nne huku Zidi anakuwa mwalimu wake.

Waidha, katika onyesho la tano, Ame anachukua nafasi ya Bosi na Zidi anakuwa msaidizi wake. Hebu tutazame madondoo yafuatayo ili kuthibitisha dai hili tunaelezwa;

Tendo hili limo ndani ya fikra za wahusika...Zidi kaketi juu ya sofa lisiloonekana. Ame, aliyejigeuza kuwa Mariam (Mari) kwa mavazi ya kike anaingia kwa madaha ya kike (Uk. 19)

Kutokana na kifungu hiki, Ame anachukua nafasi ya mhusika wa kike Mariam (Mari) katika onyesho la tatu na hivyo kukuza maudhui ya ukengeushi na elimu ya kukatisha tamaa katika tamthilia ya Amezidi. Kadhalika, kwenye onyesho la nne, Ame na Zidi wanabadilika na kukuza mandhari ya shuleni yanayotoa jazanda ya ukanganyifu wa jamii isiyojielewa; ambacho ni suala muhimu sana katika mkabala wa ubwege.

Tunaelezwa;

Tendo limo fikirani...pangoni...tendo la shuleni. Zidi ni mwalimu, kaketi mbele ya meza ambayo haionekani. Pana ubao na chaki ambavyo pia havionekani. Ame (mwanafunzi) ameketi kwenye deski lisiloonekana pia. Kuna wanafunzi wapatao sabini. Pia hawaonekani ila Ame tu! Mwalimu Zidi anasinzia huku darasa limejaa zogo la wanafunzi...kitambo...kisha kengele inasikika kulia... Mwalimu Zidi anashtuka kutoka usingizini... (Uk. 29)

Hapa tunamkuta mhusika Ame akiwa mwanafunzi na Zidi ni mwalimu asiyeweza kuelekeza wanafunzi ipasavyo. Tukio la shuleni humu linadhihirisha ubwege kwa vile hakuna uthabiti kwa elimu ila inakatisha tamaa. Waidha, kwenye onyesho la tano, pango linageuzwa na kuwa ofisi, Ame anabadilika na kuwa Bosi huku Zidi akiwa msaidizi wake. Tunaelezwa yafuatayo;

Tendo limo fikirani...pango linageuka ofisi! Amen i bosu na Zidi , msaidizi wake. Ame ameketi nyuma ya meza yenye simu

isiyokuwepo...kwa kweli ameketi chini sakafuni...matendo yanatokea ndotoni mwao. (Uk.40)

Hapa tunawapata wahusika Bosi na Msaidizi ambao walitumiwa tu ili kufanikisha matakwa ya msanii ya kukuza mazungumzo ya kiubwege. Mazungumzo tunayoyapata katika onyesho la tano kuhusu tukio la ofisi, hudhihirisha sifa ya matumizi ya lugha inayotatiza mawasiliano. Hakuna mantiki kwa yale yanayosemwa na pia ni tukio la kindoto; simu inayokamatwa ofisini ni ya uwongo, Zidi (Msaidizi) anakalia kiti kisichokuwepo mara Bosi anaokota orodha isiyokuwepo juu ya meza isiyokuwepo. Ukosefu wa uhalisia au matumizi ya vitu visivyoonekana ni mhimili wa ubwege. Tunaambiwa;

Bosi: (Anakamata simu ya Uwongo) Hallo, hallo...

Msaidizi: (Anaingia na kuketi kitini; kiti kisichokuwepo) Naam, Bosi...nipo kwa ajili yako!

Bosi: (Anaokota taratibu kwa mbwembwe orodha fulani isiyokuwepo juu ya meza isiyokuwepo...) (Uk.40-41)

Wahusika Bosi na Msaidizi wametumiwa kidhahania ili kuendeleza mazungumzo ya kidhahania; yasiyokuwa na mantiki wala mwelekeo wa maendeleo kwa jamii. Wahusika hawa wanatumia vitu visivyokuwepo kama vile meza, kiti, simu na orodha; ambayo hudhihirisha ubwege.

Aidha katika tamthilia ya *Beluwa*, mwandishi ametumia wahusika wa kiutopia kwa kubadilisha nafsi zao; kwa mfano Tanda anabadilika kuigiza Daktari, Mama, Mtangazaji, Zaida, Tamimu. Beluwa kwa upande mwingine anaiga sauti ya kobe, Chiriku. Mtu naye anajigeuza kuigiza mwanamke Rashia. Hii hali inajitokeza katika utunzi wa kazi za kiubwege, anavyoeleza Anderson (1972:2) kwamba wakati Fulani wahusika hubadilika katika hali zao, mazungumzo yao huwa yamejaa ukinzano; wanakataa kuamini yaliyomo katika ulimwengu na hivyo kukubali matukio ya

kidhahania, maelezo yao kuhusu hali n adhana tofauti tofauti huwa hayana maana.

Katika onyesho la pili, tunakuta yafuatayo;

Tanda: ...(Anageukia hadhira na kuuliza maswali huku akiyajibu yey mwenyewe kwa kuigiza sauti ya kike na kiume. Ya kiume ni ya Daktari na ya Kike ni ya mama mjamzito) (Uk.10)

Mazungumzo baina ya daktari na mama mjamzito yalitumiwa kukuza maudhui kiubwege kutokana na tamthilia ya *Amezidi*. Tunawapata wahusika hawa wakicheka kicheko cha kutisha kinachokatizwa kighafla. Wanacheka ili kujituliza kutokana na matatizo yasiyoepukika katika ulimwengu katili wanamoishi. Mama mjamzito ametungwa mimba na yule ambaye si mume wake na kuachwa kubeba mzigo huo mwenyewe.

Kadhalika, Katika onyesho la tatu Tanda anabadilika na kuwa mtangazaji wa mchezo

wa kandanda. Yafuatayo yanathibitisha hoa hili;

Tanda: Tujandae basi tusakate kambumbu. (Tanda na Beluwa wanavua mavazi yao ya gerehani. Wanabaki na sare za michezo walizozivaa ndani. Tanda anawageukia watazamaji akiigiza mtangazaji (Uk. 21)

Isitoshe, tunampata Beluwa akibadilika na kuwa mwanahabari wa kike Zeituni Zaida

katika onyesho la Sita. Tunaambiwa;

Mtu: Ebu, nyamazeni tutazame habari. (Mtu anabonyezabonyeza simu yake. *Screen* ya simu inaonesha kiwambo cha runinga. Anaketi kitandani na kuibonyezabonyeza tena akifanya kama kuiuelekeza ukutani ili picha zionekane. Beluwa anaketi kitandani kando ya mtu tayari kutazama habari. Tanda anajifanya ndiye mwanahabari. Anaingia sauti ya mwanahabari, Zaida. (Uk. 73)

Zaida: ...(Tanda anaigeuza sauti yake ili kuigiza mwanahabari, Tamimu. Sauti za waandamanaji zinasikika mwanahabari akiongea...) (Uk.74)

Vifungu hivi vinadhahirisha kigezo cha uhusika wa kiutopia ambacho ni kigezo muhimu sana katika mkabala wa ubwege. Mhusika Tanda anachukua sura na nafasi

mbali mbali ili kukuza maudhui yaliyokusudiwa na mtunzi. Beluwa naye kwa upande mwingine anachukua nafasi ya wanyama; anabadilika na kuigiza wanyama Kobe na Chiriku. Hebu tutazame mfano ufuatao;

Beluwa: (Naye pia anaketi mkabala na Tanda)...(Anasafisha koo na kubadilisha sauti yake kumwiga kobe) (Uk.27-28)

Kobe: ...(Beluwa anaiga sauti ya Chiriku) (Uk.30)

Kiubwege, mhusika akichukua nyadhifa ya mnyama hudhihirisha kwamba maisha ya binadamu huweza kulinganishwa na mnyama asiyeweza kutekeleza chochote ili aboreshe maisha yake. Kobe anashindwa kuumudu uhusiano wake na wanyama wenzake na hivyo kumsababishia matatizo. Mkabala wa kiubwege unashikilia kwamba binadamu wa kiubwege hana nguvu ya kujielewa hata anashindwa kutilia maanani mahusiano ya kijamii. Wahusika wanasawiriwa wakiwa wanajipenda wenyewe bila ya kujali wengine. Uhusiano wa mtu na mwenzake hautiliwi maanani katika ulimwengu wa kiubwege.

Mhusika Mtu kwa upande mwingine pia anaonyeshwa akibadilika kijinsia na kuwa mhasiriwa wa maandamano, Rashia. Mtu anabadilisha jinsia yake na kuigiza mwanahabari mwanamke, tunaelezwa yafuatayo katika onyesho la sita;

Tamimu:...Nimepata fursa ya kusema na mhasiriwa wa maandamano haya (Akimgeukia Mtu ambaye sasa amesimama nyuma yake) Waitwaje, mama? (Mtu anaigeuza sauti yake ili kuigiza sauti ya mwanamke, Rashia)

Rashia: (Akipumua kwa nguvu sana) Ninaitwa Rashia Mgwisho. (Uk. 74)

Mhusika Rashia ametumiwa ili kuonyesha thamani na umuhimu wa makaburini kwa binadamu wa kiubwege. Watu kutoka jimbo la Makaburini ya kati wanaandaa maandamano ili waonyeshe kwamba wanayaenzi makaburi; ambayo ndiyo hatima ya binadamu wa kiubwege.

Kijumla, kigezo cha matumizi ya wahusika wa kiutopia ni muhimu sana katika mkabala wa ubwege na ni dhahiri kwamba watunzi wa tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* wametumia wahusika wa kiutopia ili kuonyesha ukweli wa ulimwengu wa kiubwege kwamba, binadamu hawezi kutenda lolote ili kuyaboresha maisha yake na kujikomboa kutoka kwa matatizo yanayomkumba katika ulimwengu katili anamoishi. Aidha kigezo hiki cha wahusika wa kiutopia huchangia katika kuwasilisha maudhui kama ilivyokusudiwa na wasanii.

3.4.3.1.1 Wahusika wa kinjozi

Mkabala wa ubwege unashikilia kwamba tamthilia za kiubwege hazina wahusika wa kuhalisia; wahusika huwa wa kidhahania na hawatendi chochote bali hukaa na kujihusisha katika mazungumzo ya masuala kidhahania. Wahusika wa kiubwege hawawezi kutambulika au kuonekana katika mazingira ya kuhalisia, huwa wamebuniwa tu akilini mwa mtunzi ili kuendeleza mawazo na lwngo lake. Udhahania wa wahusika wa kiubwege katika maongezi yao unaifanya hadhira iwacheke na katika hali hiyo, wanajicheka wenyewe kwa namna wanavyoendesha maisha yao kiubwege; maisha yasiyokuwa na mantiki, mwelekeo wala umuhimu wowote. Maisha yao yanaendeshwa kupitia kwa ndoto au vitu vya kufikirika tu pasipo utekelezaji wowote.

Wahusika wanopatikana katika tamthilia ya *Amezidi* ni wa kinjozi. Mwandishi amewaumba wahusika wake kindoto na matendo na mazungumzo yao yakikiuka hali halisi. Mwandishi anatueleza kuwa;

Tendo linatokea mawazoni na uhalisini...Pangoni. (uk 4)

Kadhalika, katika onyesho la pili, anaeleza kuwa;

Tendo hili lote linatokea ndotoni mwa Amen a Zidi. (uk. 12)

Matukio yote katika tamthilia ya *Amezidi* yanatukia kidhahanifu. Wahusika wamo pangoni lakini wanabuni mandhari mbali mbali mawazoni mwao. Mara pango linakuwa Kasri lenye vitu vya samani vya gharama ya juu kinyume na uhalisi wa mazingira yao. Tunamkuta mhusika Mari akikiri kwamba kasri ni la kindoto, tunaambiwa;

Zidi: Unalidharau kasri zima na mwenye kasri lenyewe...

Mari: Kasri la ndoto

Zidi: Kasri bainifu...kasri la mashiko ya dhahiri!

Mari: Naam...Mwenye macho...

Zidi: Haambiwi tazama...(uk. 21)

Hapa tunapata kwamba kasri ya Zidi ni kasri la ndoto tu bali si kweli. Hata yeye mwenyewe anakiri kwamba Mari ana macho na hapaswi kudanganywa huku akitazama; ana uwezo wa kuona kwamba wamo pangoni na wala si kwenye kasri.

Aidha, sifa ya wahusika wa kinjozi inapatikana katika tamthilia ya *Beluwa* kwa kuwa kuna baadhi ya matendo yanayoelezwa kuwa yanatokea ndotoni. Hususan kwenye onyesho la nane, mwandishi anaeleza;

Tendo hili linatukia ndotoni mwa Beluwa. Tanda na Mtu wanachukulia kama mchezo. Ni mle mle chumbani, rumande.
(uk. 82)

Tamthilia za kiubwege hujikita katika mawazo, na mambo ya kufikirika tu, ya kidhahania. Mohamed anaafikiana na mkabala huu anapoanza maonyesho yake kwa mawazo na ndoto nyingi. Aidha, Kyovi hajaachwa nyuma katika suala hili, mara nyingi anatumia wahusika waliomo usingizini, wanaozungumza wakiwa bado wanalala na kufumba macho, hivyo matukio hayo yanajitokeza bila ya mmoja wa wahusika hao kujua. Tunapata mfano mzuri katika onyesho la kwanza mwandishi anapoanza kueleza kuwa;

(Tendo hili linatokea ndani ya chumba cha takribani futi kumi mraba; rumande. kuna mtuhumiwa Beluwa aliyelala sakafuni.

Anazungumza kwa fujo lugha isiyoieleweka akiwa amelala fofofu akigaragara sakafuni...)

Beluwa: (anasema akiwa amelala) Tafadhali niambieni kuwa ni ruya; ni jinamizi tu... (uk.1).

Udhahania hudhihirisha ukosefu wa uhalisia ambapo, hufanya wahusika wa kiubwege wanaamini na wanasisitiza vitu visivyo kuwepo. Vile vile, katika tamthilia ya *Beluwa*, wahusika wanajipata wakipanga harusi ya kifahari ilhali wapo kwenye rumande. Tendo hili linajitokeza katika onyesho la tano tunaambiwa;

Tanda: Na watakapogundua baadaye? Wajua harusi yetu itakuwa ya kukata na shoka, yaani harusi ya kimataifa. Wageni watafika kutoka pembe zote za dunia. (anazunguka kuonesha pembe zote) lazima sifa za harusi hii zigonge vyombo vya habari...(Uk.49)

Hii ni harusi ya ndoto ambayo haiwezi kutekelezwa katika mazingira ambayo wahusika katika *Beluwa* wanapatikana. Harusi ya kimataifa inayotangazwa kwenye vyombo vya habari haiwezi kufanywa gerezani kwenye chumba cha futi kumi mraba; hii ni ndoto inayodhihirisha kuwa wahusika hawa wanatawaliwa na ubwege. Kadhalika, harusi hii tunaelezwa kwamba haitahudhuriwa na watu wenye ufukara; ni ya watu mashuhuri walio na majina ambayo yakitajwa yanatikisika. Hoja hili linathibitishwa na kifungu kifuatacho;

Tanda: ...Harusi yetu hii si ya *every Tom, Dick and Harry*. Itahudhuriwa na wateule wachache wenye ushawishi mkubwa. Majina ambayo yakitajwa kunatikisika.
Beluwa: Kama ni hivyo, sharti tuliandae vilivyo. (Uk.53)

Kutokana na mhimili wa nadharia ya ubwege, wahusika husisitiza mambo yasiyokuwepo yaliyojaa ndoto zisizoweza kufikiwa hivyo, wahusika hawa licha ya kuwa rumande; yenye mazingira machafu, bado wanajipata wakipanga harusi ya kifahari. Tendo hili basi huonyesha maisha ya kiubwege ya wahusika hawa.

Kutokana na tamthilia ya *Amezidi*, tunawapata Amen a Zidi wakiamini kwamba maisha yao ni ya utajiri na kasri lao ni kubwa na limejaa vifaa vya samani na mapambo ya gharama ya juu. Zaidi ya hayo, unaelezwa kwamba lao lina wasaidizi wa kazi na wanaishi kwa raha na starehe. Hata hivyo ukweli ni kuwa hawa wahusika wanaota, na vifaa wanaozungumzia ni ndoto tupu. Wanaishi kwenye pango; mahali ambapo pamejaa umasikini na ukosefu wa vitu vya lazima kwa maisha ya binadamu ndiyo maana wanaomba msaada za nchi za nje. Wahusika hawa wanaota ndoto za uboreshaji huduma za kijamii, miundombinu na utokomezaji wa umasikini lakini hushia tu kwenye ulimwengu wa kidhahani abila utekelezaji wa aina yoyote ile. Katikaonyesho la tano, tunaelezwa hivi;

Tendo limo fikirani...pango linageuka ofisi, Ame ni boshi na Zidi, Msaidizi wake. Ame ameketi nyuma ya meza yenye simu isiyokuwepo...kwa kweli ameketi chibi sakafuni...Matendo yanatokea ndotoni mwao. (Uk.40)

Hali kufikiria mambo yasiyooneka au yasiyokuwepo inajitokeza pia kupitia mhusika Boshi ambaye tunaelezwa;

Boshi: Anatoa orodha ndefu kwenye mtoto wa meza isiyokuwepo. Anampa msaidizi wake aisome orodha yenyewe nayo haionekani. (uk. 42-43)

Hapa tunaonyeshwa orodha ndefu isiyokuwepo juu ya meza isiyokuwepo. Orodha hii inafikiriwa kuwa mahitaji ya kiofisi. Wahusika wa kinjozi hutekeleza shughuli za maisha yao katika ulimwengu dhahania usio na uhalisia wowote; hiki kipengele cha ubwege.

3.4.3.1.2 Wahusika Vibonzo

Usawiri wa wahusika vibonzo wasioweza kutekeleza chochote kipengele cha ubwege. Wahusika wanaonyeshwa wakiwa wamekaa tu bila kufanya juhudi za kujitafutia ukombozi kutoka kwa ulimwengu katili unaowazunguka. Kufanya mambo rahisi kama vile kumenya mhogo, kuwasha moto, kujitafutia chakula na hata kujikimu

kimaisha kunawashinda wahusika wa kiubwege. Binadamu wa kiubwege wanakaa tu bila kutenda huku wakizungumza masuala ya kindoto yasiyoweza kuwasaidia; mara nyingi wanategemea misaada isiyoaminika ambayo inawaangamiza zaidi. Kwa kuongozwa na mihimili ya nadharia ya ubwege kwamba wahusika wa kiubwege hukosa uwezo na nguvu ya kuweza kuboresha hali ya maisha na hawana uwezo wa kutekeleza chochote, tunabaini kwamba tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* zimejengwa kwa kutumia wahusika vibonzo ambao wanajipata katika ulimwengu duni, wa kinasibu na unaokatisha tamaa.

Kwanza, katika tamthilia ya *Amezidi*, Mohamed anawasawiri wahusika vibonzo ambao wanashinda wakilala na kuepukana na juhudi za kufanya kazi.

Ame: (Anakoroma) Khhhh...khhhh...

Zidi: (Anaingia na mihogo miwili mkononi) Mtazameni... bado...bado tu amelala. (Anamtikisa)

Ame: (kwa hasira) Ni...ni...nini bwana!

Zidi: Kumekucha!

Ame: Kumekucha? Tokea lini?

Zidi: Aa, haya...bado...bado kabisa! Hakujacha kamwe...(Anatikisa kichwa kwa kukata tamaa) Jua liko utosinina kila mtu amesharauka, wewe bado tu umo... (Uk. 4)

Kwa binadamu wa kiubwege, hakukuchi. Maisha wanayoyaishi yanadhihirisha usingizi usiokuwa na kikomo ndiposa tunampata mhusika Ame akikoroma huku jua lishafika utosini ambapo kila mmoja anapaswa kujishughulisha na kazi zake. Aidha, kando na usingizi usio na kikomo, tunapata wahusika hawa wakitafuna mihogo mibichi iliyovunda pamoja na maganda yake kwa sababu ya kukosa kisu; hata kutafuta kijiti cha kumenyea mihogo kunawashinda na kufikia uamuzi wa kutumia kucha ambayo pia hawawezi. Tunaambiwa;

Ame: ...Tena huu mhogo safi...bado haujavunda...(Anacheka kwa kejeli)

Zidi: Haujavunda...haujavunda...mhogo haujavunda! (Anainuka na kuimba na kucheza na kushangilia)

Ame: una kisu?

Zidi: si unajua nyumba hii haina kisu?
 Ame: kwa nini?
 Zidi: Hatujakiagizia kutoka Marekani. (Uk. 9-10)
 ...
 Ame: sasa tutafute kijiti basi.
 Zidi: nenda katafute kijiti, bwana...
 Ame: kijiti, kijiti, kijiti cha nini?
 Zidi: kumenye mhogo...
 Ame: Kwani kucha huna? Tumia kucha bwana...
 Zidi: Haya (Anamwendea na kumpa ile mihogo miwili) imenye kwa kucha basi...
 Ame: Aaaaa, hata kumenya kwa kucha zako umeshindwa...
 Zidi: ...(anatafuna mhogo wake mbichi naye) (Uk. 10-11)

Wahusika katika *Amezidi* wanategemea kupewa misaada ya vitu vyote hata vile vidogo vidogo wanavyoweza kujitafutia wenyewe kama vile, kiberiti, kijiti na hata kisu. Kukosa kutenda kunawafanya kukwama kimaendeleo na kuishi katika maisha ya kutegemea misaada kutoka kwa nchi za ng'ambo na kuwaongezea matatizo ya kiafya.

Hebu tuangalie kifungu kifuatacho;

Ame: Njaa!
 Zidi: Njaaaaa! Aaaaa, naumia! (Naye anaanguka chini na kugaragara... wanafurukuta na kugaragara chini pamoja. Mara pu! Paja la nyama ya ng'ombe linawaangukia mbele yao. Haijulikani linatoka wapi.)
 Ame: Ah, msaada (Amepata nguvu alipoliona paja la nyama. Anainuka haraka)
 Zidi: Msaada! (Anabwata) Ndiyo, msaada! ...
 (Uk. 69)

Ame na Zidi wanategemea msaada Paja la nyama ya ng'ombe lililooza ambalo linawaathiri kiafya na kuwaongezea matatizo ya kiafya katika ulimwengu wao wa kiubwege. Licha ya uvundo unaotolewa na nyama hii, wahusika hawa wanashukuru wanaotoa msaada na hata kuwaona kama wenye huruma, tunaambiwa;

Ame: msaada enh!
 Zidi: Wana huruma, hawa EC!
 Ame: Wana huruma enh...
 Zidi: Mmmmf! (*Anaziba pua na kuliachia paja la nyama lianguke chini.*)
 Ame: Nini?
 Zidi: Linanuka Uvundo!
 Ame: Uvundo?

Zidi: Limeoza (Uk.71)

Ame na Zidi wakishapata msaada wa paja la nyama ya ng'ombe lililooza, bado wanaonyeshwa wakiwa katika hali hatari kwa sababu wamekosa kibiriti, mafuta, kuni na hawajui kuwasha moto ndiposa wanakula nyama yenye uvundo ikiwa mbichi; maisha ya binadamu yakilinganishwa na wanyama wasioweza kujitegemea wala kutekeleza chochote ni kipengele cha ubwege. Kutafuna nyama mbichi kama fisi ni ubwege. Vifungu vifuatavyo vinathibitisha dai hili;

Ame: Huna kibiriti? Huna mafuta? Huna moto? Huna kuni?

Zidi: Kibiriti, mafuta, Kuni...Kwa nini havikuletwa na kige, hili paja la ng'ombe kutoka EC? (Uk. 71)

Zidi: Una meno?

Ame: N;na meno!

Zidi: Tuwe simba basi...

(wanalitafuna paja la nyama mbichi iliyooza) (uk. 72)

Kwa kutafuna paja la nyama mbichi iliyooza, wahusika hawa wanadhihirisha kwamba wahusika hawa wamekosa uwezo wa kuboresha hali zao licha ya kupewa misaada.

Wanajitokeza kama vibonzo visivyoweza kutekeleza chochote cha maana; wanaishi katika maisha ya utegemezi ambayo huakisi ubwege wao katika ulimwengu wa kiubwege.

Vile vile, kutokana na mkabala wa ubwege, wahusika wa kiubwege hawapati nafasi ya kutenda mambo yaliyo na maana. Wahusika wa kiubwege hukwepa kutenda bali wanaketi na kuzungumza mambo yasiyo na mantiki. Aidha Ame na Zidi wanaonyeshwa kama hawatendi chochote cha maana kinachoweza kuwanufaisha. Wanachorwa wakiwa wamekwama katika matatizo mengi yakiwemo umaskini, ukosefu wa maarifa na ujuzi na magonjwa yanayosababisha vifo. Licha ya matatizo haya yote, hatuwaoni wakijaribu kujinasua kutoka kwa minyororo ya uduni na ukatili

wa ulimwengu wa kiubwege wanamoishi. Wanalolifanya aghalabu ni kulala tu huku wakijihusisha na mazungumzo yasiyo na maana wala mantiki. Kwa mfano tunapata;

Ame: Kwa nini mtu apende kazi? Mungu yupo na ardhi ipo... na ardhi yenyewe bikra.. ikidondoka mbegu tu imeshaota! Ikiatika kambu za migomba kesho utakula ndizi: n ahata mwaka mzima ardhi inakubali tu, haichoki... Wewe kula tu na kulala! Ah, hata Mungu alifanya kazi siku saba, kisha akapumzika...wewe ulilala siku ngapi vile?

Zidi: Siku tisa kama wewe! (uk.7)

Kifungu hiki kinadhihirisha kwamba binadamu wa kiubwege hapendi kutenda. Utendaji katika ulimwengu wa kiubwege ni kitu kisichothaminiwa; watu huishi kwa sababu wapo bila kutenda chochote kama ilivyo katika nadharia ya ubwege.

Katika tamthilia ya *Beluwa*, Beluwa na Tanda pamoja na Mtu, hawafanyi kile kinachoweza kuwanufaisha au hata kuwatoa rumande bali wanashinda wakizungumzia masuala yasiyoweza kuwaokoa. Wahusika hawa kila mara wamo kitandani ama sakafuni wakilala. Katika onyesho la kwanza, tunaanza kwa kuonyeshwa mhusika Beluwa akiwa amelala sakafuni huku akizungumza kwa fujo lugha isiyoeleweka; hii inadhihirisha kwamba binadamu wa kiubwege hajielewi na maisha yake yamejaa zogo na fujo isiyoweza kuepukika. Tunapata maelezo yafuatayo mwanzoni mwa onyesho la kwanza;

“Tendo hili linatokea gerezani ndani ya chumba cha takriban futi kumi mraba; rumande. Kuna mtuhumiwa-Beluwa aliyelala sakafuni. Anazungumza kwa fujo lugha isiyoeleweka akiwa amelala fofofo akigaragara sakafuni...” (Uk. 1)

Mhusika Beluwa anasawiriwa akiwa ametosheka maisha ya gerezani ndiposa analala fofofo kwenye sakafu. Hasumbuliwi na jitihada za kutafuta mbinu za kujikomboa kutoka gerezani; kwake, mazingira yale yanapendeza na kufurahisha na hivyo yanaweza kutuliza roho ya binadamu asiyejielewa. Kando na Beluwa, wahusika

Tanda na Mtu pia wanaonyeshwa wakiwa wamelala katika onyesho saba na nane; tunaelezwa;

“Mahali ni mle chumbani, rumande. Tanda na Mtu wamelala...”
(Uk.78)

“Tendo linatukia ndotoni mwa Beluwa... Tanda na Mtu wamelala pia” (Uk.82)

Kipengele cha kuwa kwenye usingizi bila kutekeleza chochote ni kipengele cha ubwege na hudhihirisha kwamba binadamu wa kiubwege ni kama vibonzo visivyojua vya kutenda wala wakati wa kuvitenda. Waaidha, Kyovi anaonyesha jinsi ambavyo nchi za kiafrika, hutegemea ufadhili wa kila mara, na hawawezi tenda bila kusaidiwa. Wanaonyeshwa kukosa hata soksi za miguuni kwa wachezaji wao. Hii inaonyeshwa katika onyesho la tatu, kupitia kwa Mtangazaji (Tanda) na kuonyesha umasikini wa Beluwa (timu ya Beluwa).

Beluwa: Lakini...lakini hatuna...

Mtangazaji: (kwa sauti ya huzuni, bado akiigiza matangazaji)
Yasikitisha, mtazamaji, yatia simanzi, msikilizaji, maanake mpira hauchezeki bila soksi miguuni...inaonekana wanafanya mashauri ili kina Beluwa wakopeshwe soksi...

Beluwa: (akimkatiza kauli) mbona hatuna soksi?

Tanda: (kwa beluwa) Umasikini. Beluwa: Una hakika?

Tanda: Kuliko kifo! (akigeukia hadhira) Wamekosa wafadhili, tuseme hawana imani nao tena. Ati ni wa binafsi na wadanganyifu. Hawafuati sheria za ufadhili...(uk.22-23)

Licha ya kwamba timu ya Beluwa inapewa msaada wa soksi za kuchezea, bado wanaonyeshwa wakiwa usingizini; hawawezi kutekeleza chochote. Tunampata mlinda lango wa timu hiyo akiwa anasinzia huku mpira unachengwa na timu ya Tanda kwa nia ya kufunga goli. Kwa bahati nzuri, mpira unatoka nje. Hapa tunapata mlinda lango wa kiubwege asiyejielewa wala kufahamu muktadha husika. Tunaambiwa;

Mtangazaji: ... Mpira sasa unaelekezwa kwenye lango la Beluwa. Ni hatari kabisa, hatari langoni. Hatari kwa usalama, maana mlinda lango anasinzia. Ni kama anayeuguza shibe...lakini, Ahaa! Unatoka nje

Isitoshe, Kyovi ametumia usingizi kudhihirisha kwamba binadamu wa kiubwege amekwama kimaendeleo na hata akipata msaada wa kila aina hawezi kuboresha hali yake. Hawa ni watu masikini ambao wanatazamia kupewa msaada wa kigeni ila, tunawapata wakiandaa harusi ya kimataifa ambayo itahudhuriwa na watu waheshimiwa na walio na majina tajika. Mipango hii yote yanatokea mawazoni bila kutekelezwa; wahusika hawa bado wanabakia mle mle gerezani kwenye chumba cha futi kumi mraba; rumande kama ilivyo katika *Amezidi* ambapo wahusika wanajiona wakiwa kwenye kasri badala ya Pangoni. Hatuonyeshwi wakitafuta mbinu za kujikomboa kutokana na umasikini mkubwa unaotawala maisha ya pangoni; kwao wanaboresha maisha yao kindoto bila ya kutekeleza chochote kama ilivyo katika nadharia ya ubwege.

3.4.4 Ukosefu wa ruwaza za mazungumzo

Mazungumzo ya kubwabwaja ni kigezo cha nadharia ya ubwege. Maelezo yanayotolewa na wahusika hayafuati mantiki na hivyo wanashindwa kuelewana na kuwasiliana. Mazungumzo yenye manufaa ni yale yanayoweza kupitisha ujumbe kwa njia mbali mbali lakini tunavyopata katika mkabala wa ubwege ni kinyume. Maongezi ya wahusika huwa hayana muwala, mantiki wala umuhimu. Wataalamu wa nadharia ya ubwege wanashikilia kwamba kwenye kazi za kiubwege, kuna ukosefu wa ruwaza za mazungumzo; dai ambalo limeongoza uchanganuzi wa kigezo hiki.

Badala ya wahusika waliokuzwa katika tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* kkujishughulisha na kazi, wanachukua muda mwingi kuzungumzia masuala yasiyo kuwa na umuhimu wowote. Kigezo cha mazungumzo ya kubwabwaja; yasiyoleta uelewano ni suala nyeti katika tapo la ubwege. Hali ya mtunzi kuwasawiri wahusika dhaifu wasioweza kuelewana kwa mambo madogo madogo yanayokosa mantiki, ni

kipengele cha ubwege. na ambayo hukosa mantiki ya mazungumzo, ni kigezo muhimu kinachokuza hali ya ubwege. Kijumla, wahusika kama hawa wanatatiza mawasiliano kutokana na kuingiza masuala ambayo hayana uhusiano nay ale yanayokithiri.

Kigezo cha ukosefu wa ruwaza za mazungumzo kinajitokeza wazi kwenye tamthilia ya *Amezidi* na kifungu kifuatacho kinathibitisha dai hili;

Zidi: ...(Anageuka na Ame anatazama suruali ya Zidi na kucheka, suruali ya Zidi imechanika makalioni!!!)

Ame: Suruali au ghuba?

Zidi: Suruali! (Anageuka na kujitazama makalioni)

Ame: Suruali imeliwa na panya...

Zidi: Panya ameliwa na suruali...na nyani haoni ghubaye... (Ame anacheka)

Ame: Suruali imeliwa na panya na hapa hapana nyani...

Zidi: Aha...Unasema mhogo uliovunda? (Uk.5)

Hapa tunawapata wahusika Ame na Zidi wakibishana kuhusu suruali iliyochanika ikiwa imeliwa na panya au la. Kinachoshangaza ni kwamba hata Zidi hajui kwamba suruali aliyovaa imechanika. Badala ya kutatua suala la suruali iliyochanika, Zidi anaingiza suala lingine kuhusu mhogo uliovunda; ambalo huwa tofauti na kile walichokuwa wakizungumzia. Mara suruali imeliwa na panya, mara panya ameliwa na suruali na kisha mhogo uliovunda. Tunachojiuliza ni kuwa suala la suruali ambalo halikutatuliwa linaingilianaje na mhogo uliovunda? Hakuna uhusiano wowote na hivyo huzua kipengele cha ukosefu wa ruwaza za mawasiliano kama ilivyo katika nadharia ya ubwege.

Kadhalika, Mohamed ametumia mazungumzo ya kiduara. Wahusika Mwalimu na Mwanafunzi pia wanajiingiza katika majibizano ya kiduara yasiyo kuwa na mantiki. Tunaambiwa;

Mwanafunzi: Suala?

Mwalimu: Jibu
 Mwanafunzi: Jibu
 Mwalimu: Suala
 Mwanafunzi: Sawa
 Mwalimu: Sawa nini?
 Mwanafunzi: Sawasawa
 Mwalimu: Sawa
 (Kimya...)
 Mwanafunzi: (Haonekani) Suala!
 (uk. 29-30)

Mohamed anatupa mwalimu wa kiubwege asiyejielewa na ambaye hafuati kanuni za taaluma ya ualimu; hawezi kuwaongoza wanafunzi kwa njia mwafaka kama inavyotarajiwa. Mwalimu huyu anaulizwa swali na anakosa kulijibu kisha anahusisha mwanafunzi katika mazungumzo ya kiduara yasiyo na mwelekeo. Mazungumzo ya kiduara kwenye kazi ya fasihi ni kipengele cha nadharia ya ubwege; ambapo wahusika wanajihusisha katika mazungumzo yasiyokuwa na maana huku wakizungukia suala moja. Kifungu kifuatacho pia kinathibitisha dai hili, tunaambiwa;

Mwalimu: Mimi nilinyamaa na kusikiliza
 Mwanafunzi: Kusema
 Mwalimu: Kunyamaa
 Mwanafunzi: Kusema
 Mwalimu: Kunyamaa
 Mwanafunzi: Kusema-kunyamaa
 Mwalimu: Hapana, kunyamaa-kusema (Uk.37)

Kutokana na kifungu hiki, hatupati mantiki ya mazungumzo haya. Wahusika wanajipata wakizungumza pasipo na sababu. Mazungumzo ya kubwabwaja yanasababisha kutoelewana na kutofanikisha mawasiliano; dai ambalo linatiliwa mkazo katika mkabala wa ubwege. Hebu tutazame kifungu kifuatacho;

Zidi: Twende wa'?'
 Ame: Nje
 Zidi: Nje!
 Ame: Eh nje!
 Zidi: Si ndani?
 Ame: Si ndani enh!
 Zidi: Ndani
 Ame: Nje

Zidi: Ndani
Ame: Nje (Uk. 47)

Ame na Zidi wanabishana kuhusu ‘nje ‘ na ‘ndani’ kiasi cha kwamba hawajui kutofautisha kati ya nje na ndani. Mohamed anawasawiri wahusika ambao wamepotea na hawafahamu chochote ndiposa wanajihusisha na mawasiliano ya vibonzo; wasiojifahamu kama inavyodaiwa katika nadharia ya ubwege.

Aidha, Kyovi aliwachora wahusika wake wakijihusisha na mazungumzo yasiyo na maana wala mantiki yoyote. Tunawapata Beluwa na Tanda wakibishana kuhusu suala la falasafa hadi inawafikisha katika kumenyana. Mwandishi anatueleza;

Beluwa: (Anagutuka na kuamka) We! Hukubisha?
Unaingiaje hapa hivi hivi tu? Hujui kuwa huku kuna wenyewe?
Tanda: wenyewe kina nani?
Beluwa: Kina mimi
Tanda: Kina wewe au kina nyinyi?
Beluwa: Kina sote
Tanda: Sote? Yaani mimi na wewe... (Uk.3)

Kifungu hiki kinathibitisha kwamba wahusika wa kiubwege hawajui kutofautisha vitu na maana yao; mimi, wewe, nyinyi, sote ni maneno yanayowakanganya bila kujua kwamba ni maneno yaliyo na maana tofauti. Kwa kutumia maneno yasiyofaa katika mazungumzo, mawasiliano yanatatizika na hivyo maana kupotoshwa au hata uelewano kuzuiliwa kabisa kama ilivyo katika mkabala wa ubwege. Mfano ufuatao pia unadhihirisha ukosefu wa ruwaza za mazungumzo;

Tanda: Falsafa, eeh!
Beluwa: Ndiyo, falsafa yetu.
Tanda: Falsafa yenu ni ipi?
Beluwa: Chako n'chetu.
Tanda: Na chako?...
Beluwa: Unanitafuta, Tanda na utanipata bila shaka. (Mwishowe, Beluwa anamrukia Tanda na kumshika ukosi wa shati.Wanaanza kumenyana.) (uk.7-8)

Hapa hatupati jibu la moja kwa moja kuhusu falsafa; hata wahusika wenyewe hawaelewi ni falsafa ya nani. Kadhalika katika onyesho la kwanza, tunaelezwa;

Tanda: Ulimi uliua?
 Beluwa: La! Ulinuia kuua.
 Tanda: Nani?
 Beluwa: Idhilali.
 Tanda: Dhidi ya...?
 Beluwa: Dhidi yangu...yaani yetu.
 Tanda: Dhidi yako au yenu?
 Beluwa: Dhidi yangu ni dhidi yao. (uk.2)

Ifahamike kwamba wahusika wa kiubwege, haina mantiki ya mawasiliano. Mazungumzo yao yanabainisha utengano na hukosa umuhimu. Kawaida kazi ya drama huwa na mantiki ila tamthilia za kiubwege hudhihirisha utengano na upweke wa mazungumzo kama ilivyojitokeza kwenye kifungu hapo juu.

Wahusika wa kiubwege hukosa mtiririko katika mazungumzo yao. Hii huonyesha kwamba maisha ya binadamu katika ulimwengu anamoishi ni kama ajali na hayana maana. Mambo hutokea tu bila kusababishwa na chochote na hayana mpangilio wowote. Ukosefu wa ruwaza za mazungumzo umejidhihirisha kupitia upachikaji wa maneno yasiyo na uhusiano wowote na kile kinachozungumziwa, au hata kwa kuzungukia suala moja mara kadha bila kufikia kiwango cha kulitatua. Hii ni ishara tosha kwamba wahusika wa kiubwege wamekwama na hawana uwezo wa kujinasua kutoka kwa mtego wa ubwege unaowazunguka kama ilivyo katika nadharia ya ubwege.

3.4.5 Utupu

Dhana ya utupu hurejelea uduni wa maisha ya binadamu wa ubwege katika mkabala wa ubwege. Said A. Mohamed katika *Amezidi* anakusudia kuonyesha kuwa binadamu anaishi na amekwama katika maisha duni yanayokatisha tamaa. Kukwama kwa

binadamu bila kutekeleza chochote cha kuboresha hali ya maisha yake duni, ni kipengele cha ubwege. Mtunzi anaanza onyesho la kwanza kwa kueleza yafuatayo;

“Tendo linatokea mawazoni na uhalisini...pangoni...Spotilaiti inafuata wahusika” (Uk. 4)

Mtunzi huyu anatupatia jukwaa lililotupu kuashiria hali mbaya ya utupu katika maisha ya binadamu kwenye ulimwengu katili. Anatumia jukwaa la mawazoni, fikirani au ndotoni kudhihirisha utupu wa binadamu wa kiubwege. Kadhalika, utupu wa binadamu wa kiubwege umejitokeza kupitia mandhari ya pango; ambayo yalitumiwa kuanzia mwanzo wa mchezo hadi mwisho. Pangoni ni mahali pachafu pasipo na nuru, hivyo vitendo vinavyotukia mle lazima viwe vya kukatisha tamaa ili kudhihirisha uduni wa maisha ya binadamu katika ulimwengu wa kiubwege. Mtunzi bado anatumia mandhari yale yale ya pango katika onyesho la pili ambapo tunaelezewa;

“...Pahala ni pale pale pangoni!”(Uk.12)

Tunapata kwamba mazingira ya pango ndiyo yanatawala katika *Amezidi* Hii inaashiria kwamba mtunzi alinuia kuonyesha ubatili wa maisha yake binadamu wa kiubwege; maisha yasiyoweza kuboreshwa bali hutawaliwa kwa ndoto nyingi tu. Maelezo yafuatayo pia yanathibitisha utupu wa binadamu wa kiubwege, aliyekwama kwenye pango; ambalo ni suala muhimu katika mkabala wa ubwege. Tunaelezwa kwamba;

“Tendo limo fikirani...pangoni...Tendo la shuleni...” (Uk.29)

“Tendo limo fikirani...pango linageuka ofisi!” (Uk. 40)

“Tendo limo mawazoni; pangoni...” (Uk. 47)

Ingawa utupu wa kijukwaa umesawiriwa kama tulivyoeleza hapo juu, Mohamed anatupatia wahusika wasioweza kutenda chochote cha maana ila wanasemezana wenyewe kwa wenyewe. Mandhari tunayoyapata katika *Amezidi* yanalingana kuanzia mwanzo hadi mwisho wa mchezo huu.

Aidha Kyovi alisukumwa kuonyesha picha ya jamii iliyoathiriwa na tamaduni za kigeni, jamii isiyojielewa na isiyokuwa na maadili. Wahusika kwenye tamthilia ya *Beluwa* wametumiwa ili waweze kusawiri jamii iliyojawa na uduni na uozo. Wanajipata kwenye rumande, mazingira duni yaliyotengwa na wanaendesha maisha yao kipweke. Mtunzi anathibitishi hili kutokana na maelezo anayoyatoa kuhusu mandhari ya mchezo, anasema kwamba unaigiziwa gerezani, ndani ya chumba; rumande. Wahusika wanabuni mandhari mbali mbali wakiwa mumo humo rumande. Dai hili linaonyesha kwamba tamthilia ya *Beluwa* ni tamthilia ya kiubwege. Kama alivyofanya Mohamed katika *Amezidi*, Kyovi pia hajabadilisha mandhari ila ametumia mandhari ya kidhahania.

Aidha, katika tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa*, utupu pia unajitokeza kupitia kwa mazungumzo ya wahusika; yasiyokuwa na maana, muwala wala mantiki yoyote. Mara kwa mara wahusika hawa hujihusisha na mazungumzo yasiyo na maana; yenye ubatili tu. Maneno wanayotumia hukosa mashiko na huendeleza kuchanganyikiwa kwa wahusika hao. Hii ndiyo sababu kwenye tamthilia ya *Amezidi*, wahusika hushindwa kutoa tofauti kati ya dhana za vinyumekama vile suala na jibu, kicheko na kilio, nje na ndani, mimi na wewe, kulala na kuamka na mengine. Mfano mzuri wa utupu wa kuchanganyikiwa katika *Amezidi* ni Mazungumzo baina baina ya bosu na Msaidizi wake. Tunaambiwa;

Msaidizi: Naam, Bosu nipo kwa ajili yako!

Bosu: Kwa ajili yetu

Msaidizi: Yako

Bosu: Yetu

Msaidizi: Yako

Bosu: Yetu

Msaidizi: Yetu

Bosu: Sawa

Msaidizi: Sawa (Uk. 40)

Hapa tunapata kwamba Bosi pamoja na Msaidizi wake hawawezi kutofautisha kati ya yako na yetu. Mazungumzo yao yanaonyesha utupu na kuchanganyikiwa kwao. Haya ni mazungumzo ya kiduara ambayo yalitumiwa ili kufanikisha kusudi la mtunzi wa *Amezidi* na huzua dhana ya utupu wa binadamu wa kiubwege.

Aidha katika tamthilia ya *Beluwa* mazungumzo ya wahusika hudhihirisha ubwege kwa kuchanganyikiwa katika mawasiliano na kutoelewa mambo ambayo wahusika wanayoyazungumzia, kwa mfano;

Tanda: Ulimi uliua?

Beluwa: La! Ulinuia kuua.

Tanda: Nani?

Beluwa: Idhilali.

Tanda: Dhidi ya...?

Beluwa: Dhidi yangu...yaani yetu

Tanda: Dhidi yako au yenu?

Beluwa: Dhidi yangu ni dhidi yao (uk.. 2)

Kutokana na mifano hii, ni dhahiri kwamba ubwege umejitokeza kwenye tamthilia hizi mbili kupitia kwa suala la utupu katika maisha ya binadamu wa kiubwege, ambacho ni kipengele muhimu sana katika mkabala wa ubwege. Utupu umedhihirika wazi kupitia matumizi ya majukwaa tupu pamoja na mazungumzo ya wahusika yasiyo na mantiki, muwala wala maana na hivyo kutatiza mawasiliano katika ulimwengu wa kiubwege.

3.4.6 Matumizi ya Nyimbo

Matumizi ya nyimbo husaidia katika kuendeleza na kusisitiza maudhui katika kazi ya kifasihi. Said A. Mohamed ametumia nyimbo kama kipengele cha fani ili kuendeleza maudhui yake katika tamthilia ya *Amezidi*.

Ame na Zidi katika onyesho la tatu wanaimba wimbo unaoendeleza majivuno ya waafrika licha ya kwamba wamekwama na wamekosa nguvu za kuboresha maisha

yao duni. Wanajivunia kuwa na rangi nyeusi ambayo inayoonewa fahari na hawa wahusika ingawa haina umuhimu wowote. Mtunzi ametumia wimbo huu baada ya kumsawiri mhusika Mari kama yule ambaye amekengeuka kiasi cha kudharau mambo ya kiafrika. Mari anathamini maisha ya wazungu. Wimbo huu umekashifu waafrika ambao wanadunisha hali yao na kufuata hali za kigeni. Ame na Zidi wanaimba wimbo ufuatayo;

“Tunaimba wimbo huu wimbo wa fahari na makuu tunaimba kusifu rangi hii ya fuu” (wanaonyesha ngozi zao)...
 Na kazi , ya nini kazi?
 Haina haja kazi!
 Ya nini uvumbuzi?
 Tu huru: tumejitawala!
 Tuna kila kitu...”
 (uk 27-28)

Wimbo huu unadhihirisha suala la kutotenda na maisha ya kindoto ya binadamu wa kiubwege. Huu wimbo umebeba maudhui ya kiubwege yanayoonyesha uhuru wa binadamu wa kiubwege unaotimizwa na ndoto nyingi zisizoweza kufikiwa. Hali ya wahusika hawa yanachukiza sana kwa kuwa maisha yao yamejaa umaskini lakini wanajipa uhuru wa kidhahania kwa kufurahia visivyo vyao kama vile vyakula, magari, vifaru na mavazi. Aidha, tunapewa taswira ya binadamu wa kiubwege kuwa ni binadamu wasioweza kutekeleza chochote bali wanaotegemea msaada kutoka kwa Maulana.

Kadhalika, kwenye onyesho la nne, tunapewa wimbowa Mwalimu na Wanafunzi ambao umetumiwa kuonyesha ukengeushi. Mwalimu amekengeuka kiasi cha kwamba anabadlisha somo la fizikia kuwa la muziki wanaposhindwa kujibu maswali analoulizwa na wanafunzi. Anamwambia mwanafunzi ajibu swali mwenyewe na kudhihirisha ukosefu wa uthabiti wa elimu. Tunaambiwa;

Mwalimu: (Kwa mwanafunzi aliyeuliza suala) Enhe...jibu mwenyewe basi...

Mwanafunzi: Tatizo...Hapana...Ngoja kwanza...(Anacheka) Si tatizo,uzuri ni kwamba...ni kwamba tu matajiri...na tajiri hana haja ya kufikiri, anaweza kuwalipa watu wengine wamfikirie, wamfanyie utafiti, wamvumbulie...sisi matajiri tunapenda njia ya mkato...tunapokea, hatutoi...Badala ya kufikiri, watu wanafikiri kwa niaba yetu; badala ya kuvumbua tunavumbuliwa...badala ya kuunda tunaundiwa...badala yakujaribu tunajaribiwa....

Mwalimu: jibu zuri...jibu zuri...Haya (kwa wanafunzi wote) Imbeni wimbo wa utajiri...

(Wanaimba pamoja na mwalimu wao...)

Tajiri kasimama...

Kalala yu macho!

Au yu macho kalala!...

Tajiri kashiba

Kashiba, kashiba

Ndiyo maana kalala

Huku wengine humpakuwa

Ah-kuvumbua kwa nini?

Alalaye hafikirii, huota!

Ah-kuvumbua kwa nini?

Alalaye huvumbua ndotoni

Ah-na kuunda kwa nini?

Alalaye huunda ruwiyani....". (uk. 33-34)

Said Ahmed Mohamed anatumia wimbo unaoonyesha udhaifu wa binadamu wa kiubwege; kwamba maisha yake yamejawa ndoto na usingizi mwingi. Aidha binadamu wa kiubwege amekengeuka kiasi cha kwamba hawezi kutekeleza wajibu wake katika mazingira yake kama inavyotarajiwa. Mwalimu na mwanafunzi wake wamechanganyikiwa zaidi wanapojipata katika darasa la fizikia na kushindwa kutekeleza shughuli za masomo kisha wanajituliza kupitia wimbo wa tajiri; kwamba wao ni matajiri na hivyo wana vyote wanavyo hitaji hivyo hawana haja ya kufikiria wala kuvumbua, kuunda wala kujaribu. Haya ni mambo wanayotaka wafanyiwe huku wakiendelea na maisha yao ya kindoto. Maisha ya kukaa tu bila kutenda lolote na kutawaliwa na ndoto, ni kipengele cha ubwege. Kadhalika, Wimbo unaodhihirisha ubwege katika *Amezidi* unajitokeza katika onyesho la nane ambapo; tunaonyeshwa

kukwama kukwama kwa maisha ya binadamu wa kiubwege katika ulimwengu katili anamoishi.

“Miaka mia tulikuwa vile vile
 Leo tuko hivi hivi
 Tu papo au tumeendelea
 Tu macho tumelela
 Au tumelala tu macho
 Safari ilikuwa ndefu
 Na ndefu zaidi na zaidi
 Upeo wa usiku ni mrefu
 Hauna mipaka
 Na kiza tunakichekelea
 (Vigelegele wote wawili)
 Kiza tunakisherehekea
 (Vigelegele)
 Kiza kitamu kiza
 Kitamu kiza kitamu
 (Vigelegele)
 Kitamu kwa sababu
 Tumelala usingizi mnono
 Usingizi mtamu
 Lala mama lala
 Lala baba lala...
 (uk. 68)

Katika wimbo huu, Ame na Zidi wanasawiriwa wakiuthamini usingizi; yaani hali ya kutojua au kutoweza kutekeleza chochote cha maana katika maisha yao. Wanawashauri akina mama na akina baba kushinda usingizini bila kugutuka; yaani wasifikirie, wasiunde, wasivumbue, wasitende wala kurekebisha maisha yao duni. Wajistareheshe kwenye usingizi na ndoto zisizoweza kutimizwa.

Ingawa Said Ahmed Mohamed alitumia nyimbo nyingi zilizoendeleza maudhui ya kiubwege, mtunzi huyu anatupatia wimbo mwingine katika kimalizio chake. Huo wimbo ni wa mtoto asiyezaliwa, ambao umebeba maudhui ya matumaini. Hii ni maudhui yanayokiuka kanuni au mkabala wa ubwege. Kiubwege, suala la tumaini linatupiliwa mbali na kukata tamaa kunatiliwa mkazo. Kwa kuanzia anwani ya wimbo huu ‘*Wimbo wa mtoto Asiyezaliwa*’, tunapata mama mjamzito anayetazamia kuzaa.

Hali ya kuwapa wahusika matumaini ya siku zijazo inakiuka kaida za ubwege. Kutokana ubwege, drama za kiubwege hutazamia kuweka binadamu katika hali ya kukatisha tamaa. Tunaimbiwa kuwa:

“Huu ni mwendelezo
 Wa uhai wa watakao kuishi
 Kuishi na siyo kuwepo!...
 Huo mwisho ukifika,
 Maiti wote ‘tafufuka
 Vipofu wataona
 Visiwi watasikia
 Mabubu watasema
 Vichaa watatengama
 Wajinga ‘taarevuka
 Na wal’olala ‘taamka...”(uk. 86-87)

Kupitia wimbo huu, Said Ahmed Mohamed anawapatia wahusika wake walioshinda usingizini tumaini la kuamka siku ya mwisho; kwamba hiyo siku watagutuka usingizini, watafufuka kutoka kwa ulimwengu uliojaa giza, watakuwa na uwezo wa kuzungumza na kuelewana, wataarevuka na uchaa wao utakwisha. Hali hii inapinga kaida za mkabala wa ubwege.

Ni dhahiri kwamba, wimbo tunaopatiwa hapa sio unaokatisha tamaa japo kwa kiasi fulani mtunzi alitumia wimbo huu kukiri kwamba wahusika wake wamekufa, ni vipofu, viziwi, mabubu, vichaa, wajinga walioshinda usingizini tangu wajikute katika ulimwengu katili. Taswira ya wahusika tunaopatiwa kupitia wimbo wa mtoto asiyezaliwa inatudhihirishia wahusika duni, vibonzo ambao wameitwa maiti, wasioweza kuona uhalisia wa mazingira yao duni (Vipofu), wasiokuwa na uwezo wa kusikia, kuelewa na kutafakari masuala rahisi (Viziwi), wasioweza kunena (Mabubu), wasiojielewa (Vichaa) na wajinga wanaothamini usingizi wa kutojua.

Halikadhalika, katika tamthilia ya *Beluwa*, Kyovi pia ametumia nyimbo na mashairi. Kuna matumizi ya nyimbo na mashairi kadhaa katika kazi hii. Mthalaan, katika

onyesho la nne, kuna wimbo "*Malaika*" ambao unacheza kwa mahadhi ya wastani. Wimbo huu umetumiwa ili kudhihirisha ukengeushi wa wahusika wa kiubwege kwa kukuza tukio la mahaba kaburini. Mhusika Tanda anaanza kuuimba wimbo huo na kuanza kuonyesha hisia zake kwa Beluwa; tukio ambalo lilidhihirisha ubasha ambao ulitumiwa kama njia ya kumtuliza na kumstarehesha binadamu wa kiubwege. Tunaambiwa;

Wote: Mahaba! Kaburini (Wanaangaliana)
 Kaburini (wanainamisha vichwa halafu wanaanza maigizo.
 Wimbo, 'Malaika' unasikika ukicheza kwa mahadhi ya
 wastani)
 Malaika, nakupenda Malaika
 Malaika, nakupenda Malaika...(uk.36)

Wimbo huu huonyesha mahaba na hutoa picha ya tabia zake Tanda jinsi ilivyoathiriwa na mazingira na utamaduni aliolelewa. Alikuwa anamwona Beluwa kama chombo cha mahaba na mashine inayoweza kumstarehesha mwanamume. Tunaelezwa,

Wote: ...(Tanda anaanza kuimba kwa sauti ya chini kufuatana na mdundo wa muziki huku akielekea aliko Beluwa. Beluwa anamtazama tu bila kuonesha hisia zozote)
 Nami nifanyeje, kijana mwenzio,
 Nashindwa na mali sina wee,
 Ningekuo mlaika.
 (Tanda anamshika Beluwa mkono. Wanaanza kucheza taratibu)
 Kidege hukuwaza kidege,
 Ningelikuwa na uwezo,
 Ningekuo kidege,
 Nashindwa na mali sina we,
 Ningekuo kidege.
 (Tanda anamwachilia Beluwa haraka)

Beluwa: We! mbona unaniachilia haraka hivyo kama kiasi moto!

Tanda: umenichoma...nakuenzi, Beluwa (Beluwa anaduwa. Ni kama asiyeuelewa tena mkondo wa maigizo)

Tanda: (Akiendelea kuimba wimbo kwa hisia nzito huku akipiga magoti)

Pesa, zasumbua roho yangu,
 Pesa za tingisha roho yangu,
 Ningekuo kidege,
 Ningekuo Malaika,

Nashindwa na mali sina we,
Ningekuoa malaika. (Uk. 36)

Wimbo huu ulijitokeza katika maigizo kuhusu mahaba kaburini ambayo yalionyesha uhuru wa binadamu wa kiubwege. Tanda na Beluwa wote ni wanaume lakini wanajiona kuwa wa jinsia tofauti. Tanda anamwona Beluwa kama msichana mrembo ambaye anapaswa kuwa kitulizo cha roho yake; wanajitafutia starehe za kimahaba licha ya kuwa gerezani ambao ndio uhuru wa kiubwege.

Kando na wimbo huu, kuna wimbo wa harusi uliokuwa ukiimbwa na Tanda na Beluwa.

Tanda: (anaimba kwa furaha. Mdundo wa muziki anaoimba unasikika)
Shangilieni harusi,
Lalala, lala, lalala, lalala,
Harusi ya mtoto wetu,
Lalala, lala, lalala, lalala.
(Beluwa anajiunga na Tanda, wanaimba na kucheza) (uk.56)

Wimbo huu kidogo hukiuka ubwege kwa sababu masuala yanayozungumziwa yanaelekea kuwa ya kiuhalisia, kwa mfano ubikira, malezi mema na elimu. Kwa upande mwingine wimbo huu una ubwege kwa sababu maneno mengine yameingizwa japo hayana maana katika muktadha wa huu wimbo. Maneno yanapojitokeza bila mpango katika mazungumzo au wimbo basi ubwege hujitokeza kwa mfano;

(Beluwa anajiunga na Tanda, wanaimba na kucheza)
Tumemlea wenyewe mpaka siku ya kuolewa,
Leo, leo, lalala, lala, lalala, lalala,
Hakudanganywa na waume,
Nayo elimu tukampa,
Hakudanganywa na kaburi wala anasa za mjini...(uk. 56)

Katika wimbo huu neno kaburi limeingiza kwenye wimbo huu bila maana na mpango. Hii hutokana na sababu kwamba wahusika hawa ni wa kiubwege hivyo, wanachangamkia na kusherehekea masuala ya kifo au neno lolote linalohusiana na kifo.

Aidha, Kyovi ametumia wimbo wa Beluwa kuonyesha wazi utupu wa wahusika wake. Mhusika Tanda anasawiriwa kama mtu asiyeweza kusema mambo ya maana, anaropokwa tu na maneno bila mpango. Kwa mfano; Beluwa anaimba;

Domo tupu, domo tupu,
Kama kwako nilikuwa,
Leo naketi kwa mwenza,
Mapenzi amesomea,(Uk.62)

Utupu katika kazi za fasihi hudhihirisha uduni katika maisha ya binadamu wa kiubwege; asiye na chochote cha kumnufaisha katika ulimwengu anamoishi. Kupitia wimbo huu, mhusika Beluwa anaonyesha msimamo wake kuhusu uhusiano wake wa kimapenzi. Anasema kwamba ameshapata mpenzi mwingine (Mtu) ambaye ana ujuzi kuhusu masuala ya kimapenzi kumshinda Tanda. Beluwa anapoimba kwamba Tanda ni domo tupu, anamaanisha kwamba Tanda hana maneno matamu ya kimahaba na hata anaponena mazungumzo yake hukosa mantiki, muwala na maana. Domo tupu huweza kulinganisha na debe tupu ambayo hupiga kelele sana bila kufanikisha mawasiliano. Dai hili linajitokeza katika onyesho la sita, mhusika Beluwa pia anakiri kwamba yeye ni debe tupu lisilo na lolote, anasema;

Beluwa: Debe tupu, mmmh...Asante! Umenikumbusha. Eeeh, debe tupu. Debe tupu ni mimi, mimi hasa! Mimi Beluwa bin Zani ni debe tupu lisilo na kitu. Sina chochote; sina sinani nikiulizwa siungami! Tumbo langu halina kitu. (anashika tumbo) Kauli zangu hazina athari. Moyo wangu hauna hisia. Sina mali sina hali... (Uk. 64)

Hii inadhihirisha kwamba binadamu amekwama katika maisha duni yasiyo na matumaini na ambayo hukatisha tamaa. Beluwa anakiri kwamba yeye ni debe tupu linalopiga tu kelele, lisiloweza kuling'amua suala akiulizwa na hata akitoa kauli hukosa athari. Ni dhahiri kwamba wahusika wa kiubwege wamekwama na hawawezi kutekeleza chochote cha kuboresha hali ya maisha yao duni ambacho ni kigezo cha ubwege.

3.4.7 Matumizi ya vicheko na vilio

Matumizi ya vicheko na Vilio ni muhimu sana katika mkabala wa kiubwege.. Udhahania wa wahusika wa kiubwege katika maongezi yao unaifanya hadhira iwacheke na katika kuwacheka, wanajicheka wenyewe kwa namna wanavyoendesha maisha yao kiubwege; yasiyokuwa na mantiki wala mwelekeo. Wanatapo la ubwege wanashikilia kuwa ulimwengu ni duni, wa kinasibu na unaokatisha tamaa na kuzua hisia zinazodhihirisha uchovu, huzuni na ukosefu wa matumaini. Kutokana na msimamo huu ndipo waandishi wa tamthilia za kiubwege wanatumia vicheko na vilio ili kuonyesha kwamba wahusika wa kiubwege wamechanganyikiwa na kukata tamaa na kughihirisha kukosa matumaini kabisa.

Said A. Mohamed amrtumia vicheko katika tamthilia ya *Amezidi* kudhihirisha ukengeushi wa wahusika wake na kudhihirisha kwamba wamekata tamaa kabisa. Vicheko hivi vimetumiwa ili kusawiri utata wa ukinzano ambao unapatikana katika maisha ya watu wan chi ya Amezidi. Vicheko hivi ni majoho ya kinafiki yanayofunika vilio vyao.

Katika tamthilia ya Amezidi, vicheko vimeambatanishwa na vilio ili kuficha hali halisi inayokabiliwa na wahusika hawa. Badala ya kulia, wahusika wanajipata wakicheka ili kuficha hali halisi ya maisha duni yaliyokosa maana. Katika onyesho la nne, mwandishi anatupatia vicheko na vilio darasani;

Mwalimu: ...Mnacheka tu...kicheko tu...kicheko... kicheko...lakini
mnaloulizwa hamjui; kicheko.

Wanafunzi kwa pamoja Hapana, mwalimu...kilio...kilio...kilio

Mwalimu: Tulie pamoja basi

(Kimya -hakuna kilio)

Mwalimu: Tucheke basi

(wanacheka pamoja)

(Uk. 31)

Wanafunzi hawa wanajipata katika hali tatanishi; mwalimu walionayo ni duni na asiyefaa lolote, hana maarifa na ujuzi wa kuwaelekeza wanafunzi darasani. Anayowafundisha wanafunzi yamekosa maana n ahata wanafunzi wenyewe ni zogo. Wanafunzi hawa wanalia wanapogundua kwamba wamepoteza muda kwa kujidanganya kwamba wanasoma. Said A. Mohamed anatumia kilio ili kuonyesha kwamba wahusika wake wanasikitika kwa kujihusisha na elimu duni ya kukatisha tamaa.

Kwa upande mwingine, tunawapata wanafunzi wakimchekelea mwalimu wao ambaye hana ujuzi wa kuwaelekeza darasani. Inabainika kuwa mwalimu pamoja na wanafunzi hawaelewi mada inayoangaziwa darasani. Tunaambiwa yafuatayo;

Mwanafunzi: (Haonekani) suala!

Mwalimu: Uliza!

Mwanafunzi: Hivi ...hivi baada ya kukariri mawazo ya Archimides kwa miaka mingi, kwa nini hatujaweza kuunda nyambizi?

Mwalimu:(kwa mwanafunzi mwingine asiyeonekana) Nyambizi dude gani? (kicheko cha wanafunzi...kimya...) Hamjui?... Wewe...(Anamwelekeza kidole mwingine asiyeonekana, pia kimya) Aaaaa...(Anakwenda miayo, kicheko cha wanafunzi) (Anakasirika) Mnacheka tu...kicheko tu...kicheko...kicheko...lakini mnaloulizwa hamjui; kicheko

Wanafunzi kwa pamoja: Hapana, mwalimu...kilio...kilio...kilio

Mwalimu: Tulie pamoja basi

(kimya-hakuna kilio)

Mwalimu: Tucheke basi...

(wanacheka pamoja)

Mwalimu: Vizuri.

Mwanafunzi: Kwa vipi?

Mwalimu: Nyambizi.

Mwanafunzi: Amefanyaje?

Mwalimu: Maana yake nini?

Mwanafunzi: Maana yake nini?

Mwalimu: Nakuuliza wewe (Uk.30-31)

Wanafunzi wanamcheka mwalimu wao ambaye hawezi kuling'amua suala analoulizwa. Hata wao wenyewe wanakiri kwamba vicheko vyao ni vilio kwa sababu

walichokitarajia kutoka kwa mwalimu hakupata. Mwalimu naye kwa upande wake anakubali kwamba wanapaswa kulia wote kwa pamoja lakini wanauficha ukweli wa kilio na huzuni kwa kucheka pamoja. Aidha, wanafunzi wanajicheka wenyewe kwa kwa kukosa nguvu za kujisaidia kutokana na ulimwengu wa kutojua. Hawajui lolote na mwalimu wao pia hana msaada wowote kwao. Hali hii inaendeleza imani ya kiubwege kwamba binadamu hukosa uwezo wowote wa kuibadilisha hali yake na maisha yake yamejaa huzuni ambayo husetiriwa kwa vicheko.

Waidha, inadhihirika wazi kuwa, wahusika wa Said A. Mohamed wanacheka ili wafiche vilio vyao kutokana na hali yao ya ukengeushi, kusikitisha, kuhuzunisha na kukatisha tamaa.

Kadhalika, Said Ahmed Mohamed alitumia vicheko kutoa dhihaka na kejeli. Ndoto za maendeleo wanazoamini Ame na Zidi pia zinadhihakiwa kupitia vicheko. Kicheko cha Mari kinakejeli imani potovu za maendeleo zinazofuatwa na Ame na Zidi.

Matendo yao yanawacheka wenyewe. Tunaambiwa;

Ame: Utajiri wetu au sivyo?

Zidi: Enh!

Kicheko cha Mari: Ha, ha, ha...

Zidi: Nani huyo anayecheka?

Ame: Nafsi yako.

Zidi: Nafsi yangu imefanyaje?

Ame: Inajicheka.

Zidi: Labda inajicheka au inatucheka Mimi na wewe.

Ame: Sasa?

Zidi: Sasa nini?

Ame: KuhusuMari

Zidi: Nilimwonesha kasri letu.

Kicheko cha Mari: Ha, ha, ha... (Uk. 24-25)

Vicheko hivi, ambavyo havijulikani vinakotokea vimetumiwa na mwandishi ili kuwakilisha mtazamo wa maendeleo ya kidhahania ambayo yanahitaji wahusika wa kiubwege, Amen a Zidi, wajitolee katika kujijua na kujitambua vyema zaidi ili

waweze kuboresha maisha yao yaliyojaa ujinga na matatizo mengi. Hata hivyo, vicheko hivi haviwasaidii kurekebisha hali zao jinsi inavyotarajiwa. Ni hali inayokuza na kuendeleza vipengele vya drama ya kiubwege.

Kyovi naye kwa upande mwingine, ametumia vicheko kutoka kwa wahusika wake; Beluwa, Tanda na Mtu. Kwanza, mwandishi huyu ametumia kicheko na kulia kwa wakati mmoja katika onyesho la kwanza. Beluwa anajipata akicheka na kulia kwa wakati mmoja. Kicheko na kilio husawiri hali tatanishi ya mhusika huyu. Tutazama mfano ufuatao;

Tanda: ...Mtu anawezaje kuishi miaka mitatu na nusu gerezani?

Beluwa: (kama anayecheka na kulia kwa pamoja) Nimeshamaliza minne! (Uk.2)

Kumaliza miaka minne gerezani hakuonekani kuwa kitu kwake, analia baada ya kutambua kwambua kuwa amechukua muda mrefu gerezani bila ya kufahamu. Mwandishi anakejeli hii hjali ya maisha duni ya gerezani ndiposa ametumia kicheko na kilio kwa pamoja. Kujipata katika hali tatanishi na ya kuchanganyikiwa ni kipengele muhimu sana katika mkabala wa nadharia ya ubwege.

Isitoshe, ukosefu wa ukombozi wa nafsi ni kigezo muhimu sana katika nadharia ya ubwege. Kwa vile wahusika hukosa uwezo wa kujikomboa kutokana na mateso yanayowakumba katika ulimwengu katili usio na huruma, wanajikuta wakicheka vicheko vya kutisha vinavyodhihirisha uduni wao. Kicheko cha Beluwa hadi anadondokwa machozi husawiri hali ya ukengeushi na kukata tamaa kwa vile mhusika huyu hana uwezo wa kubadilisha nia yake hata kujielewa mwenyewe hajielewi. Tunaelezwa kuwa;

Tanda: Ndani ya kaburi mna jeneza; ndani ya jeneza mna mtu. Ndani ya kinywa chamtu mna kasha. Ndani ya kasha mna hazina. Waonaje?

Beluwa: Ha...ha...ha! (anacheka kama mwenye kichaa)

Ha...ha...ha...haa! (anacheka hadi machozi yanamdondoka)
(uk. 5)

Mhusika Beluwa anaonyesha hali tatanishi hivyo anakosa kujielewa na kuchanganyikiwa zaidi. Haelewi hadithi anayosimuliwa na mwenzake Tanda hivyo anajichekelea kwa kutokuwa na uwezo wa kujikomboa kutoka ulimwengu wa kutojua na kutoelewa. Dhana hii hudhihirisha ubwege katika *Beluwa*. Furaha inayodumu haipatikani maishani mwa binadamu wa kiubwege, maisha yake yamejaa huzuni tupu na hivyo wanajituliza kwa vicheko vinavyokejeli maisha yao duni yaliyojaa matatizo yasiyo na kikomo.

3.4.8 Lugha

Kutokana na nadharia ya ubwege, lugha ya sanaa ya kiubwege hairahisishi mawasiliano hivyo husigana na jukumu lake la mawasiliano. Ugumu wa maisha unaashiriwa na ugumu wa mawasiliano katika sanaa ya kiubwege. Lugha hutumiwa kwa sehemu kubwa katika mazungumzo ya kidhahania yasiyo na mantiki wala muwala.

Wahusika wa kiubwege wanapotumia lugha inayotatiza mawasiliano, wanafanya hivyo kimakusudi ili kudhihirisha kuwa lugha imeshindwa na jukumu lake la kimawasiliano; yaani inajirejelea yenyewe. Mazungumzo yanayovunja kanuni za kimawasiliano na yasiyo na mantiki mwafaka ni dhahirisho la lugha inayojirejelea yenyewe kuwa imeshindwa katika kutimiza wajibu wake.

Tamthilia za kiubwege hutazamwa kama vitendawili vyenye mzunguko, vichekesho vinavyosetiri huzuni, kejeli kwa maumivu, mizaha ya kijinga na masihara ya kindoto. Ni tamthilia inayoshikilia kwamba binadamu anaugua kutokana na maambukizo ya

huzuni; amekuwa bubu kutokana na kuporomoka kwa lugha na mantiki, na anaweza tu kuipaaza sauti yake ovyo ovyo kwenye ombwe tupu lisilo na furaha.

Kijumla, lugha ya sanaa ya kiubwege hukwamiza mawasiliano. Hii ndiyo hali inayojitokeza katika Amezidi, ambapo katika onyesho la kwanza, Ame na Zidi wanajadiliana kuhusu suruali ambayo imechanika na hata Zidi ambaye ameivalia hana habari kwamba suruali yake ina kasoro; wahusika hawa wamo kwenye ulimwengu wa kiubwege wa kukosa kujielewa. Tunaambiwa;

Ame: Suruali au ghuba?

Zidi: Suruali.

Ame: Suruali imeliwa na panya.

Zidi: Panya ameliwa na suruali... na nyani haoni ghubaye.

Ame: Suruali imeliwa na panya na hapa hapana nyani...

Zidi: Aha...unasema mhogo uliovunda? (uk. 5)

Haya ni mazungumao yasiyokuwa na mantiki, ruwaza wala maana yoyote. Wanazungumza juu ya suruali ambayo imeliwa na panya; mara panya imeliwa na suruali, kisha ghafla kuingiza mhogo bila kutuonyesha mwingiliano wowote. Haya ni mawasiliano ya kubwabwaja, ambapo lugha na kaida zake huvurugwa ili kuashiria hali ya maisha yenye fujo na kudhihirisha ubwege.

Kadhalika, katika tamthilia ya *Beluwa* vile vile kuna matumizi ya lugha inayotatiza mawasiliano, yaani maneno hujitokeza tu bila mipangilio yoyote na huelekea kukosa maana na mantiki. Kwenye onyesho la kwanza, kuna mfano wa mawasiliano yaliyotatizika na kukosa mantiki;

Tanda: Falsafa, eeh!

Beluwa: Ndiyo, falsafa yetu.

Tanda: Falsafa yenu ni ipi?

Beluwa: Chako n'chetu

Tanda: Na chako?

Beluwa: (hana hakika) N'cha...n'changu.

Tanda: Kwa hivyo ni changu.

Beluwa: La si chako. chako n'chetu na changu n'...ni changu.

Unaelewa?

Tanda: Sielewi kabisa...(uk.7-8)

Hapa tunapata wahusika Beluwa na Tanda wakishindwa kuelewana kwa sababu lugha inayotatiza mawasiliano. Hata Tanda mwenyewe anakiri kwamba haelewi kabisa wanachokizungumzia kumaanisha kwamba lugha wanayoitumia inatatiza mawasiliano. Wanabishana kuhusu falsafa ambayo hawajui ni ya akina nani; hatimaye wanashindwa kutofautisha nafsi na wanajipata katika mazungumzo ya kiduara; ambacho ni kipengele muhimu katika mkabala wa ubwege.

Katika sanaa ya aina hii, tunapata kuwa mawasiliano yanakwamizwa makusudi. Hakuna mawasiliano ya moja kwa moja kwa sababu binadamu ameshindwa kujifahamu, hana uwezo wa kudhibiti uhusiano unaofaa na binadamu wenziwe, au hata na mazingira au ulimwengu wake.

Kusudi la tamthilia ya kiubwege ni kuonyesha kuwa binadamu ameshindwa kabisa kuidhibiti na kuitawala dunia yake sawa na alivyoshindwa kudhibiti chombo chake cha mawasiliano; yaani lugha.

Katika mkabala wa ubwege, ukanganyifu wa lugha unaojibainisha kwenye sanaa ya kiubwege ni jazanda ya ukanganyifu wa jamii na binadamu wasiojielewa. Lugha hutumiwa tu kuonyesha upotevu na kuchanganyikiwa kwa binadamu kwa sababu ya hali ya maisha yake duni ulimwenguni. Binadamu wa kiubwege amepotea kabisa katika ulimwengu katili ambamo anajipata. Kwa wahusika wa kiubwege, mawasiliano hayapo kwa sababu kwao, lugha imekufa na ulimwengu umekuwa ombwe tupu wenye fujo. Tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* kama kazi za kiubwege zinaafikiana na madai haya.

3.4.9 Ploti

Tukimrejelea mwanafalsafa mkongwe Aristotle (1934) katika *The Poetics*, anaeleza kwamba ploti ni kama moyo wa tanzia na ndio huunganisha vitushi; ni mtiririko wa vitushi kuanzia mwanzo, kati hadi mwisho. Mwanzo huelekeza kisa kwa njia ya kupelekea kwa kingine, kati, huendeleza kilichotukia na kuelekeza kwenye kitakachotukia na Mwisho (tamati), huendeleza kilichotukia kwenye kati ila hauhitaji kupelekea kwa kisa kingine, yaani tumetosheka kwamba ploti imekamilika.

Kwa mujibu wa Cuddon (1979), ploti ni ramani, kielelezo, au sampuli ya matukio ya kazi husika ya kifasihi; ni mpangilio wa kisa na mhusika kwa namna ambayo itachochea udadisi na taharuki kwa hadhira na msomaji. Mawazo haya yanawiana na ya Forster (1927) anaposema kuwa Ploti ni usimulizi wa matukio huku mkazo ukiwa kwenye kisababishi. Madumulla (2009), anaunga mkono fasili hizi kwa kueleza kwamba ploti ni mjengeko wa kazi za kisanaa ambao huonyesha namna mtiririko wa mawazo unavyopangwa na mwandishi huku akisisitiza usababishi unaoliwezesha tukio moja kuibua kisa kingine.

Ploti kwa kifupi ni ule msuko wa vitushi na namna vitushi hivyo vinavyosababishana; ni kitu muhimu katika tamthilia. Ploti nzuri, aghalabu hubainika pale ambapo kuna migogoro, na mgogoro mmoja husababisha mgogoro mwingine, na mivutano hiyo ndiyo inayosukuma mbele tamthilia hadi kufikia upeo wa juu.

Tamthilia ya kiubwege hupuuza kipengele cha ploti; hukosa migogoro ambayo tunaweza kudai kuwa imejengwa na kutatuliwa. Kutokana na haya, ni vigumu kubainisha kilele cha kazi ya kiubwege; kinachobainika ni mzunguko wa vitushi. Maishani mwa binadamu wa kiubwege huwa ni tendo la kuzunguka duara lile lile bila

kusonga mbele. Watunzi wa drama za kiubwege huashiria hali hii kwa kutoa ploti mzunguko (duara).

Katika *Amezidi*, wahusika Ame na Zidi wanajishughulisha na vitendo ambavyo vinawafanya kutegemea na kusubiri misaada ambayo inawaongezea matatizo ya kiafya. Kusubiri na kutegemea huku kwa misaada ndicho kipengele muhimu kinachozunguka matendo yao. Hatuonyeshwi vitushi vikisababishana bali matendo yanaendelea kishaghalabaghala na kurudi pale pale yalipoanzia; yaani ni mzunguko wa matendo. Katika tamthilia hii, wahusika wanawasubiri wafadhili wawape misaada kwa mfano msaada wa nyama ya paja la ng'ombe lililooza ambalo halifai katika kutunza afya ya wahusika hawa. Wahusika hawa wana tatizo la umasikini ambapo hata hawawezi kununua kiberiti ya shilingi mbili lakini bado wanapewa nyama iliyoza ambayo inawafanya kuugua magonjwa yanayowashinda kuyatibu na hatimaye wanafikia kaburini. Haya ni maisha ya kimzunguko na ambayo yanaafikiana na mkabala wa ubwege kuwa tamthilia nyingi katika tapo hili huwa na muundo wa kiduara ambapo zinaishia zilivyoanza.

Vile vile katika tamthilia ya *Beluwa*, mwandishi ametumia ploti ya kimzunguko ambapo wahusika wanazungumzia suala la kaburi kila mara na kukaa tu bila ya kutafuta mbinu za kujiondoa kwenye mazingira mabaya ya gerezani. Hakuna jitihada au mikakati ambao wanaweka ili kuwawezesha kujikomboa. Hili ni dhihirisho kwamba matukio ya wahusika hawa hayasababishani, hivyo kuna ploti ya duara, yaani ya kimzunguko. Ploti ya mzunguko huashiria maisha ya binadamu ambayo kiubwege kamwe hayasongi mbele bali yanaendelea kuzunguka duara katili, ulimwengu dhalimu, na ambao humtesa.

Hali ya watunzi wa kiubwege kutokuza wahusika wao inazifanya ploti za tamthilia hizi kutatanisha, wanapuuza suala la ploti na hivyo kuzifanya tamthilia hizi kuwa katika mkabala wa ubwege, tamthilia ambazo zinabainisha mzunguko wa vitushi huku zikipuuza kipengele cha ploti. Tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* zimetumia wahusika wasiokuwa na mielekeo wala nia ya kuboresha maisha yao na hivyo, tamthilia hizi zimeua ploti zao.

Wataalamu wa nadharia ya ubwege wanakiri kwamba, mtindo wa ukosefu wa ploti katika utunzi tamthilia za kiubwege hudhihirisha kuwa maisha ya binadamu ni safari ya kuzunguka kwenye duara. Wahusika katika tamthilia ya *Amezidi* wanazunguka kwenye shida ya umaskini na uombaji wa misaada. Hali hii pia hubainika katika kazi ya Kyovi, ambapo wahusika wake wanazungumzia tu suala la kaburi kila mara bila ya kuchunguza umantiki katika mazungumzo yao. Said A. Mohamed katika *Amezidi* amesawiri wahusika wanaoishi katika pango; pango ni ishara ya mzunguko. Ndani ya pango ni sawa na ndani ya shimo ambamo hamna mwangaza wowote, hivyo basi, Amen a Zidi wanajipata wakizunguka duara lao ovyo ovyo kama vipofu.

Vile vile, katika *Beluwa*, mandhari yaliyotumiwa ni ya rumande, gerezani kwenye chumba cha futi kumi mraba, ambamo hamna uhuru na pia si mahali pazuri kwa maslahi ya binadamu. Hii ni hali ya maisha duni yanayoashiria mateso na utupu wa binadamu ulimwenguni.

Katika tamthilia ya *Amezidi*, matukio yote katika maonyesho yote kumi yanajitegemea yenyewe. Tuchukulie mfano kwenye onyesho la nne, ambapo tukio tunalopewa ni la mafunzo darasani, Zidi akiwa mwalimu na Ame mwanafunzi. Tunaambiwa;

Tendo limo fikirani...pangoni...tendo la shuleni. Zidi ni mwalimu, kaketi mbele ya meza ambayo haionekani. Pana ubao na chaki ambavyo pia havionekani. Ame (mwanafunzi) ameketi kwenye deski lisiloonekana pia. Kuna wanafunzi wapatao sabini. Pia hawaonekani ila Ame tu! Mwalimu Zidi anasinzia huku darasa limejaa zogo la wanafunzi...kitambo...kisha kengele inasikika kulia... Mwalimu Zidi anashtuka kutoka usingizini... (Uk. 29)

Tukio tunalopata katika onyesho hili ni la darasani lakini tukio linalofuata katika onyesho la tano, wahusika hao wako ofisini, Ame akiwa Bosi na Zidi akiwa Msaidizi.

Hebu tutazame maelezo tunayopewa na mtunzi;

“Tendo limo fikirani...pango linageuka ofisi! Amen i Bosi, na Zidi, Msaidizi wake...” (Uk. 40)

Hapa hatupati tukio la nne likisababisha tukio la tano bali kila tukio hujitegemea. Tulitarajia kupata wanafunzi wakifanya mtihani ama labda wakiwa uwanjani wakicheza na shughuli kama hizo lakini tunachopewa ni kinyume cha matarajio hii hutokana kwa kuwa hakuna ploti katika tamthilia za kiubwege na vitushi hujitegemea kipweke. Waaidha, hali hii pia inajitokeza katika tamthilia ya Beluwa ambapo tunapata tukio la mahaba kaburini linaanzia onyesho la nne hadi sita lakini mwishoni mwa onyesho la sita, tunapata tukio la Utangazaji wa habari. Kyovi alikuza tukio moja katika maonyesho matatu lakini tulitarajia kupata vitushi tofauti tofauti katika kila onyesho kama ilivyo katika tamthilia zisizoza kiubwege. Tukio moja likijirudiarudia, huzua ploti ya kiduara ambapo kisa hakielekezi kwa kisa kingine. Aidha, mwishoni mwa onyesho la sita, tunapata wahusika waliokuwa wapenzi wanakuwa wanahabari. Tunapata yafuatayo katika onyesho la nne;

Tanda: Pendo nililonaldo halijawahi kushuhudiwa. Nami sitajizuia kuwa nawe popote niendapo, kwa kuwa ninakupenda. Ninataka nikuo, Beluu. Nipe chanda chako nikuishe pete ya mapenzi yaliyoufurika moyo wangu. (Uk. 38)

Hapa tunapata kisa cha mahaba kaburini kikianza kujengwa ambapo Tanda anaanza kumtongoza Beluwa. Katika onyesho la tano, tunapata harusi ya kifahari ikiandaliwa na wahusika hawa. Tanda anasema;

Tanda: ...wajua harusi yetu itakuwa ya kukata na shoka, yaani harusi ya kimataifa...

Beluwa: Tayari tutakuwa mke na mume. Cha kututenganisha ni mauti tu!

(Uk. 49)

Tanda na Beluwa wameshapendana na wako tayari kuwa mke na mume, tunachotarajia katika onyesho la sita ni maisha yao kama familia au hata sherehe yenyewe ya harusi yao. Hii ni tofauti na kisa tunachopewa katika onyesho la sita ambapo utangazaji wa habari kwenye runinga, Mtu anasema;

Mtu: Ebu, nyamazeni tutazame habari. (Mtu anabonyezabonyeza simu yake. *Screen* ya simu inaonesha kiwambo cha runinga...Beluwa anaketi kitandani kando ya Mtu tayari kutazama habari. Tanda anajifanya ndiye mwanahabari. Anaigiza sauti ya mwanahabari, Zaida) (Uk. 73)

Inadhihirika kupitiahili dondoo kwamba tukio la mahaba kaburini limetupiliwa mbali huku wahusika wakijishughulisha na kisa kingine cha utangazaji habari, ambacho hakiingiliani kabisa na suala la mahaba. Ploti ya matukio katika utunzi wa kiubwege ni ya kimparganyiko ambapo, tukio katika onyesho moja halisababishi kutokea kwa tukio linalofuata tofauti na kama ilivyo katika tamthilia zisizo za kiubwege ambapo matukio hupangwa kimtiririko; yaani husababishana.

3.5 Hitimisho

Sura hii imemulika vipengele muhimu vya kimaudhui na kifani ambavyo hufanya tamthilia ya Amezidi na *Beluwa* kuwa na mwelekeo ulio sawa kiubwege. Aidha tumebainisha kuwa tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* zinaweza kulinganishwa kiubwege kwa kuchunguza vipengele vya kimaudhui na kifani.

Matokeo yanaonyesha kwamba Said A. Mohamed pamoja na Pauline Kea Kyovi wameathiriwa sana mkabala wa ubwege na kuchukua mwelekeo sawa, kutokana na jinsi walivyoangazia vipengele vya ubwege katika *Amezidi* na *Beluwa* mtawalia.

SURA YA NNE

MFANANO WA MWELEKEO WA KIUBWEGE KATIKA *THE MYTH OF SISYPHUS*, *AMEZIDI NA BELUWA*

4.0 Utangulizi

Katika sura hii tumedhamiria kuonyesha mfanano wa mwelekeo wa kiubwege katika utunzi wa *The Myth of Sisyphus, Amezidi na Beluwa*. Katika sura hii tuimejikita kwenye uchanganuzi wa *The Myth of Sisyphus* yake Albert Camus, kwa kuangazia vipengele vya kiubwege vilivyoangaziwa katika kazi hiyo. Vipengele hivyo vimehakikiwa ili kudhihirisha mwelekeo wa kiubwege katika utunzi wa Albert Camus na hatimaye tumedhihirisha mfanano wa mwelekeo huo katika utunzi wa *Amezidi na Beluwa*. Vipengele vya kiubwege vilivyotokana na dhana zilizoordheshwa na Camus, vilichunguzwa na kulinganishwa vilivyojitokeza katika *Amezidi na Beluwa*. Hatimaye, mfanano wa mwelekeo wa kiubwege katika *Amezidi, Beluwa* na *The Myth of Sisyphus* ulionyeshwa.

4.1 Historia ya *The Myth of Sisyphus*

The Myth of Sisyphus ni maandishi ya kifasafa yake Albert Camus, iliyochapishwa kwa mara ya kwanza kwa Kifaransa kama *Le Mythe de Sisyphe* katika mwaka wa 1942. Kazi hii ilichapishwa mwaka mmoja na riwaya yake mtunzi huyu iitwayo *The Stranger (L'Etranger)*.

Mtunzi Camus alishuhudia anguko la Ufaransa katika kipindi cha vita na hivyo, kuamua kutunga kazi hii ili kutafakari hisia za ukosefu wa maana na ubwege ulivyosababishwa na vita.

Utunzi wa kazi hii uliathiriwa sana na mawazo ya Soren Kierkegaard, Arther Schopenhauer na Fredrich Nietzsche; ambao walidadisi suala la maana ya maisha ya binadamu na uwepo wa binadamu katika falsafa zao.

Sisyphus (pia Sisyphos), ni kielelezo katika hadithi za visaviini za Kigiriki ambaye, kama mfalme wa Korintho alipata umaarufu kutokana na sifa mbaya ya kufanikiwa kuepuka kifo mara mbili. Kutokana na hii sifa, alipewa adhabu ya milele na Zeus; mfalme wa miungu wa kigiriki aliyekuwa mungu wa anga, radi, sheria, haki, umeme na amri. Adhabu hiyo ilikuwa kusukuma mwamba hadi kwenye kilele cha mlima.

The Myth of Sisyphus(1955) ni kazi iliyoungwa kwa sura nne inayoangazia masuala ya kiubwege. Kila sura imeshughulikia suala la ubwege kwa kumulika kipengele muhimu katika ubwege. Camus amevigawanya vipengele vya kiubwege kwa kategoria nne katika kazi hii. Sura ya kwanza imeangazia suala la kwanza ambalo ni; Wazo la kiubwege (*The Absurd Reasoning*). Kuhusiana na hili, Camus alijibu swali la Je, ukosefu wa maana katika maisha ya binadamu unafaa kumwelekeza mtu katika maamuzi ya kujitia kitanzi?. Alilijibu swali hili kwa kudai kwamba binadamu hujenga maisha yake kwa tumaini la kesho; kesho ambayo hutufikisha karibu na kifo; kifo ambacho ni adui mkubwa. Yaani ubwege humaanisha kukubali yote yanayosababishwa na dunia hii katili; cha muhimu si kuishi maisha mazuri bali maisha marefu. Anahitimisha kuwa wazo la kiubwege lina athari tatu kuu; kukubali kushindwa, kupata uhuru wa kiubwege na matamano ya kutaka kuishi.

Katika sura ya pili, mtunzi ameangazia suala la binadamu wa kiubwege (*The Absurd Man*) ambapo; alijibu swali alilozua kwamba Je, binadamu wa kiubwege anapaswa kuishi vipi?. Anashughulikia swali hili kwa kudai kwamba hakuna sheria inayoongoza kuishi kwa binadamu katika dunia katili ya ubwege. Katika sehemu hii, anaendelea

kwa kutolea mifano kuhusu maisha ya kiubwege kuwa ni Mtongozaji, Mwigizaji na Shujaa.

Aidha, Camus ameshughulikia suala la Uumbaji na Usanii wa Kiubwege (*The Absurd Creation*) kwenye sura ya tatu. Mtunzi alidai kwamba sanaa ya kiubwege inaangazia maarifa ya kikatili yaliyomo duniani, hivyo alichanganua kazi za Fyodor Dostoevsky; *The Diary of a writer*; *The Possessed* na *The Brothers Karamozov*. Anaeleza kwamba kazi hizi zote zilitamgulizwa kwa msingi wa kiubwege ila mbili za kwanza zilifikia kwa Kujitia Kitanzi, ambalo halikubaliwi kiubwege. Hata hivyo, *The Brothers Karamozov* imeangazia uwepo wa matumaini ambao huifanya kazi hii kukiuka kaida ya ubwege.

Kadhalika, mtunzi katika Sura ya nne ambayo ndiyo ya mwisho, ameangazia hadithi ya Usuli ya Sisyphus (visaviini) (*The Myth of Sisyphus*); ambayo imemulika vipengele mbali mbali vya kiubwege ambavyo vimetuongoza katika uchanganuzi ambao umetudhihirishia athari ya utunzi wa Albert Camus katika *Amezidi* na *Beluwa*.

4.1.1 Dhana za kiubwege za Albert Camus zinavyojitokeza katika *The Myth of Sisyphus*

Katika sehemu hii, tumefanya juhudi za kuelezea dhana ambazo Albert Camus alitumia kuangazia msimamo wake kuhusu hali katili katika maisha yake binadamu. Tunakubaliana na Chukwuka (2013) kwa kudai kwamba dhana hizo ni pamoja na; Wazo la kiubwege, Binadamu wa kiubwege na Ulimwengu wa kiubwege (Uumbaji wa kiubwege).

4.1.1.1 Wazo la kiubwege

Camus anaeleza juhudi za binadamu kwa kudadisi maana katika maisha, na ufafanuzi katika ulimwengu usioeleweka ambao hauna ukweli au maadili ya milele. Lakini,

swali la kustaajibisha la falsafa ni: Je, utambuzi wa kutokuwa na maana na maisha ya kiubwege lazima uhitaji kujitia kitanzi? Hatuwezi kumudu kuwa na swali hili la mara kwa mara kwa ziada, cha muhimu ni uhakika wa mandhari ya ubwege . Alisema kwamba lazima mtu akubali Sisyphus kuwa na furaha ya kweli.

Hisia za kiubwege huonyesha jinsi tunavyoutazama ulimwengu. Hisia ni mtazamo wa ulimwengu na huja kabla ya maneno na ni kutokana na hisia ambapo mwanadamu hutekeleza wajibu wake ulimwenguni. Ubwege kwa hivyo, unatokana na mvutano baina ya mawazo mawili yasiyo lingana. Kukabiliana na ubwege, ni sawa na kung'ang'ana dhidi yake. Na huu ndio msimamo wa Camus kama suluhisho la kupambana na ubwege; mkengeuko wa mara kwa mara dhidi ya ubwege. Kutokana na utambuzi wa ubwege, kunatokea matamano ambao ndio uchungu mkubwa sana.

Kukubali ubwege kunamaanisha kukubali magumu yote ambayo ulimwengu unatupa. Bila maana maishani, hakuna kiwango cha maadili, kinachozingatiwa sio kuishi bora zaidi bali kuishi zaidi.

4.1.1.2 Binadamu wa kiubwege

Katika *The myth of Sisyphus*, Camus anasema: “Kila kitu kinaruhusiwa, si mlipuko wa kitulizo au furaha, bali ni kukiri kwa uchungu ukweli”. Camus aliwasilisha maisha ya kiubwege na baadhi ya wahusika. Alianza na Don Juan, mdanganyifu wa kila mara ambaye anaishi maisha ya tamaa kwa ukamilifu, akiamini kwamba hakuna upendo wa milele wa heshima bali ni wa muda mfupi tu.

Mfano wa pili ni Shujaa, ambaye husahau ahadi zote za umilele kuathiri na kushiriki katika historia ya mwanadamu. Anatambua vyema kwamba hakuna kinachodumu na kwamba hakuna ushindi ulio wa mwisho. Anaeleza kwamba mfano huu unaweza kuoanishwa na tamthilia ya *Caligula* (1944). Katika tamthilia hii, ili kujaza nafasi ya

ubwege, wahusika wanajaribu kupata maana ya kile walichokuwa wakifanya. Kwa hivyo, ni katika hali za maisha ambapo watu huhangaika kutafuta maana ya kile wanachofanya na kuyapa maana maisha hayo.

4.1.1.3 Ulimwengu wa kiubwege (Uumbaji wa kiubwege)

Binadamu ili awepo, lazima aamue kutenda. Kwa Camus, wokovu wa binadamu haupatikani kwa Mungu; lazima upatikane hapa duniani kwa mikono ya binadamu. Camus anaeleza kwamba Nietzsche anadai kwamba “kwa vile ulimwengu hauna mwelekeo, binadamu tangu anapokubali hili, lazima atoe jambo ambalo hatimaye litapelekea aina bora zaidi ya ubinadamu.

Kuhusu Uumbaji au usanii wa kiubwege, Chukwuka (2013) anaeleza kwamba Kwa Camus, sanaa za kiubwege zimebanwa kwa maelezo ya matukio mengi duniani. Ikiwa uumbaji na ulimwengu ni wazi, sanaa zisingekuwapo. Kutokana na hili uumbaji wa kiubwege lazima ujiepushe na kuhukumu na kudokeza hata kivuli kidogo cha matumaini. Kwa hivyo, Camus anasema, "Ninauliza juu ya uumbaji wa kiubwege kile ninachohitaji kutoka kwa fikra... mkengeuko, uhuru, uchaguzi n.k., ni muhtasari wa hekima ngumu na matamano ya muda mfupi.

Camus alihitimisha mjadala wake kuhusu aina kadha za maisha ya kiubwege, akisema kwamba maisha huisha na kifo, lakini hadi wakati huo, vitu vyote juu yetu. Kwa hiyo, ikiwa hatuko wazi kwa mawazo yetu kwamba kuna Kiumbe aliye juu zaidi ambaye huamua ni nini kilicho sawa au kibaya, basi maisha haya yanakuwa yetu kabisa kwamba tunaweza kuishi kama tunavyochagua.

4.1.1.4 Mukhtasari wa *The Myth of Sisyphus*

Katika *The Myth of Sisyphus*, kuna mhusika mkuu, Sisyphus aliyekuwa mfalme mbaya na mjanja katika mji wa Korintho. Alijulikana kwa udanganyifu na ujanja

wake. Miungu ilimlaani Mhusika Sisyphus kubingirisha mwamba bila kikomo hadi kwenye kilele cha mlima, lakini kila mara mwamba huo ulipofika kileleni ungejibingirisha hadi chini ya mlima kutokana na uzito wake.

Miungu iliwazia adhabu hii na kujitokeza kuwa ya kutisha sana na yenye kupoteza matumaini. Sisyphus anashutumiwa kwa kukosa unyenyekevu kwa miungu na kuiba siri zao.

Mhusika Aegina; bintiye Aesopus alitekwa nyara na Mshtarii (Jupiter) hivyo, baba yake alishtuliwa na kisa hicho na kumlalamikia Sisyphus; ambaye alifahamu njama ya utekaji nyara wa binti huyo. Sisyphus alikubali kumsema aliyechukua binti huyo kwa makubaliano kwamba Aesopus angepeana maji kwa ngome ya Korintho. Miungu ilipogundua mpango huu, ilikasirika na kumwadhibu Sisyphus katika Ulimwengu wa chini.

Anavyoeleza O'brien ni kwamba Homer anatueleza kwamba Sisyphus aliwahi kuweka kifo kwenye kifungo cha minyororo. Pluto alikosa kuvumilia kwa kuona uso mkavu wa himaya yake ya kimya alivyotengwa, hivyo alimtuma mungu wa vita ambaye aliweka huru kifo kutokana na unyanyasaji wa Shujaa wa kiubwege, Sisyphus.

Baadaye Sisyphus alifikiwa na kifo na kutaka kupima upendo wa mkewe hivyo, alimwamrisha atupe mwili wake katikati ya uwanja wa umma. Agizo hili lilipotekelezwa, Sisyphus aliamka ulimwengu wa chini akiwa amekasirishwa na tendo hilo ambalo alilirejelea kuwa utiifu ulio kinyume sana na upendo wa kibinadamu. Alipewa ruhusa na Pluto ili kurudi duniani kumwadhibu mkewe kwa tendo hilo. Sisyphus alipouona dunia ilivyokuwa ya kufurahisha; iliyo na maji, jua, mawe ya joto na bahari hakutaka kurudi tena kwa giza la ulimwengu wa chini.

Miungu ilifanya juhudi za kuonyesha dalili za hasira na maonyo lakini hazikuwa na maana kwake. Kwa miaka mingi aliishi akikabiliana na ukingo wa ghuba, bahari inayometa na tabasamu za dunia, na hivyo amri ya miungu ilihitajika.

Mercury alikuja na kumkamata na kumnyima furaha yake, kwa kumwongoza kwa nguvu hadi kwenye ulimwengu wa chini; ambapo sasa mwamba wake ulikuwa ukimsubiri. Kutokana na ujanja na udanganyifu wake aliwahi kutoroka kifo mara mbili huku akiendelea kudharau miungu, hivyo kumsababisha Zeus-kiongozi wa miungu kumpa adhabu kali inayozidi kifo. Kuidharau miungu, chuki yake dhidi ya kifo na nia yake ya kuishi ilimfikisha katika adhabu ya kutisha, ambapo kiumbe hicho kinatumika kwa kutekeleza yale yasiyoweza kubadilisha hali yake duni ya kukatisha tamaa.

Alipewa adhabu ya kubiringisha mwamba hadi kwenye kilele cha mlima kwa kina cha kuzimu, ambayo ni ulimwengu wa kifo. Mwamba huo ulipofika kileleni, ungejibiringisha hadi chini ya mlima na Sisyphus angerudia kazi ya kuubiringisha tena hadi kwenye kilele cha mlima kila mara hadi milele. Mwamba unapojibiringisha chini ya mlima, Sisyphus hupuzia na kujitayarisha kusukuma huo mwamba hadi juu tena. Anavyoeleza O'brien ni kwamba Camus anatamatisha uandishi huu kwa kusema kwamba anamwacha Sisyphus akiwa chini ya mlima, na kupata mzigo wake tena lakini kwa yote anadai kwamba yote ni shwari na Sisyphus anafurahia. Furaha yote ya ukimya ya Sisyphus imo ndani yake, hatima yake ni yake. Mapambano ya Sisyphus yanaonyesha kwamba mateso yanatosha kujaza moyo wa binadamu. Binadamu wa kiubwege huitikia nguvu zake na kuamini kwamba zitafanya bila kikomo na hatima ya binadamu haiwezi kuepukika na huwa yenye dharau.

4.1.2 Mwelekeo wa Kiubwege Katika *The Myth of Sisyphus*

Katika sehemu hii, tumechunguza jinsi ambavyo utunzi wa kwanza wa kiubwege *The Myth of Sisyphus* 1942, ulivyodhihirisha mwelekeo wa kiubwege wa Albert Camus. Uchanganuzi na maelezo katika sura hii na sura zilizotangulia, ndiyo yamefanikisha sehemu hii kutimiza lengo la kubainisha mwelekeo wa kiubwege katika *The Myth of Sisyphus*

Kwa kuchunguza dhana za kiubwege alizoziorodhesha Camus katika *The Myth of Sisyphus* (1942) pamoja na hadithi ya usuli wa Sisyphus, tumefanikiwa kutimiza lengo la utafiti kwamba kuna mfanano wa mwelekeo wa kiubwege katika *Amezidi, Beluwa* na *The Myth of Sisyphus*.

4.1.2.1 Vipengele vya kiubwege kutokana na dhana ya wazo la kiubwege

Kwa kuangazia dhana ya wazo la kiubwege masuala yaliyochunguzwa ni; Kifo na Ukengeushi.

4.1.2.1.1 Suala la Kifo na Kaburi

Suala la kifo; japo limechunguzwa kwa njia ya kujiua yaani kujitia kitanzi, Camus anashikilia kwamba maisha huisha kwa kifo na kifo ndicho hatima ya maisha yake binadamu. Hata kama amekubali kuwa kifo ni hatua ya mwisho katika maisha yake binadamu, binadamu hapaswi kujiua, yaani kujitia kitanzi.

Kutokana na haya madai Camus, ubwege wa maisha hapaswi kumpelekea binadamu kujitia kitanzi bali anapaswa kuishi maisha yaliyo na uhuru wa kimawazo, na kufanya juhudi za kujipatia kitulizo cha furaha. Anasema yafuatayo;

Maisha ya binadamu yanahusishwa na mateso na uhakika wa kifo
(Uk. 28)

Je, ubwege wa maisha unatarajia mtu kutoroka na kujiua? (uk. 9)

Ninakataa kitendo cha kujitia kitanzi (Uk. 64)

(T. Y)

Mifano hii inadhihirisha msimamo wa Albert Camus kuhusiana na suala la Kifo na kujitia kitanzi. Kwake, anaamini kwamba hatua ya mwisho ya maisha ya binadamu ni kifo lakini si kwa kujiua. Anaendelea kwa kusema kwamba ubwege hutamatishwa kwa kifo, yaani ni lazima kwamba siku moja binadamu atakufa na kukombolewa kutoka kwa dunia katili ya ubwege.

Kutokana na mifano hii, tunaona kwamba utunzi wa kiubwege wa kwanza wa Albert Camus, uliangazia suala la kifo na kukubali kwamba kifo ndicho mwisho wa ubwege. Tunakubaliana naye kwa wazo kwamba kifo na ubwege ndiyo mihimili ya uhuru wa akili; ambapo moyo wa binadamu unaweza kukumbana nayo. Mtunzi huyu alijadili dhana ya wazo la kiubwege kwa nia ya kuweka wazi kwamba binadamu lazima afahamu kwamba siku moja atafa na kukombolewa kutoka kwa matatizo yanayomsibu.

Kadhalika, kama tulivyoeleza katika sura iliyotangulia, *Amezidi* na *Beluwa* pia zinadhihirisha kwamba kifo na kaburi ni vipengele muhimu vya kiubwege. Katika Tamthilia ya *Amezidi*, Said A. Mohamed anatuonyesha wahusika wanavyoathamini kifo, tunaambiwa;

Ame: Jamani raha...Kuzimu kule nakuona...Zidi yuleeeee...Zidi...
 (Anaita) Njoo, Zidi (Anampungia mkono) Njoo nikamate,
 njoo unishike mkono. Njoo unionyeshe njia wewe
 mwenzangu umenitangulia...raha...raha...kifo ni raha...kifo
 cha raha...Zidi ameniambukiza? Ah, labda ni sawa, itabidi
 twende sote kwa ujinga wetu!...aaaaa, sasa maumivu yanazidi,
 aaaaaa sasa raha inazidi. Raha ya maumivu na maumivu ya
 raha. Je, (anaigeukia hadhira) na nyinyi mnataka mwende nasi
 katika maumivu haya ya raha? Fanyeni basi au bora msifanye
 kitu basi! Ah, nakufa jamani. Kifo cha raha!
 Naku...na...naku...fa...NAKUFA! (Ame anakufa) (Uk. 85)

Ame anaonyeshwa akikienzi kifo na kufurahia anapokaribia kufa; kwake kifo ni raha, maumivu pia ni raha; huu ni ubwege. Vile vile katika Beluwa, kifo ambacho kimeashiriwa kwa kaburi kinawachangamsha binadamu wa kiubwege, tunaambiwa;

Beluwa: (Anampuza Tanda na kuendelea) Kaburi ni letu sote nishasema. Tujikazeni tulipate. Siku za kupanda huwa ngumu, watu hukosa starehe. Wakajibana na kununua mbegu hata mbolea. Siku yaja tutavuna. Tatalivuna kaburi na kuzijaza ghalazetu. Msijali kelele, vumbi au mmomonyoko wa udongo. Siku yaja.
Kaburi tukilipata hatutataka tukose.
Kaburi tukilipata tutatosheka.
Kaburi tukilipata tutapumzika...
Machozi yanayodondoka, yata...(Uk. 76)

Kwake Beluwa, kaburi ni kila kitu na mtu akilipata, hatakosa chochote, atapumzika kutokana na mzigo mzito alilobebeshwa na ulimwengu katili, machozi yatakoma na atafurahi.

Kutokana na mifano hii, ni dhahiri kwamba Albert Camus, Said A. Mohamed na Pauline Kea Kyovi wanachukua mwelekeo sawa kuhusu suala la kifo na kaburi; wote wanashikilia kwamba kifo ndicho hatima ya ubwege wa binadamu wa kiubwege. Ifahamike kwamba hata kama Camus alibaini kwamba kifo ni hatua ya mwisho maishani mwa binadamu, hapaswi kujitia kitanzi bali ajitafutie uhuru wa kiubwege kwa kupata njia nyingine ya kuendeleza maisha yake na kuyaishi hadi tamati.

4.1.2.1.2 Suala la Ukengeushi

Kama tulivyoeleza katika sura iliyotangulia, ukengeushi ni kuasi au kwenda kinyume cha utaratibu maalum ambao unajulikana kwa watu wa kikundi fulani au jamii. Katika uandishi wa Albert Camus, kuna msingi uliowekwa kuhusiana na suala hili kwamba binadamu wa kiubwege sharti ajiingize katika matendo yanayokiuka taratibu fulani katika maisha ili aweze kupata maana ya maisha yake; yaani ajiwekee maana ya maisha kivyake kutokana na juhudi zake za kibinafsi. Mtunzi huyu alipendekeza njia

tatu za kukumbana na suala la ukosefu wa maana ya maisha kuwa kifo, Imani na Ukengeushi. Anaendelea kueleza kwamba msimamo wa kifalsafa ni mkengeuko; ambao ni mvutano wa mara kwa mara kati ya binadamu na ukosefu wa uwezo wa kujitambua mwenyewe. Kiubwege, mtunzi huyu anakubaliana na dhana ya ukengeushi kwa kudokeza yafuatayo;

Ukengeushi wa mwili ni ubwege. (Uk. 14)
 Ukengeushi ni uhakika wa hatima mbaya...(Uk. 55)
 Ukengeushi huyapa maisha thamani yake. (Uk. 55)
 (T.Y)

Albert Camus anadai kwamba ukengeushi huyapa maisha thamani yake kutokana na juhudi za binadamu, kwa kutekeleza shughuli zake kivyake kwa uhuru wake mwenyewe ili kuyapa maisha yake maana. Aidha kutokana na uhakiki wa hadithi ya usuli wa Sisyphus, mhusika Sisyphus anajitokeza kudhihirisha ukengeushi wa kiwango cha juu sana. Aliasi sheria za miungu hadi akafikia hali ya kuweka Kifo katika kifungo cha minyororo; kitendo ambacho kilikasirisha mungu wa vita, Zeus na hivyo kumsababisha kupewa adhabu ya milele iliyozidi kifo.

Hali ya ubwege inayowakilishwa na kicheko pia ilianguziwa na Albert Camus. Anapotamatisha hadithi yake ya usuli wa Sisyphus anadai kwamba anamwacha Sisyphus chini ya mlima akijitayarisha kubingirisha mwamba mara nyingine tena ila ana furaha; yaani anafurahia hali yake duni ya kiubwege isiyoweza kutekeleza chochote. Kadhalika, kipengele cha ukengeushi pia kilijitokeza katika *Amezidi* na *Beluwa*. Katika *Amezidi*, tunapata yafuatayo;

Mwalimu: Barabara. (Anatabasamu) Dakika tano za kulala...tunza yenu! (wanalala na mwalimu wao juu ya meza zisizokuwepo) (uk. 35)

Hapa tunampata mwalimu aliyekata tamaa na anadhihirisha kwamba ana uhakika wa hatima mbaya na wanafunzi wake. Kama anavyoeleza Camus, Ukengeushi ni uhakika wa hatima mbaya ambayo kulingana nasi ni hatima isiyoweza kuleta manufaa yoyote wala kuboresha maisha ya binadamu. Mwalimu huyu amekengeuka na hawezi kutekeleza jukumu lake la kufundisha na kuwaelekeza wanafunzi ipasavyo. Anawaambia wanafunzi walale baada ya kushindwa kujibu maswali aliloulizwa na mwanafunzi. Vile vile, tunapata ukengeushi katika *Beluwa*, tunaambiwa;

Tanda: Njoo, njoo uniondolee janga hili. Njoo nikushike, nikukumbatie, niku...(anamshika Beluwa mara moja na kutaka kumbusu. Beluwa anamsukuma na kumwangusha)

Tanda: (analia kwa maumivu huku akijishikilia moyo) ooh! ooh!

Beluwa: (kwa ukali) unataka kunifundisha nini wewe? ushoga, usege au uhayawani?

Tanda: (kwa ukakamavu) sasa unajitia kutojua mambo haya? unaishi sayari gani? Get serious, drama si fani yako!

Beluwa: kwa hivyo wewe ni gay? (kimya kidogo)

Tanda: unangoja jibu?

Beluwa: La! dalili ya mvua ni mawingu....

Tanda: wananielewa si kama wewe unayeishi katika enzi za homo erectus. Zaitwa bling basi! Andika usije ukasahau. (uk. 41).

Kutokana na mfano huu, tunabaini kwamba maendeleo ya kisayansi na kitasnia yamemkengeusha binadamu kutoka kwa mungu, jamii na kutoka kwa nafsi yake. Tunaonyeshwa mhusika Tanda akiwa mbasha na anataka amfundishe mwenzake Beluwa. Tanda anaona Beluwa kama kifaa cha kumtuliza roho; yaani anamwona kama kitulizo cho roho; mpenzi licha ya kuwa wote ni wanaume.

Albert Camus, Said Ahmed Mohamed na Pauline Kea Kyovi wanabaini kwamba ukengeushi ni sifa muhimu ya ubwege. Anavyoeleza Camus ni kwamba Ukengeushi wa mwili ni ubwege na hudhihirisha uhakika wa hatima mbaya maishani mwa binadamu wa kiubwege na pia ni kipengele kinachoyapa maisha thamani yake.

4.1.2.2 Vipengele vya kiubwege kutokana na dhana ya Binadamu wa kiubwege

Kutokana na dhana ya pili aliyopendekeza Camus katika ubwege; Binadamu wa kiubwege, tulichunguza maana ya Maisha na Uhuru wa kiubwege.

4.1.2.2.1 Maana ya Maisha na Uhuru wa Kiubwege

Kwa mujibu wa Albert Camus, binadamu wa kiubwege hupitia mateso mengi na anashindwa kupata maana ya maisha yake. Anapendekeza njia mbadala ya kukumbana na maisha ya kiubwege kwamba binadamu atafute uhuru wake na kujitafutia maana ya maisha yake kivyake. Anasema yafuatayo;

Kwa binadamu wa kiubwege, kuna ukweli pamoja na uchungu katika maoni ya kisaikolojia hivi kwamba nyanja zote za ulimwengu ni za upendeleo. (Uk. 45)

...wakati huo huo binadamu wa kiubwege anatambua kwamba alikuwa amefungwa na hivyo kutafuta uhuru. (Uk.58)
(T.Y)

Mifano hii inaonyesha Albert Camus navyoutazama ulimwengu na binadamu. Kwake, ulimwengu una nyanja za upendeleo mwingi na hivyo ili kujisaidia, lazima atafute uhuru baada ya kutambua kwamba alikuwa amefungwa katika ulimwengu katili anamoishi. Aidha Camus alidai kwamba maisha hayana maana na hakuna maisha ya kuishi kesho, hivyo binadamu wa kiubwege anapaswa kutumia uhuru wake wa ndani ili kujituliza. Anasema,

Ubwege unamulika suala la kutokuwepo kwa maisha ya kesho na ndicho chanzo cha uhuru wangu wa ndani kibinafsi. (Uk. 59) (T.Y)

Kiubwege, maisha ni hatua ya kuelekea kwa kifo. Binadamu na vyote vinyomzunguka katika mazingira yake ni ubwege, yaani utupu. Ni dhahiri kwamba ulimwengu ni ombwe lenye giza totoro ambalo huwakilisha uduni wa maisha ya binadamu ulimwenguni. Kile ambacho ni bayana, ni binadamu kukaa tu huku akisubiri kifo au kujitafutia uhuru wa ndani wa kiubwege.

Kwa mujibu wa Camus, hakuna hata maana moja ya maisha na hatuwezi kutengeneza moja pia. Anasema kwamba haiwezekani kwetu kupata jibu la kuridhisha kwa swali kuhusu maana ya maisha pamoja na jaribio lolote la kulazimisha ulimwengu kuwa na maana litaishia kwa msiba. Anakanusha zaidi kwamba sayansi, falsafa, jamii, au dini zinaweza kufasiri maana ya maisha ambayo yangeepukwa na ubwege. Kutokana na dai hili tunapata kwamba Camus alishikilia kwamba maisha ya binadamu hayawezi kuwa na maana kamwe. Aidha anaeleza kwamba ikiwa maisha yana maana basi maana kamili ni kutenda kitendo kinachojitenga na kujitia kitanzi. Kwake, Mtu anayeweza kufahamu ukweli kwamba maisha ni ya kiubwege na kuyapitia kwa tabasamu ni shujaa wa kiubwege.

Kwa mfano, katika hadithi ya usuli wa Sisyphus katika *The Myth of Sisyphus*, mtunzi anatamatisha hadithi yake kwa kutaja kwamba “Lazima tumfikirie Sisyphus akiwa na furaha” kwa kubingirisha mwamba kila mara bila mafanikio. Furaha hii ni furaha ya kiubwege; yaani ni mbinu ambayo binadamu wa kiubwege hutumia ili kujituliza kutokana na uduni wa maisha yake.

Juhudi anazofanya mhusika Sisyphus kwa kubingirisha mwamba hadi kwenye kilele cha mlima kila mara bila mafanikio, ni kitendo cha kiubwege kinachotamausha sana. Kitendo hiki ambacho hakifanikishi shughuli yoyote huonyesha maisha ya kiubwege yasiyoweza kutumiwa kutenda lolote lakini anabaki akiwa amefurahia hali yake.

Ingawa Camus alipendekeza furaha katika *The Myth of Sisyphus* kama kipengele muhimu cha kumtuliza binadamu wa kiubwege asiyejielewa, wahusika hawa wanaonyesha hali tatanishi hivyo wanakosa kujielewa na kuchanganyikiwa zaidi. Ndiposa Albert Camus katika Cruickshank 1959:27 anakiri kuwa furaha inayodumu hakuna katika maisha ya binadamu, yaani maisha yake ni ya kuhuzunisha tu.

Msimamo wa Camus kuhusu suala la maana ya maisha ni kwamba maisha hayana maana na ni wajibu wa binadamu wa kiubwege kujipatia maana ya maisha yake kivyake, kutokana na juhudi zake mwenyewe. Mhusika Sisyphus anafanya juhudi isiyo na kikomo kwa kubingirisha mwamba kila mara baada ya kukubali kwamba uhuru wa kisaikolojia na ule wa kitendo ndio uhuru kamili; kama anavyoeleza Camus kwamba binadamu wa kiubwege hukumbana na uchungu na matatizo hadi afikie hatima ya maisha yake (Uk. 55).

Maisha ya Sisyphus yamejawa mateso ambayo hajui yatakwisha lini; maisha haya ni kama ajali ambapo Greene (1960: 7; Magare 2002) anasema;

“Binadamu ni ajali, hali yake haina utaratibu na muhimu zaidi, ulimwengu umeumbwa kwa hali ya usahaulifu.”

Kiubwege, maisha ya binadamu huonyeshwa kama fujo. Hali ambayo hubainika kupitia shughuli mbalimbali za binadamu zisizodhihirisha utaratibu wowote. Matendo ya binadamu maishani ni shaghalabaghala, yaani yanajitokeza bila mpangilio wowote, kwa vile kila mtu hutenda atakavyo na hashurutishwi na yeyote hata Mungu. Binadamu ana uhuru wa kutenda apendavyo na kusema anachokipenda bila tatizo lolote. Anavyoeleza Camus ni kwamba binadamu wa kiubwege ana uhuru wa kutenda atakavyo angali mzima; huu ndio anauita uhuru wa kiubwege unaotoa maana ya maisha ya binadamu wa kiubwege.

Kwa ujumla, kiubwege, maisha yake binadamu katika ulimwengu yamejaa utata sana na yamejawa ugumu na uvundo. Waandishi wa kiubwege pamoja na wale wa kiudhanaishi, wanakubaliana kuwa, hakuna furaha maishani mwa binadamu. Maisha ni mateso na ni kama adhabu.

4.1.2.3 Vipengele vya kiubwege kutokana na dhana ya Ulimwengu wa kiubwege na uumbaji wa kiubwege

Kigezo kingine cha kiubwege kilichopendekezwa na Albert Camus katika *The Myth of Sisyphus* ni dhana ya Ulimwengu wa kiubwege, ambayo kutokana kwayo, tulibainisha suala la ukosefu wa matumaini na kukata tamaa.

4.1.2.3.1 Ukosefu wa matumaini na kukata tamaa

Kulingana na Camus, ulimwengu wa kiubwege ambao hata yeye haelewi husababisha ukosefu wa matumaini. Anasema yafuatayo;

Ulimwengu una watu wasiofikiria. Ulimwengu wenyewe, ambao siuelewi maana yake moja, ni ujinga mwingi tu. Ikiwa mtu angeweza kusema mara moja tu...(Uk. 27)
(T.Y)

Kwake Camus, ulimwengu unapaswa kupewa mtazamo mwingine wa kutokuwa na matumaini. Anadai kwamba wanafalsafa wamehusisha ubwege na matumaini ya kuishi na kuona kesho; wazo ambalo analikana. Anatuambia;

Mtu anawezaje kushindwa kuhisi uhusiano wa kimsingi wa mawazo haya! Mtu anawezaje kushindwa kuona kwamba wanachukua msimamo wao karibu na wakati wa bahati na uchungu ambao tumaini halina nafasi kwake? (Uk. 27)
(T.Y)

Mwanafalsafa huyu alikuwa akikashifu kazi za watunzi walioibuka na kazi zilizoonekana kuwa za kiubwege ila zilidhihirisha dhana ya tumaini mwishoni. Alichunguza kazi ya Chestov na kusema yafuatayo kuihusu;

Sasa, ikiwa inakubalika kwamba ubwege ni kinyume cha tumaini, inaonekana kwamba mawazo ya Chestov yanaonyesha ubwege...(Uk.35)
(T.Y)

Aidha, Camus anaamini kwamba ameshatoa mwangaza kupitia kwa kazi ya *The Myth of Sisyphus*; ambapo alikiri kwamba wanafalsafa hao wameshajua cha kufanya kama

watunzi wa kiubwege; yaani kazi ya kiubwege isidhihirishe chembechembe za matumaini kwa wahusika ila waonyeshwe kukata tamaa. Kwa mfano anasema;

Anatambua kwamba kutokana na ufahamu huo, hakuna tena nafasi ya tumaini. (Uk. 37)
(T.Y)

Kwa kulifafanua suala hili zaidi, Camus anaeleza yafuatayo;

Na nikibeba mantiki hii ya kiubwege hadi kwenye hitimisho lake, lazima nikiri kwamba mvutano yanamaanisha kukosekana kabisa kwa tumaini (ambalo halina uhusiano wowote na kukata tamaa), kukataliwa kila mara (ambalo lazima lisichanganywe na kukataa), na kutoridhika kwa fahamu (ambayo haihusiani na kukata tamaa) (Uk. 31)
(T.Y)

Katika utunzi wa hadithi ya usuli wa Sisyphus katika *The Myth of Sisyphus*, mtunzi anatupa mhusika Sisyphus ambaye anachorwa akiwa amepewa adhabu ya kukatisha tamaa isiyoonyesha matumaini. Kwa mfano, katika sehemu ya mwisho wa uandishi huu tunapata;

Miungu ilikuwa imemhukumu Sisyphus kuviringisha mwamba bila kukoma hadi juu ya mlima, ambapo jiwe lingeinguka nyuma ya uzito wake. Walikuwa wamefikiri kwa sababu fulani kwamba hakuna adhabu ya kutisha zaidi ya kazi ya bure iliyokosa matumaini. (Uk.119)
(T.Y)

Wazo hili la Camus linaungwa mkono na Kitchin (1966:31; Magare 2002) anaposema yafuatayo;

“Haja kubwa ya tamthilia ya kiubwege ni
Kujipata katika hali ya kukata tamaa na iliyokosa matumaini na
maana yoyote ulimwenguni”

Ni wazi kwamba ulimwengu wa kiubwege husawiri matukio ya kiubwege. Vitushi vinavyojitokeza katika uandishi wa Camus , *The Myth of Sisyphus* vinadhihirisha kwamba kukata tamaa na ukosefu wa matumaini ni kanuni inayoongoza utunzi wa kiubwege.

4.2 Hitimisho

Sura hii imemulika vipengele muhimu vya kiubwege hasa vilivyodaiwa na Albert Camus kuwa vya kipekee katika utunzi wa kazi za kiubwege. Tulihakiki dhana alizoziorodhesha alipoweka msingi wa nadharia ya ubwege na kubainisha vipengele vya kiubwege kutokana na dhana hizo. Uchanganuzi huu umefanikisha kutimizwa kwa shabaha ya kuonyesha mfanano wa mwelekeo wa kiubwege katika *The Myth of Sisyphus*, *Amezidi* na *Beluwa*.

SURA YA TANO

MATOKEO, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.0 Utangulizi

Sura hii ni sehemu ya mukhtasari wa utafiti. Tumetoa mukhtasari wenyewe kwa kuzingatia suala la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, nadharia pamoja na mbinu za utafiti. Aidha, tumetoa maoni na kupendekeza tafiti za baadaye. Mapendekezo haya yatachangia katika kuwapa watafiti wajao ari ya kutafakari na kuona iwapo wanaweza kuendeleza tafiti mbali mbali. Waandishi, hasa wa tamthilia, pia huenda wakachochewa kuandika kwa njia tofauti na jinsi walivyokuwa wakiandika kazi zao.

5.1 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu uliazimia kuchunguza mwelekeo wa kiubwege katika tamthilia ya Kiswahili, mintarafu ya *Amezidi* na *Beluwa* kwa malengo ya kuchunguza vipengele vya kiubwege kimaudhui na kifani kwenye tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa*. Pili, kutathmini mwelekeo wa kiubwege katika tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* na hatimaye, kubainisha mwelekeo wa kiubwege katika *The Myth of Sisyphus*. Ili kutimiza malengo haya, tulichunguza vipengele vya kimaudhui na kifani kiubwege na kuvilinganisha kulingana na jinsi vilivyojitokeza kwenye tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa*.

Kando na dhamira na mandhari, tulichunguza vipengele vya kimaudhui kama vile suala la Mungu, suala la kifo na kaburi, ukengeushi na ukosefu wa uthabiti kwa elimu. Vipengele hivi vilichunguzwa na kulinganishwa jinsi vilivyojitokeza katika tamthilia hizi mbili. Kwa kuangazia suala la Mungu, tulipata kwamba Said Ahmed Mohamed na Pauline Kea Kyovi wanamtambua Mungu katika *Amezidi* na *Beluwa*

Mtawalia. Kwa kufanya hivi, watunzi hawa wanajitambulisha na kundi la wanaoamini kuwa “Mungu yupo” linalowakilishwa na mwanatheolojia wa Ki-Deni Soren Kierkegaard (1813-1855), ambapo anavyoeleza Wamitila (2003), alidhihirisha msimamo wake kuhusu suala la Mungu katika maandishi yake mbali mbali na hasa *The Concept of Dread, Fear of Trembling* na *Sickness unto Death*. Katika kazi hizi, Kierkegaard alieleza kuwa mwanadamu hupata kimbilio kutoka mivutano ya maisha kupitia kwa Mungu; hii ni imani ambayo iliishia kushika nguvu sana katika Ukristo.

Waidha, Said Ahmed Mohamed na Pauline Kea kyovi walichukua mwelekeo sawa wa kiubwege kwa kuangazia suala la kifo na kaburi. Katika tamthilia ya *Amezidi*, wahusika wamechorwa wakiwa na uhakika wa kifo; ambacho wanakithamini sana. Wanakiri kwamba raha ya kudumu hupatikana tu kwa kifo. Aidha, katika *Beluwa* suala la kaburi linashangiliwa kushinda mahusiano ya kimapenzi. Kuna mfanano kwa jinsi ambavyo watunzi wameangazia suala la kifo na kaburi; wote wanabaini kwamba hatua ya mwisho maishani mwa binadamu ni kifo na kaburi.

Kipengele cha ukengeushi pia kilichunguzwa katika *Amezidi* na *Beluwa* na kilidhihirisha msimamo wa kiubwege kwamba; binadamu wa kiubwege sharti ajiingize katika matendo yanayokiuka taratibi fulani katika maisha ili ajiwekee maana ya maisha kibinafsi. Watunzi wa tamthilia hizi walidhihirisha kwamba ukengeushi huyapa maisha thamani yake. Kadhalika, ukosefu wa uthabiti kwa elimu kilichunguzwa kama kipengele cha maudhui kiubwege na tulipata kwamba wahusika wa kiubwege hata wapate elimu, bado hawawezi kuboresha hali ya maisha yao duni. Said Ahmed Mohamed na Pauline Kea Kyovi walidhihirisha kwamba elimu ya binadamu wa kiubwege ni ya kukatisha tama na haina faida katika maisha ya binadamu.

Isitoshe, tuliweza kulinganisha vipengele vya kifani kiubwege. Vipengele vya kifani vilivyodhihirisha mlingano katika tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* ni kama vile; Uhusika, ambapo tulichunguza uchache wa wahusika, wahusika wa kiutopia, wahusika wa kinjozi na wahusika vibonzo. Matokeo tuliyoyapata ni kwamba watunzi wa tamthilia hizi teule walisukumwa kuonyesha kwamba maisha ya binadamu ni duara na hutawaliwa na ndoto nyingi, wanakosa uwezo wa kutenda chochote bali wanakaa tu huku wakisubiri kifo; ambacho ndicho hatima yao. Wahusika hao hubadilikabalika kuanzia mwanzo wa mchezo hadi mwisho. Kupitia kwa uhusika, imebainika kwamba watunzi hawa walidhamiria kuonyesha mateso yanayomkabili binadamu katika mazingira ya kukatisha tamaa; maisha ya kuota ndoto zisizotimizwa.

Kando na uhusika, vipengele vya ukosefu wa ruwaza za mazungumzo, lugha inayotatiza mawasiliano na utupu pia vilichunguzwa. Hapa tulipata kuwa lugha katika sanaa ya kiubwege hairahisishi mawasiliano hivyo husigana na jukumu lakela mawasiliano. Wahusika hutumia mazungumzo ya kubwabwaja na kidhahania toka mwanzo hadi mwisho wa michezo hii, hii huashiria kwamba binadamu amekosa kujifahamu hata uhusiano wake na binadamu wenzake. Kwao, lugha si chombo cha mawasiliano bali hudhihirisha kuchanganyikiwa kwake pamoja na utupu wake katika ulimwengu katili anamoishi. Kwa kifupi, lugha na mawasiliano ya binadamu zimekufa. Katika matumizi ya nyimbo, vicheko na vilio ilibainika wazi kwamba watunzi wa kazi teule wameonyesha kuwa jitihada za mwanadamu kuwasiliana kupitia nyimbo, elimu, sauti, vicheko na vilio haziwezi kufanikisha chochote. Kushindwa kutumia lugha ipasavyo, ni dhihirisho la ugumu maishani mwa binadamu wa kiubwege.

Vilevile, Said A. Mohamed pamoja na Pauline Kea Kyovi wamepuuza suala la ploti katika *Amezidi* na *Beluwa* mtawalia. Vitushi havisababishani ila kila tukio linajitokeza kipweke bila kuhusishwa na kingine. Katika *Amezidi* tunapata tukio la masomo darasani inayopatikana kwenye onyesho la Nne na lile linalofuata kwenye onyesho la Saba ni tukio la ofisini. Hapa tulipata kwamba tukio la masomo darasani halijasababisha lile la ofisini kwa sababu hata wanafunzi wenyewe hawakuhitimu; elimu waliyopata ilikuwa ya kukatisha tamaa. Aidha katika *Beluwa*, suala la ploti halikujitokeza. Vitushi vilijitokeza kipweke bila kusababishwa na kingine. Mfano mzuri tuliopata ni tukio la mahaba kaburini ambalo lilianza onyesho la nne, likaendelea kwenye onyesho la tano kisha tunapata tukio la utangazaji wa habari kwenye runinga. Hapa tunapata kuwa vitushi hivi havisababishani; hivyo watunzi hawa walipuuza kipengele cha ploti katika kazi zao.

Kwa kuvilinganisha vipengele hivi vya kimaudhui na kifani kiubwege, tulipata kwamba Said Ahmed Mohamed na Pauline Kea kyovi walichukua mwelekeo sawa wa kiubwege katika utunzi wa *Amezidi* na *Beluwa* mtawalia. Hii ilidhihirisha mwelekeo wa kiubwege katika tamthilia ya Kiswahili.

Kadhalika, vipengele vya kiubwege vilivyoangaziwa katika *The Myth of Sisyphus* vililinganishwa na vile vilivyojitokeza katika *Amezidi* na *Beluwa* ili kubainisha msingi wa nadharia ya ubwege ulivyowekwa na Albert Camus. Hapa tulipata kwamba Albert Camus aliangazia dhana tatu za kiubwege; kwanza, wazo la kiubwege, pili, binadamu wa kiubwege na hatimaye ulimwengu wa kiubwege (uumbaji wa kiubwege). Kwa kuchunguza wazo la kiubwege, masuala tuliobainisha ni kifo, kaburi na ukengeushi. Kuhusu suala kifo na kaburi, kwa mujibu wa Albert Camus, maisha ya binadamu yanahusishwa na mateso na uhakika wa kifo ila mtu hapaswi kujitia kitanzi. Said

Ahmed Mohamed, Pauline Kea Kyovi na Albert Camus walidhihirisha mwelekeo sawa wa kiubwege kwa kukubali kuwa kifo ndicho hatima ya binadamu wa kiubwege. Isitoshe, kuhusu suala la ukengeushi, Albert Camus alionyesha kwamba ukengeushi huyapa maisha thamani yake kutokana na juhudi za binadamu, kwa kutekeleza shughuli zake kivyake kwa uhuru wa kiubwege. Kwa hili, watunzi wa tamthilia teule walidhihirisha mfanano katika kazi zao. Albert Camus alidhihirisha kwamba maisha ya binadamu hayana maana na hivyo humpasa binadamu wa kiubwege kujitafutia uhuru wa kiubwege, ambao humpa furaha inayomtuliza roho. Hili pia lilijitokeza katika *Amezidi* na *Beluwa* ambapo, wahusika wanajituliza kwa vicheko vya kutisha na kujizuia kulia. Hii ndiyo maana waandishi wa tamthilia hizi teule wanatumia sana vicheko, vilio na sauti ambazo pia hazivasaidii wahusika wao kuboresha hali zao, au hata kujinasua kutokana na mtego wa ulimwengu katili anamoishi.

Uchunguzi na uchanganuzi wa data ulithibitisha nadharia tete zetu kwamba; kwanza, *Amezidi* na *Beluwa* ni tamthilia za kiubwege. Pili, kuna kufanana kwa mwelekeo wa kiubwege katika tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* na tatu, kuna mfanano wa mwelekeo wa kiubwege katika utunzi wa *The Myth of Sisyphus*, *Amezidi* na *Beluwa*.

5.2 Hitimisho

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, tunaona kwamba kuna mlingano wa mwelekeo wa kiubwege katika tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa*, kwa kuangazia vipengele vya kimaudhui na kifani kiubwege.

Kuna umuhimu wa kuhakiki kazi za kiubwege kiulinganishi, ili kurahisisha uelewekaji na kuwapa watunzi motisha ya kutunga kazi kama hizi na kuongeza maaarifa na maendeleo katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili.

Tulichunguza vipengele vya kimaudhui na kifani kiubwege, tukavibainisha na kuvichanganua kwa kuvilinganisha jinsi zinavyojitokeza kwenye *Amezidi* na *Beluwa*. Kwa kufanya hivi, tulidhihirisha mwelekeo wa kiubwege katika tamthilia ya kiswahili kupitia tamthilia teule.

Kwa kuchunguza vipengele vya kimaudhui, tulipata maudhui kama vile; suala la Mungu, kifo na kaburi, ukengeushi na ukosefu wa uthabiti kwa elimu. Kando na maudhui haya, tulichunguza dhamira na mandhari kama vipengele visaidizi vya kimaudhui vilivyojitokeza katika *Amezidi* na *Beluwa*. Tamthilia hizi zinaakisi jinsi ambavyo Said A. Mohamed na Pauline Kea Kyovi wanavyotazama mazingira ya binadamu ulimwenguni; mazingira machafu na yenye kukatisha tamaa ndiposa wakatumia mandhari ya Pango na gerezani mtawalia. Kupitia kwa wahusika wao, wanaonyesha mateso yanayomkabili binadamu katika mazingira yasiyo na matumaini na yaliyojaa ndoto zisizotimizwa. Wanatumia wahusika waliokengeuka na kuthamini kifo na kaburi kama hatima yao. Wanaonyesha kwamba hata elimu anayopata binadamu katika ulimwengu katili haiwezi kumnufaisha kwa lolote bali humzidishia matatizo katika maisha yake. Vile vile, watunzi hawa wameonyesha mwelekeo wao kuhusu kuwepo kwa Mungu, ambapo wanashikilia kwamba Mungu yupo na kuna ukombozi unaotokana na nguvu zinazomzidi binadamu. Binadamu katika tamthilia ya *Amezidi* amechorwa kama yule ambaye anategemea wokovu wa Mungu, wanaposhindwa kutenda mambo madog madogo, wanajituliza kwamba kesho kuna Mungu na atakuja kuwasaidia. Kadhalika, katika *Beluwa*, binadamu anaonyeshwa kutanguliza shughuli zake kwa maombi na wanaingia kwenye sala kabla ya kuanza kutenda.

Vilevile, tulichanganua vipengele vya kifani katika tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* na jinsi vilivyodhihirisha mlingano. Vipengele hivyo vilijumuisha; Uhusika, ambao ulihusisha uchache wa wahusika, wahusika wa kiutopia, wahusika wa kinjozi na wahusika vibonzo. Kando na kipengele cha uhusika, tuliangazia vipengele vingine kama vile; ukosefu wa ruwaza za mazungumzo, utupu, matumizi ya nyimbo, vicheko na vilio, lugha pamoja na ploti. Wahusika tunaowapata katika tamthilia hizi mbili ni wale wasioweza kutenda chochote cha kuboresha hali yake duni; wanashindwa kutenda na kukaa tu wakisubiri kifo ambacho ndicho hatima ya ubwege wa maisha yao. Kadhalika, watunzi hawa wameonyesha kwamba lugha na mawasiliano ya binadamu zimekufa. Wamedhihirisha kwamba juhudi za binadamu kuwasiliana kupitia nyimbo, vicheko na vilio, elimu pamoja na sauti hazifanikishi chochote; kushindwa kutumia lugha ni dhihirisho la ugumu wa maisha yake. Tumeona kwamba maisha ni duara na hakuna ukweli wa maisha; ukweli huo upo tu kwa kifo na kaburi. Kwa watunzi hawa, ploti si muhimu kwenye uandishi wa kazi ya tamthili hivyo, wametupilia mbali suala la ploti; vitushi hutokea kipweke bila kusababishana.

Katika sura ya tano, tulichunguza vipengele vya kiubwege katika *The Myth of Sisyphus* ya Albert Camus kudhihirisha ulinganifu wa mwelekeo wa kiubwege katika kazi hiyo, *Amezidi* na *Beluwa*. Dhana za kiubwege zilizojadiliwa na Albert Camus zililinganishwa na vipengele vya kiubwege vilivyojitokeza katika *Amezidi* na *Beluwa*. Kwa kufanya hivi, msingi wa nadharia ya ubwege ulijitokeza kwa uwazi. Dhana zilizochunguzwa ni pamoja na; wazo la kiubwege, binadamu wa kiubwege na ulimwengu wa kiubwege. Katika kila dhana, tulibainisha maudhui yanayojitokeza kwazo na kuyalinganisha nay ale yanayojitokeza katika *Amezidi* na *Beluwa*. Katika dhana ya wazo la kiubwege, tulipata maudhui ya kifo na kaburi na ukengeushi; masuala ambayo pia yalijitokeza katika tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa*. Maudhui ya

maisha na maana yake na uhuru wa binadamu wa kiubwege yalitokana na dhana za binadamu wa kiubwege na ulimwengu wa kiubwege. Haya pia yalijadiliwa kwa kulinganishwa na vipengele vya kiubwege vilivyojitokeza katika *Amezidi* na *Beluwa* hususan Mtumizi ya sauti, vicheko na vilio.

Nadharia ya ubwege ilitupatia msingi wa kuchanganua data. Baada ya kubainisha vipengele vya kimaudhui na kifani kiubwege, tulivilinganisha na hatimaye mwelekeo wa kiubwege kuhusu tamthilia ya Kiswahili kutumia mifano ya *Amezidi* na *Beluwa* ulidhihirika. Maelezo ya nadharia hii yanaeleza kuwa ubwege ni uhusiano ulio wa kidhahania kati ya akili iliyopevuka na ukweli kuhusu kuwoko kwa binadamu katika ulimwengu katili. Aidha, nadharia hii hudadisi maana ya maisha yake binadamu katika ulimwengu katili.

Utafiti huu umeakisi kuwa, Said A. Mohamed na Pauline Kea Kyovi walichukua mwelekeo wa kiubwege ulio sawa, kulingana na jinsi walivyoangazia vipengele vya kiubwege kimaudhui na kifani katika tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* mtawalia. Kijumla, tamthilia hizi teule ni za kukatisha tamaa na zinaonyesha kwamba maisha ya binadamu katika ulimwengu anamoishi hayana maana.

5.3 Mapendekezo

Kutokana na huu utafiti, tumeweza kutambua kwamba pana haja utafiti zaidi kuhusu mwelekeo wa kiubwege kwa jumla na namna unavyobainika katika tanzu ya tamthilia. Hadi sasa, ni tafiti kidogo tu zimefanywa kuhusu tamthilia za kiubwege. Utafiti zaidi kuhusu ubwege katika tamthilia mbali mbali ufanywe.

Waidha, tunatoa rai kwa wahakiki kufanya utafiti wa kiulinganishi wa *Amezidi*, *Beluwa* na tamthilia nyingine kwenye tapo la ubwege ili kubainisha zaidi ufanisi wao.

Vile vile, tunapendekeza kuwa utafiti wa mwelekeo wa kiubwege ufanywe katika tanzu nyingine za kinathari tofauti na tamthilia. Wataalamu wana uzoefu kwamba ubwege unajitokeza tu kwenye tamthilia lakini itakuwa bora zaidi kazi za kinathari hususan riwaya ikichanganuliwa kwa kutumia nadharia ya ubwege kama ilivyo katika nadharia nyingine.

Tunapendekeza kwamba tamthilia ziandikwe kwa namna ambavyo zinaweza kuakisi udhahania licha ya uhalisia ili kupitisha ujumbe kwa njia tofauti ya kindoto. Kwa kufanya hivi, hadhira itachangamshwa zaidi kutokana na jinsi wahusika wanavyoshindwa kutenda, wanavyoota ndoto zisizotimizwa na wanavyodhihirisha ukweli wa ujinga wao.

Kadhalika, tunapendekeza kwamba tamthilia ya *Amezidi* na *Beluwa* zitafitiwe zaidi kwa kutumia nadharia nyingine tofauti na ubwege, hususan nadharia ya umuundo. Kwa kufanya hivi tutapata maarifa zaidi kuhusu tamthilia hizi teule.

Kulingana na mipaka na muda uliokuwepo wa kufanya utafiti huu, tulijibana zaidi katika vipengele muhimu ambavyo waandishi hawa walitumia kupitisha mawazo yao. Hivyo basi, hatukupata muda wa kushughulikia vipengele vyote vya usanifu wa tamthilia ya kiubwege. Tunapendekeza basi kwamba tamthilia hizi mbili zifanyiwe utafiti zaidi hasa katika kitengo cha maudhui.

MAREJELEO

- Adungo, C. (2017, September 28). *Mwalimu na mwandishi mpevu wa Fasihi*. Taifa Leo. A Nation Media Group Publication, (uk.11-15).
- Alembi, E. (2000). *Appreciating Drama*. Nairobi: Acacia Stantex Publishers.
- Aristotle, (1934). *The Poetics*, New York: J.M. Dent & Sons Ltd.
- Baraza la Kiswahili la Zanzibar (h.t.). Prof. Said Ahmed Mohamed. <https://bakiza.go.tz/SAM/>
- Beckett, S. (1995). *Waiting for Godot*, London: Faber and Faber.
- Bertoncini E. Z. (1989). *Outline of Swahili Literature Pros, Fiction and Drama*. UK: Leiden, E. J. Brill.
- Bertoncini E. Z. & Wenzake; (2009). *Outline of Swahili Literature*. UK: Leiden, E. J. Brill.
- Camus, A. (1942). *Le Mythe de Sisyphe*. France: Editions Gallimard.
- Camus, A. (1955). *The Myth Of Sisyphus, translated by J. O'Brien*. London: Penguin Books.
- Camus A. (1984). *The Myth of Sisyphus*. London: Penguin Books.
- Chatman, S. (1978). *Story and Discourse: Narrative Structure in Fiction and Film*. Ithaca and London: Cambridge University Press.
- Chukwuka, U. V. (2013). *Absurdity of Life in Albert Camus: A critique*. Bachelor of Arts, Nnamdi Azikiwe University AWK. Nigeria.
- Cruickshank, J. (1958). *Albert Camus: The Literature of Revolt*. London: Oxford University Press.
- Cruickshank, J. (1960). *Albert Camus and the Literature of Revolt*. London: Oxford University Press.
- Cruickshank, J. (2022). "Albert Camus". *Encyclopedia Britannica*, 1 Jan. 2022, <https://www.britannica.com/biography/Albert-Camus>. Accessed 15 March 2022.
- Cuddon, J. A. (1979). *A Dictionary of Literary Terms and Literary Theory*. UK: A John Wiley & Sons Ltd Publication.
- Daniel, Z. L. (2012) *Mkabala wa kibwege katika fasihi ya Kiswahili, mifano kutoka tamthiliya ya Amezidi (1995) ya Said A. Mohamed* : Chuo kikuu cha Dar es Salaam. (Hakijachapishwa).

- Daniel, Z. L. (2017). *Matumizi ya Mkabala wa kiubwege katika uchambuzi wa tamthilia ya Amezidi (1995) ya S. A. Mohamed*. Dar es Salaam: Kiswahili Juz:76. <https://journals.udsm.ac.tz/index.php/kiswahili/article/view/805>
- Edeh, A. (2019). *Existential Absurdity and Alienation in Samuel Becketts's waiting for Godot and Franz's Kafka's The Metamorphosis: An Existential Analysis*. Master's Thesis: Finland, University of Oulu.
- Encyclopaedia Britannica (1st ed.) (h.t). *English Language Reference work*. <https://www.britannica.com/topic/Encyclopaedia-Britannica-English-language-reference-work>.
- Forster, E. (1927). *Aspects of the Novel*. New York. www.rosettabooks.com/AspectsOfTheNovel
- Fugard, A. (1960). *Nangogo*, London: Guernsey Press.
- Fugard, A. (1967). *The Coat*, London: Oxford University Press
- Fugard, A. (1974). *No Good Friday*, Nairobi: Oxford University Press.
- Fugard, A. (1974). *Sizwe Bansi is Dead*, London: Oxford University Press.
- Fugard, A. (1975). *Take Blood Knot*, Nairobi: Oxford University Press.
- Gerold, H. (h.t). *Historia ya Mohamed Said Abdalla, Said Ahmed Mohamed na Euphrase Kezilahabi*. Academia edu. <https://www.academia.edu/32297476/historiyamuhamedsaidabdullasaidahmedmohamednaeuphrasekezilahabi>
- Gilgen, G. (1980). *Absurdist Techniques in the Short Stories of Juan Jose Arreola*. Tasnifu ya MA, Chuo kikuu cha Wisconsin-Madison.
- Gill, R. (1985). *Mastering English Literature*. London: Macmillan Educational Ltd.
- Gill, R; (2006): *Mastering English Literature*. Toleo la Tatu. Houndmillls: Palgrave Macmillan.
- Hough, G. (1962). *An Essay on Criticism*, London: Gerald Duckworth and Co. Ltd.
- Hussein, E. N. (1983). *Mashetani*. Nairobi: Oxford University Press.
- Hussein, E. N. (1983). "Hatua Mbalimbali za Kubuni na Kutunga Tamthilia Kufuatana na Misingi ya Ki-Aristotle." katika, Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III: Fasihi. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili. (Uk. 197-205).
- Ionesco, E. (1962). *The Chairs*, London: Cox and Wyman Ltd.
- Kaplan, A. (2016). *Looking for The Stranger: Albert Camus and the Life of a Literary Classic*. .

- Kierkegaard, S. (2002). *A historical introduction to Philosophy*, U.S.A.
- Kierkegaard, S. (2008) *Fear and Trembling* quoted in S. Michelman, *Historical dictionary of Existentialism*, U.S.A.
- Killam, C. D. (Mhariri) (1973). *African Writers on African Writing*. London: Heinemann.
- King'ei, K. (1997). *Mwongozo wa Amezidi*, Nairobi: East African Educational Publishers.
- Kitchin, R. L. (1966). *Drama in the Sixties; Form and Interpretation*. Nairobi: Faber & Faber Ltd.
- Kothari, C. R. (2004) (2nd Rev. Ed.). *Research Methodology: Methods and Techniques*. India: New age International Publishers.
- Kyovi, K. P. (2012). *Beluwa*, Kenya: Oxford University Press, East Africa Ltd.
- Kyovi, K. P. (h.t). *Pauline Kea Kyovi –Translation Directory*. https://www.translation-directory.com/translators/cvs/pauline_kyovi.doc
- Lewis, A. (1962). *The Contemporary Theatre*, New York: Crown Publishers, Inc.
- Madumula, J. (1995). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar-es-Salaam University Press.
- Madumulla, J. S.(2009). *Riwaya ya Kiswahili: Historia, Nadharia na Misingi Uchambuzi*. Dae es Salaam: Mature Educational Publishers.
- Magare, A. W. (2002). *Uhakiki wa tamthilia ya Amezidi kama kazi ya Kiubwege*. Tasnifu ya MA, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Mair, L. (1964). *Primitive Government*. London: Penguin Books
- Maneno, S. K. (1997). *Mwongozo wa Amezidi*, Nairobi: Oxford Universit Press.
- Martin, E. (1974). *The Theatre of the Absurd*, London: Methuen.
- Martin, E. (h.t). *The Theatre of the Absurd*. <https://www.penguinrandomhouse.com/books/47062/the-theatre-of-the-absurd-by-martin-esslin>.
- Mary. A. N. (2017). *Configuring the Absurd; A reading of Robert Serumaga's A Play, Majangwa and The Elephants*. Tasnifu ya MA, Chuo Kikuu cha Bergen. (hajachapishwa)
- Masebo, J. A. & Nyangwine, N. (2008): *Jitayarishe kwa Kiswahili: Kidato cha 1&2, Maswali na majibu*. Dar es Salaam, Tanzania: Nyambari Nyangwine Publishers.
- Mazrui, A. A. (1982). *Africa Between Nationalism and Nationhood, A political Survey*. University of Michigan. Sage Journals.

- Mbatiah, M; (2001): *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.
- Method, S. (2015). *Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili: Mwongozo kwa Mwanafunzi na Mwalimu wa Fasihi Simulizi na Andishi*. Dar es Salaam: MEVELI Book Publishers
- Mlama, P. (1983). *Utunzi wa tamthilia katika Mazingira ya Tanzania*, Dar es Salaam: Makala katika *Fasihi III*, TUKI.
- Mohamed, S. A. (1995). *Amezidi*, Nairobi: Macmillan Kenya Ltd.
- Mohamed, S. A. (2011). *Janga la Werevu*. Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.
- Mohamed, S. A. (2011). *Kimya Kimya Kimya*. Nairobi: Longorn Publishers (K) Ltd.
- Mohamed, S. A. (2016). *Mashetani Wamerudi*. Nairobi: Sportlight Publishers (EA) Ltd.
- Mugarisi, E. O. (2014). *Drama of the Absurd: A case study of Serumaga, Imbuga & Kasigwa*. Tasnifu ya MA; Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).
- Muhando & Balisidya (1976). *Fasihi na Sanaa za Maonyesho*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar-es-Salaam: TUKI.
- Murungi, G. K. (2013). *Mtindo unavyoendeleza maudhui katika Natala*. Tasnifu ya shahada ya uzamili, chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa) http://erepository.uonbi.ac.ke/bitstream/handle/11295/59975/Kanyua_Mtindo%20unavyoendeleza%20maudhui%20katika%20natala.pdf?sequence=3&isAllowed=y
- Mushi, S. (1971). *Mfalme Edipode*. Dar-es-Salaam: Oxford University Press.
- Mwari, A. M. (2018). *Utendaji wa Kidrama wa Riwaya ya Haini ya Shafi Adam Shafi 2003*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapishwa).
- Myers, J. M. (1948). Old Testament Literature. Sage Journals <https://journals.sagepub.com/doi/abs/10.1177/002096434900300108>
- Ndal, E. A (1998). *Mwongozo wa Amezidi*. Nairobi: City Book Publishers.
- Ngara, E. (1990). *Ideology and Form in African Poetry*. Nairobi: Heinemann Kenya.
- Ngugi wa Thiong'o. (1986). *Decolonising The Mind: The Language of African Theatre*. Nairobi: Heinemann Kenya.
- Njogu, K. & Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

- Oumah, O. (2018, Mei 26). *Said A. Mohamed: I will write until my last day on this earth*. Daily Nation. <https://www.nation.co.ke/lifestyle/weekend/Said-A-Mohamed-I-will-write-until-my-last-day-on-this-earth/1220-4580376-5gxcq5z/#>.
- Panumas, K. (2019): *Albert Camus and the Problem of Absurdity*. Academic insights for the Thinking World: Oxford University Press. <https://blog.oup.com/2019/05/albert-camus-problem-absurdity/>
- Plato, (1955). *The Republic*. New York: J. M. Dent & Sons Ltd.
- Sarara, M. M. (1997). *Maudhui katika Tamthilia za Said Ahmed Mohamed*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Sartre, J. P. (1985). *Reporieve*. England: Penguin Books.
- Sartre, J. P. (1985). *Iron in the soul*. England: Penguin Books.
- Schopenhauer, A. (2005). *The World as Will and Representation*, as quoted in J. Young, *The Death of God and the Meaning of Life*, U.S.A.: Oxford University Press, p. 108.
- Semzaba, E. (1997): *Tamthilia ya Kiswahili*. Tanzania: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Serumaga, R. (1976). *Majangwa and A Play*. FA: Heinemann.
- Stein, A. L. (2019) "*Absurdity and Metaphysical Rebellion in the Philosophies of Albert Camus and Omar Khayyam*". Undergraduate Honors Thesis Collection: Indiana, Butler University.
- TUKI (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- TUKI (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.
- Van Pelt, P. (1971). *Bantu Customs in Mainland Tanzania*. Tabora: T.M.P. Book Department.
- Vuzo, A.M. (1997). *Mwongozo wa Amezidi*, Nairobi: Macmillan Kenya Ltd.
- Wafula, R. M. (1999). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo yake*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wafula, R.M. & Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi. Misingi na vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*, Nairobi: Focus Publications Ltd..

- Wamitila, K.W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.
- Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi, Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.
- Warnock, M. (1970) *Existentialism*, London: Oxford University Press
- Webb, E. (1972). *The Dark Dove: The Sacred and Secular in Modern Literature*. Seattle Washington: University of Washington Press.
- Wellek, R., na Warren, A. (1978). *Theory of Literature*. London: Penguin Books.
- Wilson, E. & Goldfarb, A. (1991). *Theatre: The Lively Art*. New York: McGraw-Hill.
- Wilson, E. & Goldfarb, A. (2002) (4th ed.). *Theatre: The Lively Art*. New York: McGraw-Hill.
- Willet, J. ed. (1967). *The Theatre of Bertolt Brecht. A Study From Eight Aspects*. London: Methuen and Co.Ltd.
- Willet, J. Trans & ed. (1978). *Brecht on Theatre: The Development of an Aesthetics*. London: Eyre Methuen.
- Williams, R. (1966). *Modem Tragedy*, London: Chatto & Windus Ltd.

VIAMBATISHO

Kiambatisho A: Said Ahmed Mohamed na Uandishi Wake

Gerold Hyera katika tovuti <https://www.academia.edu> habari iliyopakuliwa tarehe 22/02/2023 anaeleza historia ya Said A. Mohamed kwamba alizaliwa Pemba, Zanzibar mnamo Disemba 12, 1947. Anaendelea kueleza kwamba hakupata kupata malezi ya baba na mama kwa njia ipasavyo kwa sababu wazazi wake walitengana akiwa na umri mdogo sana. Alilelewa na mama zake “wakubwa”, Bi Jokha na Bi Rukia. Alisomea Wete Boys, Pemba kabla ya kuhamia Kiembe Samaki kisha Darajani, Unguja alikohitimu elimu ya shule ya msingi. Baadaye, alijiunga na Shule ya Upili ya Gulioni (awali ikiitwa King George The VI). Baada ya kumaliza masomo ya sekondari, Said A. Mohamed alijiunga na Chuo cha Ualimu cha Nkurumah, Zanzibar mnamo 1966.

Said A. Mohamed hakujiunga na Kidato cha Tano na cha Sita kwa sababu wakati huo aliyekuwa akiongoza Serikali ya kimapinduzi nchini Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume alikatiza masomo ya kiwango hicho. Said ana mke mmoja, Rahma. Aidha, ana watoto wawili. Baada ya kuhitimu Ualimu mnamo 1966, alifundisha katika Shule ya Msingi ya Kizimbani ambapo alifanya kazi kwa wiki mbili tu, kisha akaenda kufunza Bayolojia, Hisabati, Kemia na Kiswahili kwenye Shule ya Upili ya Utaani hadi 1974. Alibahatika kujiunga na shule ya “*International Correspondence*” alikosomea masomo ya sanaa katika kidato cha tano na Sita. Mnamo 1976, alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es salaam ambapo alisomea Shahada yake ya Kwanza katika Elimu. Alijikita katika isimu na fasihi ya Kiswahili.

Baada ya kufuzu, Said Ahmed Mohamed alirejea Zanzibari na kuwa mwalimu Mkuu katika shule ya msingi ya Hamamni na shule ya Upili ya Hamamni kwa miaka mitatu. Baadaye alirejea Chuo Kikuu cha Dar es salaam ili asomee shahada yake ya Uzamili katika Isimu Tekelezi. Upekee wa umilisi wake wa Kiswahili ulimvutia mwalimu Siegmund Brauner, Mjerumani aliyemfundisha kozi za Isimu Linganishi na Isimu Historia. Mohamed alipata nafasi ya kwenda Ujerumani kusomea shahada ya Uzamifu (PhD).

Said Ahmed Mohamed alienda Chuo Kikuu cha Karl Marx, Leipzig, kule Ujerumani mwishoni mwa 1981 na kukamilisha masomo yake mnamo (1985). Miezi michache baadaye, aliteuliwa na Rais wa Zanzibari kwa wakati huo, Mzee Idris Abdul Wakil, kuwa kama Mkurugenzi wa Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni (TAKILUKI) ambayo baadaye iliitwa Chuo Kikuu cha Zanzibari (SUZA).

Katika mwaka wa 1987 Said Ahmed Mohamed aliingia Kenya na kuwekwa Mwenyekiti wa kwanza katika Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret na baadaye kufundisha kozi za Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi hadi 1990. Kisha alienda Japan kufundisha Kiswahili kwenye Chuo Kikuu cha Osaka akiwa Mkuu wa Idara ya lugha za kigeni. Alipata Uprofesa na kwenda katika Chuo Kikuu cha Bayreuth, kule Ujerumani alikofundisha Kiswahili kati ya 1997 na 2012.

Isitoshe, ubunifu wake Said Ahmed Mohamed, kama alivyoeleza kwenye mahojiano yaliyoongozwa na mwandishi wa *Daily Nation*, Oumah Otieno, ulitokana na kunasa mashairi yaliyokaririwa na mjomba wake. Alipenda sana kusoma na kutunga mashairi na hadithi fupi tangu alipokuwa mwanafunzi wa darasa la tano. Alitunga mashairi ambayo mengi yalitumiwa na walimu kufundishia madarasa ya juu. '*Nimfuge Ndege Gani Ili Nipate Salama*' ni shairi lake la kwanza alilolitunga mnamo 1960. Mengi ya mashairi yake yalighaniwa katika Radio Zanzibar. Umotishaji wake ulitokana na Walimu wake; Mohamed Abdalla na Kindi Abubakary, waliomhamasisha pakubwa.

Said Ahmed Mohamed anakiri kwamba alirithi kipawa cha usanii kutoka kwa mama yake “mkubwa” aliyekuwa nyakanga. Mama yake mkubwa alikuwa bingwa kuimba nyimbo za unyago. Aidha, alikuwa mtunzi hodari wa mashairi na kupenda sana hadithi za jadi za fasihi simulizi. Zaidi ya kurithi kipaji kutoka kwa huyu mama yake, uandishi wa Said ulitokana na mafunzo ya elimu ya kidini ya Kiislamu aliyopata katika madrassa.

Aidha, Said Ahmed Mohamed aliwahi kushiriki mashindano ya Uandishi wa Hadithi Fupi za Kiswahili yaliyodhaminiwa na Shirika la Habari la BBC katika miaka ya 90. Nyingi za hadithi zake pia zilisomwa katika kituo cha Deutsche Welle (DW), Ujerumani. Hali hii ilimhimiza kuandaa Diwani *Sadiki Ukipenda na Hadithi Nyingine*, kitabu kilichochapishwa na Jomo Kenyatta Foundation (JKF) mnamo 2002. Pia, alidhihirisha uwezo alio nao kwa utunzi wa visa bunilizi vilivyoelezea uhalisia

wamaisha ya kila siku katika jamii. Upekee wa kisanaa katika riwaya za Mohamed Suleiman Mohamed, *Kiu* (1972) na *Nyota ya Rehema* (1976) ulimpa Mohamed umotishaji wa kutunga riwaya yake ya kwanza, *Asali Chungu* (1977). Baadaye alitunga *Utengano* na *Dunia Mti Mkavu* vitabu vilivyochapishwa mnamo 1980. Kazi hizo zilimzidishia umaarufu na kumfungulia milango ya kupokezwa tuzo za haiba kubwa katika Afrika na nje ya Afrika.

Akiwa mshairi mahiri, Said Ahmed Mohamed ametunga diwani mbalimbali zikiwa ni pamoja na *Sikate Tamaa* (1980), *Kina cha Maisha* (1984) na *Jicho la Ndani* (2002), kazi zinazozamia masuala ya kisiasa, kimapenzi, kiuchumi na kiutamaduni. Ujuzi wa fani katika utunzi wa fasihi ni sifa iliyomfanya kufaulu kutumia mtindo wa uhalisia mazingaombwe katika *Kivuli Kinaishi* (1990), *Amezidi* (1995), *Babu Alipofufuka* (2001) na *Sadiki Ukipenda* (2002). Ametumia sana mbinu za bunilizi na taswira katika tamthilia za *Pungwa* (1988), *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2004) na *Posa za Bi Kisiwa* (2007) aliyoiandika kwa kumshirikisha Profesa Kitula King'ei wa Chuo Kikuu cha Kenyatta. *Nyuso za Mwanamke* (2010) ni riwaya aliyoitunga miaka 36 baada ya kuchapishwa kwa *Utengano* (1980). Anajivunia pia riwaya *Kiza Katika Nuru* (1988), *Tata za Asumini* (1990), *Dunia Yao* (2006), *Mhanga Nafsi Yangu* (2012) na *Mkamadume* (2013). Ametunga Zaidi ya vitabu sitini, za hivi karibuni zikiwa tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* (2011), *Mashetani Wamerudi* (2016) na *Janga la Werevu* (2016). *Gharama ya Amani* (2014) ni kitabu chake cha hadithi kinachosisitiza umuhimu wa utu, uadilifu na utaifa miongoni mwa wanajamii.

Akiwa mmoja wapo wa waandishi wa riwaya za kimapinduzi na za kifalsafa, baadhi ya kazi za Said Ahmed Mohamed zilitasiriwa. Ametajwa kuwa mwandishi mashuhuri zaidi Afrika Mashariki kutokana na ukamilifu wake katika kuandika riwaya, tamthilia, mashairi, hadithi fupi, fasihi ya watoto na hata vitabu vile vya kiada vya kufundishia shule za Msingi, Upili na Vyuo.

Kiambatisho B: Pauline Kea Kyovi na Uandishi wake

Adungo (2017) anaeleza kwamba Pauline Kea Kyovi alizaliwa 1972 katika kijiji cha Majimboni, eneo la Shimba Hill, Kaunti ya Kwale akiwa mwanambee katika familia ya watoto sita wa Bi. Esther na Bw. Gilbert Kea. Alisoma katika shule ya msingi ya Majimboni hadi mwishoni mwa 1987 kabla ya kuhamia shule ya msingi ya Ndavaya, eneo la Kinango, Kwale. Baadaye, aliufanya mitihani ya kitaifa ya darasa la nane (K.C.P.E) mnamo 1986 na akajiunga shule ya upili ya wasichana ya Bura, Taita 1987 na kufanya mtihani wake wa kitaifa wa kidato cha Nne (K.C.S.E) mwishoni mwa 1990.

Pauline alijiunga na Chuo Kikuu cha Kenyatta, katika mwaka wa (1992), kusomea Ualimu (Kiswahili na Dini ya Kikristo) na kufuzu mwishoni mwa (1996). Kutokana na maelezo kwenye (*Taifa Leo*, 2017), uamuzi wa Pauline kusoma Kiswahili chuoni, ulichochea na nia ya kutaka kuendeleza utamaduni wa lugha hiyo. Aidha gazeti hili linaeleza kwamba Pauline anakiri kwamba upekee na ukubwa wa uwezo wa nyanya zake katika kusimulia hadithi za kiubunifu ulimjengea msingi imara wa kuwa msemaji mzuri wa Kiswahili.

Pauline Kea ni mwandishi mbunifu ambaye huandika tamthilia za kitaalamu na za kisanii zinazoshughulikia hadhira mbalimbali. Machapisho yake yanajumuisha Marejeleo kama vile; *Kamusi Ya Watoto* (2011) na *Dhibiti PTE Kiswahili* (2009). Aidha, alitunga tamthilia ya *Beluwa* (2012) na *Kigogo* (2016) ambayo iliteuliwa kutumiwa na wanafunzi katika shule za Secondary nchini Kenya. Vile vile, kazi za Novela pia hakuziacha nyuma hivyo alitunga *Kipendacho Roho* (2010) na hadithi fupi zikiwemo; *Isiponyenza* katika *Maskini Milionea* (Mhariri: Ken Walibora), *Njugu Karanga* katika *Gitaa* (Mhariri: Timothy Arege), *Fatuma Ninja* katika *Takrima Nono* (Wahariri: Clara Momanyi, Rayya Timammy), *Mwasi* katika Safari ya Ahadi (Wahariri: Jeff Mandila na Ben Mkote), *Mdharau biu* katika *Homa ya Nyumbani* (Wahariri: Ken Walibora na Said A. Mohamed) na *Vazi la Mhudumu* katika *Vazi la Mhudumu* (Wahariri: P.I Iribemwangi na Hamisi Babusa). Katika uwanja wa Ushairi ameandika *Waja Leo* (Mhariri: Ken Walibora) bila kuacha Hadithi za watoto; *Vituko Vya Sungura* (2008), *Pupa Za Bupa* (2009), *Njiwa Mweupe* (2012), *Msiba wa Kujitakia* (2013) na *The Last Comes First* (2013).

Katika wasifu wa Puline Kea Kyovi, anaeleza kwamba kuna kazi zijazo akizitaja kuwa; Hadithi fupi- *Chupu Chupu, Kiriba na Nusura, Hadithi za Lona na Katika Utashi wa Dola, Tumbiri Mtundu*; kitabu cha Kiada kwa darasa la tatu na *Twitty My Parot Pet* ambacho ni kitabu cha kiada kwa darasa la saba.

Kiambatisho C: Albert Camus na Uandishi Wake

Anavyoeleza Cruickshank katika *Encyclopedia Britannica* (2022), Camus alizaliwa nchini Ufaransa mnamo tarehe 7 Novemba, 1913 kule Mondovi, Algeria. Alikuwa na wake wawili; Simone Hie na Francine Faure-ambaye alimzalia mapacha waliowaita Catherine na Jean. Kwa sababu ya kifo cha baba yake; Lucien Auguste Camus (1888-1914) katika Vita vya I vya Dunia, alilelewa na mama yake katika mazingira ya umasikini mkubwa na hatari. Aliishi maisha ya upweke kwa kutengwa kutokana na ugonjwa wake wa Kifua Kikuu alioanza kuugua akiwa na miaka kumi na saba.

Alipofikia umri wa utu uzima, alisoma falsafa katika Chuo Kikuu cha Algeria na baadaye, aliandika Gazeti la *Alger Republicaine* kuhusu hali za kisiasa Nchini Algeria. Gazeti hilo lilipigwa marufuku kwa sababu ya kuangazia masuala nyeti ya kisiasa. Akiwa na umri wa miaka 25, alihamia Paris, ambapo baadaye alifanya kazi kama mwanahabari, mtunzi na mwigizaji. Alijiingiza katika harakati za kisiasa na kuanza kutumika katika Chama cha kikomunisti Ufaransa. Muda mfupi baadaye alifukuzwa kutokana na sababu ya kutofautiana kwake kwa malengo yaliyofuatwa katika hatua za kisiasa. Katika kipindi cha vita vya pili vya Dunia, alishiriki kikamilifu kwenye vyombo vya habari vya kisiri na aliandika sehemu ya kazi zilizomfanya awe maarufu.

Mnamo 1957, alipokea Tuzo ya Nobel ya Fasihi akiwa na akiwa na miaka arubaini na nne. Miaka miwili baadaye, alikufa kutokana na ajali ya gari lililokuwa likiendeshwa na rafiki na mchapishaji wake; Michell Gallimard, akiwa ametimia ,iaka arubaini na sita (tarehe 4 Januari, 1960) Sens, kule Ufaransa.

Albert alianza kuweka msingi wa falsafa yake katika mwaka wa (1937) lakini ilikuja kupata upenyezo mnamo (1942). Mtunzi huyu aliathiriwa sana na wanafalsafa aliowasoma ambao walidadisi maana ya maisha yake binadamu. Wanafalsafa hao ni pamoja na; Arthur Schopenhauer (1813-1860), Soren Kierkegaard (1813-1855) na Fredrich Nietzsche (1844-1900). Schopenhauer ndiye alikuwa mwasisi wa falsafa ya udadisi wa maana ya maisha ya binadamu na kuathiri sana mawazo ya Nietzsche. Kwake, maisha ya binadamu humanisha nia inayohusu mateso ya binadamu na kuadhibiwa kwake kutokana na dhambi zake. Kierkegaard naye hakuwa msomi bali aliathiriwa sana na hali yake ya maisha duni yaliyojawa na mateso, utupu,

ukosefu wa matumaini na uhakika. Kulingana naye, maisha ya binadamu huwa na maana ikiwa tu ataamini kwa Mungu wa Ukristo. Aliona kwamba maisha yake hayana maana na kushikilia kwamba binadamu huipa maisha yake maana kibinafsi kutoka na juhudi zake mwenyewe (Kierkegaard, 1843).

Nietzsche kwa upande mwingine anadai kwamba maisha hayana maana kwa wazee wakongwe na wagonjwa. Kwake, juhudi za kutumia nia na nguvu za kubuni, hujenga maisha ya binadamu na maana yake. Mawazo haya aliyoyasoma Albert Camus yalimpelekea katika kuwa na msimamo imara kuhusu suala la uwepo wa Mungu na nguvu dhahania zinazoweza kumtuliza binadamu asiye na uwezo wa kubadili mazingira yake katili yenye mateso mengi. Kwake Camus, wanadamu wanapaswa kukubali uwepo wa ubwege wa maisha.

Aidha, kutokana na urafiki wake na Jean-Paul Sarte, aliangaziwa kama mdhanaishi japo alipendelea kutohusishwa na falsafa yoyote ile.

Albert Camus alisifika sana katika taaluma ya utunzi wa kifasihi. Aliandika Tamthilia, Riwaya, Hadithi Fupi na Insha. Kazi zake ziliandikwa kwa Kifaransa na kutafsiriwa baadaye. Tamthilia alizotunga ni kama vile; *The Revolt in Asturias* (1936) iliyoangazia sana maudhui ya siasa, *Caligula* (1944) ambayo ilianika masuala ya ukosefu wa maana maishani mwa binadamu japo ilijitokeza kama kazi ya kihistoria zaidi, *The Misunderstanding* (1944) iliyoangazia falsafa ya ubwege ikiwa imejumuisha ukosefu wa furaha, kutatizika kwa mawasiliano na kifo kama kitulizo cha roho ya binadamu, *The state of Siege* (1948) ambayo ilijitokeza kuanika ukandamizaji na tauni iliyokuwa ikiangamiza wakaazi wa Uhispania, *The Just Assassins* (1949) iliyoangazia Mauaji na Ugaidi, *The Possessed* (1959) ambayo ilichora uwepo wa binadamu, ukosefu wa Ukweli na ukosefu wa Imani huku *Requiem for a Nun* (1962) ikijitokeza kumulika ukosefu wa mantiki katika mazungumzo.

Riwaya alizotunga ni pamoja na; *The Stranger* (1942) iliyojitokeza kama kazi ya kifalsafa zaidi kwa kuangazia Ubwege na Udhanaishi, *The Plague* (1947) iliyoanika athari za tauni katika mji wa Oran kule Algeria na ukosefu wa uwezo wa binadamu kukadiria hatima ya maisha yake, *The Fall* (1956) ambayo ilianguzia maudhui ya kutokuwepo na Ukweli, *A Happy Death* (1971) ambayo ilikuwa riwaya ya kwanza kabisa ila haikuchapishwa hadi baada ya kufa kighafla kwa Camus; ilianguzia

maudhui ya Nia ya kuwa na furaha ambayo haifikiwi, na *The First Man* (1994) ambayo ni kazi ya mwisho kabisa iliyokosa kukamilishwa kutokana na ajali iliyosababisha kifo cha mtunzi. Kazi hii ilihusisha maisha ya Camus ya utotoni na kudhihirisha hali yake duni ambayo hakuwa na uweza wa kuibadili.

Kwa upande wa Hadithi Fupi alitunga *Exile and the Kingdom* (1957) ambayo ni mkusanyiko wa hadithi nyingine sita zikiwemo; *The Adulterous Woman*, *The Renegade*, *The Silent Men*, *The Guest*, *The Artist at work* na *The Growing Stone*. Kijumla, hadithi hizi zinaangazia maudhui ya Uhamishoni, Upweke na Utamaushi pamoja na Ugeni katika taifa alimokulia mtu.

Kando na hayo, aliandika makala mengine yakiwemo *The Myth of Sisyphus* (1942) ambayo yalijitokeza kuwa ya kwanza ya kifalsafa zaidi ya kazi zote za Camus; wazo lililoathiriwa na Kierkegaard, Schopenhauer na Nietzsche. Aidha, *The Rebel* (1951) ilijitokeza kuwa maandishi yaliyoangazia maendeleo ya kihistoria, Ukengeushi na Dunia iliyokosa maana. *Reflection on the Guillotine* (1957) pia ni makala yaliyoangazia suala la adhabu ya Kifo kwa watenda kosa; suala ambalo alilikashifu sana. *Resistance, Rebellion and Death* (1960) ndiyo maandishi ya mwisho iliyokamilika kabla ya kifo cha Camus na ni mkusanyiko wa insha za mtunzi huyu alizoteua. Maudhui yaliyotawala kazi hii ni suala la mgogoro katika taifa lake la Algeria; huku akikashifu adhabu ya Kifo.